# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA SABA

**Kikao cha Nane – Tarehe 19 Aprili, 2007**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI:-

Hati ifuatayo iliwasilishwa mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA(MHE. MUSTAFA H. MKULO):**

Taarifa ya Mwaka ya Utekelezaji wa Soko la Bima Nchini kwa Mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba, 2005 *(The Annual Insurance Market Performance Report for the Year Ended 31st December, 2005)*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 99

**Zoezi la Uandikishaji Wapiga Kura**

**MHE. MARIAM S. MFAKI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ilifanya kazi ya kuwaandikisha wapiga kura mwaka 2004; na kwa kuwa, kuna vijana watakaokuwa wamefikisha umri zaidi ya miaka 18 ifikapo mwaka 2010; na kwa kuwa, kuna baadhi ya wananchi hawakuandikishwa mwaka huo:-

(a) Je, Serikali itaanza lini maandalizi ya zoezi la uandikishaji wa wapiga kura?

(b) Je, Serikali itatoa elimu ya uandikishaji huo lini ili isitokee tena kwa wananchi kutojiandikisha?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. DR. LUKA J. SIYAME)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nami niungane na wenzangu kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Mbozi hususan wale wa Jimbo la Mbozi Magharibi, kutoa salamu za rambirambi kwa kifo cha aliyekuwa Mbunge wa Gairo na Waziri wa Afya kwa nyakati mbalimbali marehemu Dr. Aaron Chiduo. Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba mwaka 2004 tulifanya kazi ya kuwaandikisha wapiga kura nchini kote. Watanzania wengi wenye umri wa miaka 18 na kuendelea waliojitokeza waliandikishwa. Utekelezaji huo ni kwa mujibu wa Ibara ya 5(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Ni kweli pia kwamba vijana ambao walikuwa chini ya umri wa miaka 18 wakati huo, baadhi yao watakuwa wametimiza umri huo na kupita ifikapo wakati wa Uchaguzi Mkuu mwaka 2010. Kwa kutambua hivyo, matayarisho ya kuboresha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura yanaendelea. Lengo ni kuwaandikisha watanzania ambao hawakujiandikisha, kuwaondoa katika Daftari waliokuwa wameandikishwa lakini kwa bahati mbaya wamefariki na pia kubadilisha taarifa kwa watakaotaka taarifa zao zibadilishwe. Matayarisho hayo yanajumuisha kutenga fedha kwenye Bajeti, kuboresha mfumo wa kompyuta na kuweka utaratibu wa namna ya kuboresha Daftari hilo.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huo utawasilishwa kwa wadau mbalimbali ili kupata maoni yao kwa lengo la kusaidia kufanyika maandalizi yote kwa ufanisi. Mpango huo wa kuboresha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura unatarajiwa kuanza katika kipindi cha mwaka wa fedha 2007/2008.

(b) Mheshimiwa Spika, elimu ya jumla inayolenga kuhamasisha wananchi wenye sifa kuhusu umuhimu wa kujiandikisha kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura itaanza kutolewa mapema mwezi Julai, 2007. Elimu maalum itatolewa kwa kila kanda kabla na wakati wa uandikishaji ili kuwawezesha wahusika wote kufanikisha zoezi hilo kwa kushiriki katika muda utakaopangwa na kuelewa utaratibu mzima utakaotumika.

Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu, kwamba maandalizi na zoezi zima la kuboresha Daftari la Wapiga Kura vitafanyika kwa umakini mkubwa.

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, inaonyesha kwamba ni jinsi gani Serikali imejiandaa kukabili zoezi hilo.

Mheshimiwa Spika, swali langu ndogo ni kama ifuatavyo:- Kwa sasa hivi Serikali kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri ni kwamba kuna baadhi ya watu ambao tayari huko nyuma hawakundikishwa kwenye zoezi la mwaka 2004. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kuwatumia Watendaji wa Vijiji na Kata ili kuweza kupata orodha angalau ya kuanzia kazi kabla wao hawajaanza zoezi hilo, maana yake idadi ya wengi ambao hawakuandikishwa katika Daftari la kudumu la wapiga kura bado wengi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. DR. LUKA J. SIYAME):** Mheshimiwa Spika, taratibu za kuwatayarisha wananchi huwa linatokana na daftari la kila

kijiji. Kwa hiyo, ni watendaji ambao kwa kawaida wana orodha ya wananchi, sisi kwa taratibu za Serikali huwa ni wafuatiliaji tu wa hiyo orodha na kuhakiki.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa uchaguzi wa Jamhuri wa Muungano na uchaguzi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar unafanyika wakati mmoja; na kwa kuwa Waheshimiwa Wabunge, wanatawaliwa na sheria ya mwaka 1985 ambayo ilifanyiwa marekebisho mwaka 2005; na kwa kuwa wakati wa uchaguzi huo Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar inakuwa kama ni *agency* ya Tume ya Uchaguzi ya Jamhuri ya Muungano; na kwa kuwa sheria hizo mbili zinatofautiana.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaeleza nini juu ya wapiga kura wa Zanzibar ambao wakati huo huo wanatakiwa wapige kura kwa uchaguzi wa Rais wa Zanzibar na Wawakilishi na wakati huo huo wanatakiwa wapige kura kwa Uchaguzi wa Jamhuri ya Muungano wa Rais pamoja na Waheshimiwa Wabunge kwa sheria mbili tofauti. Ni utaratibu gani utatumika kuhakikisha kwamba daftari la kudumu la wapiga kura la Zanzibar ambalo limelalamikiwa na lina upungufu na Tume yenyewe ya Uchaguzi ya Zanzibar imekiri katika taarifa yake kwamba kuna upungufu katika Daftari hilo na Jamhuri ya Muungano inalitumia daftari hilo hilo kwa kupiga kura. Je, uhakiki wa daftari hilo utafanyika lini? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. DR. BATILDA S. BURIAN):** Mheshimiwa Spika, kama tulivyokwisha kusema katika jibu letu la msingi kwamba tuko katika kuboresha daftari la kudumu la wapiga kura, lakini katika kuboresha tunaangalia taratibu tutakazotumia na katika kuangalia taratibu hizo tutapata maoni mbalimbali kutoka kwa wananchi. Tunasema kwamba tutaboresha daftari hilo mara mbili katika kipindi hiki kabla ya kufika mwaka 2010. Namwomba Mheshimiwa Mbunge avute subira tutapata maoni kutoka kwa wananchi. *(Makofi)*

Na. 100

**Uchakavu wa Hospitali ya Wilaya ya Rufiji**

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Hospitali ya Wilaya ya Rufiji ilijengwa mapema wakati wa ukoloni; na kwa kuwa, hospitali hiyo ilifanyiwa ukarabati na upanuzi mkubwa katika miaka ya 1962-1965 wakati wa Ubunge wa Hayati Bibi Titi Mohamed; na kwa kuwa sasa hospitali hiyo ina hali mbaya, chakavu na huduma zake ni finyu hazikidhi mahitaji ya hospitali ya Wilaya:-

(a) Je, ni lini Serikali itawaonea huruma wananchi wa Rufiji kwa kuipanua, kuikarabati *(Rufiji basement)* na kuinunulia vifaa, vyombo vipya na kujenga wigo (*fence*) katika hospitali hiyo?

(b) Je, ni muda gani umepita bila Waziri wa Afya au Naibu wake kutembelea hospitali hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU –TAMISEMI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Idris Mtulia, naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika ni kweli hospitali ya Rufiji (Utete) ilijengwa wakati wa ukoloni na kumbukumbu zilizopo zinaonyesha kuwa ilijengwa mwaka 1945. Kulingana na sensa ya idadi ya watu wa mwaka 2002 Wilaya ya Rufiji ina wakazi wapatao 218,983 ambao wote hao wanategemea huduam za afya katika hospitali hiyo. Lakini pia viko vituo vya afya vitano na zahanati 53 ambazo zinahudumia wananchi. Aidha, iko hospitali ya Mchukwi ambayo ni ya dhehebu la dini. Nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbunge kuwa mwaka 1962 – 1965 ukarabati ulifanyika katika hospitali hiyo. Lakini pia naomba nitoe taarifa kwamba kati ya mwaka 1977 -1998 ukarabati ulifanyika kupitia Mradi wa "*Tanzania Essential H*ealth *Intervetion Project*."

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Idris Mtulia, Mbunge wa Rufiji, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni wajibu wa Serikali kuhakikisha kuwa wananchi wanapata huduma mbalimbali wanazostahili ikiwa ni pamoja na huduma za afya na sio suala la kuwaonea huruma.

Aidha, katika taarifa zilizopo zinaonyesha kwamba kuanzia mwaka 2002/2003 mpaka mwaka 2005/2006, hospitali imeendelea kufanyiwa ukarabati kwa gharama ya jumla ya Shs.30,474,000/=. Aidha, maeneo yaliyohusika ni kujenga baraza, wodi tatu, mfumo wa maji safi na maji taka, chumba cha upasuaji, chumba cha maiti, ujenzi wa wigo na chumba cha maabara. Hospitali hii kwa sasa ina vitanda 100 vya kulaza wagonjwa.

Majengo yanayohitaji ukarabati hivi sasa ni jengo jipya la Kifua Kikuu na Ukoma, jengo la *MCH,* sehemu ya kuchomea taka, mfumo wa maji safi na taka, uzio, vyoo na jengo la upasuaji. Kazi hizi zimepangwa kufanyika katika Bajeti ya mwaka 2007/2008 kwa gharama ya shilingi milioni 52,700,000/=.

Mheshimiwa Spika, hospitali hii hupata mgawo wa mahitaji ya dawa na vifaa vya tiba kutoka Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa kila robo ya mwaka kwa kiasi cha shilingi milioni 9.2. Manunuzi ya dawa pia yanafanyika kwa kutumia fedha za *cost sharing*. Hospitali hii pia ilipata vifaa vya *X-Ray* na *Ultra sound* kupitia mradi wa Kitaifa wa *Overseas Related External Trade*.

(b) Mheshimiwa Spika, ni zaidi ya miaka minne tangu hospitali hiyo ilipotembelewa na aliyekuwa Waziri wa Afya Mheshimiwa Anna Abdallah, tarehe 30 Agosti, 2002. Mheshimiwa Mbunge atakumbuka kwamba mwaka 2006 hata mimi nilitembelea Wilaya ya Rufiji. Ni wajibu wa Wilaya husika kumpangia Waziri ambaye anafanya ziara katika Wilaya yao sehemu ambazo zina ulazima wa kutembelewa. Hata hivyo, tutawasiliana na Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii ili tuweze kutembelea Hospitali hiyo.

**MHE. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Naomba nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri na yanayotia imani.

Mheshimiwa Spika, hospitali ya Wilaya kwa kawaida inachukua wagonjwa wengi kutoka kwenye zahanati na kutoka kwenye vituo vya afya. Hivyo vituo vya Afya Allilamdulahi vipo, lakini watu wanazidi kuzaliana na huduma hazitoshi, vijiji vyetu vingine havina *dispensary*, na hivi karibuni Sera ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ni kupeleka huduma kwa wananchi vijijini na inasema kila kijiji kinaruhusiwa kuwa na *dispensary.* Mpaka sasa tuna matatizo ya Waganga Wakuu wa Wilaya ambao wanazuia ufunguzi wa *dispensary* hizo. Je, Serikali itapeleka Waraka kuwaarifu hao Madaktari wa Wilaya kwamba sasa kila kijiji kikitaka kujenga *dispensary* kiruhusiwe? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** Mheshimiwa Spika, ni azma ya Serikali kwamba kila kijiji kiwe na zahanati na hakuna Mganga yoyote wa Wilaya atakayezuia kijiji fulani kisijenge zahanati. Kwa kweli hilo niseme kwa kuwa ni Sera ya Serikali na kila mtu atafuata sera hiyo. Kwa sasa mpango wa Serikali unakarabati Vituo vya Afya, Zahanati zilizopo ili ziwe katika hali nzuri na kwa Rufiji pia kwa mwaka huu watatengewa shilingi milioni 188 ili kukarabati vile Vituo vya Afya vilivyopo na zile Zahanati zilizopo. Kwa hiyo, hizo Zahanati zingine ambazo zitaongezeka zitakuwa ni za ziada katika vijiji mbalimbali. Lakini kwa sasa hali katika Zahanati na Vituo vya Afya inaridhisha kutokana na ukarabati mkubwa ambao umefanyika kuanzia mwaka 2004 hadi sasa hivi.

**MHE. ABDUL JABIRI MAROMBWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji ilitenga zaidi ya shilingi milioni 20 kununulia dawa kutoka *MSD,* na ni muda mrefu sasa hivi umepita dawa hizo hazijapatikana na kusababisha upungufu mkubwa wa madawa pamoja na vitanda katika hospitali yetu. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa vifaa hivyo ambavyo Wilaya imeomba kutoka *MSD* kwa kutoa fedha vinapelekwa kule haraka iwezekanavyo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU –TAMISEMI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli wakati nikiwa kwenye ziara yangu katika Wilaya ya Rufiji kulikuwa na tatizo la upungufu wa madawa kutoka *MSD,* na tatizo hili sasa hivi limeanza kutatuliwa. Nafikiri Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi kwamba sasa hivi *MSD* inaimarishwa na imeanzisha *zones* mbalimbali ili kuhakikisha kwamba madawa yanapelekwa kwa wahusika. Nimwombe tu Mheshimiwa Mbunge kama tatizo lile la vitanda kama halijapatiwa ufumbuzi tukitoka hapa ahakikishe tumefuatana kuangalia kwamba ni tatizo gani ambalo limekwamisha hivyo vitanda ambavyo havijapelekwa katika Kituo cha Afya ambacho mimi mwenyewe nilikitembelea.

Na. 101

**Utekelezaji wa Mradi wa *TASAF II***

**MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali inatekeleza mradi wa *TASAF II* katika Wilaya zote nchini; na kwa kuwa, mradi huo una fedha kwa ajili ya makundi maalum kama vile walemavu; yatima na wajane:-

(a) Je, ni wanawake wajane wangapi katika Mkoa wa Ruvuma wamenufaika na fedha hizo?

(b) Je, ni kitu gani kinasababisha watu wa makundi maalum kutonufaika na fedha au fursa zilizopo kwa ajili yao. Je, ni kwa sababu watu hao hawazifanyii kazi taarifa wanazopata juu ya fursa zao au hawapati kabisa taarifa za fursa hizo kutokana na Halmashauri kutokuwa na orodha ya watu hao na mahitaji yao?

(c) Je, Serikali inafanya nini ili kurekebisha hali hiyo ili watu hao wapate na kuzitumia fursa zao?

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kwa niaba ya wananchi wa Mbinga, nami nijumuike na wenzangu katika kuwatakia pole familia ya Marehemu Dr. Aaron Chiduo, huko Kilosa.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Devota Likokola, Mbunge wa Viti Maalum, naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Ni kweli kwamba Mradi wa *TASAF II* umetenga fedha, kiasi cha dola za Kimarekani milioni 21, kwa ajili ya watu wa makundi maalumu wanaoishi katika mazingira magumu ikiwa ni pamoja na watu wenye ulemavu, watoto, yatima, wajane, wazee, walioambukizwa virusi na waathirika wa UKIMWI na kadhalika ili kuanzisha miradi ya uzalishaji, ufundi stadi, huduma ya afya ya majumbani kwa waathirika wa UKIMWI na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Devota Likokola, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha kuanzia Julai, 2006 hadi Machi 2007 Mkoa wa Ruvuma ulikuwa wa miradi 13 iliyokwishapatiwa fedha na ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Katika miradi hiyo walengwa wa makundi maalum waliofaidika ni 375, kati ya hao, wanawake wajane ni 145.

(b) Mheshimiwa Spika, kama tulivyoeleza hapo juu, watu wa makundi maalum wamenuifaka na fursa ambayo *TASAF II* imetoa. Hata hivyo, kwa kiasi gani makundi hayo yananufaika inatokana na jinsi jamii yenyewe inavyojitokeza na kubainisha mahitaji yao. Makundi haya yanazo taarifa kuhusu fursa zilizopo kupitia *TASAF II* ambazo zinaendelea kutolewa kupitia Mikutano ya uamsho katika ngazi mbalimbali yaani Taifa hadi vijijini kwenye jamii na vilevile katika semina, makala mbalimbali kwenye magazeti ya kila siku, magazeti ya *TASAF,* mabango ambayo yamesambazwa sehemu zote ambako semina zilifanyika na kupitia watumishi wa ugani katika kila Kata, hasa kwa mawasiliano ya ana kwa ana na makundi maalum yenye watu wasioweza kuhudhuria mikutano/semina ya uamsho; pia kwa wasiojua kusoma na kuandika.

(c) Mheshimiwa Spika, kama ilivyoelezwa hapo juu awali watu wa makundi maalumu wanazitumia fursa zilizo mbele yao. Ili kuhakikisha ufanisi wa kuwafikia walengwa hao, Halmashauri za Wilaya zimeunda timu zinazoshughulikia na uhamasishaji.

Jukumu kubwa la timu hizo ni kuhakikisha zinatoa habari na kuelimisha wananchi juu ya kuwepo kwa fursa hizo. Pamoja na hilo Halmashauri za Wilaya zinazo pia timu za uwezeshaji ambazo kazi yao kubwa ni kuwasaidia walengwa kuandaa miradi inayoweza kufadhiliwa kupitia *TASAF II.*

**MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Nashukuru kwa majibu mazuri ambayo Mheshimiwa Naibu ameyatoa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na takwimu ambazo Mheshimiwa Naibu Waziri amezitoa ionekana kwamba walionufaika na mradi huu wa *TASAF* ni wachache sana, na sasa hivi tunalo tatizo kubwa sana la yatima na wanawake wajane. Je, Serikali inafanya nini ili kuhakikisha kwamba wanawake wengi wajane wananufaika na mradi huo wa *TASAF* ukitoa *figure* ambapo wanawake wa Ruvuma ni 145 tu ambao wamenufaika na mradi huo na *figure* hii ni ndogo sana?

Mheshimiwa Spika, la pili ni kama ifuatavyo:- Kutokana na taarifa nilizozipata kutoka kwa wanawake wa Songea Vijijini na Wilaya ya Namtumbo mpaka sasa hivi wanawake wajane wa Wilaya hizo mbili hawajanufaika na Miradi hiyo ya *TASAF.* Je, Serikali inasema nini ili kuwafanya wanawake wa Namtumbo na Songea Vijijini wanufaike kama wanawake wenzao wajane katika maeneo mengine? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Devota Likokola, kwa kufuatilia kwa karibu sana masuala ya yatima, wajane na wanawake katika Mkoa wa Ruvuma ambako pia mimi ni mdau.

Mheshimiwa Spika, kuhusu idadi ndogo ya watu waliofaidika katika makundi haya ya yatima na wajane. Kama ambavyo nilijibu katika jibu langu la msingi *TASAF* imeweka utaratibu kutoka katika ngazi za Wilaya na kuna watu maalum na Kamati maalum inayoshughulika katika uhamasishaji na uelimishaji katika jamii katika Halmashauri zinazohusika.

Sasa ni jukumu la jamii kuchukua hizo fursa sasa baada ya kupata hiyo elimu na kuweza kujua ni miradi gani inayotakiwa na kujaza fomu zinazotakiwa ili waweze kufaidika na fursa hizo ambazo Serikali imezitoa.

Mheshimiwa Spika, sasa pengine ningependa kuchukua nafasi hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge watusaidie katika hili, kwa sababu Waheshimiwa Wabunge pia ni wadau wazuri sana katika hizo Halmashauri.

Lakini kwa sababu Taifa nzima sasa linatusikia ningependa kuchukua pia fursa hii kuwahamasisha Halmashauri hususan Wenyeviti wa *Council* pamoja na Madiwani kuhakikisha kwamba fursa hizo ambazo Serikali imezitoa sasa zinachukuliwa na zinafanyiwa kazi na hayo makundi maalum yanayoweza kufaidika. Kwa sababu ni makundi ya Watanzania wenzetu yanahitaji msaada maalum.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo na Songea Vijijini ni kweli kwamba hao wanawake hawajaanza kufaidika na fedha hizo ambazo *TASAF II* imetoa.

Lakini miradi yao imeshapokelewa na iko katika mchakato ili baadaye waweze kupata. Ni suala kwamba wao walichelewa kuchangamkia mambo hayo, na kwa hiyo baada ya muda si mrefu mimi nina hakika watakuwa wamepatiwa. Ahsante.

Na. 102

**Mikataba mbalimbali ya Serikali**

**MHE. MASOLWA C. MASOLWA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali iliingia mikataba mingi na wawekezaji mbalimbali hapa nchini ambayo imekuwa na matatizo na kuwafanya Watanzania wasinufaike na mikataba hiyo kutokana na kasoro nyingi zilizojitokeza baada ya utekelezaji wa mikataba hiyo kuanza; na kwa kuwa, pamoja na kwamba, inasemekana mikataba hiyo itaangaliwa upya katika awamu hii:-

Je, Serikali haioni kwamba, sasa ni wakati muafaka wa mikataba itakayotayarishwa katika awamu hii ipitie katika Kamati husika za Bunge ili ziweze kutoa maoni yake kwa maslahi ya Taifa kabla haijasainiwa na pande zote husika?

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, kabla ya kujibu swai la Mheshimiwa Cosmas Masolwa, Mbunge wa Bububu, naomba kutoa maelezo yafuatayo:- Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 4, utekelezaji wa shughuli za mamlaka ya nchi umegawanyika katika mihimili mitatu yaani, (a) Serikali itasimamia Utendaji (b) Mahakama itasimamia utoaji wa haki na (c) Bunge litashughulikia utungaji wa sheria na kusimamia shughuli za umma.

Masuala ya kuingia mikataba ya aina yoyote ni masuala ya kiutendaji na kwa hiyo yanaangukia kwenye mhimili wa Serikali. Kulingana na wajibu wao wa kusimamia shughuli za umma, Wabunge wanayo haki na wajibu wa kuhoji jambo lolote linalohusu utekelezaji wa kazi za Serikali, ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa mikataba. Wabunge wanapohoji mikataba wanachopaswa kupata kutoka kwa Serikali ni maelezo ya kuridhisha kuhusu utekelzaji wa mikataba hiyo. Wao hawapaswi kuchukua wenyewe jukumu la kuipitia mikataba hiyo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wanaweza kuishauri Serikali mambo ya kimsingi ya kuzingatiwa ili kuboresha mikataba ya Serikali, na siyo kufanya uchambuzi wa mikataba yenyewe.

Aidha, pale inapodhihirika kwamba kumekuwepo na vitendo vya rushwa, wizi na au uhalifu mwingine wowote, Bunge linaweza kutumia Sheria Na. 3 ya 1988 ya Kinga ,

Madaraka na Haki za Bunge, pamoja na Kanuni za Bunge, kuelekeza kwamba hatua za kisheria zichukuliwe.

Utaratibu huo kwa mujibu wa Fungu la 12 la Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge ni wa kumtaka Mwanasheria Mkuu achukue hatua hizo, na yeye Mwanasheria Mkuu ndiye kiungo kati ya Bunge na Serikali katika utekelezaji wa maelekezo ya namna hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Cosmas Masolwa, Mbunge wa Bububu, kama ifuatavyo:-

Serikali haiko tayari kuzipa Kamati za Bunge Mikataba ya aina hii maana ni ya utendaji na kibiashara kati ya Mwekezaji na Serikali. "*Best Practice*" kote duniani ni kutoitangaza aina hii ya mikataba.

Hata hivyo, jukumu la Wabunge ni kuhoji utendaji wa Serikali na vyombo/Taasisi zake ambapo wahusika wanawajibika kutoa maelezo. Hili ni suala la mipaka na mgawanyo wa kazi kati ya Utawala *(Executive),* Mahakama *(Judicial)* na Bunge *(Legislature). (Makofi)*

**MHE. MASOLWA C. MASOLWA:** Mheshimwia Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja ndogo la nyongeza. Namshukuru Naibu Waziri kwa kunielimisha japo naona mihimili hii ingefaa pia ikasaidiana. Katika maelezo yangu kwenye swali la msingi nilisema kwamba mikataba hiyo ingefaa ikaangaliwa upya?

Je, nataka kufahamu ni mikataba mingapi mpaka sasa imeishaangaliwa upya na inahusu maeneo gani? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, Serikali iliahidi kupitia mikataba hasa ile ya madini ili kuweza kuona kama nchi itafaidika zaidi ya pale ambapo imekuwa ikipata. Kwa sasa ni mapema mno kutoa jibu ni mikataba mingapi imeshafanyiwa marekebisho kwa sababu mchakato huo bado unaendelea.

**SPIKA:** Nitoe nafasi kwa upande wa Upinzani, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Peter Slaa.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona. Kwa kuwa kazi ya kusimamia inifanywa vizuri kama una taarifa na kwa kuwa usiri ulioko katika suala la mikataba haliwezeshi Bunge kusimamia kikamilifu masuala yanayohusika; na kwa kuwa kuna mfano halisi wa *William Diamond mines* kuna taarifa na juzi Waziri alijibu kwamba kwa miaka 27 haikulipa kodi na kwa kuwa Bunge halipati nafasi ya kuona mikataba ya namna hiyo. Je, Waziri haoni kwamba kuendeleza mtindo huu kama alivyoueleza kwanza si kweli kwamba dhana ya kusimamia haina maana kwamba usione mkataba na wala dhana ya kusimamia haina maana kwamba ni kuingilia utendaji kazi wa Serikali? (*Makofi*)

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI**: Mheshimiwa Spika, sikubaliani naye kwamba dhana ya mipaka ya majukumu kati ya Serikali na Bunge haitoe mwanya kwa Serikali na Bunge kuwa na mgawanyo wa namna hii. Kwamba mambo ya utendaji yanafanywa na Serikali na mambo ya kushughulikia usimamizi wa Serikali

inafanywa na Bunge. Mimi naamini kabisa kwamba pamoja na kwamba kuna siri katika baadhi ya mikataba lakini maelezo yanaweza yakatolewa kwa Kamati ya Bunge na Bunge zima ili Wabunge wakapata fursa ya kuihoji Serikali si lazima wasome mikataba yenyewe.

Kwa sababu mikataba hii ni siri; na *best practise* duniani kote ni kwamba mikataba hii inashughulikiwa na Serikali na Wafanyabiashara. Bunge jukumu lake ni kuihoji Serikali; na mimi nafikiri kuhojiwa tunahojiwa sana na moja ya kazi ya kuhoji ni hii tunayotoa maelezo hapa. Kwa hiyo, mimi nafikiri suala la mipaka lazima tulizingatie na *best practise* tuizingatie.

**SPIKA**: Ila Serikali ihakikishe hatuliwi tu. *(Kicheko/Makofi)*

Na. 103

**Uhusiano wa Tanzania na China**

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH – (K.n.y. MHE. LAZARO S. NYALANDU)** aliuliza:-

Kwa kuwa China na Tanzania zina uhusiano mkubwa sana kihistoria; na kwa kuwa, Taifa hilo kubwa Duniani sasa linawekeza katika sekta ya Nishati, Madini, Miundombinu na Mafuta katika nchi nyingi za Afrika:-

(a) Je, Serikali ya China imewekeza miradi gani Tanzania katika miaka mitano iliyopita?

(b) Kwa kuwa, China imeamua kuwekeza katika Bandari ya Mombasa. Je, juhudi gani za kidiplomasia zimefanyika kushawishi China kuwekeza Bandari ya Tanga?

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Nyalandu, Mbunge wa Singida Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b), napenda kutoa maelezo mafupi ya awali kama ifuatavyo:-

Ni kweli kuwa Tanzania imekuwa na uhusiano mkubwa na nchi ya China kwa muda mrefu. Uhusiano huu ulianza kabla ya uhuru na kuimarika zaidi mara tu baada ya kupata uhuru hasa chini ya ushirikiano baina ya nchi zinazoendelea *(South-South Cooperation).* Ushirikiano huu umekuwa katika sekta mbalimbali ikiwa ni pamoja na fedha, viwanda, ujenzi, kilimo, usafirishaji, madini, mawasiliano, ulinzi, biashara, afya, elimu na utamaduni. Miradi mingi imekuwa ikiendeshwa kwa njia ya ruzuku (*grants*) pamoja na mikopo nafuu isiyokuwa na riba na mikopo yenye masharti nafuu *(soft loans)* kwenye sekta hizo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya awali sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nyalandu, Mbunge wa Singida Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka mitano China imewekeza katika miradi mikubwa ifuatavyo:-

- Ukarabati wa miundombinu ya maji mjini Dodoma ambao kwa ujumla umegharimu dola za kimarekani milioni 4. Mradi huu umeongeza uzalishaji wa maji kutoka mita za ujazo *cubic metres* 24,000 kwa siku hadi mita za ujazo *(cubic metres)* 40,000.

- Mradi wa Maji wa Chalinze ambao umejengwa ili kusaidia wananchi 62,961. Mradi huu ni mmoja kati ya miradi mikubwa ya maji ambayo imetekelezwa kwa msaada wa China.

Pamoja na kuweka mabomba kwa umbali wa kilomita 160, mradi huu ulihusisha ujengaji wa sehemu ya kuhifadhia pampu na sehemu ya kuweka dawa maji. Awamu ya kwanza ya mradi huu iligharimu shilingi 23.54 bilioni na ulikamilika Desemba, 2003.

- Mradi wa ujenzi wa uwanja wa michezo wa kisasa wa Dar es Salaam ambao unatazamiwa kuwa uwezo wa kuingia watu elfu sitini (60,000) uwanja huu unahusisha pia ujenzi wa kijiji cha michezo, viwanja vya mazoezi, mabwawa ya kuongelea, uwanja wa ndani wa michezo, pamoja na ukarabati wa uwanja wa Taifa wa zamani.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Ushirikiano wa kiufundi (*TCDC*) kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita wataalam wa Tanzania wamekuwa wakihudhuria mafunzo mbalimbali ya vitendo na nadharia nchini China ikiwa ni pamoja na Tahadhari na Kinga dhidi ya Matetemeko ya Ardhi, Nishati ya Maji, ukulima wa uyoga kwa ajili ya chakula, teknolojia ya nishati mbadala, teknolojia ya mianzi uzalishaji na usambazaji wa mboga, teknolojia ya tarakishi, uchimbaji wa maji, uzalishaji wa maua, uzuiaji wa jangwa, utabiri wa hali ya hewa, matibabu ya magonjwa ya kisukari kwa kutumia dawa za kiasili za kichina, utunzaji salama wa mabwawa, utafiti wa madini, utumiaji na utengenezaji wa vyombo vya hali ya hewa, utunzaji wa mazingira, utunzaji wa nafaka, ukulima wa mboga, usindikaji wa vyakula na bidhaa na teknolojia ya ukadiriaji wa viwango. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa juhudi tayari zinaendelea ili kuvuta wawekezaji kutoka nchi mbalimbali kuja kuwekeza nchini chini ya dhana ya soko huria; na kwa kuwa bandari ya Tanga ni moja ya maeneo yaliyoainishwa kama *Export Processing Zones* na *Special Economic Zones* ikiwa ni pamoja na bandari nyingine za Mbegani (Bagamoyo) Mtwara, Kigoma, Bukoba ni wazi kuwa China ni moja ya nchi ambazo zimepewa nafasi kubwa ya kuwekeza nchini. Hii inatokana na kuwa na ushirikiano wa muda mrefu kati ya nchi hizi mbili pamoja na mipango maalum ya maendeleo kama vile *Forum For China Africa Cooperation* 2007 -2009 *(FOCAC)*.

Mheshimiwa Spika, lakini wakati namalizia kujibu swali hili naomba pia nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Nyalandu kwa juhudi anazozifanya katika kuleta wawekezaji hapa nchini. Ni juzi tu alikuja na mwekezaji kutoka Korea na nimshukuru sana na ningeomba pia Wabunge wenzangu kama mna nafasi hizo tunawakaribisha Ofisini kwetu na muwalete Ofisini kwetu tunawahitaji sana. (*Makofi*)

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Spika nashukuru sana, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri nina swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa miradi au sekta alizozitaja Mheshimiwa Naibu Waziri nyingi sana ambazo kwa kweli ni muhimu sana katika nchi yetu lakini moja kati ya sekta muhimu ni sekta ya kilimo na kilimo ni uti wa mgongo. Sisi kilimo tunahitaji kwa ajili ya chakula na kwa ajili ya biashara, Sasa naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri.

Je, Wizara ipo tayari sasa kuishawishi Serikali ya China ikaja na kuwekeza katika sekta ya kilimo husasani katika mikoa ya Dodoma na Singida ambayo mara zote ni kame na inahitaji kupata utaalam ili kuweza kuwa na chakula cha kutosha?

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, Wizara si tu kwamba iko tayari lakini kazi hiyo inafanyika kwa sasa na itaendelea kufanyika.

Na. 104

**Uhaba wa Vitendea Kazi kwa Jeshi la Polisi Mkoa wa Kaskazini Unguja.**

**MHE. RAJAB HAMAD JUMA** alijibu:-

Kwa kuwa ukuaji wa Sekta ya utalii ni wa kazi katika Mkoa wa Kaskazini Unguja hususani maeneo ya Nungwi, Mitembwe, Pwani Mchangani na Kiwengwa na kwa kuwa ukuaji huo unachangia ongezeko la uhalifu na ajali za barabara jambo linalochochea haja ya Jeshi la Polisi kuwa imara kukabiliana na hali hiyo kwa ulinzi na doria za uhakika:-

(a) Je, Serikali inafahamu kuwa Polisi Mkoa humo wana upungufu mkubwa wa vitendea kazi hasa vya usafiri?

(b) Je, Serikali inaahidi nini katika kupunguza tatizo hilo Mkoani humo?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali kwa ruksa yako naomba kutoa mkono wa pole kwa Mheshimiwa Bakari Mwapachu, familia yake, Ndugu na jamaa kwa kifo cha mama yao mpendwa kilichotokea jana usiku. Mungu ailaze mahala pema roho ya marehemu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia napenda kumjibu Mheshimiwa Rajab Hamad Juma, Mbunge wa Tumbatu, swali lake lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wakati nikijibu swali namba 44 la Mheshimiwa Ligallama, Mbunge wa Kilombero, nililitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba Serikali inatambua upungufu mkubwa wa vitendea kazi unaolikabili Jeshi letu la Polisi, hasa vyombo vya usafiri. Tatizo hili ni la nchi nzima ukiwemo Mkoa wa kaskazini Unguja. Serikali inaendelea

kuyashughulikia kwa awamu matatizo yanayokwamisha ufanisi na utendaji kazi za kila siku za Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba Jeshi la Polisi limepanga vizuri kupambana na uhalifu wa aina zote hapa nchini ili wananchi na wageni wetu waweze kuishi katika hali ya usalama.

Aidha Wizara yaUsalama wa Raia ina mpango wa kuanzisha kitengo cha maalum cha Polisi kitakachoshughulikia masuala ya usalama wa watalii kwenye maeneo ya utalii. Hata hivyo, ombi la Mheshimiwa Mbunge limezingatiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako napenda kutoa shukrani maalum kwa Kamisheni ya Utalii Zanzibar, kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi katika kupambana na uhalifu katika ukanda wa utalii hususan kwa kutoa usafiri wa kuimarisha doria katika ukanda huo.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa suala hili la Tumbatu, Matembwe Nungwi, sambamba nilinaoana na tatizo la Jimbo la Chwaka. Jimbo la Chwaka lina mahoteli mengi sana na mara nyingi kunatokea ubadhilifu wa aina mbalimbali na kufikia hadi vituo vya petrol kuingia majambazi; na kwa kuwa huu ni mwaka wa 12 niko katika Bunge hili Tukufu nadai vitendea kazi hususan gari.

Je, katika gari zilizokuja unalihakikishia Bunge hili Tukufu kwamba Chwaka nayo itapata gari ili kuondoa matatizo haya?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika suala langu la msingi kwamba Serikali ingependa sana kuhakikisha kwamba inaondoa tatizo la vitendea kazi hasa suala la usafiri wa askari wetu ili waweze kupambana na uhalifu nchini. Kuhusiana na magari mapya ningependa ufafanuzi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, magari yale tayari yameshagawiwa kwa Mikoa mbalimbali ikiwemo Makao Mkuu ya Polisi huko Zanzibar, kwa hiyo itategemea Makao Makuu ya Polisi huko Zanzibar kufikiria wapi patapewa kipaumbele kwenye suala hilo. Hata hivyo tutaendelea kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge tuangalie siku za usoni kuhakikisha kwamba tunaondoa tatizo la Chwaka.

Na. 105

**Bunduki za Magobore kwa Ajili ya Uwindaji Wanyama Waharibifu**

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA** aliuliza:-

Kwa kuwa kuna wananchi waliowahi kupewa bunduki aina ya magobore vijijini kwa ajili ya kuwindia wanyama waharibifu wa mazao na kwa kuwa wananchi hao waliambiwa warudishe bunduki hizo sehemu husika kwa ahadi kuwa watarudishiwa tena, kitendo ambacho hakijafanyika mpaka sasa hivyo wananchi kuathirika na uharibifu wa mazao yao kwa wanyama kama nguruwe, kima na wengine:-

(a) Je, Serikali ina mpango wowote wa kuwarejeshea wananchi hao bunduki hizo ili waondokane na uharibifu wa mazao yao mashambani?

(b) Je, ni sababu zipi za msingi zilizosababisha bunduki hizo kukusanywa toka kwa wananchi licha ya kuwa walipewa kisheria kwa ajili ya uwindaji wa wanyama waharibifu?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika. Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia napenda kumjibu Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mbunge wa Chwaka, swali lake lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Bunduki zilizoko Zanzibar zinazotumika kuwindia wanyama ni aina ya *shortgun*, bunduki hizo zinamilikiwa na Serikali chini ya uangalizi wa Jeshi la Polisi kwa kuwa Sheria ya Zanziba hairuhusu mtu binafsi kumiliki silaha.

Hivyo wananchi huwa wanaazimwa silaha hizo kwa muda maalum ili wazitumie kwa shughuli za uwindaji wa wanyama waharibifu. Endapo wakati wowote Serikali ikiona pana haja ya kuzikusanya hufanya hivyo bila kujali wakati kwa watumiaji.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi linaandaa utaratibu maalum wa kuwarudishia wananchi bunduki hizo ili waweze kupambana na wanyama waharibifu. Aidha silaha hizo zitarejeshwa kwa wananchi wale tu wenye udhibiti mzuri wa silaha ili kuepuka silaha hizo kuangukia mikononi mwa wahalifu.

Mheshimiwa Spika, sababu ya msingi kukusanya bunduki hizo toka kwa wananchi ni kudhibiti matumizi yake na pia kuimarisha usalama na amani ya visiwa hivyo.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kilimo ni uti wa mgongo na toka kukusanywa kwa bunduki hizi na wao walichukuwa kwa kupewa kwa njia maalum. Je, hadi muda huu kwamba wananchi hawana kilindo katika mashamba yao huoni kwamba tuna wadhoofisha kiuchumi?

Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba wanaweza kurejeshewa licha ya kwamba muda utakuwa mkubwa lakini anaweza kuwakikishia wananchi walioko huko na sasa hivi wananisikia; kwa muda gani unaweza kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba wananchi hao wanaweza kurejeshewa bunduki hizi ili wajikimu kimaisha yaliyowakabili?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba wananchi wamepata kero hasa wakulima wakati ambapo ilibidi kuzirudisha zile silaha mikoni mwa Jeshi la Polisi na hili hatukufanya hivi hivi tu.

Hili lilitokana na Mheshimiwa Mbunge na nishahidi kwamba hizi siku za karibuni kulitokea vurugu kubwa ya wizi kule visiwani Zanzibar na baadhi ya silaha hizi zilitumika na ndiyo maana ikatubidi tufanye uhakika wa kina ili kuhakikisha usalama wa raia na mali zao.

Baada ya kumaliza huu mchakato ninamhakikishia Mheshimiwa Yahya, kwamba yale ambayo anayatarajia yafanyike yatafanyika muda si mrefu. Kwa hiyo, swali la (b) nimhakikishie kwamba kuanzia sasa wakati wowote wale waaminifu watakaoonekana wanafaa kurudishiwa salaha hizo ndiyo wale tu watakaorudishiwa silaha hizo.

**MHE ALI SAID SALUM:** Mheshimiwa Spika, kwanza na mimi niungane na Mheshimiwa Naibu Waziri kutoa pole kwa Mheshimiwa Waziri kwa kufiwa na mama yake mzazi mungu ailaze mahala pema peponi roho yake. Lakini pia nitoe pole kwa wafiwa wote waliohusika na ajali ya basi Mwanga.

Baada ya salaam hizo za utangulizi naomba niulize swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa hivi karibuni kumejitokeza suala la ujambazi ambao unatumia silaha katika visiwa vya Unguja na Pemba; na kwa kuwa Sheria hairuhusu kwa upande wa Zanzibar kumiliki silaha. Je, Serikali itakubaliana na mimi kwamba sasa imefika muda mwafaka wa Sheria hii kufanyiwa marekebisho ili wananchi hawa nao waweze kupewa silaha na kujilinda kwa ajili usalama wao na mali zao?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali siku zote itachukua kila hatua kuhakikisha kila usalama wa raia na mali zao kwa wananchi wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla. Kwa wakati huu Serikali kwa upande wa Zanzibar inawawia vigumu sana kufikiria kuibadili Sheria ile kuwakabidhi silaha raia wa kawaida kwa sababu mbalimbali. Lakini sababu kubwa ni kwamba hata hizo ambazo tumewapa tu wakulima kwa ajili ya kujikinga na wanyama waharibifu basi baadhi yake zimetumika kufanyiwa uhalifu sembuse kuwapa silaha kali na hasa tunavyoijua Zanzibar wanayo pia matatizo ya kutokuelewana kisiasa. Inawezekana wakati mwingine ikawa ni tatizo kubwa zaidi. (*Makofi*)

Na. 106

**Tatizo la Maji Safi na Salama Mji wa Wilaya Kasulu**

**MHE, JOSEPHINE J. NGENZABUKE (K.n.y. MHE. KILONSI M. M. MPOROGOMYI)** aliuliza:-

Kwa kuwa maji katika Wilaya ya Kasulu ni suala nyeti sana; na kwa kuwa hata wakati wa uchaguzi mkuu wapinzani walitumia suala la maji wakisema kwamba Serikali ya CCM imeshindwa kuwapatia maji safi na sala wakazi wa Mji wa Kasulu, na kwamba Mtanzania aliye huru kwa zaidi ya miaka 40 hastahili kunywa maji ya matope kama yale ya Kasulu na kwa kuwa, vijiji vingi katika tarafa za Manyovu na Heru Juu havina maji hivyo wanawake hutembea mwendo mrefu kutafuta maji:-

(a) Je, ni lini Mji wa Kasulu utapatiwa maji safi na salama?

(b) Je, ni lini Tarafa nilizozitaja kwenye swali hili zitapatiwa visima virefu husasan katika vijiji vya Heru Juu, Muhunga, Kahunga, Mganza, Mwanga

(Tarafa ya Heru Juu) na Munanile, Kibwigwa, Mkasanga, Mwayaya, Nyambona, Mbanga, Rusaba na Kirungu. (Tarafa ya Manyovu)

(c) Je, Serikali inayo taarifa kwamba ipo milipuko ya magonjwa mbalimbali yatokanayo na matumizi ya maji yasiyo safi na salama na kwamba maradhi hayo yamedhoofisha nguvu kazi ya wananchi wa Wilaya ya Kasulu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mporogomyi, Mbunge wa Kasulu Magharibi, naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mji wa Kasulu unapata huduma ya maji ya mtiririko kutoka kwenye vyanzo vitatu vya maji vya Nyanka, Nyakatoke na Miseno. Vyanzo hivyo vina uwezo wa kuzalisha jumla ya meta za ujazo 2,800 kwa siku sawa na asilimia 80 ya mahitaji ambayo ni meta za ujazo 3,500 kwa siku. Vyanzo hivi hususan chanzo cha Miseno vinaathiriwa na shughuli za kilimo katika vijiji vya Heru Juu na Kirunga ambako wakazi wake hulima juu ya vyanzo na kuhamisha mkondo wa asili wa maji kwa kupeleka maji kwenye mashamba yao, hivyo kusababisha upungufu mkubwa wa maji.

Mheshimiwa Spika, baada maelezo hayo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Kasulu Magharibi, lenye vipengele (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Serikali kwa kushirikiana na wafadhili ikiwa ni pamoja na wa *KaDP* na *UNHCR* imechukua hatua mbalimbai kuboresha huduma ya maji katika Mji wa Kasulu. Vyanzo vya Nyakatoke na Nyanka vilifanyiwa ukarabati na hivyo kupunguza uwezekano wa kuwepo kwa tope kwenye maji hususan wakati wa masika.

Aidha, chanzo kipya cha Miseno kimejengwa pamoja na tanki la kuhifadhia maji lenye mita za ujazo 227. Ili kuimarisha huduma ya maji, Serikali pia imepima chanzo kipya cha maji cha mto chai ambapo ujenzi wa mradi utafanyika kulingana na upatinaji wa fedha.

(b) Vijiji vilivyotajwa na Mheshimiwa Mbunge vina huduma ya maji kama ifuatavyo:-

Katika Tarafa ya Heri Juu Vijiji vyote vinahuduma ya maji ambapo wana maji ya chemchem ina chemchem tano, Muhunga kumi, Kahunga ina saba, Mganza saba na Mwanga chemchem moja. Katika Tarafa ya Manyovu Munanile kina chemchem 11, Kibigwa 12, Mkasanga 11 na Mwayaya 20. Vijiji vya Nyambona, Mbanga, Rusaba na Kirunga havina huduma ya maji kwa sasa. Lakini hata hivyo vijiji vya Mbanga na Kirungu vimeingizwa kwenye Programu ya maji na usafi wa mazingira vijiji mwaka huu wa fedha 2006/2007. Naomba kumshauri Mheshimiwa Mbunge kwa kushirikiana na Halmashauri yake vijiji vilivyobaki vipewe kipaumbele katika awamu zitakazofuata.

(c) Wizara haijapata taarifa ya kuwepo milipuko ya magonjwa mbalimbali yatokanayo na matumizi ya maji yasiyo safi na salama kama mji wa Kasulu. Serikali itandelea kushirikiana na wananchi ili kukabiliana na hali hiyo mara itakapojitokeza.

**MHE. JOSEPHINE J. NGENZABUKE:** Mhesimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa tatizo la maji Wilayani

Kasulu limekuwa ni tatizo sugu hususani katika Tarafa zile ambazo ziko Milimani kama vile Buhoro, Heru Juu na Manyovu; na mimi mwenyewe kwa sababu ni mwenyeji wa Wilaya ya Kasulu na ni mzaliwa wa Tarafa ya Heru Juu. Vijiji hivyo mara nyingi wataalam huwa wanatoa maelezo kwamba maji kuyapeleka kule kwa kutumia mabomba ni tatizo kwa sababu viko milimani. Je, kwa kutumia mradi wa maji wa Benki la Dunia, tatizo hili haliwezi likatatuliwa?

Pili, je ni mahali gani ambapo mpango huu wa Benki ya Dunia umeshaanzishwa na umeshaanza kutekelezwa? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha mwaka huu 2006/2007 katika Wilaya ya Kasulu vijiji vifuatavyo vimeingizwa katika programu ya maji safi na usafi wa mazingira vijijini. Kwa upande wa Kasulu Magharibi kuna vijiji vya Mbanga, Nyamkorongo na Kirungu na kwa upande wa Mashariki kuna Vijiji vya Munzege, Kigungwe, Nyumbwiga, Kitagata, Nyachenda, Kasangezi na Nyarugusu. Kwa upande wa miradi midogo midogo ya haraka napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa Wilaya ya Kasulu jumla ya shilingi milioni 249,825,400 zitatumika kuhudumia miradi kumi midogo midogo kwa sababu ya muda naomba nimwombe Mheshimiwa Mbunge orodha hiyo nitampatia baadaye kidogo ahsante. *(Makofi)*

Na. 107

**Utekelezaji wa Miradi ya Maji Vijijini**

**MHE. DR. ABDALLAH O. KIGODA** aliuliza:-

Kwa kuwa fedha za utekelezaji wa miradi ya maji vijijini inayofadhiliwa na Benki ya Dunia kupitia utaratibu wa *IDA Credit No*. 3623 Wilayani Handeni kupitia Serikali haitumiki vizuri kutokana na ushauri hafifu wa washauri stadi (*Consultant*) na Makandarasi wasio na uwezo kuwapatia wakandarasi waliochaguliwa:-

(a) Je, Serikali inasema nini kuhusu kukamilika kwa mradi wa visima wa Kijiji cha Mkata, mradi wa maji wa wa bwawa la Komnala Wilayani Handeni?

(b) Kwa kuwa shida kubwa ya maeneo hayo kwa ujumla ni maji; na kwa kuwa Benki ya Dunia imetoa fedha hizo ili kukabili tatizo la maji maeneo hayo; na kwa kuwa fedha hizo zinatolewa lakini inaonyesha hazina ufuatiliaji wowote juu ya matumizi yake wala ufuatiliaji wa waliopewa kandarasi hizo. Je, fedha za mirad hii zilitotumika bila mafanikio zitafidiwa ili utekelezaji wa miradi uendelee?

(c) Kwa kuwa fursa ya kumaliza kero hiyo hadi sasa inaonekana kufifia au kufutika. Je, Serikali inaahidi ni lini miradi hiyo itakamilika au wananchi waone ni fursa iliyopotea?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda, Mbunge wa Handeni, lenye sehemu (a), (b) na (c), naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, baada ya kufanya ziara za Wilaya ya Handeni na Kilindi kwa mwaliko wa Waheshimiwa Wabunge hao wawili mawili Serikali ilibaini yafuatayo:- Ni kweli kuwa wakandarasi katika Wilaya ya Handeni wameonyesha utendaji hafifu kutokana na

uwezo mdogo. Hii inachangiwa na uchanga wa sekta binafsi kwani sekta hiyo imeonyesha kukosa uwezo wa kifedha na kitaaluma.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba nijibu swali la Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda, Mbunge wa Handeni, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Mkandarasi *MS-Mega Builders* anayejenga mradi wa maji uliopo kijiji cha Mkata alichimba kisima lakini hicho hakikuwa na maji ya kutosha, hivyo Mhandisi Mshauri anaendelea na utafiti kwa lengo la kupata chanzo kingine.

Mkandarasi *Tan Afric Ltd* anayejenga Bwawa la Kwanyange ametelekeza mitambo yake naye kutoweka bila taarifa. Ujenzi wa bwana la Komnala bado hii inatokana na udhaifu wa utendaji kazi wa Mkandarasi *Richer Investment Co.* Alichofanya ni kujenga tanki la maji na kuanza kutandaza nusu ya mabomba na mpaka sasa mambo mengine hayajaendelea.

(b) Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Handeni tayari imekwishasitisha mikataba ya Wakandarasi watatu ambao utendaji wao hauridhishi. Wakandarasi hao ni *M/S Richer Investiment Company, M/S Mega Company Ltd* na *M/S Tan Afric Ltd.*. Wizara yangu itaendelea kuzishauri Halmashauri kufuta mikataba ya wakandarasi pale ambapo inaona kuwa kuna haja ya kufanya hivyo. Kabla ya kuanza kazi mkandarasi huwekeana mkataba na Halmashauri. Katika mikataba mkandarasi huwasilisha dhamana ya kufanya kazi ambayo ni *perfomance security* ya asilimia tano ya gharama yote ya kazi ambazo hufanyika. Kwa hali hiyo gharama hii ya asilimia tano ikiwa kutatokea tatizo lolote na mkandarasi basi hutumika kama fidia kugharamia kumtafuta mkandarasi mwingine ambaye atafanya kazi alizobakiza huyu aliyeshindwa.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia hatua zilizochukuliwa kama nilivyoeleza katika majibu yangu ya (a) Serikali inaahidi kukamilisha mradi wa maji kwa ajili ya vijiji vya Mkata, Kwanyange na Komnala ifikapo mwezi Desemba 2007. *(Makofi)*

**MHE RAMADHAN A. MANENO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, amekiri kwamba baadhi ya Wahandisi, ufanisi wao katika utendaji wa kazi si mzuri.

Je, Serikali sasa ina tamko gani juu ya Wahandisi ambao kazi zao haziridhishi kwenye Halmashauri zetu ambapo baadhi ya Halmashauri nyingi nchini, wanapokwenda Wahandisi kasi zao zinakuwa siyo nzuri? Handeni pamoja na Jimbo la Chalinze, baadhi ya Wahandisi, kazi zao si nzuri kwenye ufanisi wa suala hili la maji!

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge kwamba wanaochagua Wakandarasi ni Halmashauri zenyewe kwa kupitia njia ya zabuni na katika zabuni hizo, ndizo zinazokidhi haja kwamba Mkandarasi gani achaguliwe.

Sasa, hapo napenda kuwaomba Halmashauri zetu tukiwemo na sisi wenyewe, Waheshimiwa Madiwani, tuhakikishe kwamba yale majina ya Wazabuni tuangalie sifa zao siyo zilizoletwa tu, bali na utendaji wao wa nyuma katika kampuni mbali mbali na kazi zilikuwaje ili tuweze kuhakikisha tunachagua Mkandarasi anayefaa.

Mheshimiwa Spika, lakini pia, kwa kufuatana na mikataba yetu na wafadhili ni kwamba tumekubaliana tuendeleze sekta zetu ndogo ndogo za hapa nchini. Sasa kwa hali hiyo basi, katika sekta hizi ndogo kama nilivyosema katika jibu la awali, wengi bado wachanga na baadhi yao fedha bado haijatosheleza na ni kweli kwamba lazima tuwasaidie kuwanyanyua hawa.

Mheshimiwa Spika, tusipowanyanyua, itafikia hatua kwamba tutakuwa tegemezi daima, tutachukua wakandarasi wakubwa wakubwa kutoka nchi za nje. Cha msingi ni sisi wenyewe tuhakikishe katika Halmashauri tunachagua wale kweli wenye uwezo wa kazi.

Na. 108

**Ubovu wa Barabara ya Ngare Nairobi – Londrosi *Gate***

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI** aliuliza :-

Kwa kuwa muda mrefu sasa, wananchi waishio Londrosi *West* Kilimanjaro katika Wilaya ya Siha, wamekuwa wakitaabika kutokana na ubovu wa barabara itokayo Ngare Nairobi Londrosi *Gate*; na kwa kuwa ubovu huo unakwamisha shughuli za kiuchumi hasa kwa upande wa watalii wanaotaka kupanda Mlima Kilimanjaro:-

(a) Je, ni Mamlaka gani inayotakiwa kushughulikia barabara hiyo?

(b) Je, ni hatua gani zinachukuliwa na Serikali kurekebisha hali hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu**:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aggrey D. J. Mwanri, Mbunge wa Siha, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Ngare Nairobi - Londrosi *Gate* inashughulikiwa na Mamlaka mbili tofauti; sehemu ya Ngare Nairobi hadi Simba *Farm* yenye urefu wa kilomita 1.5 kwa upande moja ambayo ni barabara ya Mkoa (Sanyajuu – Kimwanga) iko chini ya uangalizi wa Wakala wa Barabara Mkoa wa Kilimanjaro na kwa upande mwingine, barabara itokayo Simba *Farm* – Londrosi *Gate* yenye urefu wa kilomita 10, iko chini ya uangalizi wa *KINAPA* na kampuni ya *West* Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Ngare Nairobi - Simba *Farm* iliyoko chini ya uangalizi wa Wakala wa barabara, imekuwa ikipata matengenezo karibu kila mwaka. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2006/2007, sehemu husika imepata matengenezo ya kawaida kwa kuchonga barabara na kusafisha mifereji ya tupa maji kwa gharama ya shilingi milioni 31.18. Hali ya barabara hiyo ni nzuri hata baada ya kunyesha mvua kuba za vuli za mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Simba *Farm* – Londrosi *Gate* yenye urefu wa kilomita 10 ni *access road* inayotoka Simba *Farm Junction* na kuelekea Londrosi *Gate* kwa kupitia mashamba ya misitu ya *West* Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa barabara hii inafanyiwa matengenezo makubwa na *TANAPA* kupitia *KINAPA*. Matangenezo hayo yanahusisha kuchonga upya barabara na kuweka changarawe yenye tabaka la unene wa mm.150 (inchi 6) lililoshindiliwa vizuri, kujenga miundombinu bya makalavati mbali mbali na *drift* moja lenye urefu wa meta 20 na kuweka mifereji ya tupa maji. Kazi hizo zitagharimu zaidi ya shilingi milioni 304. Utekelezaji wa kazi hivi sasa ni asilimia 55.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ambayo ameyatoa hapa. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekubali kwamba kuna mamlaka mbili mambazo zinashughulikia barabara hii na hiki ndicho chanzo cha swali

langu. Je, haoni kwamba kuna haja sasa ya kuwa na chombo cha kuratibu shughuli za hii barabara kwa sababu ni mamlaka mbili zinafanya kazi hiyo ili tusijikute katika hali hii ambayo mimi nimeizungumzia katika swali langu? La kwanza hilo!

La pili, kwa kuwa shughuli hizi ambazo zinafanyika sasa hivi na ambazo ameelezea kwamba zinaendelea na kwamba kiasi cha asilimia 55 kimetekelezwa, ningependa Mheshimiwa Naibu Waziri akanithibitishia hapa kwamba yeye anadhani ni nini ambacho kitafanyika pale ambacho wakati wa mvua hakitasababisha barabara ile wananchi waendelee kukwama kama wanavyokwamba hasa ikizingatiwa kwamba barabara hii ni muhimu sana kwa shughuli za utalii na kilimo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, leo Mungu akijalia na Wabunge wakijalia, tutapitisha sheria mpya ya barabara. Katika sheria hii, inaeleza wazi kwamba mwenye mamlaka ya barabara zote *public roads* ni Waziri anayeshughulikia barabara. Lakini, amekasimu shughuli za barabara kwenye *Authorities* mbali mbali kwa mfano, *TANROADS*, *Local Government Authories* na vile vile baadhi ya Taasisi kama *TANAPA* ambayo inashughulikia barabara hii. Baada ya sheria hii kutakuwa na utaratibu mzuri wa namna gani Waziri anayehusika na barabara apate taarifa ya namna *authorities* hizi mbali mbali zinavyoendesha na kusimamia barabara zilizoko chini yao kama ni *public roads*, *unless* hiyo iwe ni *private road*. Lakini, kwa mfano barabara hii ni *public road* na kwa hiyo Mamlaka ambayo imekasimiwa kwa *TANAPA* watakuwa wanatoa taarifa nzuri.

Kwa hiyo, baada ya sheria hii kupita, nina hakika kutakuwa hakuna matatizo kwa sababu *information* itakuwa inakuja kwa Waziri anayehusika na anaweza akatoa kauli kulingana na hali halisi ya barabara hizo. Kwa hiyo, hilo namhakikishia kwamba kama lilikuwa na matatizo, baada ya sheria hii sasa itakuwa haina matatizo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uhakika kwamba hiyo barabara baada ya mvua bado itaendelea kuwa nzuri. Taarifa tulizozipata na ambazo nimezitoa hapa kutoka *KINAPA* ni kwamba wanaitengeneza hiyo barabara katika kiwango ambacho kitadumu, kitawezesha barabara ile ipitike hata wakati wa matatizo ya mvua. Na kama mlivyoona, hela si haba, ni nyingi ambazo zimetumika kama nilivyowaeleza. Kwa hiyo, naamini kwamba barabara hii itakuwa ni ya kudumu.

Lakini kama anayo taarifa yoyote kwamba bado kutakuwa na matatizo ama kutokana na uhaba wa fedha, basi nadhani tunaweza tukawasiliana au yeye akawasiliana moja kwa moja na *KINAPA* kupata taarifa kamili.

Na. 109

**Matatizo ya Kivuko cha Kigamboni**

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Kivuko cha Kigamboni huwa na matatizo mbali mbali ya kiufundi hali inayosababisha shida kubwa wakati wa kuvuka; na kwa kuwa Wanajeshi wa *Navy* hukumbwa na matatizo ya ucheleweshwaji wa shughuli za Kijeshi kutokana na Kivuko hicho:-

Je, Serikali haioni kuna haja ya kutafuta Kivuko kitakachotumiwa na Wanajeshi peke yao kutokana na uzito wa shughuli zao?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mbunge wa Mfenesini, naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wanajeshi wa *Navy* hutumia muda wote Vivuko vya Kigamboni wanapokuwa kwenye shughuli za kikazi au kibinafsi. Aidha, Wanajeshi hao huvuka bure pamoja na magari wanayotumia. Sasa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mbunge wa Mfenesini, kama ifuatvyo:-

Mheshimiwa Spika, kama tulivyokwishaeleza mara kadhaa, Wizara yangu itanunua Kivuko kipya chenye uwezo wa kubeba tani 500, yaani kitakuwa na uwezo wa kubeba watu 2000 pamoja na magari 60 kwa ajili ya matumizi ya wananchi wa Kigamboni ikiwa ni pamoja na Wanajeshi *(Navy*), Polisi, Magereza na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, pia, Wizara kwa kutumia mkopo wa fedha kutoka Benki ya Dunia itakarabati Kivuko cha *MV Kigamboni* pamoja na kununua injini mbili mpya za Kivuko cha *MV Alina.* Kutokana na hatua mbali mbali zilizochukuliwa na Wizara, tatizo la kuharibika mara kwa mara kwa vivuko hivyo, tunadhani litamalizika kabisa kwani kutakuwa na Vivuko vitatu vya uhakika katika Kivuko cha Kigamboni.

Tunaamini kwamba baada ya hatua hizi za kuboresha huduma hii ya Vivuko, hakutakuwa na haja ya Wanajeshi kuwa na Kivuko chao peke yao kama anavyopendekeza Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. MOSSY SULEIMA MUSSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuwa Serikali ilikuwa na mipango mizuri ya kujenga daraja la kisasa katika eneo hili ili kuondoa tatizo kabisa na kudumu. Je, Serikali inaweza kulieleza Bunge hili tukufu suala hili limefikia hatua gani?

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali imedhamiria kwamba ijenge daraja kuweza kuwasaidia wananchi wa Kigamboni ambao kwa sasa wanapata shida kutokana na vivuko hivi ambavyo vimekuwa havifanyi kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, hatua ambayo imefikiwa katika suala hili ambalo kwa kweli linashughulikiwa na Shirika letu la *NSSF* kwa kushirikiana na wadau kutoka nje ya nchi na wa ndani. Lakini, baada ya kufikia hatua kwamba mradi huu sasa uanze kutekelezwa,

imeonekana kabisa kwamba Serikali ya Tanzania na yenyewe itahusika kwa kiasi kikubwa katika kuweka *input* ya kujenga daraja hilo.

Kwa mfano, kufidia wananchi, kujenga barabara au wanaita *approach roads* ng'ambo ya kule Kigamboni na upande huu na hii ina maana kwamba Serikali lazima iweke Bajeti katika mradi huu. Sasa hatua ambayo ina kwenda ndani ya Serikali ni kuangalia sasa uwezo wa Serikali kuweka na yenyewe fedha, lakini vile vile kutoa dhamana ili *NSSF* waweze kukopa nje ya nchi. Kwa hiyo, hatua zote hizi zinaendelea katika ngazi ya Serikali na tuna hakika kwamba baada ya taratibu zote kukamilika, basi ujenzi wa daraja hilo utaanza.

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Spika, suala la Mheshimiwa Mossy linafanana kabisa na kivuko kilichoko mpakani mwa Mbinga Magharibi na Ludewa. Kwa kuwa Serikali iliweka vivuko viwili na vyote vimezama na maji na wananchi wa Ludewa na wananchi wa Mbinga Magharibi hawawezi kuwasiliana kwa kuvuka. Je, Serikali ina mpango gani wa kurudisha kivuko hicho?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba vivuko katika Mto Luhuhu vilizama. Vile ni vivuko vilikuwa vinatumia nguvu ya kuvutwa kwa maana ya binadamu kuvuta na kile cha mwisho ambacho mimi na yeye tulikipanda wakati nikitembelea Jimbo lake, kilikuja kuzama katika masika na mvua zilipokuwa nyingi na maji yakawa mengi. Kile kivuko bado kimezama na tutakiopoa baada ya maji kupungua kwa sababu maji bado ni mengi kwa sababu ya mvua ambazo zimenyesha kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Lakini, kama ambavyo tumeishaeleza, Serikali tayari imeagiza kivuko kingine cha tani 50 ambacho kinatoka Ufaransa na kitaingia nchini mwezi Juni mwaka huu na baada ya hapo kutakuwa na kivuko kingine cha kusaidia. Na kile kingine tutakiopoa baadaye.Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Mbinga pamoja na wale wa Ludewa ambao wamekuwa wakifuatilia sana kivuko hiki, wawe na subira mwezi Juni tunategemea kivuko kile kifike. *(Makaofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kaboyonga umehangaika kweli kweli. Natoa swali la mwisho la nyongeza kwa Wizara hii.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona na kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Katika majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri Miundombinu kuhusu daraja la Kigamboni, kwa kiasi fualani ningependa taarifa hii iwe *recorded* ili tuone jinsi ambavyo Serikali kwa nini inalega lega kulijenga daraja hili.

Mheshimiwa Spika, kufuatana na tathmini ya gharama ya daraja kama ambavyo *NSSF* wanavyotaka kulijenga chini ya ubia na makampuni ya nje, huko nyuma zilikuwa ni *Euro 45* milioni. Katika *Euro 45* milioni, Serikali ya Netherlands (Nasisitiza), ilikuwa tayari kutoa *grant* kwa Serikali ya Tanzania ya asilimia 50 ya hizo *Euro 45* milioni. Na *Euro 22.5* zinazobaki, Serikali ya Netherlands ilikuwa tayari kutoa *guarantee* ili mkopo wa miaka takriban 15 utolewe kwa ajili ya daraja hilo. Kwa maana hiyo, gharama za daraja hilo kwa

kiasi kikubwa zingelikuwa zimetolewa na Serikali ya Netherlands pamoja na mabenki ya Netherlands. Tanzania walichotakiwa kufanya...

**SPIKA:** Mheshimiwa fika kwenye swali!

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Spika, swali, baada ya kupata *grant* na nafuu ya mkopo leo hii Serikali inasema bado inatafuta pesa, ni pesa gani hizo?

**NAIBU WZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kama anavyosema kwamba gharama ambazo awali *NSSF* na wadau wenzao walikuwa wamekadiria ni hizo *Euro* milioni 45. Lakini ni kweli kabisa kwamba hizo *Euro* milioni 45 hazikuhusisha kilomita 5 za barabara upande huu na kilomita 5 upande mwingine ambao Serikali ilitakiwa kufanya, hazikuhusisha miundombinu ambayo ingeweza kuondolewa pale, haikuhusisha *compesation*, gharama ambazo zote zinatakiwa Serikali iangalie ni namna gani inaweza ikaingia. Na Serikali iko tayari kusaidia kwa sababu imeona unafuu ambao upo katika hizo *Euro* milioni 45, kuna *grant* ndani yake na ndiyo maana Serikali inajaribu katika ngazi ya Serikali kuangalia.

Je, tunawezaje kuweka Bajeti hiyo na masuala mengine ambayo kwa kweli ni ya kitaalam ambayo lazima yakamilike kabla ya kuweza mradi kuanza na vile vile Bajeti kuwekwa ndani ya Seriakli. Kwa maana hiyo, kwa sababu bado tunakwenda kwenye mwaka wa Bajeti, tutaangalia kama Serikali itakuwa imefika katika uwezo wa kuweka hiyo Bajeti ya kugharamia barabara na vile vile *compesation* na mambo mengine ambayo yatahusu sisi kama Serikali ya Tanzania kugharamia.

Na. 110

**Hitaji la Umeme Njombe – Magharibi**

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA (K.n.y. YONO S. KEVELA)** aliuliza:-

Kwa kuwa umeme ni nishati muhimu katika Jimbo la Njombe Magharibi, hasa katika Tarafa za Mdandu, Wang'ing'ombe na Imalinyi:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka umeme wa uhakika (Gridi ya Taifa) katika Tarafa hizo?

(b) Kwa kuwa umeme wa Ilembula na Igwachanya unategemea magogo ya *Tan-wattle Njombe* na si wa uhakika. Je, ni lini umeme huo utakuwa wa Gridi ya Taifa; na kwa nini *TANESCO* haijajenga kituo cha kulipia umeme karibu na wananchi wa Ilembula kama ilivyo sasa ambapo wananchi wanalazimika kulipia umeme nje ya Jimbo lao yaani Njombe Mjini au Makambako?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Yono S. Kevela, ninaomba nami niungane na wenzangu kumpa pole Mheshimiwa Mwapachu na familia yake kwa msiba

uliowapata na tumwombe Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi, amin.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Yono S. Kevela, Mbunge wa Njombe Magharibi, naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, katika Tarafa ya Mdandu, vijiji vya Igwachanya na Mpela vina umeme toka mwaka 1997. Vile vile, katika Tarafa ya Wang'ing'ombe, Kijiji cha Ilembula kilipatiwa umeme mwaka 1998 na kijiji cha Mtwango kilipatiwa umeme mwaka 1981. Vijiji hivi vinapata umeme unaotokana na nishati ya magogo ya miwati ya *Tan-wattle* ya Njombe. Pamoja na kwamba umeme huo umekuwa siyo wa hakika kutokana na kutegemea upatikanaji wa magogo hayo, umekuwa ukiwasaidia wananchi wa vijiji hivyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yono S. Kevela, Mbunge wa Njombe Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kijiji cha Kidugala mkilichopo katika Tarafa ya Imalinyi kilifikishiwa umeme wa Gridi baada ya kukamilika kwa mradi wa kupoza umeme wa kutoka *220KV* hadi *33KV* uliopo Makambako. Umeme wa Gridi ya Taifa uliwashwa kwenye kituo hicho mwisho wa mwezi Machi mwaka huu 2007. Vijiji vya Tarafa za Mdandu na Wang'ing'ombe vitaendelea kuunganishwa kwenye Gridi ya Taifa kadri Bajeti itakavyoruhusu.

(b) Mheshimiwa Spika, katika kijiji cha Ilembula kuna kituoa cha *TANESCO* kwa ajili ya kutoa huduma za kiufundi. Kituo hiki hakina sehemu za kulipia Ankara za umeme kutokana na kutokuwepo huduma ya kibenki ambayo ni muhimu kwa ajili ya kupokea makusanyo ya mapato.

Mheshimiwa Spika, Shirika la *TANESCO* linaagalia uwezekano wa kulipia umeme kijijini hapo ili kuwapunguzia adha wananchi.

Na. 111

**Umeme Vijijini – Jimbo la Ngara**

**MHE. PROF. FEETHAN F. BANYIKWA** aliuliza:-

Kwa kuwa umeme ni nyenzo muhimu katika kuchochea maendeleo ya wananchi Mijini na Vijijini; na kwa kuwa umeme umeishasambazwa katika Mji wa Ngara:-

Je, ni lini Serikali itasambaza umeme katika Mji wa Kabanga na Rulenge na katika Vijiji vya Murugalama, Mabawe na Jululigwa katika Jimbo la Ngara ili kuongeza kasi ya maendeleo katika Wilaya ya Ngara?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Feethan F. Banyikwa, Mbunge wa Ngara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa umeme ni kichocheo kikubwa cha maendeleo ya wanmanchi, hivyo imekuwa ikifanya kila linawezekanalo ili kuhakikisha wananchi wake wananufaika na nishati hiyo muhimu.Upelekaji wa umeme Mji wa Kabanga ulijumuishwa kwenye mradi wa kupeleka umeme Wilaya ya Ngara. Licha ya nguzo zote katika njia ya kupeleka umeme Kabanga kusimamishwa, mradi huo haukuweza kukamilika kutokanana matatizo ya kifedha yanayoikabili *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wake, mradi huo uliwekwa kwenye program ya ufadhili chini ya *Energy Rural Transformation* ambao sasa unajulikana kwa jina la *Access Expansion Programme*. Taratibu za kukamilisha maandalizi ya programu hii zinaendelea na pindi utekelezaji utakapoanza, miradi ya umeme iliyo katika programu hiyo ukiwemo wa kupeleka uememe Kabanga itapatiwa umeme.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa *Access Expansion Programme* una kipengele cha kupeleka umeme vijijini. Chini ya kipengele hicho, vijiji ambavyo viko katika *Rural Electrification Master Plan* vikiwemo vijiji vya Rulenge, Jululigwa, Murugalama na Mabawe vitapangiwa utaratibu wa kupatiwa umeme.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Pamoja na majawabu mazuri ya Naibu Waziri, nataka kujua, mwka jana kwenye Bajeti tulipitisha hapa pesa kwa ajili ya kupeleka umeme vijijini. Ninataka kujua ni vijiji vingapi mpaka sasa vimepatiwa umeme sasa?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, suala hilo hilo linahitaji takwimu, kwa hiyo atupe muda tutamletea siku nyingine.

Na. 112

**Viwango vya Lishe Bora kwa Wanajeshi**

**MHE. COL. SALEH ALI FARRAH** aliuliza:-

Kwa kuwa kuna malalamiko ya chini chini juu ya posho ya chakula *(Ration Allowance)* kwa Askari waliooa na wale wasiooa (kapera) ambapo mlo wanaopata una viwango vya chini vya lishe na pia ni kidogo kwa faradhi ya Askari mmoja mmoja; na kwa kuwa wazabuni pia wanalalamikia bei ya vyakula kupanda kiholela baada ya kusafirishwa kutoka Dar es salaam hadi Zanzibar ambapo kwa heshima ya kazi yao hulazimika kutoa huduma hata kwa hasara ili kuepuka kuvunja mkataba wa zabuni zao:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kupandisha viwango vya lishe kwa Askari mmoja mmoja ili pawepo na Askari waliojengeka kwa kazi zao ngumu na za dharura zinapotokea?

(b) Je, Serikali haioni kuna haja ya kupandisha thamani ya mlo wa Askari kutoka shilingi 3,000/= hadi kufikia shilingi 6,000/=?

(c) Kwa nini Kuruta na Askari Kapera hawapatiwi mmgao wa karanga na zabibu kavu katika mlo wa mchana kwa maslahi ya afya zao?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Col. Saleh Ali Farrah, Mbunge wa Jimbo la Raha Leo, lenye sehemu (a), (b) na (c), napenda kwanza kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, posho ya chakula inayotolewa na Jeshi la Wananchi wa Tanzania hupangwa kwa kuzingatia mahitaji ya lishe na bei za vyakula vinavyohitajika kwa siku. Chakula kilichopangwa kwa Askari kwa siku kina virutubisho vya kutosha kumwezesha Askari kutekeleza majukumu yake. Hata hivyo, kutokana na kupanda kwa bei za vyakula, posho ya chakula hulazimika kufanyiwa marekebisho ya mara kwa mara ili kukidhi mahitaji ya mlo wa Askari uliopangwa. Baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Col. Saleh Ali Farrah, Mbunge wa Raha Leo kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa wakati huu Serikali haioni sababu ya msingi ya kupandisha viwango vya lishe kwa Askari mmoja mmoja kwani viwango vinavyotumika sasa vinatosheleza. Aidha, viwango vinavyotumika ni kwa mujibu wa viwango vilivyowekwa na Jumuiya ya Madola.

(b) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa kima cha posho ya chakula kinachotolewa cha shilingi 2,000/= kwa Askari kwa siku, na siyo 3,000/= ni kidogo na hivyo kudhoofisha kiwango cha lishe. Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kushirikiana na Hazina inafanya juhudi za kungeza kiwango cha posho ya chakula ili kuweza kukidhi ubora na kiwango cha lishe inayohitajika kwa Askari na Maafisa.

(c) Mheshimiwa Spika, ni kweli Askari walikuwa wakipatiwa karanga na zabibu kavu, lakini utoaji huo umesitishwa kwa muda kutokana na ufinyu wa Bajeti. Hata hivyo vyakula vinavyotolewa na wazabuni vina virutubisho vya kutosha.

**MHE. COL. SALEH ALI FARRAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mimi nina swali moja dogo la nyongeza kuhusu chakula cha Askari. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kunielezea Askari kwa kufanya kazi zake za dharura za kila siku za kutumia nguvu nyingi, anatakiwa atumie *calories* ngapi?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Spika, Askari wa Jeshi ili aweze kukidhi majukumu yake ya kitaifa, analazimika kuapata *calories* 3500 kwa siku.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante kwa jibu zuri na fupi na fasaha pia.

Na. 113

**Fedha za Kuendeleza Soka Nchini**

**MHE. COL. FETEH SAAD MGENI** aliuliza:-

Kwa kuwa kuna taarifa kuwa Shirikisho la Soka Duniani *(FIFA)* huipatia *TFF* kiasi cha Dola 250,000 kwa ajili ya kuendeleza soka kila mwaka; na kwa kuwa *TFF* ina ushirikiano mzuri na *ZFA* hasa nyakati ambazo nchi yetu inapokuwa ikijiandaa na mashindano ya kimataifa ambapo huteua walimu kutoka pande zote mbili:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa ni vyem,a sasa *TFF* kuipatia *ZFA* kiasi fulani cha fedha hizo ili zisaidie maendeleo ya soka Zanzibar?

(b) Kwa kuwa *TFF* ina uzoefu mkubwa na utaalam wa kuongoza na kusimamia timu Tanzania Bara katika michuano ya Kimataifa. Je, kwa nini wasiwashirikishe *ZFA* ili kupata uwiano mzuri wa kitaalam katika kusimamia timu za Zanzibar zinazoshiriki michuano ya Klabu Bingwa Afrika na zile za Shirikisho hasa baada ya kupata uanachama toka *CAF*.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. JOEL N. BENDERA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali, naomba ruhusa yako niweze kutoa rambi rambi kwa familia ya Dr. Aaron Chiduo pamoja na familia ya Mzee Bakari Mwapachu. Naomba Marehemu roho zao zikae mahali pema peponi. Napenda kujibu Swali la Mheshimiwa Col. Feteh Saad Mgeni, Mbunge wa Bumbwini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Serikali inatoa umuhimu mkubwa na vile vile inao wajibu wa kuisaidia Zanzibar katika kuleta maendeleo ya soka Visiwani humo. Lakini pia napenda kulifahamisha Bunge hili Tukufu kwamba fedha hizo zitolewazo na *FIFA* kwa mikupuo minne kila mwaka, nyingi huombwa kwa miradi maalum na kwamba fedha zote zitolewazo hutakiwa kutumika kama zilivyopangwa.

Hata hivyo kwa kuzingatia umuhimu wa maendeleo ya Michezo katika Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Wizara yangu imewashauri *TFF* washauriane na *ZFA* katika kuandaa michanganuo ya miradi ya mpira wa miguu kwa pande zote mbili za Muungano ili *ZFA* nao wapate kufaidika na fedha zitolewazo na *FIFA* kwa *TFF* kwa kila mwaka.

(b) Ushirikiano wa shughuli za mchezo wa mpira wa miguu, baina ya Tanzania Bara na Visiwani umekuwa mzuri kwa miaka mingi iliyopita. Panapokuwa na Kambi kwa timu ya Taifa, makocha na viongozi wa timu hutoka pande zote mbili za Muungano. Huu ni utaratibu waliojipangia *TFF* na *ZFA* wenyewe.

Aidha, *TFF* wako tayari kusaidia kitalaamu katika kusimamia timu za Zanzibar ambazo zinashiriki katika mashindano makubwa wakiombwa kufanya hivyo na *ZFA*. Moja ya shughuli za kitaalamu ambazo *TFF* wako tayari kuwasaidia *ZFA* ni mafunzo kwa makocha, wakufunzi wa makocha, waamuzi, madaktari wa michezo na pia mafunzo ya utawala na uongozi wa mpira wa miguu.

**MHE. COL. FETEH SAAD MGENI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru nafasi nyingi kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri na pia namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyonipa ambapo yamenipa matumaini na amewapa matumaini Wazanzibar. Suala langu naomba kuuliza. Je, mgao huu wa fedha ambao ameuzungumza hapa utafanyika lini ili wafaidike na wao? Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mtaona bado tunaendelea kidogo kwa sababu muda ambao tulitangulia kuutumia kwa ajili ya Hati za Kuwasilishwa Mezani.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. JOEL N. BENDERA):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye swali langu la msingi nimesema Wizara yangu imeishauri *TFF* na *ZFA* wakae ili waweze kujadiliana waone namna gani ambavyo wanaweza kuanza kugawana ama kuanza nao Zanzibar kufaidika na miradi ya fedha ambazo zinatoka *FIFA* kwa hiyo, suala hili siwezi kusema ni lini kwa sababu sisi tumeshashauri na ninaamini kabisa *ZFA* na *TFF* huwa wana vikao vyao.

Kwa hiyo, na sisi tumeshawashauri nina imani kabisa kwamba sasa kwa ushauri wa Wizara wataanza kukaa chini na kuanza kulishughulikia suala hili.

**MHE. NURU AWADHI BAFADHILI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali. Kwanza na mimi naungana na wenzangu kuipa pole familia ya Mheshimiwa Mwapachu Mwenyezi Mungu awajalie moyo wa subira.

Kwa kuwa *TFF* ni watalaam na wazoefu wa kuchagua wachezaji katika timu yetu ya Taifa na kwa kuwa Tanzania sisi tuna wachezaji kutoka Wilaya mbalimbali. Je, *TFF* ina mpango gani wa kuunganisha wachezaji kutoka Wilaya mbalimbali katika nchi yetu badala ya kuchagua tu wachezaji kutoka timu za Simba na Yanga kuunda timu ya Taifa? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. JOEL N. BENDERA):** Mheshimiwa Spika, suala la kuchagua wachezaji wa timu ya taifa ni suala ambalo linahitaji utalaam na ndiyo maana tunakuwa na *coach, coach* ndio mtaalam ambaye anaweza kutambua kipaji hiki kwamba kimeshafikia hatua ya kufikia Timu ya taifa.

Lakini nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wote ni kwamba uchaguzi wa timu ya taifa sasa hivi kwa sababu tunaye kocha wa taifa, tunaye kocha wa taifa wa vijana, tunayo Kamati maalum inayoshughulikia uchaguzi wa timu ya taifa na mashindano mbalimbali. Sasa hivi katika Wilaya zetu kuanzia ngazi ya nchini hasa kwa shindano hili *Kopa Coca cola* ambalo linashirikisha Wilaya zote na Mikoa yote. Nina imani kwamba kocha anapata nafasi ya kwenda kuchagua wachezaji anapokwenda kwenye maeneo husika.

Sasa hivi ninavyozungumza kocha yuko Iringa. Sasa hivi kuna mashindano ya *mini league,* akitoka Iringa anakwenda Morogoro, akitoka Morogoro anakwenda Arusha, akitoka Arusha anakuja hapa Dodoma. Kwa hiyo, utakuta atapata nafasi ya kuona wachezaji wengi. Yale mashindano ya Wilaya na Mkoa pia nayo yanahusika katika kusaidia kutafuta hawa wachezaji. Kama nilivyokwishasema ni suala la kitalaam ni vizuri tukamwachia kocha mwenyewe ili aweze kuzunguka katika nchi na jopo lake aweze kupata wachezaji. Hatuwezi kuokoteza mchezaji. Mchezaji ni mtalaam. (*Makofi*)

**SPIKA:** Upendeleo maalum Waheshimiwa Wabunge mnisamehe. Mwenzetu Hafidh Ali alikuwa refa wa kimataifa. (*Makofi*)

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Spika, na mimi nikupe shukrani maalum kwa kunipatia nafasi hii ya kuuliza swali. Pia nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa jibu lake la swali mama lililoulizwa na Mheshimiwa Kanali Feteh.

Mheshimiwa Spika, masuala ya michezo hasa mpira wa miguu katika Jamhuri ya Muungano si ya Muungano. Zanzibar wana shughuli zake za michezo na Bara wana shughuli zao za michezo. Kwa bahati nzuri Mheshimiwa Naibu Waziri ni mtalaam na alikaa katika chama cha mpira kwa miaka mingi. Hivi Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza akaliambia Bunge hili haya mamlaka ya kuiwakilisha Tanzania iliyochukua *TFF* wamepewa na nani na mwaka gani na kwa makubaliano yepi baina ya Zanzibar na Tanzania Bara katika chama hiki cha *TFF*? (*Makofi*)

**SPIKA:** Ningejua swali litakuwa gumu namna hii nisingempa nafasi. *(Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. JOEL N. BENDERA):** Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri mimi nimekuwepo *TFF* takriban miaka mingi nikiwa mtalaam pale. Nataka nimhakikishie Ndugu Hafadh kwamba *FIFA* wanaitambua Tanzania na unapozungumza Tanzania maana yake ni Zanzibar na Tanzania Bara. Ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, kinachofanyika hapa ni ule ushirikiano wa Jamhuri ya Muungano na ndiyo unakuta kuna baadhi ya mikutano, kuna baadhi ya mashindano yote tunafanya pamoja. Timu ya Taifa ni ya Tanzania yaani Zanzibar na Tanzania Bara kwa pamoja. Siyo Tanzania Bara, wala Zanzibar ni ya pamoja. Timu ya taifa ya vijana ni ya pamoja, timu ya wanawake ya Taifa ni moja. Zanzibar pamoja na Tanzania Bara. Kwa hiyo, ni kwamba ni suala la Muungano *automatically* hata kama hupendi ni Muungano *automatically*. Ndiyo maana hata shughuli zetu tunazifanya sasa hivi Kimuungano. Vipi vikao vya *ZFA* na *FAT* wanakaa pamoja wanakubaliana. Tunafanya kila juhudi kuhakikisha kwamba Zanzibar nayo inaingia *FIFA* ndiyo maana leo unaona Zanzibar wako *CAF*, wako *CECAFA*. Iko siku Zanzibar nao wataingia *FIFA*. *(Makofi*)

Na. 114

**Kanuni za Mfumo wa Kodi**

**MHE. JAMES D. LEMBELI (K.n.y. MHE. EZEKIEL M. MAIGE)** aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kwa mujibu wa Kanuni za mfumo wa kodi bora *(principle of good tax system)* ni pamoja na mfumo wenyewe kutokuwa wa kibaguzi *(fair to all tax payers)* pato moja kutotozwa kodi mara mbili na kuzingatia kipato na uwezo wa kulipa na kwa kuwa mfumo wa kodi ya mapato kama ilivyo kwenye sheria ya kodi ya mapato ya mwaka 2004, umeweka mzigo wa kodi kuwa mkubwa sana kwa wafanyakazi *(employment income)* ukilinganisha na vyombo vingine vya mapato:-

(a) Je, Serikali inatambua kuwa pato la mfanyakazi linalotozwa kodi si pato lake halisi *(net income from employment)* kwani linakokotolewa kwa kuzingatia pato la jumla *(gross employment income)* yaani kabla ya kutoa gharama za msingi za kumwezesha

mfanyakazi kufanya kazi *(expenses wholly and exclusively incurred for the production of employment income)* kama gharama ya usafiri kwenda na kurudi kazini, gharama ya chakula cha mchana wakati wa kazi na gharama ya nyumba?

(b) Kwa kuwa, sehemu kubwa ya mapato ya mfanyakazi hutumika kulipia gharama za usafiri, chakula na makazi, huduma ambazo huendeshwa na kampuni au watu binafsi ambazo pia ni walipa kodi.

Je, Serikali haioni kuwa mfumo huo unatoza kodi mara mbili kwenye pato moja, yaani toka kwa mwajiriwa, kama *employment income* na kwa mwenye nyumba kama *rent*?

(c) Kwa kuwa kifungu cha 12 (2) cha sheria ya kodi ya mapato ya mwaka 2004, kinatambua na kutoa unafuu wa kodi kwenye pato litokanalo na uwezekezaji au biashara kwa ajili ya gharama za lazima kwenye shughuli hizo *(wholly and exclusively incurred to the production of incom from investment or business)* lakini hakuna kipengele kama hicho kwenye pato litokanalo na ajira. Je, Serikali haioni kuwa sheria hiyo inawabagua na kuwabebesha mzigo wa kodi zaidi wafanyakazi?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ezekieli M. Maige, Mbunge wa Msalala, lenye sehemu (a), (b) na (c), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu 7 kifungu kidogo cha (1) cha sheria ya kodi ya mapato ya mwaka 2004, mapato ya ajira ya mfanyakazi kwa mwaka wa mapato, haijumuishi mapato halisi au mapato yaliyosamehewa au kutoshirikishwa katiaka ukokotoaji yaani *exemption and exclusion in calculating employment income* kwa lengo la kuwa na sera ya kukuza hali ya kimaisha, kijamii na kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, maana ya mapato ya ajira yaani *employment income* katika sheria ya kodi ya mapato ya mwaka 2004 ililenga kupanua wigo wa kodi tofauti na sheria ya kodi ya mapato ya mwaka 1973 ambayo imefutwa. Hata hivyo hii haina maana kuwa kila kipato au malipo yanayofanywa na mwajiri yanatozwa kodi, ndiyo maana mapato yatokanayo na ajira peke yake katika kuzalisha faida ya mwajiri yaani *wholly and exclusively in the production of income* hayatozwi kodi. Katika sheria hiyo, mapato yamebainishwa katika maeneo makubwa matatu mapato ya kwenye ajira, biashara na uwekezaji. Kanuni adilifu ya kodi *neutrality principle* imefuatwa ndani ya sheria hii ambapo utaratibu wa ukokotoaji unaotumika hufanywa kwa kila eneo peke yake yaani *scheduler approach*. Sheria ya kodi ya mapato ya mwaka 2004 haijawabagua waajiriwa wala haitozi kodi mara mbili kwa vile kodi ya pango (*rent)* itolewayo na mwajiriwa ni pato kwa mwenye pango ambaye anafanya biashara na kwa upande wa mwajiriwa ni matumizi yake ya kawaida ambayo hayapo katika mkataba wa ajira na kama mkataba wa ajira upo ambapo mwajiri anamlipia, sheria ya kodi ya mapato ya mwaka 2004 inatoa nafuu ya nyumba yaani (*housing benefits)*.

Mheshimiwa Spika, sheria ya kodi ya mapato ya mwaka 2004 inatoa nafuu ya kodi kwenye magari, nyumba na hata usafiri kwa mwajiriwa anayeishi zaidi ya maili 20 kutoka mahala pake pa kazi, gharama za chakula, matatibu, gharama za bima ya afya na kadhalika. Pale mwajiri anapomlipia mwajiriwa kama ilivyobainishwa kwenye kifungu cha 7 (3) (a) mpaka (i) cha sheria ya kodi ya mapato ya mwaka 2004. Hivyo sheria hii inatoa unafuu wa kodi kwa mwajiri na mwajiriwa kwa upande mwingine.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza swali kama ifuatavyo:-

Je, Serikali ina utaratibu gani wa kutoza kodi pale mtumishi au mfanyakazi anapokuwa na ajira mbili?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Mheshimiwa Spika, kama una ajira mbili na zote zimetolewa taarifa mamlaka ya mapato zote zitatozwa kodi kutegemeana na vifungu maalum vya sheria.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda wa maswali umekwisha. Sasa kabla sijasoma matangazo nina shughuli mbili za kufanya, moja mtakumbuka Waheshimiwa Wabunge, kwamba katika Kikao cha Sita Mheshimiwa Chacha Wangwe, Mbunge wa Tarime, alikuwa amedhihirisha asingekuwa tayari kusahihisha usema wake kuhusu mauaji ya Tarime wakati wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005. Lakini baadaye, baada kuona tofauti ya yale aliyotamka kabla aliniandikia barua kwamba angependa sasa kutoa ufafanuzi kuhusu tamko lake. Nampa nafasi sasa. *(Makofi)*

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa ufafanuzi kuhusu tamko nililotoa Bungeni tarehe 10 Julai, mwaka jana kuhusiana na mauaji Tarime. Kwanza, kabisa na mimi pia natoa rambirambi kwa kifo cha mama yake Mheshimiwa Mwapachu, nawatakia uvumilivu.

Mheshimiwa Spika, pili, mimi kama Mbunge niliyechaguliwa kuingia katika Bunge hili na wananchi wa Tarime kwa niaba yao napenda kusema ya kwamba wananchi wa Tarime wana heshima kubwa sana na Bunge hili, ndiyo maana wanashiriki katika uchaguzi na kwa sababu hiyo, chochote ninachokisema hapa kwa niaba yao kama Wabunge wengine wanavyozungumzia majimbo yao na siyo kwa nia mbaya wala nia ya kutaka kuonyesha ukaidi au kiburi au dharau. Ni kwa nia njema kabisa nikiwa mkweli kwangu mimi mwenyewe na kwenye nyumba hii na kwa taifa la Tanzania. (*Makofi*)

Kwa hiyo, yale niliyoyazungumza tarehe 10/7/2006 nilikuwa nagusia suala ambalo lilikuwa limetokea na baada ya kuwa nimeagizwa na Bunge kwamba nithibitishe nilifanya hivyo na Kamati yako mwenyewe uliyoiteua ilikwenda kule jimboni na kuthibitisha kwamba kweli mauaji yale yalitokea. Pia wewe mwenyewe katika mazungumzo yako hapa Bungeni ulikubaliana kwamba kweli mauaji yalitokea. Kwa hiyo, hilo ndiyo suala la msingi ambalo nilikuwa nimezungumza. Isipokuwa tulikuja kuhitilafiana ambapo ni kawaida ya Bunge kwa sababu Bunge ni sehemu ya majadiliano na mabishano kwa nia njema kwamba je, yale mauaji yalikuwa ni mauaji ya aina gani?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ukawa umesema ya kwamba yale ya mauaji hayakuwa mauaji ya kisiasa. Kwa hiyo, niondoe ile kauli. Sasa hapo kidogo nikawa nimekuwa na utata ikibidi kwanza niwasiliane na wale ninaowawakilisha. Katika kipindi hicho basi sikuweza kufanya kama ulivyosema na nikaonekana kama nimekuwa mkaidi kwako.

Mheshimiwa Spika, lakini mimi nina kuheshimu sana kama mzee wa nyumba na unaendesha vizuri nyumba yetu na nina hakika ya kwamba huna upendeleo wowote, wote unatupenda kwa hiyo, naomba usichukulie ya kwamba nilikuwa ninakudharau au kukufanyia ukaidi. (*Makofi*)

Kwa hiyo, katika hili eneo la tafsri kwamba yale mauaji yalikuwa ya kisiasa au vipi hilo ndilo nilikuwa nasema ya kwamba basi hapo hata Waheshimiwa Wabunge, wengine watatusaidia wengine wamesomea mambo ya falsafa za kisiasa na kadhalika. Wanaweza wenyewe wakatusaidia vile kutafsiri lakini la msingi nililokuwa nalisema ni kwamba yale mauaji yalitokea na wewe kwa uwezo wako na maoni yako unaweza ukaielekeza Serikali kuchukua hatua na hiyo ndiyo ilikuwa *interest* ya wananchi wa Tanzania.

Kwa hiyo, mimi naomba kwa yale ambayo uliona kwamba labda nimekudharau uniwie radhi. Lakini lile suala ulishughulikie. Nashukuru (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, ufafanuzi nilikuomba ulihusu siyo tu kwamba mauaji yalikuwa ya kisiasa. Lakini kwamba kulikuwa na njama ambazo zilielekezwa kwako binafsi hilo ndilo lilikuwa suala ambalo tulikubaliana utalifafanua kwa sababu haitoshi tu kusema ya kisiasa wanaweza kuwa watu walikuwa wanapigana kweli kisiasa lakini kusema njama zinazotokana na takrima na mauaji kama vile yalikulenga wewe binafsi. Hilo ndiyo naomba ufafanue.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa nyingine tena. Ni kweli mimi hilo la kusema ya kwamba kulikuwa na njama binafsi iliyokuwa inaelekea kwangu, basi, hilo nalifuta. Pia sikuwa na maana ya kwamba kuna Chama chochote kilichokuwa kimepanga njama hiyo. Kwa hiyo, nashukuru sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Chacha Wangwe, kwa uungwana huo. Kwa maneno hayo nasitisha kabisa shughuli za Kamati za Maadili kumjadili Mheshimiwa Wangwe. Kwa hiyo, sasa jambo limekaa vizuri. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Benedict Losurutia, aliugua kwa muda mrefu na akapelekwa nje ya nchi. Aliniomba atoe shukrani kwa sababu wengi wenu mlikuwa msaada mkubwa kwake. Kwa hiyo, namtambua naomba asema maneno machache. (*Makofi*)

**MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA:** Mheshimiwa Spika, na mimi nachukua nafasi hii kwanza kukushukuru wewe mwenyewe Spika kwa kunipa fursa hii muhimu ya kutoa shukrani na kuelezea kwa Wabunge wenzangu hususan Wapiga Kura wangu wa Jimbo la Kiteto na wengine tu ambao walionisaidia wakati nilipokuwa naumwa kwa njia moja au nyingine. Kwa kumbukumbu zangu nilianza kuugua tarehe 15/7/2006 nikiwa kwenye *session.* Kwa kawaida huwa nalala *Center* kule *Roman Catholic* nikamwita Mheshimiwa Christopher Ole – Sendeka, aje akanipeleke hospitalini.

Nilikuwa mzima, nilihudhuria kipindi cha asubuhi, lakini ilipofika mnamo kama saa 9.00 hali ilianza kubadilika ndipo akaja akanipeleka hospitalini pale *General Hospital*. Kufika *General Hospital* nilipokelewa vizuri sana nikapelekwa kupimwa *X-ray* hali yangu ya mapafu ilikuwa siyo nzuri. Nikapelekwa kulazwa. Baada ya hapo ndiyo mambo yakaharibika. Nina maana kwamba ugonjwa ulizidi. Ilipofika jioni taarifa ilipelekwa Bungeni ikamfikia Mheshimiwa Spika, wetu hapa na wengine wengi Waziri Mkuu na viongozi wengi. Profesa Mwakyusa - Waziri wa Afya, Mheshimiwa William Lukuvi. Taarifa ilitapakaa kwamba niko hospitali na wote walifika hospitalini kuniangalia kunijulia hali. Kwa kweli nawashukuru sana nilifarijika jioni hiyo lakini nilikuwa nimezidiwa baada ya hapo hali ilianza kuwa mbaya zaidi kwa kweli na sikuweza tena kuwatambua hadi asubuhi. Asubuhi wakafanya utaratibu

kuniingiza kwenye matibabu. Kwa hiyo, matibabu yangu yalianza tarehe 15/7/2006 siku hiyo hiyo. Tarehe 17/7/2006 wakanisafirisha kwenda Muhimbili huko wakanipokea vizuri. Profesa Mwakyusa Waziri wa Afya, alifanya maandalizi mazuri nikapolewa vizuri, nikapelekwa kwenye chumba cha wagonjwa, nikalazwa vizuri tu, nikapewa dawa nikapata vipimo vya kutosha. Baadaye nikapata matibabu wakaona kwamba wanipeleke India.

Tatizo kubwa ambalo nililipata ni suala la figo. Napenda kuwa wazi kabisa, kwamba nilikuwa na kisukari kwa kipindi cha miaka 15. Niligundulika mwaka 1989. Nilikuwa naishi nacho. Lakini baadaye ikawa masuala ya macho, masuala ya figo, zilikuwa *kidney* zote zili-*fail*. Kwa hiyo, wakanipeleka India. Nawashukuru wale wote ambao walionitembelea hospitalini. Viongozi wote, Ofisi ya Bunge, imekuwa karibu sana na mimi na viongozi na Wabunge wote. Nasema Wabunge wote kwa njia moja au nyingine waliniulizia wakaniombea. Kwa hiyo, nawashukuru kwa kusema kweli. Baada ya hapo napenda tena nitoe shukrani zangu sitakaa mbali sana na Ofisi ya Bunge ikiongozwa na Spika, kwa umuhimu wake. Wamekuwa karibu sana na mimi, nikiwa mgonjwa wala siyo mimi tu na Wabunge wote ambao tulikuwa nao. Kwa kweli waliweza kututunza kwa kila hali. Hatukupata matatizo yoyote nahitaji jirani, nahitaji ndugu nyumbani, Ofisi ya Bunge, ilikuwa badala ya jirani na ndugu kwa kusema kweli. (*Makofi*)

Vile vile natoa shukrani zangu za dhati kwa Serikali ikiongozwa na Waziri Mkuu, wamekuwa vile vile karibu, wametoa huduma mahali pale ambapo panaweza kutolewa. Waliweza kuingilia kati na kufuatilia matibabu yangu katika Hospitali ya Muhimbili ambapo wanahusika kwa kweli kwa huduma ya namna ya hiyo. Mimi binafsi niliona kabisa kwamba kiongozi akiugua Serikali iko karibu na taasisi ambazo ziko karibu, zitakuwa karibu nawe. Ila naomba tu kwamba utaratibu mzuri uimarike vizuri sana juu ya viongozi hasa wanapopelekwa katika hospitali ya Muhimbili. Viongozi wawe na utaratibu hususan ambao unaofuatwa ambao unanyooka. Ambao kila mtu angepeswa afuatwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo napenda kutoa shukrani zangu kwa vikundi mbalimbali. Kuna shukrani zangu kwa vikundi mbalimbali, kwanza kwa Wabunge wa Mkoa wa Manyara wakiungana na Wabunge wa Mkoa wa Arusha. Napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwamba waliweza kunijulia hali kwa kila jambo. Waliweza kutuma tume mpaka wakafika hospitalini, mpaka wakafika nyumbani kwangu Kurasini, wakanipa chochote kile. Kwa kweli sikuona ugumu wowote. Narudia tena kusema kwamba nawashukuru sana Wabunge wa Mkoa wa Arusha, Wabunge wa Mkoa wa Manyara kwa jinsi ambavyo walinifanyia. Vile vile napenda kutoa shukrani zangu kwa Kamati za Bunge. Nilipata ujumbe wao, wametuma nao ujumbe wao, wametuma salaam, wamepiga simu Wenyeviti, siwezi kutaja mmoja mmoja lakini karibu kila Kamati iliniulizia hali yangu inavyoendelea. Kwa hiyo, napenda vile vile kutoa shukrani zangu kwa Kamati za Bunge zote. Kamati ya Maadili walifika wote wakiongozwa na Mheshimiwa N'hunga na Christopher Ole Sendeka. Kwa hiyo, walifika wao wakanijulia hali pale hospitalini. (*Makofi*)

Vile vile napenda kutoa shukrani za dhati za binafsi kwa wale wote kwa jumla kabisa wale wote ambao walikuwa wananipigia simu mimi ulipofika mwezi wa 8 nilinyang'anywa kwamba usitumie tena simu, basi simu akakabidhiwa mke wangu Sarah. Baadaye nitamwelezea vizuri sana akawa ndiyo anaratibu mambo yangu yote. Kwa hiyo, simu zangu zote alikuwa anazipokea mama kulingana na hali yangu ilivyokuwa. (*Makofi*)

Kwa hiyo, alikuwa ananijulisha tu fulani kapiga simu, watu wengi Kwa hiyo, nawashukuru wale wote ambao wametumia fedha zao kutujulia hali. Vile vile nawashukuru

ambao waliweze kuniulizia kwa mwingine kwamba hali yangu namna gani. Naomba Mungu awabariki na nawashukuru sana. (*Makofi*)

Lingine ambalo napenda nilizungumzie ni suala la maombi. Hili nazungumza kwa dhati kabisa kwamba maombi yameendeshwa katika sehemu mbalimbali. Kuna maombi ya watu binafsi tu, mtu anakaa ananikumbuka ananiombea. Nawashukuru sana. Kuna maombi ambayo yanatokana na vikundi mbali mbali sikujua kwamba jamii ambayo iliyokuwa inanizunguka pale. Kuna watu walikuwa wananiombea. Nashtukia tu wanakuja wanaomba, sikushtukia wala sikujua kwamba kuna mchungaji yuko Nairobi au yuko sehemu anapiga simu anakuombea wala hakujui, sikujua. *(Makofi)*

Anapata tu habari kwenye intaneti sehemu nyingine unaombewa. Kwa hiyo, nimepata maombi mengi sana na yote yameelekezwa kwa Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Kwa kweli, naweza kusema kwamba katika Jimbo langu Makanisa yote yameomba, Misikiti yote imeomba, na kwa kusema kweli sala zote zimesikika kwa Mwenyezi Mungu, ndiyo maana nasimama hapa mbele yenu kwa sababu ya uwezo wa Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Baada ya hapo napenda sasa nitoe shukrani zangu za mwisho kabisa lakini zenye umuhimu kwa mke wangu Sara. *(Makofi)*

Sara ambaye tumemtwika, tumwekea mzigo mzito akaubeba kwa niaba ya familia. Sara ni mke wangu ambaye tumeishi naye kwa miaka 40 kwa sasa hivi. Yeye ndiye amenisindikiza mpaka India na ameniweka kwenye ndege kwenye *stretcher,* kwa hiyo ameniweka niko hoi. Alimpeleka mtu ambaye hajui kwamba atamrudisha na anakwenda nchi ambayo hajaikanyaga hata siku moja. Afadhali mimi natembea hii dunia, lakini yeye ndiye anakwenda India hajui India! Anampeleka bwana wake *(Makofi)*

Anampeleka mume wake, sisi hatutofautishi, yote ni sawa tu. Baada ya pale amenipeleka kwa kweli sina kitu cha kumwambia. Yeye yuko sasa hivi Dar es Salaam anafuatilia masuala ya dawa zangu kwa sababu yuko *in tought* na madaktari, kwa hiyo, yupo Dar es Salaam, amekwenda jana, atarudi kesho au keshokutwa kufuatilia hizi dawa za figo katika Mfamasia Mkuu na bado ndiye ananihudumia mpaka dakika hii. Kwa hiyo, sina kitu cha kumweleza, amefanya kazi kubwa kabisa na ni mfano. Nilifika Bombay nasema tu kwa mazungumzo mimi sina habari, ilikuwa ananitafutia *oxygen,* amesafiri kama kilometa 60 kutafuta kwenye Zahanati mbalimbali kama anaweza kupata *oxygen,* bahati mbaya nilisafiri na mtoto mwingine ambaye naye alikuwa anatafutiwa *oxygen* ambayo baadaye yeye alikuja kufariki tulipofika kule hospitalini.

Kwa hiyo, baadaye tukabahatisha halafu tukaendelea na safari yetu. Tulipofika kule hospitalini baadaye tukabahatisha halafu tukaendelea na safari yetu. Kwa niaba ya familia yangu nataka tu niseme kwamba namtakia Sara afya njema na maisha marefu na mimi nipate nafasi na yeye siku moja kumhudumia. *(Makofi)*

Kwa uzuri hasa na nasema vile vile na familia yangu hakuna kitu chochote ambacho nasikitika kwamba nimeikosa wakati nikiwa nauguwa miezi sita. Kila nilichoacha nyumbani nilikuta salama salimini. Kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu na watoto hawa ambao niliwaacha nyumbani wamefanya kazi kama tulivyotarajia, maana yake kabla hatujaondoka

tulikuwa tumejipanga watu wote wakae katika hali ya tahadhari. Kwa hiyo, wale wote ambao walikuwa katika tahadhari walitekeleza majukumu yao. Maana yake wakati huo mimi nilipokuwa sipo shughuli zote zilikuwa nusu nusu, kwa hiyo kila mtu alichukua nafasi yake inavyotakikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nataka tu niseme nawashukuru vijana wangu kwamba wamefanya kazi ambayo walitakiwa kufanya. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwamba nimerudi, nipo mzima, sasa nasema kwa maneno haya kwamba Mungu ni mkubwa wote tunamtumaini. Yeye ndiye aliyeniponya hakuna mwingine. Ahsanteni sana kwa kunisikiliza. Nawashukuruni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, bado Mheshimiwa Losurutia, basi malizia.

**MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA:** Mheshimiwa Spika, naomba nielezee kuhusu mtu mmoja muhimu ambaye kwa kusema kweli nimemsahau kwa umuhimu wake. Nilikuwa na kijana mtoto wa Mjomba wangu anaitwa Abel. Huyu Abel Mainge ni mtoto ni wa dada yangu. Huyu kijana, yeye walikuwa wanakula nyama kule nyumbani, wamechinja, sasa vijana wakaenda kula, sasa wakati huo nilituma habari kusema kwamba Mbunge ni mgonjwa anahitajika apatiwe figo, ikiwa pale Kiteto watu wakahangaika, Mbunge mgonjwa, tatizo figo. Fikiria Mbunge ni mgonjwa, kwanza hawatarajii kwamba Mbunge anaugua.

Sasa tatizo moja kwamba Mbunge huyu ana tatizo la figo. Kwa hiyo, anatakiwa mtu akatoe figo. Kwa kabila la Kimasai, kutoa kipande kama figo, sehemu ya mwili wako kumpa mwingine ni tatizo. Kutoa damu tu ni kazi, ni bora mimi nikulipe shilingi milioni moja au pesa kiasi chochote. Sisi wagonjwa pale hospitalini, kama mtu anapungukiwa na damu tunatafuta watu wa kutoa damu kwamba wewe damu utatoa kiasi gani. Lita moja ile tunaweza kununua mpaka shilingi laki moja, laki mbili, hiyo haina shida. Sasa figo, ilikuwa kazi kubwa. Lakini kwa kudra ya Mwenyezi Mungu sisi kazi yetu ilikuwa ni kusali kwamba tunamwomba Mwenyezi Mungu atupatie mtu wa kutufaa kutupatia figo, hiyo ndiyo ilikuwa sala yetu kubwa.

Kama kijana yule alivyofanya, sasa jamaa ndiyo wakaanza kujitokeza, na kwa kawaida ya jamaa ndiyo wanaotakiwa wajitokeze katika haya mambo. Maana yake huwezi kununua mambo hayo, huwezi! Lazima uwe kidogo uwe na uhusiano. Watoto wangu wote walipimwa wakaonekana wana damu tofauti, isipokuwa wawili tu, mmoja yuko Chuo Kikuu, mwaka wa kwanza na mwingine amejifungua mtoto kwa operesheni yupo na mume wake. Baada ya pale wakaja sasa kaka yangu mkubwa, lakini sasa ana miaka 60, kwa hiyo, amechokachoka. Sasa huyu kijana wakaenda na wenzake kupimwa, walikuwa 20 akapatikana kwamba ana damu sawa sawa na yangu. Akaambiwa sasa wewe ndiyo umepatikana.

Akasema basi kama ni baba, mimi nitakwenda. Baada ya kusema hivyo ndiyo sasa akaja. Alipofika India ingawa hajui kusoma na kuandika lakini ni mjanja kweli kweli, ni mjanja ukimwona hivi basi amesafiri mpaka India kwa ndege na Wazungu na Wahindi lakini anapenya kati kati mpaka akanifikia huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kufika kule yeye akaja, baada ya kuja tukasalimiana, tunafahamiana, habari ya nyumbani akasema nimekuja kukusaidia. Tarehe 21 ndiyo tukapata wote operesheni, baada ya operesheni, naye akapata, tukabadilishiwa akanipa. Yeye baada ya siku 4 akapona na kurudi. Sasa hivi napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Abel ni

mzima, amenenepa ana ng'ombe wa kutosha. Zawadi yake ya kwanza kabisa nimempa ng'ombe 100. Hiyo si rushwa, wala nini, ni zawadi. Sasa hivi yule kijana ni sehemu ya familia ya Losurutia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa na hayo ya kuongezea. Nashukuru kwa kunipa fursa hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Nala hapa Dodoma, naomba wasimame, naona ni wale pale upande wa kushoto! Karibuni sana wanafunzi wa shule ya Nala pamoja na walimu wenu, tunawashukuru walimu kwa kuwaleta vijana kuona demokrasia ya nchi yao inavyoendeshwa karibuni sana! Tunawatakia heri katika masomo mfanye vizuri. *(Makofi)*

Tuna vijana 15 kutoka Taasisi ya *Tanzania Youth Trust Aware (TAYOA)* sijui wapo wapi wasimame tafadhali. *TAYOA* wale pale! Karibuni sana Bungeni. Tunawatakia kazi njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Waziri, Emmanuel Nchimbi, ameniomba nitangaze kuwepo kwa mgeni wake ndugu Amos Makala ambaye ni Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Vijana wa CCM. Labda ametoka.

Pia Mheshimiwa Meryce Emmanuel, ameniomba nitambue kuwepo na kuwatambulisha wageni ambao ni kaka yake anaitwa Mwesigwa Emmanuel na mkewe Mwesigwa anaita Flora Msuka. Tafadhali, wale pale, ahsante. Karibuni sana! *(Makofi)*

Matangazo mengine Waheshimiwa Wabunge, kutakuwa na kikao cha Wabunge wote wanaotoka katika mikoa inayolima zao la korosho saa 5 asubuhi yaani mara baada ya matangazo haya chumba namba 227, Jengo la Utawala. Tangazo hili limeletwa na Mheshimiwa Zainab Matitu Vulu, Katibu wa Wabunge wa Mikoa inayolima zao la korosho.

Kama mlivyotangaziwa, kwa masikitiko mwenzetu Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Rais, Mheshimiwa Bakari Mwapachu, amefiwa na mama yake mzazi. Utaratibu wa shughuli hizo nimearifiwa na *Chief Whip* ni kama ifuatavyo kwamba leo msiba unaendelea nyumbani kwa Mzee Bomani, karibu na *Sin Club Msasani* na kesho ndiyo mazishi. Kwa hiyo, kuhusu msafara wa maziko, kesho saa 9 alasiri jeneza litaondoka nyumbani kwa Mzee Bomani kupitia Msikiti wa *Al Mamri* na maziko yatakuwa saa 9.45 baada ya alasiri katika makaburi ya Kisutu, Dar es Salaam. Natangaza hili ili wenye kujaliwa kuweza kushiriki waweze kwenda kumfariji mwenzetu na kushiriki katika maziko.

Tangazo kutoka kwa Kaimu Katibu wa Umoja Wabunge Vijana, umoja huu sijui kama ni rasmi lakini leo ndiyo nausikia, basi hata hivyo, Wabunge wote wenye umri chini ya miaka 40 nadhani ni pamoja na miaka 40 pia sio kwamba 39 na chini yake, wanaombwa kukutana na Waheshimiwa Wabunge kutoka Denmark saa 6.30, Ukumbi Na. 231. Mheshimiwa Kabwe Zitto ndiyo Kaimu Katibu wa Umoja huo.

Mheshimiwa Anne Makinda, Naibu Spika, ambaye ni Mwenyekiti wa *Tanzania Women Parliamentary Group* (*TWPG)* anaomba leo saa 7mchana Waheshimiwa wanachama wa *TWPG* mkutane pale ukumbi wa Pius Msekwa.

Mheshimiwa Abdallah Kigoda, Mwenyekiti wa Wabunge wa Mkoa wa Tanga, ameomba niwafahamishe Wabunge wa Mkoa huo kwamba kutakuwa na kikao saa 7 hapo nje ya Ukumbi, inaonekana hiki ni kikao kifupi tu.

Kuna tangazo lingine la Tanzia, Mheshimiwa Waziri, Peter Msolla, Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia, alikuwa amefiwa na mdogo wake hapo Hospitali ya Muhimbili tarehe 15, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikwenda kushiriki kwenye mazishi hapo

jana. Kwa niaba yenu namtakia subira Mheshimiwa Waziri Msolla yeye na familia yote, Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi.

Waheshimiwa Wabunge leo saa 7.30 kutakuwa na kikao cha Kamati ya Kanuni za Bunge. Hiki ni kikao cha kwanza. Hii ni Kamati yangu ambayo haijakutana. Kwa hiyo, nalazimika niwataje ili wajifahamu ni akina nani. Ukiacha Spika na Naibu Spika, Wajumbe wengine wa Kamati ya Kanuni ni Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Balozi Hamisi Kagasheki, Mheshimiwa Janet Kahama, Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib, Mheshimiwa William Lukuvi, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Dr. Harisson Mwakyembe, Mheshimiwa Profesa Mwalyosi, Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, Mheshimiwa Dora Mushi, Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mheshimiwa William Shellukindo na Mheshimiwa Dr. Wilbroad Slaa, saa 7.30 Ukumbi wa Spika, kwa kikao kifupi cha Kamati ya Kanuni.

Mheshimiwa Capt. George Mkuchika, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ameniomba nitangaze kwamba Kamati ya Ulinzi na Usalama itafanya kikao chake ukumbi Na. 219, ghorofa ya pili Jengo la Utawala leo baada ya matangazo haya.

Waheshimiwa Wabunge baada ya matangazo hayo orodha yangu ya wachangiaji katika Muswada wa Barabara wa 2007 bado ni 18. Sasa ukipima shughuli zilizo mbele yetu haitawezekana hata kidogo kuendelea na mjadala huo. Kwa hiyo, nalazimika tuishie hapo na kufunga. Hakutakuwa na uchangiaji tena kwa sababu ya shughuli nyingine na Miswada ama sivyo mnaelewa kesho ndiyo mwisho kwa shughuli zile za Bunge zilizo rasmi zilizopangwa ingawa Jumatatu na Jumanne ijayo tarehe 23 na 24 tutakuwa na mjadala kuhusu mchakato wa bajeti ya Serikali kama mlivyoomba na Serikali ilivyokubali. Hivyo tuna siku moja tu na nusu sasa.

Kwa hiyo, kama nilivyosema nalazimika tuishie hapo. Kuhusu Muswada huu mtapata nafasi kubwa wakati wa Bunge la Bajeti kuchangia zaidi kuhusu masuala ya barabara. Hivyo, utaratibu ni kwamba kwa robo saa ataongea Naibu Waziri mmoja, yupo mmoja tu! Baada ya hapo nitamwita mtoa hoja Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu na tutaendelea kama kawaida kwenye Kamati.

Kuna tangazo tena hapa ambalo linabadili sura ya mambo. Kutakuwa na kikao cha *briefing* kwa Wabunge wote ambacho kitaendeshwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, saa 7.30. Kwa hiyo, shughuli nyingine zote basi zisogezwe mbele hadi baada ya *briefing.* Wale wote tuliokuwa tunakutana saa 7, sasa haitawezekena hadi baada ya *briefing* kwa sababu ni muhimu tuwe pamoja katika *briefing.*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu kwa kuleta Muswada huu Bungeni.

Mheshimiwa Spika, mimi napenda kuzungumzia barabara ya Ubena – Ngere – Kiganila – Mvuha– hadi *Kisaki Station.*

Barabara hii ya Ubena – Kiganila – Mvuha ilitolewa ahadi ya kutengenezwa kila mwaka. Ahadi hii ilitolewa na Rais wakati wa kampeni. Kama vile haitoshi imo katika hotuba yake Rais ya kushukuru kwenye uwanja wa Jamhuri, mjini Morogoro. Rais alirudia kuahidi barabara hii na daraja la Mto Ruvu pale Kigamila. Halikadhalika CCM katika ahadi za Rais nayo ikaiweka barabara hii na daraja la Mto Ruvu pale Kigamila ambapo yeye binafsi alivuka chini wakati wa kampeni.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi hii pamoja na urefu wa barabara hii (Ubena – Kigamila – Mvuha) kuwa kilometa 160 ingefaa sasa ibadilishwe hadhi na kuwa barabara ya Mkoa. Hii itaiwezesha *TANROADS* kuitengenezea na kufanya ukarabati kila wakati na kwa Bajeti ya uhakika.

Mheshimiwa Spika, narudia kumpongeza Mheshimiwa Waziri, siyo kwa hili tu bali kwa kazi nzuri kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:**Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Miundombinu Mheshimiwa Andrew Chenge, Naibu Mawaziri wake Mheshimiwa Dr. Maua Daftari na Mheshimiwa Dr. Makongoro Mahanga, Katibu Mkuu pamoja na wataalamu wa Wizara ya Miundombinu waliohusika katika kuandaa Muswada huu.

Aidha, ningependa kumpongeza Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu kwa mchango wao mzuri. Kwa jumla naunga mkono hoja na naamini utekelezaji wake mwema utachangia sana maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara za Wilaya mpya ya Mkinga ambazo zimeorodheshwa chini ya Wilaya ya Muheza katika kurasa za 133 na 134 kuna barabara ambazo hazikuorodheshwa. Barabara hizo ni pamoja na barabara kutoka Kagera Makao Makuu ya Wilaya kuunganisha na Karatano katika Tarafa ya Maramba. Barabara hiyo ni kutoka Kagera kupitia Mkinga, Magodi, Mwanyumba na Mbambakofi hadi Makufaraji barabara ya Mabokoreni - Maramba. Barabara hii muhimu, niliulizia katika swali la Bunge Na. 15 tarehe 10/04/2007 katika Mkutano wa Saba wa Bunge unaoendelea hivi sasa. Endapo barabara hii ilisababishwa kwa makosa, naomba iorodheshwe.

Mheshimiwa Spika, nyingine ni barabara kutoka Duga - Maforoni hadi Mwakikonge (Kata ya Duga), pia barabara ya Duga Sigaya hadi Kibewani (Kata ya Duga), nyingine ni Manza – Sigaya – Vibarabarni (Kata ya Manza), Gezani – Tawalani (Kata za Mkinga na Manza), Monga Vyeru – Kichalikani (Kata ya Kwale) na mwisho, Kichangani Jeye – Mwanyumba (Kata ya Gombero na Maramba).

Mheshimiwa Spika, barabara nilizoziorodhesha zipo japokuwa bado zinahitaji maboresho. Kumbukumbu zangu ni kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Muheza ilileta mapendekezo kwa Wizara ya Miundombinu ili barabara hizo ziorodheshwe pamoja na hizo nyingine. Nauri ziorodheshwe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu fidia kwa wananchi ambao ardhi zao na mali zao zilizopo katika maeneo yanayohitajika kwa ajili ya ujenzi wa barabara, nashauri sheria hii na kanuni

zake ziweke taratibu nzuri za kuwafidia wananchi hao kwa kiwango stahiki na bila kuwepo urasimu mwingi na ucheleweshaji wa malipo ya fidia.

Mheshimiwa Spika, suala la viwango katika ujenzi au ukarabati wa barabara lipewe mkazo maalumu katika utekelezaji wa sheria hii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii ya kuchangia kwa maandishi katika hoja hii pia nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri na Naibu Mawaziri wote wawili pamoja na wataalamu wote kwa kuweza kuleta Muswada huu mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, katika nchi yetu tuna tatizo kubwa sana la barabara zinazopitika hasa wakati wa mvua, Watanzania wengi hasa mikoa ya Kusini na Mikoa mingine wananchi wameteseka sana, wameshindwa kusafiri na hata kusafirisha mazao yao kwenda kwenye masoko ambayo yako nje ya mikoa yao. Tatizo hili la usafirishaji wa mazao ya wakulima nimeliona katika mkoa wa Kigoma na Rukwa pamoja na Mungu kuwajalia wakapata mazao mengi wameshindwa kujikwamua toka kwenye lindi la umaskini kwa sababu ya ubovu wa barabara zetu.

Mheshimiwa Spika, swala lingine ni utunzaji wa barabara uchimbaji wa vifusi barabarani na upitishaji wa mabomba ya maji katika barabara na kuacha bila kufukia barabara hizo ambazo baada ya muda mitaro hiyo huchimbika na kuweka mashimo makubwa na kusababisha msongamano mkubwa wa magari hasa katika jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, tunaomba swala hili litazamwe kwa umakini mkubwa wa wale wote wanaopewa kazi hizo Wizara zinazohusika ziakikishe kazi hizo. Zimefanyika kwa umakini na bila kuacha kasoro na kama mkandarasi huyu hatafanya hivyo basi asilipwe mpaka akamilishe kazi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni bodi ya barabara ya mkoa tumeona wajumbe wake naomba kusiwe na swala la siasa hasa katika wale wajumbe wasiozidi wawili Wabunge wa Viti Maalum, kuna mikoa ina Wabunge zaidi ya wanne toka vyama tofauti vya siasa, tungeomba kuwe na uwakilishi sawa mmoja akitoka chama kinachoongoza Serikali mwingine atoke upande mwingine wasije toka wote chama kimoja.

Jambo lingine ni ujenzi wa madaraja imara hivi karibu tulishuhudia kubomoka kwa madaraja mengi wakati wa mvua za vuli, sijui zitakapoanza mvua za masika itakuwaje ni vizuri kuchukua tahadhari kabla mvua hizo kuwa nyingi. ili tuweze kuwaruhusu wananchi wetu katika balaa hilo.

Mheshimiwa Spika, nashukuru tena kwa kupata nafasi hii.

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuchangia yafuatayo:-

Kuhusu ujenzi wa barabara nadhani kabla ya ujenzi kuanza ingezingatiwa kujenga kwanza mifereji ya maji ya mvua ndipo barabara inafuata, hii itasaidia kuzuia matengenezo ya mara kwa mara ambapo mvua huharibu barabara zetu na kuifanya Serikali (Halmashauri)

zitenge bajeti za matengenezo kila mwaka na hali haibadiliki na pia itapunguza matumizi ya Serikali kila mwaka.

Kuhusua barabara za mkoa wa Dar es Salaam naomba Serikali ingetoa upendeleo maalumu kwa mkoa huu wenye idadi kubwa ya watu wanaokadiriwa milioni 4, ambao wanahitaji huduma mbalimbali za kijamii kama afya, maji, uzoaji wa taka, elimu, usafiri, ulinzi na usalama na barabara uruhusiwe kutoza ushuru wa barabara *(Road Toll)* kwa baadhi ya barabara ambazo wananchi na wadau wengine watakazokubaliana katika mitaa husika.

Serikali itafute uwezekano wa kuwapata wawekezaji wa Miundombinu ya barabara waje kujenga *flying-over* na waziratibu barabara kwa kutoza fedha kwa watakaopenda kutumia barabara hizo hata kama mpango utakuwa ni wa muda mrefu ni bora Serikali ingefikiria hivyo.

Kuhusu barabara za pembeni kidogo toka katikati ya jiji la Dar es Salaam zingetengenezwa ili kupunguza msongamano wa magari. Katika maeneo yafuatayo nadhani yangestahili barabara ya Tabata Dampo/Kawawa Road kupitia Kigogo, barabara Baracuda/Nyerere Road kupitia Vingunguti, barabara ya Uhuru, barabara ya Ubungo maziwa/*Mama Land Mandela Road,* barabara ya Kigogo, Mburahati hadi Kagera *(Morogoro Road)* na barabara toka Kitunda Wilaya ya Ilala mpaka Tandika Azimio Wilaya ya Temeke. Hii itasaidia kwa kiasi kikubwa kutokana na ukweli hizi ndizo za mkato kwa kwenda katikati mwa hii na kurudi majumbani kwa baadhi ya wananchi wa mkoa huo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia yafuatayo:-

Muswada umekuja kwa wakati, utaokoa mali, watu na heshima ya nchi itajengeka. Aidha, uendeshaji vyombo vya moto na waendeshaji watafuata taratibu zilizowekwa. Nashauri Serikali, ione uwezekano wa kuweka makandarasi katika kuendesha mizani, na kuangalia barabara. Naamini, anayeangalia mizani akiwa amepewa uwakala pia wa kuangalia barabara hataruhusu kupitisha magari yaliyozidi uzito.

Mheshimiwa Spika, nyumba zilizo barabarani kabla ya Muswada na hasa ambazo zilijengwa katika viwanja vilivyopimwa na zililipiwa kodi, zimewekwa fungu gani? Nashauri wenyewe wapewe fidia na wapewe viwanja vingine na Serikali.

Kuhusu matuta ya barabarani, yawekwe kila palipo na watumiaji wengi wakiwemo wanafunzi, hospitali, mijini na maeneo ya kuabudia. Itasaidia kupunguza ajali hasa za kuua watoto. Katika jimbo langu, watoto wengi wengi wanajengwa wakienda/wakirudi toka shule.

Napendekeza barabara zinazokwenda ziwani zote na hasa zilizopo sasa, ziondolewe katika orodha ya Halmashauri/Manispaa ziwekwe kwenye orodha ya mikoa. Barabara hizi zinapofika ziwani zinaunganisha na mikoa mingine na nchi nyingine. Mfanowa Kagera,

Majimbo ya Chato, Muleba Kusini, Muleba Kaskazini, Bukoba Vijijini, Bukoba Mjini na Nkenge zina barabara zinawaunganisha na Ziwa. Ukitumia usafiri wa ziwa unafika Mwanza, Mara hata Uganda ambayo ni nchi jirani.

Mfano, barabara ya Izigo –Kyamkwikwi ina bandari ndogo ambayo Serikali inaitafutia pesa za kuiendeleza hii itakuwa kubwa kupindukia uwezo wa Wilaya kuimudu. Vile vile barabara ya Kigoma – Rwazi inaishia ziwani, iwekwe katika orodha ya mkoa.

Mfano mwingine, ni barabara ya Katoma – Kanyigo – Bukwali ambapo ni ziwani. Hii ikaendelea hadi Kashenshero. Hii iko Misenyi katika Jimbo la Nkenge, zamani ilikuwa na bandari. Hata sasa inahitaji Kivuko ambacho Wilaya haiwezi kukimudu. Naipendekeza iwe ya mkoa.

Mfano mwingine, ni barabara ya Kyela – *Itungi Port* (Ziwa Nyasa) inahudumiwa na Halmashauri. Uzoefu umeonyesha kwamba barabara ya mkoa itokayo Dar es Salaam – Kasumulu (Malawi) inapoharibika basi hata magari mazito hupitia ile ya Kyela ambayo ni Halmashauri. Ikishaharibika, basi mzigo unairudia Wilaya.

Mheshimiwa Spika, napendekeza barabara zingine zote zenye kufanana na hizo nilizotaja ziwe za mikoa na zihudumiwe moja kwa moja na mikoa.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, ninapenda kuunga mkono hoja mia kwa mia.

Muswada huu ni mzuri sana na sasa ndiyo wakati muafaka wa kuleta habari hii Bungeni. Vikao vingi tumekaa katika *Board* ya *TANROAD* kuzungumzia kupandisha hadhi ya barabara, lakini zilikuwa zinagonga ukuta, tukisubiri sheria hii. Kwa mfano sisi wananchi wa Lindi, tulizungumzia kupandisha barabara hadhi, ziwe za mkoa kama zifuatavyo:-

(a) Namichiga - Mbwemkuru – Naiwanga ambayo ilikuwa ya Wilaya tunataka iwe ya mkoa.

(b) Barabara ya Wilaya ya Nyegedi – Rondo Mandawa iwe ya Mkoa.

(c) Barabara ya Wilaya Mchinga – iwe la Mzungu Lushungi iwe ya mkoa.

(d) Barabara ya Wilaya ya Liwale – Kilimarondo – Tunduru iwe ya mkoa.

Hizi zote zinangojea Sheria hii. Kwa hiyo hii sheria ni nzuri sana. Naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, *Board* ya *TANROAD,* kifungu cha 10, tunaomba Serikali iimarishe bodi ipate pesa za bodi ili wajumbe wafanye ukaguzi wa barabara kwanza, kabla ya kikao cha bodi ili waweze kujua nini kinaendelea. Ziara ya kuona miradi ni muhimu sana kuliko kikao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu msongamano wa watu barabarani Dar es Salaam. Tumeshaona watu ni wengi sana barabarani Dar es Salaam, wakisubiri usafiri siku hizi huwezi kwenda eneo hadi eneo kwa muda mfupi. Lazima utachukua muda wa saa nyingi. Ushauri wangu ni kwamba ili kupunguza msongamano wa watu asubuhi na jioni barabarani Dar es Salaam, afadhali kuongeza usafiri wa reli ambao tayari miundombinu yake ipo. Reli zipo, mabehewa

yapo na stesheni zipo, kuna uwezekano mkubwa wa kuwachukuwa abiria wa Ubungo, Tabata, Mabibo, Buguruni,, Yombo Vituka na Tabata Reli, angalau asubuhi na jioni tu, sehemu hizo hapo juu tayari reli inapita.

Mheshimiwa Spika, Kibiti - Lindi, la mwisho ni barabara ya Kibiti Lindi kipande cha kutoka barabara ya Mkapa kwenda Kilwa, kilomita 67 tusaidie kupiga grader – kuna majambazi sana, gari ikienda polepole – majambazi huvamia.

ahsante sana naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. DR. LUKA J. SIYAME):** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono moja kwa moja hoja hii.

Kwa kujali muda, naomba nimpongeze Waziri wa Miundombinu, Naibu Mawaziri wake na watendaji wote wa Wizara hiyo.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Mbozi Magharibi lenye eneo lipatalo kilometa za mraba 6,000 na kijiografia limegawanyika katika sehemu mbili. Sehemu ya ukanda wa juu *(plateau)* yenye *trunk road* Tunduma – Lwasho yenye urefu wa kilometa 107 bila *Regional Road* yoyote. Barabara ya Kakozi – Ilonga yenye urefu wa kilometa 50.6 na inapita kwenye mpaka na nchi ya Zambia na kuungana na ile ya Jimbo la Kalambo (Rukwa) ambayo yenyewe ni ya mkoa.

Mheshimiwa Spika, barabara hii naomba ipandishwe hadhi na kuwa ya mkoa. Sehemu ya pili ya Ukanda wa Bonde la Ufa. Ukanda huu hauna *trunk road* yoyote kutokana na umuhimu wa eneo hili na hali nzuri ya ardhi kwa kilimo, ufugaji, uvuvi na misitu ya asili (pamoja na hifadhi ya msitu wa Msangano, Isalalo) iwe barabara ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, Chapwa - Chindi iendelezwe hadi Msangano - Chitete - Chilulumo - Mkulwe hadi Kamsamba kilometa zipatazo 120 na kupandishwa hadhi kuwa ya mkoa. Eneo hili kuwa takribani miezi saba kwa mwaka kati ya Novemba na Juni hakuna usafiri wa barabara na hivyo kuwa na mateso makubwa na kikwazo kikubwa kwa maendeleo ya wananchi wa Jimbo hili. Kwa kuanzia naomba kuwasilisha.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kupongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 7(1), *Establishment of Regional Roads Boards* katika Wajumbe ni muhimu wakiwemo Wabunge wa Viti Maalum maana wao ni wawakilishi wa Mikoa na hii bodi ni ya Mkoa.

Mheshimiwa Spika, katika Muswada huu kuna vyombo mbalimbali *(machinery)* mfano *Regional Road Board, TANROADS, Ministerial Advisory Board* na kadhalika. Hizi bodi wajumbe wake wamewekewa *qualification* pamoja na hizo *qualification* ni muhimu *gender* ikazingatiwa sana, maana ni rahisi sana vyombo na kadhalika hivi kukosekana wanawake ambao ndio watumiaji wazuri sana wa barabara na mazao wanayozalisha wanawake vijijini lakini hawaonekani katika vyombo hivyo.

Mheshimiwa Spika, katika kipengele cha 12(1) cha Muswada huu kunapoelezea *classes of public roads*, Muswada umesema kuna *National Roads, District Roads, Feeder*

*Road, Regional Roads* kimsingi barabara hizi ni vema zipewe maana kamili ikiwa ni pamoja na upana wake katika Muswada huu mfano *National Roads 25 metres from centre* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 51(d) ya Muswada huu *nuisance on roads* kwenye adhabu inasema; *"imprisonment for a term of one year,"* nashauri *imprisonment* iwe *for a term not exceeding two year* itegemeane na kosa isiwe *strictly one year* kama ilivyoelezwa katika kifungu 48(e) ambacho kwa maoni yangu ni sahihi sana.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia madhumuni na sababu za Muswada huu kuletwa hapa ya kwamba ile iliyokuwa ikitumika ya mwaka 1932 ilikuwa haikidhi mabadiliko ya kisera, kijamii, kiuchumi na kwamba Muswada huu utaboresha masharti kuhusu uendelezaji mtandao wa barabara nchini. Nami basi kwa niaba ya wananchi wa Iringa nikiwa Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Iringa, naunga mkono Muswada huu kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuja na Muswada huu muhimu. Nina mapendekezo matatu mafupi ambayo natumaini Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu atayazingatia.

Kwanza utekelezaji wa miradi ya barabara za mkoa unakosa usimamizi mzuri kutokana na Halmashauri kuwekwa pembeni katika zoezi zima la uteuzi wa makandarasi na usimamizi wa utekelezaji. Hilo lisahihishwe chini ya sheria mpya ya barabara.

Pili, katika Ibara ya 30; "*Protection of Environment*" inatazamia kuwepo kwa *Guidelins and Regulations.* Naomba Mheshimiwa Waziri kuwa chini ya *guidelines* au *regulations* mpya, liwekwe kipengele cha kuhakikisha kuwa vyoo vya kulipia vinajengwa kila baada ya kilometa 200 ili kuepukana na wanaume wanachanganyika na watoto vichakani ati kuchimba dawa. Kuchimba dawa ni mfano mahsusi wa Taifa kukosa ustaarabu.

Tatu, barabara ya Kyela hadi *Itungi Port* ni bandari ya Mkoa. Lakini wakati wa kipindi cha kiangazi, *Itungi Port* inajaa mchanga unaozuia meli zisitie nanga bandarini. Hivyo basi, meli zinatia nanga bandari ndogo ya Kiwira ambayo inaunganishwa na barabara ndogo ya Halmashauri kutoka barabara ya Mkoa. Barabara hiyo ndogo ya Halmashauri ya urefu wa kilometa 10 hivi, inalazimika kupitisha malori yenye uzito wa tani 15 hadi 30, yakiwa yamebeba shehena kwenda Malawi.

Mheshimiwa Spika, nafurahi kuwa Naibu Waziri wa Miundombinu, Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, alitembelea bandari zote mbili za Kiwira na Itungi na kujionea hali hiyo ya barabara. Naiomba Wizara ikipandisha kipande hicho cha barabara kwenda Kiwira kuwa barabara ya Mkoa. Aidha, fedha iliyotengwa mwaka wa fedha huu kumalizia kukarabati kwa lami, barabara ya Kyela hadi *Itungi Port,* iwe *released* mara moja ili ukarabati ukamilike.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwapongeza Waziri wa Miundombinu, Naibu Mawaziri wote wawili na watendaji wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanazofanya katika kuboresha Miundombinu Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, napongeza pia kazi nzuri na ngumu ambayo imefanywa kuandaa Muswada huu wa Sheria ya Barabara na jinsi orodha ya barabara ilivyoainishwa kwa nchi nzima. Pamoja na hayo ningependa yafanywe masahihisho katika eneo lifuatalo kwa barabara za Mkoa wa Tanga katika Wilaya ya Muheza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 64 barabara *R. 517* barabara kutoka Bombani – Kimbe jina limekosewa ni Kimbo yaani Bombani – Kimbo kilometa 7.4. Sahihisho hilo lilitolewa pia katika kikao cha bodi ya barabara Mkoa wa Tanga. Hata hivyo licha ya barabara hiyo kuishia kijiji hicho cha Kimbo, *TANROADS* Mkoa wamekuwa wakitengeneza barabara hiyo kwa kuishia kitongoji kingine kabla ya kufikia hapo Kimbo. Hili ni tatizo lililoko ndani ya Bodi ya Barabara ya Mkoa, lakini ni vema ndani ya sheria hii, lakini ni vema ndani ya sheria hii ikaeleweka na kama Wizara kwa maelezo haya sasa muweze kuishauri Bodi ya Mkoa kutengeneza barabara hiyo hadi Kimbo na kusahihisha jina kuwa Kimbo badala ya Kimbe. Hakuna Kijiji wala Kitongoji kinachoitwa Kimbe ndani ya barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya masahihisho hayo ningeomba kupata maelekezo katika maeneo yafuatayo:-

(a) Kiwango cha juu kabisa cha urefu wa Barabara ya Mkoa ni kiasi gani.

(b) Yapo maelekezo kwamba barabara za Mkoa zianzie kutoka katika mojawapo ya Barabara ya Mkoa na kuishia katika barabara nyingine ya Mkoa. Iwapo ni kweli basi ni vema zile barabara ambazo zinaonekana katika jedwali hazikutimiza vigezo hivyo zinaendelezwa ili kukidhi vigezo muhimu. Kwa mfano Barabara ya Mkoa iliyo katika Wilaya ya Muheza *R 517* inayotoka Bombani – Kimbo kilometa 7.4 inaishia katikati badala ya kutokeza ili kuungana na barabara *R 518* inayotoka Maguzoni kwenda *Old Korogwe.*

Kwanza Maguzoni ipo Muheza Kata ya Potwe na Kimbo pia iko Kata ya Potwe. Ipo barabara inayounganisha Kimbo na Maguzoni kiasi cha kilometa tano tu, lakini badala ya kipande hiki kuunganisha na *R 518* sehemu hiyo imeachwa kuwa barabara ya Wilaya. Bodi ya Barabara ya Mkoa wa Tanga ilishakubali pendekezo hilo na kuliwasilisha Wizarani (TAMISEMI na Miundombinu) lakini rekebisho hilo halipo katika orodha hii mpya. Sioni sababu za msingi kuacha kufanya marekebisho hayo sasa badala ya kungoja mpaka sheria hii itakapoanza kutekelezwa. Mheshimiwa Waziri kwa hili tunaomba ushauri wako.

Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara ya Miundombinu isaidiane na Wizara ya TAMISEMI ili kuainisha orodha ya barabara za miji na miji midogo inayopandishwa daraja kwa msingi kwamba Halmashauri kwa kutumia fedha wanazopata kwa matengenezo ya barabara za Wilaya hazitawezesha uboreshaji wa barabara zao hasa kwa viwango vya lami. Naunga mkono hoja.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia katika Muswada huu wa Barabara wa mwaka 2007. Napenda kumpongeza Waziri na Naibu Mawaziri pamoja na watendaji kwa kundaa Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, barabara ni kichocheo muhimu cha maendeleo hasa vijijini, watu wengi walipo wanapata matatizo ya usafirishaji wa mazao kutoka vijijini hadi mjini ili

ipelekwe kwenye miji mikubwa. Mara nyingi matatizo haya yanaelekezwa ni kutokana na uchache au upungufu wa pesa zilizotengwa kutengeneza barabara hiyo. Kwa mfano barabara iliyopo Moshi Vijijini Tela (Moshi) haijatengewa pesa za matengenezo takribani miaka 10 sasa, ile siyo barabara tena ni korongo. Kuna haja ya Serikali kuangalia ni jinsi gani ya kufanya au kuzuia uharibifu wa barabara ili kuzuia matengenezo makubwa. Serikali inaweza kufanya kama ilivyokuwa zamani makambi ya kutengeneza barabara yalikuwa yakiendeshwa na *Public Work Department (PWD).*

Mheshimiwa Spika, ubaya wa barabara nyingi unachangiwa pia na kuweka makandarasi ambao hawana sifa na usimamizi mbovu wa utengenezaji wa barabara hasa za vijijini ambazo hazifanywi kitaalamu. Barabara nyingi mjini hazina majina jambo ambalo wakati wa majanga kama moto, ajali ni tatizo kwa wahusika kujua maeneo ya matukio kamili. Sheria isisitize uwekaji wa majina ya barabara nchi nzima, pia ijaribu kutumia teknolojia ya sasa kwa kuhifadhi majina haya *electronically* ili yaweze kutumika na vyombo husika katika *navigator*. Nchi yetu kwa sasa tuna-*promote* utalii sana na wengi wa watalii hawa wana-*drive* kutoka Ulaya kwa kutumia *navigator* wakifika Tanzania inakuwa ni tatizo, kwanza hakuna hata majina ya barabara katika baadhi ya sehemu.

Mheshimiwa Spika, ningependa kujua Serikali inatoa vigezo gani katika kutoa majina ya barabara? Tusibadilishe majina ya barabara hata kwa zile zinazoweza kufuta historia. Kwa mfano kuna Wilaya ya Kinondoni na kuna barabara inayoitwa Kinondoni ambayo itakupeleka mpaka Kunduchi. Ukiifuta hii na kuiita Lucy, mgeni atapotea hatafika Kinondoni lakini kwa kutumia lile jina lililokuwepo atafika Kinondoni.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu matumizi/uharibifu wa barabara, kinachochangia barabara kuharibika ni pamoja na magari yenye uzito mkubwa kuliko barabara yanapita kwenye barabara hizo. Kingine kinachochangia ni pamoja na kufanya biashara katika barabara hasa sehemu za mjini, bidhaa kupangwa barabarani, hii inachangia ajali kutokea. Mfano mwendeshaji wa gari akimgonga mfanyabiashara mwenye kosa ni mwendeshaji wakati muuzaji kavunja sheria kuuza bidhaa barabarani. Pia kumekuwepo na ajali nyingi barabara kutoka Morogoro, Chalinze hadi Dar es Salaam pamoja na kupanua barabara ya Morogoro, Serikali inabidi kuangalia ni jinsi gani ya kufanya barabara ya Chalinze - Dar es Salaam iwe na *lane* nne kupunguza ajali.

Mheshimiwa Spika, Serikali ishirikiane na Halmashauri husika waongeze taa mijini. Kwa mfano mji wa Dar es Salaam *traffic lights* ziwe *upgraded* ili ziweze kukidhi idadi ya magari, tuweze kuondokana na kuweka askari barabarani kuongoza magari badala ya taa kupunguza msongamano wa magari. Kukiwa na usimamizi madhubuti wa kutengeneza zile *feeder road* hii itasaidia sana kupunguza msongamano wa mgari.

Mheshimiwa Spika, sheria/Wizara iwasiliane na mamlaka husika iangalie ni jinsi gani ya kuboresha matumizi ya *traffic* sababu barabara nyingi mikokoteni, baiskeli, wapita kwa miguu wote wanatumia sehemu moja. Iwasiliane na sheria ya *traffic* ili iweze kutengeneza njia tofauti ya baiskeli, mikokoteni na waenda kwa miguu.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa ni kuhusu elimu, pamoja na vipeperushi, vitolewe hasa kwa vijana wanaotoka mikoani kuja mjini waelewe hairuhusiwi kufanya biashara barabarani.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo naomba kuwasilisha.

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri na Naibu Waziri kwa Muswada. Naomba kusema kwamba bila barabara uchumi wa nchi yoyote inakuwa finyu kwa hiyo, Muswada huu umekuja wakati muafaka, naomba upitishwe kupitia Bunge hili na Serikali utausimamia vyema.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kwa kasi mpya, ari mpya na nguvu mpya itafute fedha kwa hali zote kuzingatia Mikoa, Wilaya, Majimbo hadi Vijiji ili tuweze kujenga barabara zetu au kuzitengeneza kwa maslahi ya Watanzania pia na Tanzania yenyewe kama nchi miongoni mwa nchi.

Mheshimiwa Spika, ikifikia barabara inayotoka kujengwa naomba sana Serikali izingatie kwanza mazingira ya miji na ikifika mtu anakaa mahali inapotaka kupita barabara na mtu mwenyewe amemiliki apewe siku zisizopungua 30 badala ya siku 14 na kwa utaratibu mzuri bila vitisho na watu au wananchi kama hawa watazamwe kwa kupata haki zao zote zinazomuhusu.

Mheshimiwa Spika, bodi zisimamie na kasma ya mikoa zipewe matumizi ya kasma kwa maslahi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Magogoni, naunga mkono hoja na Muswada huu upitishwe.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, kila mtu anaelewa umuhimu wa barabara katika maendeleo, barabara zetu zimekuwa mbovu mno na hazikarabatiwi. Lakini pia Serikali imekuwa haijengi barabara kwa uwiano wa maeneo ya nchi nzima. Hivi karibuni nilikuwa Tunduru katika uchaguzi. Kule ni hatari tupu, utadhani Mwenyezi Mungu ameiumba Tunduru mwaka 2007 na ndio wanaanza kutengeneza miundombinu. Kimsingi hakuna barabara, magari yamepinduka, Wabunge wamevamiwa na majambazi, nashukuru Mungu hawakufanyiwa lolote baya zaidi ya kupigwa kwani hapa tungekuwa tunaongea mengine.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niende kwenye Muswada wenyewe Ibara ya 7(2) kwamba Wabunge wawili kutoka Viti Maalum. Wabunge wa Viti Maalum katika mikoa yenye Wabunge koka Vyama vya Upinzani ni zaidi ya wawili au Muswada haukuzingatia Upinzani? Tunaomba uweke bayana kuwa Wabunge wawili hao mmoja awe kutoka Kambi ya Upinzani pale penye zaidi ya Mbunge mmoja wa CCM. Lakini pia ni kwa nini Wabunge wote wa Viti Maalum wasiingie kwenye *board* ya barabara wa mkoa hasa ikizingatiwa wanatoka mkoa huo?

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 12, *Classification of Roads,* katika uainishaji wa barabara hakuna barabara za miji *(Urban Road)* ambazo kwa kawaida huainishwa peke yake *(separately).* Ibara ya 12(5) kuhusu upana wa hifadhi ya barabara ni lazima upana wa eneo hili uwe *specified* na usiachiwe Waziri na watendaji wake tu. Hivi akitokea Waziri kichaa akaamua iwe mita 300 wananchi watapata hasara kiasi gani ya kubomoa? Wote tunatambua jinsi bomoa bomoa ya Ubungo mwaka 2002 ilivyogharimu watu. Bado Serikali haitaki kutoa elimu kwa wananchi waelewe mipaka yao. Lakini la kusikitisha Serikali inasubiri hadi watu wanajenga, wanakuwa na mali, zao wanaishi kwa miaka mingi ndio wanabomolewe. Hivi Serikali inakuwa wapi? Hivi Serikali inafurahi sana kuona wananchi wake wanabomolewa?

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 17 *Private Roads*. Ni lazima Ibara hii itamke wazi kwamba barabara hizi zitengewe kwenye eneo linalomilikiwa na mtu huyo. Haiwezekani *private road* iwe inapitwa na watu wengine, hii ni fujo na vurugu.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 24, *Execution of Road Work*, katika kuzuia udongo usivamie barabara. Haiwezekani wananchi watakiwe kuzuia udongo unaotembea mfano *landslide* kwa gharama zao wakati haya ni mabadiliko ya tabia ya dunia *(Earth Works).*

Hii ni kazi ya *authority* na hii ipo duniani kote, gharama za kuzuia ni kubwa mno na tufikiri watu wetu walivyo maskini na wanavyolima katika mteremko mikali iliyo karibu na barabara halafu aambiwe ajenge *earth retaining structures*.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 31, *Road Safety,* ni watu wa wapi na wa aina gani ambao wanapewa msamaha na Waziri wasipofuata alama za barabara na sababu ni zipi?

Mheshimiwa Spika, sehemu ya *IX (a), Offences*, kwa kweli *fine* ni kubwa sana hasa ikizingatiwa vipato vya Watanzania na hata hivyo ni kubwa kuliko nchi zilizoendelea kama Marekani. Pia ieleweke kuwa *fine* kubwa zinakaribisha rushwa kwa wale watendaji wapenda rushwa ambao watawatishia ili wapate rushwa. Sheria haisemi chochote kuhusu mbinu gani itakayotumika kuhakikisha kwamba gharama za uharibifu wa barabara zinazolipwa kweli zinatumika kutengeneza barabara na si vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba kujua wanaopitisha mabomba na kuacha bila kurudisha katika hali yake. Naamini wamiliki wa barabara wanalipwa kabla ya uchimbaji hiyo ni jukumu la wamiliki kuzijenga, fedha inayolipwa huenda wapi?

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu pamoja na watumishi wote wa Wizara yake. Huu ni Muswada mzuri na ni ukombozi kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kilio chao cha matatizo ya utekelezaji makini wa shughuli za ujenzi wa barabara hapa Tanzania.

(a) Ibara ya 5, 6 na 7 zinatia imani sana kwa wananchi, lakini kandarasi nyingi za barabara inatekelezwa vibaya yaani barabara hizi zinajengwa kwa kiwango cha chini sana. Pengine hubomoka baada ya miaka michache tu.

(b) Barabara za nchi nzima zinahitaji usimamizi na matengenezo ya mara kwa mara *(proactively wala sio passively).*

(c) Katika kandarasi za *TANROADS* Mikoani na zile za Wilayani (TAMISEMI) hutolewa bila kuzingatia uwezo wa makandarasi hao na mara kwa mara, barabara huonekana katika vitabu tu lakini barabara zenyewe haipo *(on the ground).* Kuna wizi mkubwa katika kandarasi hizi. Tafadhali Mheshimiwa Waziri tutafutie ufumbuzi wa *syndicate* hii ya wizi wa mali ya umma.

Mheshimiwa Spika, barabara za Rufiji, *TANROADS* mkoa iliomba barabara Na.65016, *code 65* na *class 6* ya Ikwiriri – Mloka ipandishwe daraja toka wilaya (TAMISEMI) ichukuliwe na *TANROADS* mkoa. Hakika barabara hii ni ndefu kilometa 99, ndio njia kuu inayotumiwa na watalii waendao Mbuga za Hifadhi ya *Selous* pamoja na

wafanyabiashara wote na ni barabara hii yaani Ikwiriri – Mloka inaunganisha na barabara iendayo Vikumburu – Chole – Kisarawe – Kibaha (Makao Makuu ya Mkoa wa Pwani).

Mheshimiwa Spika, barabara hii inakidhi sifa zilizotolewa katika Muswada huu kifungu cha 3(b). Kwa hiyo, naomba barabara Na. 65016 yaani Ikwiriri – Mloka ya kilometa 99 ipandishwe hadhi na kuwa Barabara ya Mkoa.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya Muswada huu umesahau kuingiza *feeder roads* ya Jimbo la Rufiji yaani barabara ya Kikobo – Tausi – Nyamwage – Utete, barabara ya Utunge – Siasa – Utete. Barabara hizi ni muhimu sana katika jimbo langu.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, Mungu aibariki Wizara ya Miundombinu.

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba nimechangia kwa maongezi hapa Bungeni, kwa sababu ya umuhimu wa swala hili nimeona niongeze kwa kuchangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Omuge Korongo – Kigarama – Murongo na kwenda Uganda (Na. 181004 – 181: P.64 ya jedwali): urefu wa kilometa 105 (Mkoa unasema ni kilometa 124) inahudumiwa na Halmashauri. Tunaomba ipandishwe daraja kuwa *Regional Road*. Ilishaombewa na Mkoa tangu zamani, nikichangia bajeti mwaka jana Waziri alinipa matumaini makubwa, barabara hii inakidhi vigezo kwani inaunganisha nchi yetu na Uganda na barabara hii ni ndefu mno, katika jedwali lote ni Wilaya nne tu ambazo Halmashari zake zinahudumia barabara zenye urefu wa zaidi ya kilometa 100 kwa barabara moja. Wilaya hizo ni Kilwa, Igunga, Simanjiro na Karagwe.

Ni dhahiri sisi ni muhimu barabara hizi ndefu ziangaliwe. Urefu wa zaidi ya kilometa 105, ni barabara muhimu kwa ulinzi mpakani na Uganda na ni muhimu kiuchumi, soko kubwa la wananchi wa maeneo haya ni Uganda. Tunaweza ku-*export punishable products* nyingi kwenda Uganda. Lakini haiwezekani wananchi wabebe kichwani.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kimsingi, barabara zote zenye urefu wa kilometa 100 *as a rule,* zisiachiwe Halmashauri, ni ndefu mno na ni mzigo kwa Halmashauri, zinafanya Halmashauri isihudumie vizuri barabara nyingine zinazostahili. Naambatanisha vielelezo ili kukazia suala hili.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kigarama – Mabira – Kyera (Na. 181005 – 181: P.64 ya jedwali), urefu kilometa 49 inahudumiwa na Halmashauri. Tunaomba ipandishwe daraja na kuwa *Regional Road*.

Mheshimiwa Spika, ilishaombewa na Mkoa, nikichangia bajeti mwaka jana Waziri alinipa matumaini makubwa, inaunganisha barabara tajwa hapo juu katika Na.1 na *Regional Road* ya Kyaka – Bugene – Nkwenda – Kaisho – Murongo kwenda Uganda. Barabara hii ni ndefu, hasa kwa sababu ziko barabara nyingine za urefu wa kati sababu ya ukubwa wa wilaya na taarifa ya barabara hii ni ngumu, vilima na mimawe, inahitaji utaalamu zaidi.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kyaka – Bugene – Kyanyamisa – Kasulo, urefu ni kilometa 180, hii ni *Regional Road.* Tunaomba itengenezwe kwa kiwango cha lami.Hii ni

ahadi ya Mheshimiwa Rais, inaunganisha Tanzania na Rwanda na Burundi, ni muhimu sana kwa uchumi, itazidi kutuwezesha ku-*export* kwenda nchi za Rwanda na Burundi. Wilaya ya Karagwe inaweza kufanya biashara kubwa kwa kuuzia nchi za Rwanda na Burundi mazao mengi ya kilimo na mifugo.

Mheshimiwa Spika, namuomba Mheshimiwa Waziri aongeze vyanzo vya mapato (kodi *levy on fuel)* mbona magari mengi? Tukusanye kwa asilimia mia moja ya *requirement* yetu, tuwe na barabara.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa matumaini makubwa.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, kabla ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Andrew Chenge na wasaidizi wake wote kwa niaba ya Serikali kwa kuileta sheria hii muhimu sana kwa maendeleo ya nchi hii. Naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia.

Mheshimiwa Spika, pamoja na sheria kuwa nzuri, lakini bila kuwa na fedha zetu wenyewe za kutengeneza barabara zetu, hatutaweza kuitekeleza Ilani ya CCM ya mwaka 2005 hadi 2010. Dira hii ya Ilani ni budi iendane na maandalizi ya utekelezaji wa Sheria hii.

Moja ya barabara zilizooanishwa katika Ilani hiyo ni pamoja na Tunduma-Sumbawanga, ambayo ningeomba kwa dhati Serikali sasa ituambie nini mipango ya Serikali katika kutekeleza maagizo hayo ya msingi katika kuendeleza Mikoa ya Kanda ya Kusini Magharibi.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikai kwa kuweka kipengele cha kutoa fidia kwa wale watakaoathirika na ujenzi wa barabara. Lakini ni vizuri tahadhari ikawekwa ili masharti yatakayotumika katika kutoa fidia hizo yasije yakatumika vibaya na wajanja wachache.

Mheshimiwa Spika, mpango wa barabara wa Afrika ya Mashariki unaonyesha kuwa barabara ya Tunduma hadi Kigoma na Nyakanazi – imepewa kipaumbele cha tano. Je, hali hii inaashiria nini katika hali ya barabara zilizoachwa kwa miaka mingi bila kushughulikiwa? Kwa nini basi, barabara hizi zipewe umuhimu wa kwanza ni sisi wenyewe Watanzania? Tuanze na mipango yetu wenyewe kupanga ni kuchagua, kuchagua ni kutangulia. Hii ina maana vianzo vingine vitafutwe ili tuweze kufikia azma yetu hiyo.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii itaendelea kulaumiwa kwa kuwa haijatengewa fedha za barabara za kutosha na ni matumaini yetu sisi Wabunge kuitaka Serikali iongeze fungu la fedha kwa kuona maeneo mbalimbali ya kodi hasa kwa upande wa tozo ya mafuta kwa kila lita.

Hifadhi ya barabara kwa sasa bado ni ndogo kwa maendeleo ya baadaye. Kuweka mita 50 hazitoshi kwa mipango yetu ya baadaye. Waziri mhusika aone uwezekano wa kuongeza kiwango hicho kwenye kanuni zake. Pia tunashauri Waziri aone namna ya kuanzisha kambi za kusiamia utengenezaji na ukarabati wa barabara kwenye barabara kuu zote muhimu, hasa zile za udongo.

Mheshimiwa Waziri, aone uwezekano wa jinsi ya kusaidia makandarasi wazalendo ili kuwawezesha ili baadaye waweze kuingia mikataba mikubwa ya ujenzi wa barabara kuu za humu ndani na nje ya nchi. Uamuzi wa makusudi wa kuwawezesha wazalendo wetu,

utakaosaidia kuwaimarisha kiuchumi na kiutaalamu ili washindane na wageni na hivyo fedha nyingi za kigeni kubakia nchini.

Mheshimiwa Spika, mimi ni shabiki wa kuiomba Serikali itumie utaratibu wa kuwashirikisha *Private Public Partiners* katika miradi ya barabara hasa kwenye miji yenye msongamano wa magari. Lakini kwa nini Waziri asilieze Bunge na wananchi, kwa nini Serikali inaona uzito wa suala lenyewe? Je, ni nchi ipi katika Afrika ambayo inatumia ujenzi kwa utaratibu huo? Naunga mkono hoja hii.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Spika, barabara kuu ya Dar es Salaam-Morogoro kuna *accident* nyingi zinazotokea katika barabara hii katika eneo la Mailimoja, daraja la Mpigi na Visiga (Kibaha Mjini).

Mheshimiwa Spika, kuna mitaa ambayo *accident* zinatokea nyingi. Mitaa hii ni Mailimoja na Kongowe. Kinachotisha zaidi ni *accident* za watoto wa shule wanapokatisha barabara. Ombi langu tumekewa vidhibiti mwendo *(Road Bumps),* madereva hawasikii au kuelewa ishara za barabara. Maisha ya watu wanateketea. Pia naomba ishara za barabara hasa barabara kuu ziweke juu kama Ulaya.

Mheshimiwa Spika, namuomba Waziri wa Mindombinu aje Mailimoja, Kibaha. Wananchi wa eneo hili wana kilio cha upana wa *road reserve* katika eneo lao badala ya kuwa futi 75 kama ilivyo kwa barabara kuu nyingi, kwa Mailimoja *road reserve* ni upana wa mita 225. Wananchi wanasikitika kukosa maelezo mazuri kwa viongozi wao wa Wilaya na Mkoa, sasa wanamtaka Waziri aje. Familia karibu 600 zitaathirika katika kubomolewa. Wengi wamepimiwa viwanja katika eneo la *road reserve* na kupewa hati. Tarehe 24/10/04 wana Mailimoja wapatao 59 walikutana katika hoteli ya Njuweni kuzungumzia suala hili la upana wa *road reserve* Mailimoja, je, upana huu uliwekwa kwa lengo/madhumuni gani?

Mimi kama Mbunge naamini kuna sababu nzuri ya kuendeleza jimbo la Kibaha Mjini, ila na mimi Mbunge siijui na mimi naungana nao ututembelee, uje kutuelimisha. Ni ukweli usiofichika suala likizungumzwa na mgeni linakubalika zaidi kuliko mtu ambaye yuko nao kila siku.

Kuhusu fidia, naomba fidia ya halali itakayotolewa kwa kutengeneza barabara, ilingane na thamani ya shilingi iliyopo wakati huo.

Mheshimiwa Spika, magari yanayosimama Mbezi Luisi katika barabara ya Dar es Salaam - Morogoro. Ombi kama ni lazima magari makubwa yasimame sehemu hiyo, tunaomba barabara hiyo ipanuliwe magari yanayopita sehemu hiyo yanaendeshwa kwa wasiwasi kwa sababu barabara inakuwa nyembamba, magari kupishana kuna uwezekano kupata *accident* mbaya sana.

Mheshimiwa Spika, makandarasi wanaojenga barabara pesa nyingi za Serikali zinatumiwa vibaya au kwa fujo *(value for money)* naomba tuweke kwenye sheria kila baada ya barabara kutengenezwa zifanyiwe *audit.* Ni ukweli usiofichika kwamba barabara hasa za Wilaya na za Halmashauri zinajengwa chini ya kiwango. Makandarasi watakaojenga barabara yoyote ile na hasa zile za Mkoa, Wilaya/Hamashauri asipewe tenda mpaka bodi ya makandarasi wamemthibitisha. Hii ningeomba iwekwe kwenye sheria.

Mheshimiwa Spika, ombi la mwisho, tunaiomba Wizara tushirikiane na Jimbo la Kibaha Mjini kupanga mji. Tayari tunaandaa mkutano na wadau mbalimbali ili kufanya mji wetu uwe wa kisasa. Tuwe na barabara nzuri na za kitaalamu. Kibaha bado haijavamiwa na ni sehemu ndogo watu waishi kwenye *shant town.* Naamini Waziri na Wizara yake tutaungana nayo katika kufanya mji wa Kibaha kuwa wa kisasa.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kuunga mkono hoja kwa vile Muswada huu ni muhimu sana kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii pamoja na maelezo hayo, japo nimekwisha kuwasiliana na Mheshimiwa Waziri narudia kuwa kwa vile wakati Wizara ya Miundombinu na TAMISEMI watakapokaa sisi hatutakuwepo; na kwa kutekeleza kifungu cha 11(1) na (2) ni vema Waziri akazingatia pia maombi ya *Road Boards* za Mikoa husika; matamko ya Serikali kuhusu ahadi ya kupandisha barabara wakati Muswada wa *Roads Bill* unapowasilishwa Bungeni kuweka uzito wa hili ni maombi ya siku nyingi ya barabara ya Njiapanda au Oldeani Jct hadi Qanded – Matala kuwa barabara ya mkoa chini ya *TANROADS.*

Hii ni utekelezaji wa ahadi ya Rais wa awamu ya tatu na sasa Rais wa awamu ya nne pia. Umuhimu wa barabara hii nimekwisha kumwandikia Mheshimiwa Waziri. Waziri anihakikishie ni lini kazi hiyo itafanyika ili tuwe na uhakika.

Mheshimiwa Spika, ni imani yangu pia kuwa barabara ya Manyara *(Trunk Road)* – Kambi ya Simba, Slatitiamo – *Upper Kitete* – Lositete hadi Selela (Monduli) itaingizwa kwenye utaratibu wa barabara za mkoa chini ya *TANROADS.* Barabara hii inaunganisha Wilaya ya Karatu na Wilaya ya Monduli. Mazingira muhimu ya wananchi wa Lositete ambao ni kama wako kisiwani baada ya kuzungukwa na msitu wa Ngorongoro yatakuwa yameshughulikiwa hasa ikizingatiwa kuwa eneo la Lositete ni muhimu sana kwa kilimo cha ngano.

Kwa kuwa Serikali imeshafanya *pre-feasibility study* kwa barabara ya Oldeani Jct – Qanded – Matala Mkoa wa Arusha hadi Lalago Mkoa wa Shinyanga na kuweka *beacons* na kwa kuwa Serikali ilitoa taarifa hapa Bungeni kuwa sasa Serikali inatafuta mhisani wa kufadhili barabara hii, na kwa kuwa barabara hii haikuonekana katika *budget speech* za miaka mitatu hivi na sasa haiko kwenye *schedules* za Muswada, ni vema Waziri akalieleza Bunge hili hatma ya barabara hii.

Mheshimiwa Spika, ni imani yangu kuwa Waziri atatoa ufafanuzi nilioomba na hasa kulieleza Bunge hili ni lini atakaa na TAMISEMI ili kupandisha hadhi barabara nilizoomba na mamlaka husika siku nyingi, ikiwa ni pamoja na barabara ya Oldeani Jct – Qanded – Matala katika Wilaya ya Karatu.

**MHE. USSI AME PANDU:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majukumu mengi aliyonayo Mheshimiwa Waziri, nachukua nafasi hii kukumbusha kilio changu cha ujenzi wa barabara Amani-Mtoni Zanzibar. Ahadi hiyo aliahidi Rais Mstaafu wa awamu ya tatu wakati wa kampeni za uchaguzi.

Mheshimimiwa Waziri Mkuu kwa kushirikiana na Mheshimiwa Dr. Hussein Mwinyi, aliniomba kufuta suala hilo ndani ya Bunge na mimi nikafanya hivyo. Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa heshima naomba kukumbusha utekelezaji wake. Mheshimiwa Waziri Mkuu nakutakia kila la kheri. Ahsante.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia Muswada wa barabara wa mwaka 2007 kama ifuatavyo:-

Naomba nilete mchango wa kwa lugha ya Kiingereza kutokana na maneno mengi katika Muswada huu kukosa tafsiri ya Kiswahili.

*Section 3,Centre of the Road, the existing definition has to be amplified to include multi carriage way roads, the present definition suffices only for a single carriage way road.*

*Mheshimiwa Spika, Road Furniture, the definition be rephrased as folows:- includes traffic lights, sign posts and traffic signs that provide information to road users, fences and guard rails. The terms Road Reserve and Right of Way, need not be defined. Trunck Roads need not be defined hence be deleted as the term is defined in section 12(2).*

Mheshimiwa Spika, *Regional Board roads need not be defined.*

*Part II, section 4(e), Road Management, this section should be rephrased to read: To formulate appropriate policies and frameworkd where necessary for the involvement of the private sector in development, maintenance and managtement of roads.*

*Section 5(3) and (4), the term public officer appearing in the second line of sub section (3) and in line two and three of sub section (4) be replaced by the term public institutgion.*

*Delegation of the powers or functions of the Road Aluthority to a public officer might bring about confusion in the management of road. I prefer the term public institutions bearing in mind that public institutions like TANAPA are currently managing some roads.*

*Section 6(2)(g), I propose the deletion of the term vehicle appearing in line one as it limits the powers of the road authority to vehicle use only. The Road Authority should have powers to control usages of roads in general. I also propose the addition of the following sentence after the term country at the end of the sentence including axle load control, and issuance of exemptions or permit where necessary.*

*Section 6(2)(i), add the term establish before the twem maintain, delete the term the before the term road and ass s at the end of the term system. Section 7, I propose that the composition of the Regional Roads Board should be reviewed and the number of the members be reduced. The Board should retain the members appearing in section 7(2) from (a) to (f).*

*The ones appearing from (g) to (j) are the executors of the regional road program, they should therefore appear before the Board as invitees where required to submit their implementation reports and receive guidance from the Board. Being members of the Board brings conflict of interest in their two roles one being a member of the Board and the other an implementer of the programme set out by the Board.*

*Further to the above the composition of the Board should be confined to the 4the Schedule. At present it appears in both, in the main ACT under section 7 and in schedules, this is uncommon. Also sources of funding the activities of the Board should be defined.*

*Section 8, add the following sentence after the term established in line with the national roads investment and development programme.*

*Section 9, the purpose of this section is not clear. If the intended purpose is to confer full autonomy of TANROADS, then retaining the Ministerial Advisory Board for TANROADS will defeat the purpose. I propose therefore lthe term Ministerial Advisory Board be replaced by the term Management Board.*

*The composition of the members of the Management Board is proposed to be as follows:-*

*(a) A Chairman, who shall be appointed by the President from amongst persons outside the public service.*

*(b) Not more than eight members appointed by the Minister from Sectors, institutions or associations as follows:-*

*(i) One representative from the road transporters associations*
*(ii) One representative from associations concerned with development and upkeep of roads and travelling public.*
*(iii) One representative from associations representing commcerce industries and agriculture.*
*(iv) One representative from an academic institution with interest in the roads sector.*
*(v) One representative from the Ministry Responsible for Finance*
*(vi) One representative from the Attorney General's Chambers.*
*(vii) One representative from the Roads Fund Board*
*(viii) One representative from the Ministry reposible for Roads.*

*In the alternative, I propose that TANROADS autonomy be a matter of another law all together where details of its functions, structure and management will be specified as is the case with other authorities e.g. TPA, TCCA, TAA to mention a few. Section 9 can therefore lbe removed from the Bill.*

*Section 10, this section is not clear. The intended functions listed as functions of TANROADS Ministerial Advisory Board appear to be more of the activities of TANROADS. I therefore propose the list of the functions of the management Board as follows:-*

*(i) Receive strategic policy/objectives from the Minister,*
*(ii) Approve organizational structure/employment conditions for the agency.*
*(iii) Approve internal policies and procedures,*
*(iv) Approve work programme*
*(v) Monitor agency performance*
*(vi) Enter into agreements with other agencies.*

*Part III, road classification and declaration, section 12, I propose the following wording to be contained in this section. Classes of Public roads, 12(1) the public road network in Mainland Tanzania is hereby clasified as national roads, district roads and urban roads.*

*The national roads shall include a truck road which is primarily national or international through route that, directly links two or more regional headquarters, or links headquaters and another major or important city or town or major port or border post.*

*A regional road which is a secondary natinal road that connects a trunk road and a district headquarters, a reginal headquarters and a distric headquarters, a trunk road and a trunk road, a trunk road and an important socio-economic centre and arterial roads within the urban centre carrying through traffic which predominantly originates from and is destined to outside the town/Municipality?city and links with either regional or a truck road.*

*The District road shall include a road linking:-*

*(i) a district headquarters and a division centre*
*(ii) a division centre and a division centre*
*(iii) a divisin centre and a ward centre*
*(iv) a ward centre and a village centre*
*(v) a village centre and a village centre*
*(vi) a village headquarters and an important socio-economic centre.*

*The Urban roads shall include collector roads which form the link between the arterial roads and the roads within the environmental areas and collect/distribute traffice between the residential, industrial and principal business districts of the town. Local colector roads which form the link between collector and access roads, and collect and distribute traffice within the residential, industrial and principal business district of the town.*

Mheshimiwa Spika, *access roads which give direct accesss to buildings/plots and lands within environmental areas and include residential streets and all other motorable roads.*

*Honourable Speaker, Part V, road safety, Section 31, add the term and marking after the term signs where it appears in sub section (1) (2) and (3) of this section. Add a new section with the following contents:-*

*(1) Road signs and markings shall be prescribed in the Regulations, sub section (4) be renumbers as (5) accordingly.*
*Part IX, offences, penalties and recovery, section 54(1) and (2), add the following term or road furniture after the term road in line one of sub section (1) and in line two of sub section (2).*

*Honourable Speaker, may I plead to the Government to declare some of Karagwe District Roads as Regional Roads because of their length.*

1. *Omugakkorongo-Kigarama-Murango (105.8 km)*
2. *Nyakasimbi-Nyakaiga-Nyabiyonza (27.1 km)*
3. *Kakiro-Rwakiro-Rwambouzi (21 km)*
4. *Rubina-Bukangara-Bisheshe (16.7 km)*
5. *Katoju-Ihembe-Kilobe (19 km)*
6. *Kigarama-Mabira-Kyerwa (49.3 km)*

*Honourable Speaker, with this interventin I believe Karagwe District Council will be relieved the burden and concentrate to other shorter roads. Humbly submitted. I support the motion accordingly.*

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri, Mheshimiwa Andrew Chenge na Naibu wake Mheshimiwa Dr. Milton Makongoro Mahanga, Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, kadhalika nawapongeza watendaji wote wa Wizara chini ya Katibu Mkuu kwa kuandaa Muswada huu muhimu. Pia niipongeze Serikali kwa kazi nzuri ya kutengeneza barabara nyakati za mvua. Barabara ni kiungo muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu hasa katika kuwaletea uchumi bora wananchi na hata kuondokana na umaskini.

Mheshimiwa Spika, ni wajibu wetu sasa kuangalia kwa umakini juu ya hali halisi ya miundombinu yetu hususan barabara. Sheria ya kuzilinda na uhakika wa matengenezo kutafanya pawepo mabadiliko makubwa katika sekta hii muhimu kama inavyojulikana kwamba barabara ni siasa.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kwa kifupi nizungumzie yaliyomo kwenye Muswada na marekebisho yake *(schedule of amendments)* kifungu cha 7(2) pamoja na mabadiliko yake kipengele l(a) kimemtaja Mwenyekiti wa Bodi ambaye ni Mkuu wa Mkoa, kifungu hiki hakuna tatizo lakini kifungu (h) kinawazungumzia Meneja wa Mkoa wa *TANROAD* ambaye ndiye anayestahili awe Katibu wa Bodi na wala sio vinginevyo. Vile vile sheria itaje Mwenyekiti Msaidizi huyu atokane na Wabunge kwa wao kuchaguana.

Kifungu cha (8) pia *TANROAD* iwe mshauri Mkuu wa barabara zote za Wilaya. Nimeona jedwali la mtandao wa barabara za Kitaifa Kimkoa, Kiwilaya na zile za Vijijini. Yapo mapungufu makubwa katika barabara za jimbo la Iramba Magharibi, barabara ya Shelui – Mtoa – Mtekente hadi Ndago barabara hii kwa nini isipewe hadhi ya Mkoa? Inao wakazi zaidi ya 70,000 na mara nyingi magari makubwa hupita huko baada ya kukwama mlima Sekenke.

Barabara za Wilaya ziingizwe, Kiomboi-Ruruma-Sheti-Uwanze hadi Kinampanda, Kibaya-Luzikukuku (Kata ya Ndogo) na Ufungu-Msai-Malendi.

Mheshimiwa Spika, sheria na elimu itolewe kwa wananchi ili kutojenga ndani ya mipaka ya barabara. Matengenezo ya barabara zile za changarawe uwe wa mara kwa mara. Wakati tunapitisha Muswada huu Serikali itimize ahadi yake ya kukamilisha barabara ya Dodoma – Singida – Shelui kwa kiwango cha lami. wajenzi *(Contractors)* wanaojenga barabara zetu lazima ziwe na ubora wenye viwango vilivyotakiwa. Alama za usalama barabarani zipewe vipaumbele na lazima zitunzwe na mamlaka sheria kali zichukuliwe kwa wanaozihujumu.

Mhesihmiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiaw Spika, naunga mkono hoja hii kwa ujumla, hata hivyo naomba nielekeze mchango wangu sehemu ya tisa.

Mheshimiwa Spika, *Part IX, offences: penalties and recovery,* aya ya 52 nashauri barabara ikishatengenezwa kusiwe na ruhusa yoyote ya kuikata barabara hiyo kwa ajili ya

kupitisha mabomba na nyaya mbalimbali. Sehemu nyingi zilizokatwa kwa ajili ya mabomba ya maji, zimekuwa ndiyo chanzo cha uharibifu wa barabara yote hasa barabara ya Mbeya-Makongolosi. Badala yake ujenzi uwe na *tunnels* au kalvati mahususi za kupitisha nyaya na mabomba.

**MHE. ZUBEIR ALI MAULID:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kutoa rambirambi kwa wale wote waliotangulia mbele ya haki. Mungu atazilaza pema roho za marehemu. Vile vile nitumie nafasi hii kuwapongeza Wabunge wapya walioapa ndani ya Bunge hili Tukufu.

Napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Mawaziri wote kwa pamoja kwa Muswada huu muhimu sana kwa Taifa. Barabara kama walivyochangia wengi ni uti wa mgongo wa uchumi wa Taifa lolote duniani. Kwa namna moja au nyingine barabara inaamua hata bei za baadhi ya bhidhaa au huduma. Barabara nzuri daima inashusha bei ya vitu kutokana na urahisi na wepesi wa kusafirisha bidhaa au kutoa huduma husika. Kwa hivyo, Muswada huu ni hatua moja muhimu ya kuelekea kwenye azma ya Serikali ya kumuondolea mnyonge ukali wa maisha na hatimaye kuelekea kwenye maisha bora kwa kila Mtanzania. Kutokana na ukweli huu basi sina budi kutamka kwamba naunga mkono Muswada huu kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga kwangu mkono, naomba nichangie mambo machache. Kwanza kabisa, Serikali ianzishe utaratibu wa kuwaelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa barabara inazotumia fedha nyingi kuzijenga.

Hili ni muhimu ili kuwe na matumizi bora na ya usalama katika hizi barabara. Mambo kama ya ujenzi kando kando ya barabara, masuala ya kuchimba mitaro ya makusudi ili kuvusha huduma kama za maji bila ya kuishirikisha Serikali, mambo ya kumwaga mafuta *(oils, diesels, parafin)* kwenye barabara zilizojengwa kwa lami na mambo mengi ambayo yanachangia uharibifu wa barabara.

Suala lingine ni suala la Serikali yenyewe kuweka na kuwaelimisha watumiaji na wananchi umuhimu wa alama za barabarani. Hili ni muhimu kwa sababu linampa dereva na mtumiaji mwingine wa barabara hadhari ya hali ya barabara na kinachofuata mbele.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni suala la mwendo upi dereva aende wapi *(speed limits).* Mwendo wa kasi ni hatari sana, lakini haina maana kwamba sehemu zote za barabara huwezi kuendesha gari mwendo wa kasi. Sasa sheria ieleze wazi suala la *speed limits.* Waswahili husema kawia ufike, sawa lakini kwa ukubwa wa nchi hii ulivyo na matatizo ya baadhi ya maeneo hasa tatizo la ujambazi kwa kweli maeneo kama hayo kwa usalama wa dereva na abiria basi wanahitajika wakaze mwendo kidogo. Sasa Serikali i-*define* wapi mwendo uwe upi.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema kwamba mimi binafsi jimbo langu la uchaguzi liko upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano ambako Sheria hii haigusi moja kwa moja. Hata hivyo napenda nikumbushie ahadi aliyoitoa Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa aliyoitoa Zanzibar wakati akifungua barabara ya Amani-Mtoni-Zanzibar. Barabara hii ni barabara ya *dual carriage* ambapo Mheshimiwa Rais Mstaafu aliahidi eneo hilo kulijenga kwa kiwango cha lami upande wa pili alipokuwa akifungua sehemu ya kwanza ya barabara hii. Barabara hii ni fupi haifiki hata

kilometa 5. Mheshimiwa Waziri ataitekeleza lini ahadi hii ndogo japo kwa ushirikiano na SMZ? Naomba Mheshimiwa Waziri suala hili aliangalie.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema naunga mkono Muswada huu kwa asilimia mia moja.

**MHE. IDDI M. AZZAN:** Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono hoja hii naomba nisisitize baadhi ya mambo, sheria hii ni nzuri sana isipokuwa kuna haja kubwa sana kutoa elimu juu ya sheria hizi kwa wadau/wananchi wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, pamoja na elimu kwa wananchi kuhusu sheria hizi ni vyema na Wizara ya Usalama wa Raia kupitia Jeshi lake la Polisi wa Usalama barabarani kushirikishwa kwa kina katika kusimamia sheria hizi.

Mheshimiwa Spika, barabara kuu kuwe na timu maalumu ya kuzikagua kila siku ili kubaini uharibifu unaofanyika kila siku hasa kwa wanaotengeneza magari barabarani yanapoharibika na kumwaga mafuta barabarani *(diesel, oil* na kadhalika) ambayo yanaharibu sana barabara. Kuwe na vituo maalum vitakavyopokea taarifa za uharibifu toka kwa wananchi. Madereva wanaohitaji leseni mpya iwe ni lazima wawe wamejifunza udereva katika shule/vyuo vinavyotambulika ili tupate madereva ambao watazijua sheria hizi na kuzifuata. Vyuo/shule za udereva wahamasishwe kufundisha sheria hizi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, sheria hizi zitafsiriwe ili ziwe katika lugha ya Kiswahili.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Spika, kulingana na maana ya *Regional Roads* katika Muswada huu, maana yake barabara za pili Kitaifa *(2nd National Roads)* ambazo zinaunganisha 12(3)(a) *A trunk Road and District or Regional Headquarter* (zinazounganisha barabara kuu na makao makuu ya Wilaya au Mkoa. 12(3)(c) Inayounganisha barabara kuu hadi barabara kuu nyingine.

Mheshimiwa Spika, nimeacha maana ya kipengele *Regional Road* Kifungu 12(3)(b) kwa kuwa barabara ninayotoka kuieleza haiingie katika maana hiyo. Barabara ninayotaka kuizungumza ni barabara ya *TAMCO* Mapinga yenye kilometa 23 inakidhi masharti yakuwa barabara ya Mkoa, kwa maana kipengele 12(3)(a) na (c) maana kifungu (a) barababa inaunganisha Makao Makuu ya Mkoa wa Pwani na Makao Makuu Kibaha na barabara kuu ya kutoka Dar es Salaam kwenda Bagamoyo na pia inakidhi kwa maana ya kifungu (c).

Mheshimiwa Spika, kutoka barabara kuu hadi barabara kuu nyingine barabara ya *TAMCO,* Mapinga kilometa 23 inatoka barabara kuu ya Dar es Salaam – Morogoro kwa maana hiyo barabara hii ya *TAMCO* Mapinga yenye urefu wa kilometa 23 inakidhi kupandishwa daraja na kuwa barabara ya Mkoa.

Je, Mheshimiwa Spika, Serikali itatamka hivi sasa au ikaingizwa hivi sasa kuwa barabara ya Mkoa, badala ya kuwa ya Halmashauri?

Umuhimu wa barabara ni njia fupi kwa wote wanaotumia barabara ya Dar es Salaam – Morogoro kwenda Jimbo la Kawe au Kinondoni na hata kwenda *Sea View* Jimbo la Ilala. Pia watu wanaotoka Dar es Salaam kuja Kibaha na hata kwenda Morogoro pia inapunguza

msongamano unaotokea eneo la Ubungo kwa saa za asubuhi na jioni. Barabara hii mara nyingi imetumika inaptokea accident na kufunga njia baada ya *TAMCO* kwenda Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, katika *schedules* kuna kitu kimeandikwa *Road Class (Rd Class)*. Barabara zilizoorodheshwa, zimepewa daraja *(class)* kwa kutumia namba mfano, 3,4,6. Je, Mheshimiwa Waziri atatufafanulia hizo namba zina maana gani?

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, mimi napenda kutoa maoni yangu kwanza na kuwapongeza sana Wizara hii kwa Muswada huu na naunga mkono lakini napenda niongezee mambo mawili kuhusu wakandarasi wanaopewa ujenzi wa barabara hatujui wana matatizo gani wote wana tabia moja ya kutomaliza kazi yao sijui ni kwa sababu gani wanaanza kuchimba chimba mashimo nusu nusu jambo ambalo linaleta matatizo mengi sana kwenye barabara zetu.

Kwa mfano, majambazi kwa sababu magari yanakwenda pole pole sana dereva anashindwa kwenda *speed,* inabidi aende anakwepa mashimo kwa mfano kama sisi tulipotekwa barabara hii ya Ikwiriri barabara ina mashimo mengi sana

Barabara ya Singida nilipita kipindi cha mvua nyingi kwenye mto Msisi, mkandarasi aliyebomoa Daraja la Kabura hajaandaa daraja lingine, tulipata shida sana mpaka tulianza sisi wenyewe kubeba mawe na kupanga kwenye mto ili tupite lingine wanamwaga vifusi kwa muda mrefu bila kusambazwa zinasababisha ajali nyingi sana unakuta kipande kidogo sana. Lakini kinakaa hivyo hivyo kwa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Spik,a halafu naomba kujua swala la vyombo vya majini Sheria inayozuia baiskeli kubeba abiria isizuie mitumbwi inabeba abiria, kwa sababu hiyo yote na Miundombinu. Naomba kwenye Bajeti inayokuja barabara za Mkoa wa Kagera za kwenda kwenye Mikoa kwa sababu barabara zote ni mbaya sana tena sana. Chonde chonde Waziri naomba msaada wa Wizara yako utusaidie sisi tunaotoka huku kwenda kwenye Majimbo. Ahsanteni.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, hongera sana kwa kazi kubwa uliyoifanya kuandaa Muswada huu. Wizara yako ni kubwa hasa kuhudumia. Napenda kuchangia Muswada huu kwa machache

Kwanza, naomba kuungana na Kamati kuhusu vyanzo vya mapato. Hatuwezi kunyang'anyana kasungura kadogo kwa barabara zote iongeze kodi za mafuta pamoja na magari makubwa.

Pili, naomba sana Mheshimiwa Waziri kuna barabara ya Monduli – Ketumbeine kikao cha *Road Board* ilipotuma maombi ilikuwa ni Monduli – Ketumbeine – Longido, kwenye jedwali Longido haipo.

Mheshimiwa Spika, wananchi wanapata huduma kwenye Barabara ya Longido – Ketumbeine, magari zaidi ya 20 yanapita kila siku kuliko barabara hii ya Monduli/ Ketumbeine. Hii inawezakana hata kwa mwezi kusiwepo hata gari litakaopita.

Naomba ikumbukwe Ketumbeine ni Tarafa kwenye Wilaya ya Longido kama umuhimu wa kutengeneza barabara ya Monduli ambayo ni Wilaya nyingine halafu isiende

Longido ni maajabu. Wananchi wa Longido wanashangaa sana kuona barabara ambayo haitumiki inatengenezwa na kuacha barabara inayotumika ili wananchi wa Longido wapate mafanikio na Miundombinu ya barabara ya Longido iwekwe kwenye *Regional Road* iwe Monduli – Ketumbeine, Ketumbeine – Longido. Nategemea maombi yangu yatazingatiwa.

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote ningependa kueleza kuwa hatimaye Serikali imeleta Muswada wa Barabara hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuikumbusha Serikali juu ya barabara ya Nyigo-Mgololo. Barabara ambayo nikiwa Mbunge wa Jimbo la Mufindi Kusini takriban kwa miaka 12 nimekuwa nikiomba Serikali Kuu kuichukua na kuihudumia. Lakini siyo mimi tu au siyo wananchi wa Jimbo la Mufundi Kusini bali wananchi wa Mkoa mzima wa Iringa wanaumia sana na barabara hiyo. Isitoshe hata mwakilishi wa Benki ya Dunia alizungumzia sana kuhusu barabara hiyo alisema kuwa Benki ya Dunia wangeweza kutusaidia kama Serikali yetu ingeonyesha kuijali. Rejea gazeti la ubinafsishaji la mwezi Desemba, 2006.

**MHE. MERYCE M. EMMANUEL:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa maelezo yangu kwa ufupi kuhusu hali halisi ya barabara zetu tulizonazo.

Mheshimiwa Spika, ningependa kusema kuwa barabara ya kutoka Dodoma- Singida, Singida kuelekea Shelui, kwa kweli barabara hiyo imekuwa ni tatizo kubwa na kikwazo kwa wananchi waelekeao Kanda ya Ziwa hususan Tabora, Shinyanga, Mwanza na Musoma pamoja na Kagera.

Mheshimiwa Spika, mwaka huu kipindi cha mvua zilizokuwa zikiendelea kunyesha wananchi wamepata taabu sana kupita eneo hilo hata kupelekea abiria kukwama Sekenke zaidi ya siku tatu. Hii ni kutokana na ubovu wa barabara hiyo. Zaidi uzembe wa hali ya juu uliosababishwa na mkandarasi anayetengeneza eneo hilo na Serikali haikuonyesha kuwa *serious* kabisa kumfuatilia mkandarasi huyo na kuwajibika kwa muda unaotakiwa. Hii inatokana na kuwa waliokuwa wanaathirika zaidi kuhusu tatizo hili ni wananchi wa kawaida au niseme wa hali ya chini ambao hawawezi kupanda ndege au kuzunguka Arusha, mahali ambapo kuna barabara ya lami hadi Mwanza.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali itilie maanani na kumfuatilia mkandarasi huyo ili aweze kumaliza barabara hiyo ili wananchi waweze kupita kwa usalama zaidi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono Muswada huu kwa asilimia mia moja.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na ofisi yake kwa kuwasilisha Muswada wa sheria mpya ya barabara, kwani huu ndiyo mlango wa ufumbuzi wa masuala mengi ambayo tumekuwa tukiyaleta katika Wizara hii. Hongera.

Pili, namshukuru Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla kwa ushirikiano mkubwa mnaotupa sisi wananchi wa Kilindi katika matatizo yetu makubwa ya barabara. Tatizo limekuwa ni fedha. Hivyo, mimi pamoja na Wabunge wengine tumeamua kutetea bajeti ya barabara kwa nguvu zetu zote. Kwani pasipo barabara zinazopitika, masuala mengine mengi nayo yanakwama, hasa ya maendeleo.

Tatu, kwa muda mrefu wananchi wa Kilindi wamekuwa na subira, wakiamini Serikali inawashughulikia. Wamejitolea kwa uwezo wao kukarabati barabara zinazopita katika maeneo yao, lakini tatizo ni utaalamu. Barabara ya *TANROADS* ni moja fupi tu Handeni/Kibirashi maombi ya ku-*upgrade* nyingine ambayo maombi yako mezani kwako tunasubiri sheria hii ili uweze kukubali maombi yetu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kiwepo kipengele cha kusisitiza *TANROADS* wanapofika kwa matengenezo katika barabara zinazowahusu, wawasiliane angalau na mamlaka ya Wilaya au *Engineer.* Ilivyo sasa hivi *TANROADS* hawatoi taarifa, hufika na kufanya wanalofanya na kuondoka. Kwanza, ieleweke kuwa barabara zote zinamilikiwa na vijiji wanapopita katika hizo barabara zina mamlaka ambamo zinapita, ni vyema sana kutushirikisha . Hii iwe lazima.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ZULEIKHA YUNUS HAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Andrew Chenge, Waziri wa Miundombinu pamoja na Naibu Mawaziri wake, Katibu Mkuu na wasaidizi wake kwa kuweza kuwasilisha Muswada huu muhimu Bungeni leo.

Mheshimiwa Spika, nimefika Wilaya ya Makete mwezi Januari, 2007 na nimeshuhudia jinsi barabara ya kufika kwenye Makao Makuu ya Wilaya ilivyo mbaya mno. Wananchi wa Wilaya hiyo wanahitaji msaada ili barabara yao iweze kupitika wakati wote!

Mheshimiwa Spika, naunga mkono Muswada huu.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Kwanza, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kiasi kikubwa jinsi alivyowasilisha Muswada huu. Kwenye Muswada huu nimeona barabara za Mkoa wa Tabora naendelea kuishauri Serikali kuzifanyia matengenezo barabara zote ili ziweze angalau kupitika kwa mwaka mzima. Ninao mfano wa barabara kuu kipande cha Ipole - Rungwa kimeachwa kwa muda mrefu bila kufanyiwa matengenezo kiasi cha kufanya barabara hiyo kuharibika sana na kushindwa kabisa kupitika.

Pili, ningeiomba Wizara iingize kwenye orodha kipande cha barabara kinachoendelea kutengenezwa kwa nguvu za Halmashauri kinachotokea Mibono - Kipiri, barabara hii ni ya mkato hata Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, amepita katika barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, nakushukuru na naunga mkono Muswada huu. Ahsante.

**MHE. STEPHEN J. GALINOMA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono Muswada huu. Kwa sababu ni *long overdue*. Sababu nyingine zimetajwa na Waheshimiwa Wabunge wengine wengi ambao wametoa maombi ya barabara zao mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mimi ombi langu ni moja tu katika hatua hii nalo ni barabara ya Iringa - Dodoma. Imeahidiwa mara nyingi kwa miaka mingi. Tumefikia mahali hata barabara za vichochoroni zinatengenezwa iweje barabara muhimu kama hii haitiliwi maanani. Naomba sana.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Spika, Muswada huu umekuja wakati muafaka, hasa ikizingatiwa kwamba umekuja wakati kabla ya Bunge la Bajeti.

La kwanza, barabara huafuata bidhaa. Bidhaa zinaposafirishwa kwenda kwenye masoko, uchumi wa mahali hukua. Ninapendekeza pafanyike tathmini ya kitalaamu kujua aina ya barabara zenye kutoa mchango mkubwa kiuchumi kwa maana ya kusafirisha mazao mengi. Katika kugawa pesa, basi barabara za namna hiyo zipewe kipaumbele katika kuzipatia pesa.

La pili, utunzaji wa barabara *(routine maintenance)*. Kambi za barabara. Barabara nyingi huwa hazifanyiwi *routine maintenance* kwa mapema kiasi cha kuzifanya ziharibike mapema.

Mheshimiwa Spika, napendekeza zile kambi za barabara kama zilivyokuwa wakati wa ukoloni enzi ya *Public Works Department (PWD)* zirudishwe. Wakoloni waliweka kambi kila baada ya kilometa 30 ili wale watu wachache waweze kutatua matatizo mara barabara inapoonyesha kuanza kuharibika. Wafanyakazi hao kwenye makambi wapewe vitendea kazi kama vile *tipper* moja, *spades,* sululu na kadhalika. Hali hii itaipunguzia Serikali kazi ya kutengeneza barabara nzima kila mwaka. Kwa hali ilivyo sasa, udongo au changarawe unaowekwa ni lazima uchukuliwe na mvua za masika hali hii inafanya Serikali ifanye kazi hiyo hiyo kila mwaka.

Tatu, kuhusu barabara za lami, sisi sote tunahitaji barabara za lami, lakini hali ya pesa Serikalini siyo nzuri. Mimi napendekeza kuwa angalau kila Wilaya ipewe kilometa 20 kila mwaka na kwa kipindi cha miaka mitano, kila Wilaya itakuwa imetengeneza barabara yenye urefu wa kilomita 100. Ikibidi vyanzo vyote vya fedha za barabara vitazamwe upya ili tuweze kupata fedha za kutosha kukidhi mradi mzima *(fuel levy).*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri mhusika aliwasilisha hili na nina uhakika kila Mbunge ataliunga mkono jambo hilo, kwa sababu tunatambua upungufu wa fedha za kujenga barabara.

Nne, kuhusu kuunganisha Wilaya ya Kilombero na Njombe, Wilaya yangu ya Kilombero ina barabara inayohudumiwa na *TANROADS* kutoka Kidatu hadi Taweta. Wilaya ya Njombe ina barabara inayotoka Njombe mpaka Madeke kupitia Lupembe ambayo pia ni inahudumiwa na *TANROADS.* Kati ya Madeke na Taweta ni umbali usiopungua kilometa 20 -30. Wenzetu wa Njombe wametengeneza barabara kuanzia Lupembe mpaka Madeke kwa namna ya ku-*open up.* Ili kukuza biashara kati ya Wilaya yangu ya Kilombero na Njombe ningeomba Serikali ituunganishe kwa kujenga barabara kati ya Taweta na Madeke. Barabara hii ikifunguliwa wananchi wa pande zote mbili watafanyabiashara. Wilaya yangu itauza katika Wilaya ya Njombe, mpunga, machungwa na mbao *(hard wood)* na tukachukua kutoka Njombe *soft wood,* viazi mviringo na mahindi.

Mheshimiwa Spika, naomba barabara hiyo iwe chini ya *TANROADS* kwa vile inaunganisha *Regional Roads* za Njombe na Kilombero.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuunga mkono Muswada huu na pia niwapongeze watendaji kwa maandalizi mazuri ya kuleta Muswada huu kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia sehemu ya tisa inayohusu fidia kwa yeyote atakayeharibu, hii itasaidia sana kutunza barabara ambazo tayari zimejengwa kwa gharama kubwa.

Mheshimiwa Spika, mfano ni barabara ya Mwanangwa Misasi hadi Salawe ni barabara ya Mkoa ilijengwa kwa gharama ya shilingi milioni 360 mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, cha kusikitisha mradi wa maji toka Ziwa Victoria kwenda Kahama na Shinyanga unapitishwa mizigo mizito kuliko uwezo wa barabara hiyo kitu ambacho kimepelekea kuharibu barabara na madaraja na Mkandarasi huyo hakufidia chochote na wananchi wa maeneo hayo wanapata shida hivyo Muswada huu utasaidia sana.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tatu ya Muswada huu inazungumzia upandishwaji wa madaraja ya barabara toka vijiji hadi Wilaya, Mkoa hadi Taifa. Nikumbushe kuwa Wilaya ya Misungwi inayo barabara iliyo na utata kutoka Misasi hadi Mbarika kupitia Nduha - Kasololo na Ngaya ilisajiliwa kwa Na. *165 R,* lakini pamekuwa na utata wa nani aihudumie ni vyema Waziri akaihudumia, kwa ngazi ya Mkoa imekuwa na matengenezo duni tangu mwaka 1984.

Mheshimiwa Spika, pia naomba kushauri kuwa barabara toka Buhingo - Seele Nyamayinza –Mbalama hadi Ihelele (Ilujamale) iwe daraja la Mkoa, hii ni kwa sababu ya mradi mkubwa wa maji ulioko Ihelele hivyo vitu vizito vitahitajika mara kwa mara ni vyema tukaepusha fidia kwa wale wataopeleka mizigo sehemu hiyo.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya nane ya Muswada huu inazungumzia fedha, nashauri mkazo uwekwe kwenye mfuko wa barabara . Mfuko huu umesaidia sana na pia wafadhili imewatia nguvu kutusaidia, hivyo Serikali ione umuhimu wa kutunisha mfuko kwa kuruhusu ongezeko la makato toka kwa watumiaji mbalimbali wa barabara ili mfuko ukidhi mahitaji kwa asilimia 75 kutoka ulipo sasa asilimia 35 tu . Makusanyo ya mfuko kutoka kwa watumiaji pesa zake zipelekwe moja kwa moja kwenye mfuko ili kuwahi mahitaji. Suala la ukaguzi lizingatiwe robo ya mwaka hesabu zijulikane.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nimpongeze Waziri kwa kazi nzuri za usimamizi wa kazi za umma. Ombi la pekee naiomba Serikali itenge pesa za kuifanyia matengenezo barabara ya Mwanangwa- Misasi -Salawe ambayo imeharibika sana pia ujenzi wa madaraja ya Mwamagembe.

Mheshimwia Spika, hapa si mahali pake lakini nimeona ni vyema nikamkumbusha Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono Muswada huu.

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, juu ya Muswada alioleta hapa Bungeni siku ya leo. Ninaunga mkono Muswada huu kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya ya wananchi wa Jimbo la Kibiti, napenda kutoa mchango wangu kuhusu Muswada huu katika maeneo yafuatayo ya barabara. Barabara za Wilaya, barabara ya Kibiti –Ruamke kilometa 28.5 na Ruamke –Mtunda kilometa 19.2.

Mheshimiwa Spika, barabara hizi mbili ni muhimu sana kwa maendeleo ya wananchi wa Jimbo hili. Barabara hii ni miongoni mwa barabara ambazo Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati wa wa kampeni ya mwaka 2005 aliahidi kuwa itajengwa kwa kiwango cha changarawe na hivyo kupunguza adha ya usafiri katika maeneo ya vijiji ambavyo barabara hiyo inapita.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ifuatilie kwa karibu utekelezaji wake. Hadi sasa hakuna jitihada zozote zinazofanywa ili kutekeleza ahadi hiyo ya Rais.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *feeder road,* hili ni eneo la pili ambalo nataka kuchangia. Napenda nianzie kuzizungumzia barabara ambazo zipo kwa ajili ya kufungua mawasiliano na wananchi zaidi ya 35,000,000 waliokuwa eneo la *Delta* lenye urefu wa kilometa 60. Ili kuwafikia wananchi hao barabara mbili zimeainishwa, nazo ni Mohoro – Ruma kilometa 19 na Mohoro Mbwera kilometa 14.

Mheshimiwa Spika, eneo hili la *Delta* ndilo duni *(under-saved)* kwa huduma zote za jamii ikiwamo miundombinu. Naipongeza Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji kwa kuweka mikakati ya kuendeleza barabara hizo mbili ambazo zinafungua mlango kwa wananchi hao.

Mheshimiwa Spika, barabara hizi mbili ni vizuri sasa kwa Serikali Kuu kuongeza fedha za utengenezaji ili ziweze kupitika mwaka nzima. Kati ya barabara hizo ni barabara ya Mohoro-Ruma ambayo haipitii katika maeneo ya mafuriko *(flood plains).* Barabara hii kwa kiasi kikubwa ina uwezo wa kupitika mwaka mzima iwapo Serikali itaongeza mgao wake. Kwa kujenga barabara hii, itasaidia sana kufungua mawasiliano kwa upande wa Kusini mwa *Delta.*

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya imeandaa mpango wa kukarabati/matengenezo barabara hii ya Mohoro/Ruma kwa thamani ya shilingi 580,000,000. Mpango huo utawasilishwa Wizarani hivi karibuni ili Wizara nayo ione namna ya kusaidia upatikanaji wa fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono Muswada huu.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu wa Sheria ya Barabara wa mwaka 2007 ili kuboresha na kusimamia vyema barabara zote nchini. Aidha, napenda kuipongeza Serikali kuanzisha bodi za barabara ambazo naamini kuwepo kwake kutasaidia Serikali kushauri kwa uhakika barabara zinazozihusu. Pamoja na pongezi hizo nina ushauri ufuatao:-

Mosi, barabara ni kichocheo kizuri cha maendeleo lakini ujenzi wake ni gharama kubwa. Ni vema basi kukaanzishwa kitengo imara cha kutoa mafunzo kwa makandarasi wazalendo ambao mara nyingi ndio unafanya ujenzi/ukarabati wa barabara zetu za Mikoa na Halmashauri ili wakipata uwezo *(capacity),* barabara hizo zitapunguza gharama inayotokana na ujenzi wa barabara usio na viwango.

Watanzania wengi hufa kutokana na matatizo ya barabara au vifaa vinavyotumia barabara kama vile magari, pikipiki, madaraja na kadhalika ni vizuri kitengo cha usalama barabarani kiimarishwe na kufanyakazi wakati wote ili kulinda usalama wa raia na mali. Hali iliyoko sasa ya kufanya ukaguzi wa magari na barabara/madaraja kunapotokea ajali haipendezi. Barabara inaweza kukarabatiwa haraka kama kutakuwepo na ukaguzi wa barabara wa mara kwa mara ikiwa ni pamoja na magari/vitumia barabara zenyewe.

Mheshimiwa Spika, napenda kushauri pia kuwepo kwa usimamizi imara wa viwango vya nauli vinavyotozwa na wenye mabasi. Hali ya sasa ya bei za nauli zinazopanda kiholela kila kukicha haipendezi mfano nauli ya Dar es Salaam – Mtwara kila siku inabadilika badilika na hakuna nauli ya huko. Leo utaambiwa Dar es Salaam – Mtwara ni 25,000/= Lakini Dar es Salaam – Newala ni 25,000/= hizo hizo. *SUMATRA* inaelekea kushindwa kazi ya kusimamia matumizi ya vifaa vya majini na nchi kavu.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mtwara - Tandahimba – Newala – Masasi ni msingi wa uchumi wa Mkoa wa Mtwara. Aidha, barabara hiyo ndiyo pekee inayounganisha wilaya zote za Mkoa wa Mtwara, kwa nini sasa isipandishwe kuwa barabara ya Kitaifa *(trunk road)?* Tamko la Rais, wakati wa kampeni kuwa barabara hiyo itaboreshwa kwa wananchi wa maeneo hayo tuliamini maboresho hayo ni pamoja na kuibadilisha barabara hiyo ili iwe ya kitaifa na hivyo isaidie kupeleka mazao yetu kwenye masoko kwa kutumia bandari ya Mtwara. Ikiwa ni pamoja na kuiweka lami. Wakati umefika sasa barabara hiyo kupewa sifa stahili.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1990 Mkoa wa Mtwara ulipata maafa ya mafuriko yaliyosababishwa kuvunjika na kuharibika kwa madaraja likiwemo daraja la Nangoo. Hivi tatizo ni nini kiasi cha muda wote huo kuwa halijakarabatiwa kwa miaka 17 sasa? Tuelewe nini?

Mwisho, naomba sana Serikali kuipa kipaumbele barabara ya Kibiti – Lindi hasa eneo la Ndundu – Somanga liweze kukamilisha. Wananchi wa Kusini wamechoka sasa kwa kutokuwa na barabara ya uhakika miaka 46 baada ya uhuru.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya naunga mkono hoja.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuipongeza sana Serikali kupitia kwa Waziri na timu yake kwa kuleta Muswada huu Bungeni. Muswada huu umekuja wakati muafaka kama kweli tunataka kutimiza dhana ya maisha bora kwa kila Mtanzania yanawezekana na kama tunataka ku-*achieve objective* ya kukwamua Watanzania vijijijini kutoka lindi la umaskini kwa kuwa Muswada huu unalenga kuboresha na kusimamia, nadhani sasa tutafikia lengo zima la maendeleo kama tutazingatia hivyo.

Suala la zima la biashara linahitaji barabara ya uhakika hivyo ujasiriamali utafanikiwa iwapo tu barabara zinapitika, *SACCOS* zilizopewa mikopo sasa ni zile zinazofikia, wafadhili

wana *establish NGOs* za kimaendeleo kama maeneo yana *accessibility,* walimu waliopangiwa shule za kata wanakataa kwenda huko kama hakuna barabara za uhakika na Mawaziri wengi na viongozi wengine wanatembelea sehemu zinazofikika mara kwa mara. Huko Mbulu na maeneo ya pembezoni tunawaona kwa nadra. Hakuna faraja kubwa kwa wananchi kama kufikiwa na viongozi wao.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete alipokuwa kwenye kampeni alitoa ahadi mbalimbali za kuwajengea wananchi barabara na kuondoa kero hizo. Alipokuja Wilaya ya Mbulu, akitokea Hospitali ya Haydom alishindwa kabisa kufika kwa wakati Makao Makuu ya Wilaya ili kuhutubia wananchi na hivyo kufika usiku na kushindwa kuhutubia. Nina hakika kama angezungumza jambo la kwanza ingekuwa ahadi ya kutengeneza barabara ya Haydom – Mbulu iliyomchelewesha.

Mheshimiwa Spika, ubovu huo ulikuwa wakati wa kiangazi. Mvua zilizonyesha sana na zinazoendelea kunyesha zimefanya barabara hiyo isipitike au kupitika kwa shida na kwa magari yanayoaminika na kusababisha kero. Tatizo kubwa sasa hivi ni wagonjwa au wanawake wajawazito kuathirika vibaya na hivyo barabara aidha, wanafikishwa hospitalini wakiwa hoi na pengine kupoteza maisha au kujifungua watoto waliofia tumboni. Ushahidi wa maneno haya upon a wananchi wa Wilaya ya Mbulu wanailaumu sana Mkoa na Serikali kwa ujumla bila mafanikio. Mheshimiwa Waziri Mkuu ni shahidi maana alikuwepo kwenye ziara ile ya Rais na Naibu Waziri wa Miundombinu ni shahidi pia wa ubovu wa barabara hiyo kwa kuwa naye alikuwepo.

Mheshimiwa Spika,wakati mwananchi mmoja alipotangazwa kufa kutokana na njaa Serikali iliunda timu ya watu kwenda kupata uhakika maana kifo cha njaa ni cha aibu na huzuni. Ndipo mikakati ya haraka ikachukuliwa na Waziri Mkuu kutangaza kuwa hafi Mtanzania kwa njaa. Naiomba Serikali ione hivyo hivyo kuwa vifo vya wanawake wajawazito au viumbe walivyobeba kwa miezi tisa tumboni viwe vya aibu na huzuni kama vitatokea kutokana na barabara mbovu hususan barabara ya Haydom – Mbulu.

Mheshimiwa Spika, naomba zile fedha zilizotengwa na Serikali yetu inayojali wananchi wake kwa ajili ya barabara mbovu kupindukia zimegwe kwenda kutengeneza barabara ya hospitali ya Haydom Mbulu (kilometa 78). Barabara hii itengenezwe haraka kunusuru maisha ya wagonjwa, mimi sizungumzii biashara au jambo lolote lingine kwa sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuwa unajua barabara hii na kwa kuwa nakufahamu una huruma sana naomba utoe tamko kuhusu barabara hii kunusuru maisha ya wanawake na wagonjwa wanaopelekwa haydom kwa matibabu kutoka sehemu zingine za Mkoa wa Manyara na Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo kwa uchungu naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, naomba kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Simanjiro kutoa mapendekezo yanayoweza kuboresha mawasiliano yanayounganisha Wilaya yetu na maeneo muhimu ya jirani. Kwanza napendekeza barabara ya Monduli Jeshini – Lolkesalie – Emboreet – Orkesumet ipandishwe kuwa ya Mkoa kutokana na umuhimu wake.

Pili, napendekeza ahadi ya Serikali ya kujenga barabara ya *KIA* hadi Mererani kwa kiwango cha lami itelezwe.

Tatu, nashauri barabara ya Orkesumet – Ruvu Remil – Gunge ipandishwe hadhi kuwa ya Mkoa. Aidha, barabara ya Gunge – Msitu wa Tembo zinastahili kupandishwa hadi kuwa ya Mkoa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na jiografia ya Wilaya ya Simanjiro ambayo umbali kati ya kijiji kimoja hadi kingine si chini ya kilometa 55 Wilaya yetu inahitaji barabara hizo zipandishwe hadhi ili kupunguzia mzigo Halmashauri yetu. Hii ni pamoja na ile ya Orkesumet – Lendanai – Mererani hadi mpaka wa Arumeru.

Mheshimiwa Spika, nakumbushia ahadi ya Serikali ya kuunganisha Simanjiro na Makao Makuu ya Mkoa (Orkesumet - Babati) itengewe fedha za kutosha. Aidha, nimesikitishwa kutokuiona orodha ya barabara na hasa ikizingatiwa ahadi hii ilikuwa ndiyo faraja pekee wakati wa uamuzi wa Rais wa kuunda Mkoa wa Manyara. Ahsante sana na naunga mkono hoja.

**MHE. DORAH H. MUSHI:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mbunge wa Jimbo la Tunduru. Nimpongeze pia Mheshimiwa Florence Kendesya, kwa kuteuliwa kuwa Mbunge Viti Maalum Mkoa wa Mbeya. Nitoe pia salaam za rambirambi kwa familia ya aliyekuwa Waziri wa Afya Hayati Dr. Aaron Chiduo. Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi.

Mheshimiwa Spika, naomba niunge mkono hoja na nimpongeze Waziri na watalaam wote walioandaa Muswada huu na kuuleta hapa mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, suala la barabara ni kilio cha wananchi wengi katika nchi yetu ya Tanzania. Lakini niipongeze Serikali sana kwa jitihada zake za kuimarisha miundombinu sehemu nyingi katika nchi yetu pamoja na kwamba ujenzi wa barabara ni gharama kubwa ukizingatia kwamba Serikali haina fedha za kuweza kuenga barabara zote kwa wakati mmoja.

Lakini kuna jambo moja la kuzingatia na kwa kuwa barabara ni nyenzo muhimu na kivutio kwa wageni na wawekezaji. Je, ni lini Serikali itatilia maanani zile ahadi za Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete katika kampeni za mwaka 2005? Marais wote wa Awamu tatu na ya nne waliahidi kuwa barabara nyingi zitajengwa kwa kiwango cha lami ikiwemo barabara ya Mererani katika machimbo ya *Tanzanite.*

Mheshimiwa Rais aliona kwamba barabara hii ni muhimu kwa sababu inaunganisha mikoa mitatu Mkoa wa Kilimanjaro, Mkoa wa Arusha na Mkoa wa Manyara. Kuna wachimbaji wakubwa ambao ni *Tanzanite one* kampuni ya *Kilimanjaro mine,* kampuni ya *Tanzanite Africa (Ltd.)* na wachimbaji wadogo wadogo wafanyabiashara.

Mheshimiwa Spika, ikiwa ahadi hizi za Marais wote wawili zilitolewa mbele ya wananchi wapigakura wetu na wageni wawekezaji wakisikia. Je, hawa wageni hawataona ajabu kusikia au kuona kuwa ahadi ya Rais zikipuuzwa? Kwa kuwa katika nchi zote ahadi inayotolewa na mtawala ni lazima itekelezwe mara moja. Je, ahadi hizi zitatekelezwa lini ili wageni na wawekezaji wetu waone kuwa tumejali na tumewatengenezea mazingira mazuri ya kufanyia kazi zao?

Mheshimiwa Spika, kampuni ya uchimbaji ya Afrika Kusini, *Tanzanite one* imejaribu sana kutengeneza barabara hiyo bila mafanikio. Mvua ikinyesha tatizo ni lile lile barabara inageuka mto na watu wanavua kambale. Mheshimiwa Waziri Mkuu alishuhudia ubovu wa barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa nini Waziri wa Miundombinu au Serikali isione umuhimu wa kukaa na kampuni zote tatu za uchimbaji waone uwezekano wa kuweza kujenga barabara hii ya Mererani mpaka *KIA* yenye kilometa 20 tu?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, nilitegemea kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu nikitaka niombe azipandishe barabara zifuatazo:-

(i) Busambara- Mugara yenye kilometa 15;

(ii) Bulamba – Kamkekere – Mwiruruma yenye kilometa 20; na
(iii) Nakatuba – Igundu – Mwitende yenye kilometa 12.

Mheshimiwa Spika, namuomba Mheshimiwa Waziri barabara hizi ziwe za Mkoa *(Regional Roads)* kwa vile kwanza zinaunganisha watu wengi kata zaidi ya moja, maeneo hayo yanazalisha sana samaki na mazao ya chakula, zinaunganisha masoko mengi ya samaki, pamba, mahindi na mihogo.

Mheshimiwa Spika, natanguliza shukrani zangu.
**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Spika, nataka kuchangia kuhusu barabara za Mkoa wa Manyara. *First schedule, classification and declaration of roads.* Kwanza barabara ya Babati – Singe- Gedmar – Kimotorok. Katika *schedule* niliyoitaja, barabara mpya ambayo inaunganisha Makao makuu ya Mkoa wa Manyara – Babati na Wilaya ya Kiteto na Simanjiro haipo. Hii ndiyo barabara iliyoahidiwa na Serikali wakati wa kuunda Mkoa mpya wa Manyara. Endapo barabara hii haitakuwa sehemu ya barabara kuu *(first schedule)* basi maana ya kuundwa kwa Mkoa wa Manyara itakuwa haipo. Nashauri marekebisho yafanyike na iingizwe kwenye jedwali hilo.

Mheshimiwa Spika, pili, barabara ya Babati – Imbilili – *Kim Six*- Erri hadi Mbulu. Barabara hii ilipitishwa na *RCC* ili iwe ya Mkoa kwa sababu inaunganisha Makao Makuu ya Mkoa wa Babati na Wilaya ya Mbulu kwa njia fupi sana. Hivyo naomba marekebisho nayo yafanyike ili iwe barabara ya Mkoa.

Tatu, Wilaya ya Babati sasa ina Halmashauri mbili yaani Halmashauri ya Wilaya na Halmashauri ya Mji wa Babati. Ni muhimu kuonyesha zipi ni za Halmashauri ya Wilaya na Halmashauri ya Mji wa Babati. Kwa namna ninavyozifahamu barabara za Halmashauri ya Mji naona ikama ifuatavyo:-

Katika ukurasa wa 598, *Babati Town Council* inaanzia *Road No. 211021* hadi 21103 na 211105 hadi 21108. Zingine naona zipo chini ya *Babati District Council*. Ni muhimu sana marekebisho yafanyike.

Mwisho, nashauri kuwa Wizara itengeneze vitabu vidogo vyenye mtandao wa barabara kwa kila Mkoa ili iwe rahisi kwa rejea na maendeleo ya barabara mpya na za zamani.

Mheshimiwa Spika, nakutakia kazi njema na mategemeo hoja zangu zitapata majibu. Ahsante.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, Muswada huu ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu kwani maendeleo maana yake ni barabara au *connectivity* na kwa hiyo napenda kusisitiza yafuatayo:-

Kwanza ni kuhusu Bajeti. Ni vibaya sana kutegemea wafadhili kwa sekta hii na kwa hiyo, napendekeza Bunge liamue sekta hii ipewe asilimia isiyopungua asilimia 7 ya Bajeti ya Serikali na ziwe fedha za ndani ili tuwe na uwajibikaji wa sekta hii bila kisingizio cha wafadhili.

Pili, mtandao *(connectivity)*. Serikali ya awamu tatu ilijitahidi sana kujenga mtandao wa Kitaifa. Jambo hili liendelezwe. Barabara ya Arusha – Dodoma – Iringa, Tunduma – Sumbawanga – Kigoma na Itigi – Tabora – Kigoma ni mifano ya mitandao ambayo itaunganisha nchi yetu na kuleta kukua kwa uchumi wa ndani na mauzo ya nje.

Tatu, *rural roads/district roads*. Barabara hizi hazina ramani *(mapping)* ni barabara zenye uwezo lakini hazina mwisho. Wakati umefika barabara zijulikane orodha kwenye Muswada ni mwanzo mzuri lakini si kamili *(not exhaustive)* naipongeza Wizara kwa kusema turudi tuziangalie na orodha itengenezwe vizuri zaidi, hili litafanyika *mapping* itafanyika. Serikali ya wamu ya nne itajivunia kuwakomboa watu wa vijijini kama itatoa kipaumbele kwa kuunganisha Wilaya kwa Wilaya, Wilaya kwa Kata.

Mheshimiwa Spika, Bariadi Kata zifuatazo hazina mtandao wa barabara wa kuziunganisha ambazo ni Mbita, Mhunze, Gambosi, Nkwama, Ngwalwale, Ny'wadobawa na zingine ambazo Halmashauri inazishughulikia kwa kidogo sana. Orodha ilihitajiwa katika Muswada haikutaja barabara Kwaloto- Maswa Luguru- Giliku – Chimaurili- Bumera – laini – Junotion – R 44- haikutajwa sana. Barabara – Bariadi – Rudohujega – Gambasingu inapaswa kuwa *regional road* kwani inaunganisha Wilaya ya Bariadi – Meatu – Singida. *Ref. 171006 171011.* katika orodha Mwamapalala – Gombaringu haipo. Hii ni mifano michache kuonyesha orodha siyo *exhaustive.*

Nne ni kuhusu mamlaka ya barabara, kwa Shinyanga kuna udhaifu juu na mikutano ya *regional road.* Mikutano hii inaitwa wakati Wabunge wako Bungeni. Jambo hili lirekebishwe ili Wabunge washiriki sababu kwamba *RAS* hajui ratiba ya Bunge halina msingi.

Tano ubora wa barabara, kuweka kifusi wakati wa mvua ni njia mojawapo ya kutafuta njia ya kuiba na kuficha ushahidi wa uwajibikaji *(accountability).*Sita, *all in all* ni Muswada mzuri na naunga mkono juhudi zinazofanywa.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara. Napenda kupata maelezo ya ziada juu ya madaraja *(classification)* ya barabara

kwanza tafsiri ya tarakimu zilizotumika kama 3, 4, 6 na kadhalika hakuna mahala katika Muswada au kiambatanisho kinachotoa ufafanuzi juu ya matumizi ya hizo tarakimu.

Mheshimiwa Spika, ninayo sababu ya kutaka kufahamu madaraja hayo nitatolea mfano wa eneo ninalolifahamu Mkoa wa Rukwa, Mji wa Mpanda, Sumbawanga na Nkasi, barabara *(streets)* zote Mpanda ni *class 6* Sumbawanga *T/C* nyingi *class 6* na Nkasi zote *class 4,* naomba kupata maelezo ya vigezo vilivyotumika katika miji hii mitatu yenye kupishana na katika mambo mengi.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu mimi ni mjumbe wa Kamati ya Miundombinu, katika kikao cha *PH,* mwakilishi wa polisi, usalama barabarani alitoa pendekezo la uzito wa magari na ubora na uwezo wa barabara zetu ni vyema tukazingatia ushauri huu, mizigo mizito ni sababu inayopelekea barabara kuharibika mara kwa mara, nitafurahi kupata maoni ya Serikali katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo nadhani linahitaji uangalizi wa haraka sana ni baada ya kuweka matuta katika barabara zetu ni vyema basi yakatolewa maagizo ya kitaalamu juu ya umbo, ukubwa, alama na rangi zinazotumika zifanane kwa nchi nzima. Matuta haya pamoja na faida zake lakini pai yanaleta madhara kwa magari kwa namna yanavyojengwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwepo alama za makatazo katika baadhi ya barabara kwa kuweka alama za uzito unaoruhusiwa katika barabara kama vile yanaporuhusiwa magari ya tani 10 kupita, unakuta magari ya tela *(Truck and Trailer)* ya uzito wa tani 50 yanapita katika barabara hizo, nani anasimamia. Wizara/Polisi na Maafisa wanaohusika wakizembea basi wachukuliwe hatua ili sheria hizi zisimamiwe vyema.

Mheshimiwa Spika, mwisho ningependa kupata maelezo ya ziada juu ya bodi za mkoa, ni kwa nini Meneja wa *TANROAD* anakua mjumbe badala ya Katibu wa Bodi ya Mkoa mmoja ni mtaalamu/mtendaji wa barabara, mwingine ni mtawala *Administrator RAS.* Kwa maoni yangu muundo wa sasa ni vyema ukaendelea, labda kama zipo sababu zinazopelekea kuwepo na mabadiliko hayo, nitapenda kupata ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, hongera kufikia hatua hii kwenye Muswada huu muhimu.

Tafadhali utakapofanya masahihisho ya *First Schedule Sections 12* na 13 ukumbuke maombi yangu kuwa barabara ya Lembeni – Kilomeni kilometa 11.8 iwe katika *Regional Roads,* Kilimanjaro.

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, naona katika jedwali la barabara. Barabara zifuatazo sijaziona:-

Kwanza, Mbinga – Litembo – Kitura – Nkiri. Pili, ni barabara ya Mbinga – Mkumbi.

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

**MHE. LAUS O. MHINA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nipongeze maandalizi mazuri ya Muswada huu yaliofanywa na Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu pamoja na Naibu Mawaziri wake ukijumuisha na watendaji wa Wizara ya Miundombinu.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu mfupi napenda niuelekeze sana kwenye yafuatayo, kwanza utamaduni wa ukarabati wa Miundombinu yetu na pili, sheria za barabara.

Mheshimiwa Spika, nikiwa kama mhandisi ujenzi *(Civil Engineer)* nimegundua kuwa barabara zetu nyingi hufikia hatua ya kutopitika kabisa kutokana na kutofanyiwa ukarabati kwa wakati unaotakiwa. Ukarabati huo unahusisha *carriage way* yenyewe pamoja na mifereji ya maji ya mvua. Ni vema tuwe na utamaduni wa ukarabati miundombinu yetu kwani usipoziba ufa hutajenga ukuta.Muswada huu umebainisha sheria na adhabu kwa wahusika wanaoharibu barabara zetu tu.

Mheshimiwa Spika, kuna ajali nyingi pia zinazotokana na matatizo ya barabara zenyewe. Kwa mfano mashimo makubwa, madaraja/vivuko na ukosefu wa alama husika barabarani. Je, Serikali inawajibikaje kwa madhara yanayotokea kutokana na athari zilizotajwa hapo juu. Wananchi hupoteza maisha, mali zao na magari/mitambo katika ajali hizi. Ni vema suala hili liwekwe bayana kwenye Sheria ya Barabara ya mwaka 2007. Naomba kuunga mkono hoja hii.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuipongeza Wizara ya Miundombinu kupitia Waziri wake Mheshimiwa Andrew Chenge na Naibu wake Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga.

Kimsingi naunga mkono hoja, hata hivyo nina maomba ya marekebisho yafuatayo:-

Katika kifungo cha 7(2) chenye marekebisho (c) kinachosomeka, *"Constituency Members of Parliament and not more than two members of Parliament special seats in the respective region."*

Hii inakiuka *SADC Convention. AU forms of discrimination against women special seats members* wake ni wanawake. Hakuna haja ya kuandika ibaki kwenye sheria ambayo haitabadilika mara kwa mara.

Ushauri wangu ni kuwa iwe *silent* isomeke: *"Constituency Members of Parliament and Members of Parliament from Special Seats in the respective regions."*

Kipande cha barabara Kipapa - Matuta – Mango kikamilishwe kwa kuongeze Mango –*Njambe Port.* Hii barabara ni muhimu sana kwa ukuaji wa uchumi na tushukuru sana kwa kuipa kipaumbele *(Reg. 103039/103/10/3)*

Pia kwa sababu hizo hizo kipande (103041/103/10/3) Langiro - Mkoha. Kisomeke Langiro - Mkoha –*Mkiri Port* wakati wa upembuzi yakinifu wataalamu wetu wawe na *data* za wakati wa jua na wa mvua ili kuhakikisha kuwa tabia za maeneo na mito zinafahamika vizuri na hivyo kuchukua *pre-caution* wakati wa ujenzi wa barabara yakiwemo madaraja. Pia wananchi washirikishwe ili kuweza kusaidia uonyeshaji wa vifusi vizuri kutokana na mazoea ya maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, mwisho nazidi kupongeza jinsi ambavyo barabara zimeweza kuainishwa na hivyo zitakapowekwa kwenye ramani zitasaidia kuwafikisha kirahisi wawekezaji wetu pamoja na watalii katika kila pembe ya Tanzania. Endeleeni kututengenezea barabara nzuri zisizoondolewa na mvua mara tu ikinyesha. Pia napongeza adhabu kwa makandarasi wabovu kwani ni aibu kuona daraja linajengwa ndani ya miezi mitatu linazolewa na mvua.

Lakini pia katika mambo yaliyojitokeza wakati wa kikao chetu cha barabara ilionekana bajeti ni ndogo. *TANROADS* na wahusika wote wapewe bajeti ya kutosha.

Mheshimiwa spika, hata hivyo tunapongeze juhudi za Serikali kwani huwezi kulinganisha hali yetu ya barabara na nchi kama *DRC.*

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba kusema naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Sheria ya Barabara 2007 itasaidia sana kuboresha miundombinu ya barabara na hivyo kuongeza kasi ya maendeleo.

Barabara ya Katoma -Bukwali *(R 105)* yenye kilometa 39.7 ni muhimu sana katika maendeleo ya Mkoa wa Kagera na Taifa kwa ujumla. Barabara hiyo inaunganisha Tanzania na nchi ya Uganda. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa barua hake iliyokubaliana na umuhimu wa kuwekea barabara hiyo lami fedha ikipatikana. Naomba fedha ikipatikana basi barabara hiyo iwekwe lami. Ikiwezekana tunaweza kuweka barabara hiyo lami hatua kwa hatua.

Mheshimiwa Spika, vile vile naomba kushukuru Wizara kwa kukubali kutoa ushauri wa kiufundi katika ujenzi wa daraja la Kibingo. Daraja hilo kama likijengwa litasaidia kuunganisha Tarafa mbili zilizo Wilaya moja ya Misenyi. Sheria mpya tunayotunga leo inaleta dhana mpya ya *Private Roads.* Ni matarajio yangu sekta binafsi itakubali fursa hii na kushirikiana na Serikali katika harakati ya kuboresha Miundombinu. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Spika, kuna barabara mbili zinazoanzia Ludewa na kuishia kwenye Wilaya nyingine za Makete na Njombe.

(a) Kutoka Mkiu kupitia Makete hadi Mbeya kwenye Uwanja wa Kimataifa wa Ndege. Kuna daraja kwenye barabara hii upande wa Ludewa lililofunguliwa na Rais Mstaafu Benjamin Mkapa. Barabara hii iko *under developed.* Kwenye *RCC* tulikubaliana ipandishwe hadhi kuwa ya Mkoa hili halikufanyika tunaomba hili lifanywe.

(b) Kutoka Luimbili katika mwambao wa Ziwa Nyasa (Ludewa) kuna barabara inayopita Makete na kutokea Njombe Mjini. Kwenye *RCC* tulikubaliana barabara hii ipandishwe hadhi kuwa ya Mkoa. Barabara hii ipo *underdeveloped* lakini ingeweza kutumika kusafirisha mazao ya majini kama samaki kwenda Njombe Mjini na kwenye soko la Kimataifa linalojengwa Makambako.Tunaomba barabara hii ipandishwe hadhi kuwa ya Mkoa.

Pili vile vile kuna mipango ya kujenga kiwanda mama cha kuyeyusha chuma Liganga (Mundingi) na kwa kuwa kilometa 30 kutoka hapo ni soko la Kimataifa la Mlangali. Barabara hii kutoka Madaba hadi Mlangali ni ya Mkoa lakini ni ya udongo tunaomba mawili:-

(i) Barabara ya Madaba hadi Mlangali ikiwezekana hadi Njombe iwe ya lami ili kuhudumia shughuli za maendeleo kwenye eneo hili.

(ii) Barabara ya Madaba hadi Mkiu ipandishwe hadhi kuwa ya Kimataifa *(Trunk Road).*

**MHE. EPHRAIM N. MADEJE:** Mheshimiwa Spika, Muswada ni mzuri na bila shaka utaleta mabadiliko katika utaratibu wa ujenzi na ukarabati wa barabara nchini. Mimi ni Mjumbe wa Kimataifa wa Miundombinu na nimeshiriki katika kumpitia Muswada kwa kina na kupendekeza marekebisho kama ilivyoainishwa na Waziri pamoja na taarifa yalivyoainishwa na Waziri pamoja na Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, kutokana na *road classification criteria* zilizomo kwenye sheria, barabara itokayo Ihumwa hadi Mayamaya inastahili kuwa ya Mkoa kwani inaunganisha barabara kuu mbili yaani ile ya Morogoro/Dodoma na ile ya Dodoma/Arusha kwa hiyo ninamuomba Mheshimiwa Waziri afanye marekebisho husika kwenye first schedule. Naomba kuwasilisha.

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata fursa ya kuuchangia Muswada huu muhimu sana katika kukuza uchumi wa nchi yetu. Kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Andrew Chenge na wasaidizi wake wote Wizarani kwa maandalizi mazuri ya Muswada huu. Napenda kuchangia mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, uchumi wa nchi utakua na kuenea katika sehemu mbalimbali nchini kadiri ufanisi wa uwezo wa uwezo wa kusafirisha bidhaa na huduma *(goods and services)* haraka utakavyowezekana kwa kusafirisha kutoka sehemu zenye bidhaa na huduma nyingi na kuzipeleka kuzifikisha ambako bidhaa na huduma ni chache, ili kutimiza dhana hii ni lazima *network* ya barabara zote hata kama sio za lami ziweze kupitia wakati wote wa masika na kiangazi.

Mheshimiwa Spika, *network* ya barabara nchini ni sawa na *network* ya mishipa ya damu katika mwili wa binadamu ambayo ni lazima iwezeshe kupitisha mazunguko wa damu ni lazima iwezeshe kupitisha mzunguko wa damu kipindi chote cha masika na kiongozi. Pakitokea *blockage* popote katika *network* hiyo hitilafu na udhoofu wa afya ya mwili hutoka.

Kwa hiyo, naishauri Serikali ichunguze kwa makini sana *distribution* ya barabara za vijijini *especially* kunakozalishwa chakula kwa wingi ili kiweze kusafirishwa kwenye upungufu na vivyo hivyo kunakolimwa mazao ya biashara yanayousisimua uchumi wetu haraka.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo yafuatayo hivi punde naiomba sana Serikali itoe kipaumbele kuwaagiza *TANROAD,* pale panapostahili kutoa huduma zake kwa utaalamu na usimamizi wa vifaa kwa barabara chache za vijiji ambako *bread basket* ya Kata au Wilaya kuliko kuacha vyakula vinavyozalishwa kuoza na kusababisha njaa sehemu ambako ingeepukwa kama vingesafirishwa andapo barabara ingekuwa imara.

Mheshimiwa Spika, maana yangu hapa ni kwamba *TANROAD* isiwe *excessively rigid* kwa kutambua wao hawahusiki na barabara za vijijini *(feeder roads)*. Serikali ni budi itambue chakula kingi kinazalishwa kwenye maeneo yenye *feeder roads* nyingi na fedha za Halmashauri kamwe haziwezi kutosha kuzitengeneza njia hizo zihilimi uzito mkubwa wa chakula chote katika barabara na madaraja mengi mabovu vijijini.

Mheshimiwa Spika, ni kwa maana hii naiomba tena Serikali inavyoandaa mradi na michezo ya barabara ya lami kutoka Mikumi kuelekea Kilosa chonde chonde katika kijiji cha *Ulaya junction* ya kwenda Nyameni kuna madaraja matatu Mita 500 katika *feeder road* inayokuja kuunganisha *planned tarmac road* hiyo ambayo ni budi gharama na ujenzi wake zijumuishwe katika mradi mzima wa barabara ya Mikumi – Kilosa –Handeni, Korogwe. Hii ni kwa ajili ya ku-*boost economic* na *finacial viability* ya barabara hii kwa sababu mazao mengi sana ya mahindi hulimwa mara mbili kwa mwaka, ufuta, alizeti maharage na kadhalika yanalimwa ng'ambo ya hayo madaraja, kwenye mto mkubwa ambao hufurika vibaya wakati wa masika.

Mheshimiwa Spika, hali hiyo hiyo katika kijiji cha Zombo katika barabara iendayo Kilosa. Hapo kutahitajika kujumuisha daraja moja mita 500 toka itakapopita barabara kuu.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya mwisho ni katika Kijiji cha Miyombo ambapo kuna *junction* ya barabara inayoelekea mashariki kwenda Kivungu na Kilangali ambako kuna shamba kubwa la kitaifa linalozalisha mpunga kwa wingi sana. Hii ni barabara ambayo Tan-road ingepaswa kuishughulikia *on exceptional basis* kadiri nilivyopendekeza.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atujulishe hatua iliyofikiwa kwa barabara hii. Natambua uhaba wa fedha ni tatizo kubwa lakini kupanga ni kuchagua *the most basis need* kwa wananchi wetu wengi ni kuwa-*facilitate* wazalishe na wauze chakula ili waingie katika kundi la watanzania wanaopata pesa kidogo kujiinua kiuchumi kwa hiyo katika eneo la Miyombo *survey* ya barabara mpya siyo lazima ifuate barabara ya zamani bali uangaliwe uwezekano ku *divert* kuelekea vijiji vya Gezaulole, Mlangali, Muungano kupitia Kimamba au Kondoa, Mkono wa Mara hadi Ludewa. Hii inamaana barabara iwafuate watu wanakozalisha chakula cha biashara na waweze kukisafirisha kwa urahisi kwa mauzo. Nilishamwandika barua Mheshimiwa Chenge sijui kama barua zngu alizipata ka vile sikupata *acknowledgement*.

Mheshimiwa Spika, wengi wanashauri mpango wa zamani wa kuweka Magenge vijijini ya kudumu yenye usimamizi mzuri wa kutengeneza kujaza mashimo barabara kwa mwaka mzima utaleta faidaza kuzifanya barabara zipitike vizuri zaidi kila zinapoharibika na pia zitatoa ajira kwa  ajira kwa vijana wengi vijijini wasio na kazi na hivi kumsaidia Rais wetu kutimiza azma yake ya kuongoza ajira. Hata hivyo ni bora fedha zinazofujwa kijanja katika Halmashauri zikatumika kwa kazi hii ambayo itaonekana. Magenge yarudishwe katika *system* kama inavyofanyika katika njia za reli.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya naunga mkono hoja muswada huu.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, nimesome *schedule* iliyoambatanishwa na Muswada wa Barabara. Katika Wilaya ya Bunda, kuna barabara ya Balili, Mugeta,  Manduimweru hadi Gusuli. Hii inaunganisha Wilaya ya Bunda na Serengeti. Kamati ya Barabara ya Mkoa ilikwishaleta  mapendekezo ya kuifanya

barabara hii  kwa Mkoa. Hili ni ombi mahususi bila kusahau sehemu ya Isinda - Nyauswa ambayo ni *trunk road*.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakupongeza  kwa kuleta  Muswada huu Bungeni.

Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Pamoja na kuunga mkono hoja hii napenda kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, makandarasi wanaoteuliwa kutengeneza barabara  wawe na uwezo wa kifedha na vifaa vya kutosha ili kutengeneza barabara kwa kiwango kinachotakiwa.

Kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa imependekeza barabara zifuatazo zihudumiwe  na *TANROADS* kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya  haina uwezo wa kuhudumia barabara hizi kifedha. Barabara ya Gulwe - Berege – Mima – Seluka, barabara ya Mpwapwa – Kimagai – Godegode – Pwaga – Mbuga hii ni pamoja na kujenga daraja la Godegode ambalo lipo karibu na *Godegode Railway Station* na inaunganisha Jimbo la Mpwapwa na Kibakwe.

Kwa kuwa Serikali iliahidi kuweka lami barabara ya Mbande  - Kongwa – Mpwapwa, je, ahadi hiyo itatekelezwa lini ili kuwaondolea  wananchi wa Wilaya ya Mpwapwa kero ya usafiri hasa wakati wa mvua?

Kwa kuwa, barabara ni uchumi na  maendeleo katika nchi yetu, je, kwa  nini Serikali isitenge fedha za kutosha kutengeneza  barabara? Je, Serikali inatenga fedha  kiasi gani katika Bajeti yake ya mwaka  kutengeneza barabara?

Kwa kuwa daraja la barabara ya kutoka Hospitali ya Wilaya kwenda Vinghawe  eneo la *TANESCO*/Hazina  limeshabomoka  na  hii ni dharura. Je, Serikali itaanza lini kujenga daraja hilo?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, Naibu Waziri Dr. Milton Mahanga alipotembelea  mkoa wa Rukwa alitembelea na kuona ubaya wa barabara ya kutoka Nyangalua mpaka Kipeta (Kilyamatundu) inayotenganisha Wilaya ya Mbozi, pia aliona  barabara ya kutoka Kalambazita kwenda Ilemba Rukwa. Alitoa ahadi kuwa Serikali itaangalia  uwezekano wa kuzichukua barabara hizo ambazo zitakuwa kuingokati ya barabara kuu ya Tunduma – Sumbawanga.

Kwa kuwa sasa  tunapitisha sheria, naomba barabara hizo mbili ziwekwe.

**MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO:** Mheshimiwa Waziri napenda kukupongeza sana kwa hoja yako ambayo umeiwasilisha kwa wakati muafaka. Pongezi hizi pia ziwafikie Naibu Mawaziri wako wawili, Katibu Mkuu na maofisa wenu wasaidizi. Nawapongeza pia kwa jinsi mlivyoweza kushirikisha wadau mbalimbali tukiwemo sisi Wabunge.

Kwa mara ya kwanza Wizara imeweza kuorodhesha barabara za Kitaifa, Kimkoa, Wilaya hata Vijijini na kuweka urefu, upana na maeneo ya kila barabara. Sheria hii na viambatanisho vyake vitatusaidia sana kwa njia mbalimbali. Kwa kuwa barabara zetu nyingi

hasa zile za vijijini ni za udongo na changarawe, sheria hii itasaidia katika maeneo yafuatayo:-

Moja, kujua gharama za matengenezo ya barabara hizo hasa pale tunapotaka kupandisha daraja (Kiwango) la barabara, kufahamu upana wa barabara kutasaidia wananchi kufahamu mwisho wa kila barabara hivyo kuzuia ujenzi wa nyumba katika maeneo ya barabara. Kwa maana hiyo kuzuia hatua za bomoa bomoa jambo linalowafanya wananchi kuilalamikia Serikali yao.

Mapendekezo ni kwamba Serikali ijitahidi kuweka vibao angalau mwanzoni na mwishoni mwa kila barabara kuonyesha mapana ya barabara hizo ili wananchi/watu wasiingilie maeneo ya barabara.

Pili, Mheshimiwa Waziri napendekeza pia siku zijazo zinapoorodheshwa au kutengeneza barabara hasa kule vijijini, wananchi wakazi wa maeneo hayo washirikishwe angalau kwa ushauri. Kwani nimegundua kuwa barabara nyingi za Mkoa wa Pwani ama zimekosewa majina au urefu wa barabara. Kwa hili nategemea kukuarifu baada ya kurudi Kisarawe, baada ya kuyahakiki makosa hayo ili yasahihishwe.

Matengenezo ya barabara za Wilaya ya Kisarawe. Barabara ya Pugu – Vikumbulu, urefu wa kilometa 95.9. Hii ndiyo barabara kuu ndani ya Wilaya. Lakini ni barabara pekee itokayo Dar es Salaam kwenda nje ambayo haina lami isipokuwa kilometa 16 tu ambazo zimepatikana kwa meno kwa kuwafuata Mawaziri wenzako wote waliokutangulia katika Wizara hii, maswali mengi tangia 1996 hadi leo na mwishoni kutaka rufaa kwa Rais wa awamu ya tatu ambaye ameingilia kuagiza ijengwe angalau hizo kilometa 6 kufikia Ofisi ya Wilaya. Tafadhali Mheshimiwa Waziri hebu iangalie barabara hii kuanzia bajeti ya mwaka huu tupatiwe angalau kilometa 20 kila mwaka.

Tatu, barabara ya Maneromango hadi Mlandizi kilometa 65.2. Barabara hii ni kuu ya pili kwa ile ya Pugu – Maneromango. Pia barabara hii inaunganisha Wilaya Kisarawe na Kibaha, ni ya Mkoa ingefaa ipandishwe daraja kuwa ya lami kama haiwezekani basi tuanzie na ngazi ya changarawe ya kuaminika.

Barabara ya Kibaha Maili Moja – Mpuyani yenye kilomita 20. Barabara hii ina umuhimu wa aina mbili, moja, inaunganisha Wilaya za Kibaha na Kisarawe na pili, inakwenda sanjari na barabara ya Kibaha – Dar es Salaam.Kwa kuzingatia msongamano wa magari katika barabara ya Kibaha – Dar es Salaam na ajali zinazotokea, hii barabara ya Kibaha – Mpuyani – Kisarawe itakuwa mbadala kama itawekwa kwenye kiwango cha lami.

Mheshimiwa Waziri, kama unavyofahamu barabara ni roho ya maendeleo. Wilaya ya Kisarawe iko nyuma sana kimaendeleo. Kwa hiyo, nakuomba sana uzitupie macho sana barabara hizo tatu nilizozitaja ili kuwasogeza wananchi wa Wilaya ya Kisarawe karibu na Watanzania wenzao kimaendeleo.

Mheshimiwa Spika, naiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, barabara inayounganisha Wilaya ya Bukoba na Wilaya ya Misenyi, barabara hii inaanzia Kafunjo, Kata ya Nyakimbili, kupitia Kata za Ibwera, Burelankuzi, Rubale, Izimbya, Ruhunga, Kyamulile, (Bukoba Vijijini), Kilimilile na kuishia Kyaka ( Kata za Wilaya za Misenyi)

Barabara hii inaunganisha Kata tisa zenye jumla ya wakazi zaidi ya 90,000 kufuatia sensa ya mwaka 2002. Barabara hii imezunguka Ziwa Ikimba eneo linalochangia zaidi ya 70% ya uchimi wa Wilaya ya Bukoba Vijijini na kuifanya hii barabara kuwa na magari mengi sana yanayofanya shughuli za kibiashara ikiwemo kusafirisha mazao ya wananchi wakazi wa maeneo niyoyataja.

Barabara hii kwa sasa iko chini ya Halmashauri ya Bukoba vijijini, lakini Halmashauri imeishakiri kushindwa kuihudumia barabara hii. Tatizo hili limeisha wakilishwa kwenye kikao cha *Regional Road Board* na kupitishwa kupandisha hadi ya barabara hii kuwa ya mkoa. Shabaha ya maelezo yangu ni kuona namna gani sheria hii inaweza ikawezesha kufanikisha kilio cha kuondoa adha ya barabara hii ambayo kwa namna ilivyoharibika imebatizwa jina la utani la Karamagi. Hii ikiwa na maana nimeshindwa kuwasemea juu ya tatizo lao hili.

Mheshimiwa Spika, nashukuru na ninawasilisha.

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia kwa maandishi hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ningependa kupewa maelezo sababu zilizopelekea barabara inayounganisha Wilaya za Makete (Lupila) na Ludewa kutokuwepo kwenye orodha ya barabara za mkoa. Vikao vya mkoa vya ushauri vilikwishapendekeza kuwa barabara hii ipandishwe hadhi na ni muhimu sana kwa kukuza uchumi wa Wilaya hizi mbili.

Mapendekezo ya kuboresha barabara nchini. Wakala wa Barabara *(TANROADS)* wafanye utafiti wa barabara. Utafiti wa kina kwa barabara za Mkoa unaweza kusaidia sana wakati wa kugawa mafungu ya fedha kwa mfano, udogo wa barabara za Makete haulingani na ule wa Njombe, kina cha mvua Makete siyo sawa na mahali pengine nchini hii ina maana kwamba *effects* za shilingi 1,000,000/= katika barabara za Makete itakuwa ndogo au siyo sawa na zile *effects* za fedha hiyo hiyo kwa barabara za Njombe au Dodoma.

Mheshimiwa Spika, *research* zikifanyika zitasaidia Wizara /wakala kuonyesha ni barabara zipi katika kila Wilaya Kitaifa zinahitaji fedha zaidi kwa kila kilometa kuliko sehemu nyingine. Kama tutaendelea na mtindo wa sasa a kugawa *equally*, basi hatuwezi kufanikiwa kujikwamua katika dimbwi hili la barabara mbovu.

**SPIKA:** Baada ya hilo sasa namwita Mheshimiwa Naibu Waziri wa Miundombinu.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kukushukuru kunipa nafasi hii niweze kuchangia na mimi katika Muswada huu wa Barabara wa mwaka 2007. Lakini kabla ya hapo na mimi nichukue nafasi hii kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kuzungumza, nitoe rambi rambi zangu za dhati kwa ndugu wa marehemu waliofiwa kutokana na kifo cha Dr. Chiduo, vile vile kifo cha mama yake mzazi, Mheshimiwa Bakari Mwapachu na wale wote waliopata maafa kwenye ajali ya basi. Nichukue nafasi hii vile vile kumpongeza Mheshimiwa Mtutura kuwa Mbunge katika Bunge hili kupitia Jimbo la Tunduru.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, niseme kwamba kama mlivyoona hoja zilikuwa nyingi, hakika Mheshimiwa Waziri atakuwa na mengi ya kusema na kujibu. Mimi nitachangia hoja chache kutokana na muda wenyewe ulivyo. Lakini kwa ujumla kama ambavyo bila shaka atasema Waziri tunashukuru kwamba michango imekuwa mizuri sana katika kuuboresha Muswada huu, na kwa kweli tumechukua michango yote na kama tutakavyokuwa tunajibu ni kwamba michango mingi kwa kweli tunaichukua kwa maana ya kuifanyia kazi ili tuwe na sheria nzuri ya barabara.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo labda nijibu hoja chache tu kati ya wale waliochangia kwa maandishi, nikianzia na Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, ambaye kwanza alizungumzia kuhusu barabara ya *TAMCO* Kibaha kwenda Mapinda, Bagamoyo kwamba iwe ni *Reagional Road.* Kama ambavyo tumesema, Waziri alieleza na kama ambavyo tutakuwa tunajibu hapa, kwa kweli, maombi mengi haya ambayo yameletwa kwa maana ya kupandishwa daraja, yote tutayafanyia kazi na mengine ambayo yatakuwa yanaletwa.

Mheshimiwa Spika, mimi ningeshauri kuwa Waheshimiwa Wabunge ili kuweza kuendelea kupata faida ya wadau wengine, basi tutakaporudi na lile Jwedwali tuwashirikishe na Madiwani pamoja na mabaraza yetu kwenye Halmashauri ili kuona ni barabara gani zimesahauliwa na ziweze kuletwa haraka ili tuweze kukamilisha lile Jedwali na maombi hayo yote tutayazingatia kulingana na ibara ya 12 kama ambavyo inamruhusu Mheshimiwa Waziri kuweza kuziainisha barabara hizo.

Kwa hiyo, barabara hii kwenda Mapinga vile vile itaangaliwa wakati tunaangalia kulingana na vigezo. Amezungumzia vile vile maana ya maneno tatu, nne, sita katika *road class* ambavyo yamefafanuliwa katika ukurasa wa lile Jedwali la kwenye ule upande wa barabara za Wilaya pale chini kuna *key* inaonyesha kwamba namba tatu, maana yake ni *District Road* namba nne maana yake ni *feeder road* namba sita maana yake ni *urban roads.*

Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, na yeye amezungumzia barabara zake za Ubena-Kiganila kwenda Mvuha ambayo ni kilomita 60. Imekuwa ikishughulikiwa na *TANROADS* lakini kwa kweli ilikuwa haijashughulikiwa. Sasa itaangaliwa kwa vigezo ambavyo nimevitaja tuone kama vinakidhi na kama vinakidhi hakuna shaka yoyote hiyo barabara itawekwa kwenye *class* ambayo inahusika.

Mheshimiwa Pindi Chana, alizungumzia kuhusu Bodi ya Barabara ya Mkoa na akazungumzia kuhusu Viti Maalum. Kwa kweli ukiangalia marekebisho tuliyofanya na ambayo kwa sasa yanaonyesha kwamba ni Wabunge wa Majimbo pamoja na Wabunge wasiozidi wawili wengine wa viti vingine, viwe ni viti maalum, au viwe ni wa kuteuliwa, angalau wawili kwa kila mkoa. Na utakuta kweli ukishachukua Wabunge wawili wa viti vingine Mikoa mingi sana kwa kweli wako Wabunge wawili wawili.

Sasa tulifanya hivyo kwa sababu ya uwakilishi ambao tumeona kwamba ukishachukua Wabunge wote wa Majimbo na Wabunge wawili wa viti maalum au wa kuteuliwa kwa kweli uwakili wa Ubunge unakuwa ni mkubwa katika mkoa huo. Lakini kuna mikoa mengine ambayo kwa kweli tungeacha tu wazi, kwa mfano, Dar es Salaam ukweli ni kwamba wapo Wabunge wa aina nyingine zaidi ya Wabunge wa Majimbo katika Mkoa ule. Sasa tukaona kwamba wawili kwa kweli watakuwa ni uwakili mzuri na mikoa mingine hiyo wote watakuwa wamo.

Aliulizia Mheshimiwa Pindi Chana vile vile maana ya maneno *Regional Roads, Feeder Roads*. Mimi nadhani ukisoma katika kifungu namba 12, 2, 3, na 4 utaona tafsiri yake ni nini. Kwa sababu inaelezwa tafsiri yake inaelezwa, ndiyo *classfication* yenyewe. Pia alizungumzia kifungu cha 51(d) kwamba muda wa adhabu ile ya kifungu isome siyo chini ya miaka miwili. Ttunakubaliana naye na hiyo tutawekea marekebisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa George Simba Chawene, alizungumzia barabara za jimboni kwake, na kwa kweli mimi nakubaliana naye kwamba hilo jimbo katika mkoa huo ambao hakuna hata barabara ya Mkoa, barabara zote ni za Wilaya. Lakini kitu muhimu ni kuangalia vile vigezo. Hiyo barabara kama alivyoelezea, kwamba inakwenda mpaka inajitokeza kule Mbuyuni Ruaha kama ndivyo itakavyokuwa hivyo, tutaangalia vigezo basi tuweze kuipandisha iwe ya Mkoa.

Mheshimiwe Gaudance Kayombo, Mbunge wa Mbinga Magharibi, na Naibu Waziri naye alizungumzia barabara za Mbinga-Litembo-Kirura-Mkiri na Mbinga-Mkumbi. Kama nilivyoeleza maombi haya au hoja hizi za barabara kupandishwa au kuwekwa na zingine ni kwamba zinatakiwa zipandishwe, zimeombewa zipandishwe na zingine hazionekani kabisa, masuala yote mawili yataangaliwa kwa mujibu wa Sheria hiyo na Kifungu Na. 12. Kwa barabara ambazo hazionekani kabisa ni vema kwa kweli tuendelee kuzileta ili tuweze kuzielewa na kuziainisha ipasavyo..

Mheshimiwa Mgana Msindai, naye alizungumzia nyingi tu, karibu 26 za Iramba Mashariki ziingizwe kwenye Jedwali. Tumezingatia hilo kwa sababu ameziorodhesha, lakini vile vile kwa maana ya kuzi-*categorize* tutaangalia kwa mujibu wa Sheria na Waziri atafanya inavyopasa.

Mheshimiwa Ussi Pandu, alizungumzia ahadi ya Mheshimiwa Rais Mstaafu, Benjamin William Mkapa, kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Amani-Mtoni Zanzibar. Hili tumelipokea na tutalifuatilia tukishirikiana na Serikali ya Zanzibar. Tuone hiyo ahadi ilikuwaje na nani anatakiwa ashughulikie, ukizingatia kwamba Wizara yetu kwa kweli si ya Muungano. Sasa tutaangalia tuishirikishe Serikali ya Zanzibar tuone ahadi hiyo imefikia wapi.

Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mbunge wa Babati alizungumzia vile vile suala la barabara za kutoka Babati kwenda Kiteto na Babati kwenda Simanjiro. Kama unavyojua Mkoa wa Manyara ni Mkoa mpya na barabara nyingi utazikuta kwamba hazijaainishwa.. Niwahakikishe kwamba kwa kweli tunalijua tatizo la Mkoa wa Manyara ambapo barabara zake hazipo katika Jedwali katika hii *inventory.* Tutaziingiza na kuziainisha ipasavyo kama hiyo barabara anayoieleza. *(Makofi)*

Vilevile alizungumzia barabara ya Babati kwenda Imbilili na ile inayokwenda Mbulu iwe ya Mkoa , vigezo vitaangaliwa. Wilaya ya Babati ina Halmashauri mbili kama alivyosema, barabara zitengwe kwa namna hiyo, ushauri huo umezingatiwa.

Kuhusu utaratibu wa kuwa na vitabu vidogo vidogo, mimi nadhani kwamba ni ushauri mzuri, tutazingatia baada ya kukamilisha kazi yote hii ya kuweka majedwali vizuri ili tuweke kwa kila mkoa na iweze kusambazwa. Ushauri huo umezingatiwa.

Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mbunge wa Mwanga na Waziri alizungumzia barabara yake Lembeni-Kilomeni kilomita 11 kwamba iwe ya mkoa. Tutaangalia kwa mujibu wa vigezo.

Mheshimiwa Spika, hoja zingine zilitoka kwa Mheshimiwa Mbaruk Kassim Mwandoro, Mbunge wa Mkinga, kuhusu baadhi ya barabara ya Mkinga. Nikubaliane naye kwamba tutaangalia kwa sababu nilipokuwa na ziara ya Waziri Mkuu tukiwa pamoja naye suala hili lilijitokeza sana. Barabara ya kuunganisha makao makuu ya Mkinga na maeneo mengine.

Mheshimiwa Blandes, kwa sababu ni Mwanasheria, alitoa ushauri mwingi tu wa kubadilisha, lakini inavyoonekana kwamba Mheshimiwa Blandes ile *schedule of amendments* ambayo tulikuwa tumeshatoa, mapendekezo yake mengi kwa kweli yalikuwa yamezingatiwa. Mengine yalikuwa kutaka kujua kama tafsiri kweli inajitosheleza, ingawaje kuna maeneo alisema kwamba tusiweke tafsiri zingine, kwa mfano, *right of way*, *road reserve, truck road, regional roads, board*.

Mheshimiwa Spika, sisi tunadhani kwamba tafsiri hizi ni muhimu ili kuweza kupata maana halisi kwa urahisi badala ya kutoziweka, na kwamba hatukuweka maneno ya kwenye suala la *multi courage road ways* kwamba tafsiri haionyeshi kwamba *the centre of the road.* Kwa kweli tafsiri hii inajitosheleza, *whether* barabara ni njia moja au ni *multi carriage*, tafsiri ile inajitosheleza.

Alizungumzia kuhusu wajumbe wa bodi, nadhani kwamba wale wajumbe waliowekwa kwa kweli wanakidhi katika kutekeleza yale majukumu ya barabara ya mkoa. Alizungumzia *composition* ambayo sisi tunadhani kwamba tuliyoweka inatosheleza . Kama nilivyosema mengine ni kwamba yamezingatiwa katika sheria na vilevile katika jedwali la nyongeza au *schedule of amendments* ambalo tumelishaliongeza.

Mheshimiwa Savelina Mwaijage, alizungumzia ubovu wa barabara unaotokana na matengenezo hafifu kutoka kwa makandarasi. Sasa ukiangalia kifungu cha 6 Mheshimwia Mwijage utagundua kwamba tunatoa msukumo mkubwa juu ya umuhimu wa barabara kutengenezwa kikamilifu kutokana na kuwepo na mipango bora. Sheria hii na kifungu hiki kitatuwezesha basi kufuatilia pale ambapo kuna wakandarasi wabovu na kuchukua hatua ambazo zinastahili. Barabara za mkoa wa Kagera kwamba zijengwe ziwekewe bajeti ya kutosha, hili kwa kweli inategemea na fedha ambazo zitakazokuwa zimeidhinishwa na Bunge hili katika maombi yetu ambayo tumepeleka Serikali.

Mheshimiwa Said Arfi wa Mpanda Kati, alizungumzia kuhusu tafsiri na hizo ambazo nimeshazitoa namba tatu, nne, na sita *district road*, *feeder roads* na *urban roads,* amezungumzia kwamba sheria itamke uzito wa magari. Hili amepewa Waziri mwenye dhamana ya barabara kwamba awe anaanda kanuni ambazo zitaeleza uzito huo, hakuna sababu ya kuweka moja kwa moja kwenye sheria.

Mheshimiwa Spika, kwamba mafuta yanayowekwa barabarani yawe na ubora wa aina moja unaoeleweka kwa wote. Nadhani ushauri ni mzuri. Kuhusu masuala ya alama tumezingatia maelezo kwamba *TANROADS* imeondolewa kuwa Katibu wa Bodi ya Barabara ya Mkoa na badala yake amewekwa RAS. Hilo limeangaliwa baada ya kuangalia kwamba

suala la uwajibikaji ni muhimu pamoja na utawala bora. Tumeona kwamba ni vema kwa sababu yeye meneja wa *TANROADS* ndiye hasa anawasilisha mambo mengi kwenye bodi hiyo na basi ingekuwa vema asiwe ndiye Katibu. Vilevile ukiangalia *composition* ya wale wajumbe inatakiwa mtu kama *RAS* ambaye ana nafasi kubwa ndani ya mkoa ule, aweze kuitisha vikao vile kama Katibu.

Mheshimiwa Wilbrod Slaa amezungumzia suala la madaraja ya barabara kushirikiana na TAMISEMI, hili limewekwa vizuri kwenye sheria, Waziri atakuwa anashauriana na TAMISEMI. Barabara anayozungumzia ya Odean, *Junction* kwenda Kande, Matara, mpaka Lalavo, hilo tumezingatia kwa sasa hayumo kwenye *schedule* lakini itawekwa kwa sababu ni barabara, ni muhimu *class* gani iwekwe, tutaweka kulingana na sheria. Mheshimiwa Herbert Mntangi, tumepata masahihisho, kuhusu barabara ambayo umeitaja, Bombani hadi Kimbe isomeke kwamba Bombani kwenda Kimbo, na baadhi ya barabara katika wilaya ya Muheza tumezingatia na tutaendelea kuweka.

Mheshimiwa Mercy Emmanuel, Dodoma, Singida, Sherui umesema barabara ni mbovu, ni kweli kwamba barabara imekuwa mbovu lakini jitihada ambazo zimefanywa kwa siku za karibuni tungeweza kabisa kufikia mwaka wa kesho barabara kutoka Dar es Salaam kwenda Mwanza iwe na lami, lakini kuna kipande hicho ambacho kimeleta mgogoro tumechelewa, ambacho ni cha Manyoni mpaka Isuna. Sasa kipande hicho cha kilomita 55 kwa kweli ndicho kitachelewesha barabara yote kutoka Dar es Salaam kwenda Mwanza kwa sababu kipande hicho kwa utaratibu tuliouweka kitaanza bila shaka kupata mkandarasi kabla ya mwisho wa mwaka na baada ya miezi labda thelathini, tuseme katikati ya mwaka 2010, kipande hicho kitakuwa kimekwisha. Kwa hiyo, barabara nzima itakuwa imekamilika. Lakini vipande vingine vyote vilivyobaki ukiacha hicho tunategemea kufikia mwakani mwishoni vyote vitakuwa vimekamilika.

Lakini Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, tena alizungumzia kuhusu masuala ya *road bumps* maeneo ya Maili Moja, ishara ziwekwe juu. Suala la upana wa *road reserve*, fidia izingatie thamani, magari mazito mbalimbali pale Mbezi *technical audit*, masuala yote haya ni mazuri, ushauri huo tumeuchukua. Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, naye alizungumzia kuhusu kuunga bajeti mkono kwamba bajeti iongezwe na hivyo kwa kweli tumeshukuru na tumepokea huo ushauri lakini kupandisha barabara za wilaya ya Kilindi tumekubaliana naye kwamba tutaangalia barabara hizo.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa hoja ya Mheshimiwa Harison Mwakyembe ambaye alizungumza kuwepo kwa kipengele cha kujenga vyuo, hili ameshalizungumza hata kwenye maswali na ndani ya Bunge, na hili tumelizingatia katika *designs* za barabara ambazo ni *truck roads* ambazo zitaendelea kujengwa, na vilevile kuweze kuwepo hata barabara ambazo tayari zimeshajengwa, tutaangalia uwezekano wa ku-*provide* ili tujenge maeneo hayo, badala ya watu kwenda kuchimba dawa.

Suala la barabara ya Halmashauri iendayo bandari ndogo ya Kiwira ipandishwe daraja kuwa Mkoa, tumelizingatia, tutaangalia kulingana na vigezo na kuwe na kipengele kwenye sheria hii kinachogusa Halmashauri, ziruhusiwe katika ujenzi na usimamizi wa makandarasi wanaotengeneza barabara za mkoa. Suala la uteuzi wa makandarasi na usimamizi wake ni la kiutendaji, hivyo, ni bora likafanywa na mamlaka husika, kwa sababu Waziri ametoa mamlaka. Kulingana na barabara hiyo ipo kwenye mamlaka; ipo kama ni ya *TANROADS* ifanywe na *TANROADS* kama ni Halmashauri, ifanywe na Halmashauri, na kama ni mamlaka zingine kama TANAPA na kadhalika zitafanywa na mamlaka husika. Lakini kutakuwa na

ufuatiliaji na *feedback* kufika kwa Waziri kuona kwamba kweli barabara hizo zinajengwa kwa mujibu wa sheria hii mpya ya barabara.

Baada ya kusema hayo, nashukuru sana. Kama nilivyosema Mheshimiwa Waziri atakuwa na nafasi ya kujibu hoja zingine zilizobaki na vilevile kutoa maelezo mengine ya ufafanuzi. Naomba kusema tena kwamba nakushuru na naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii tena ili niweze kuhitimisha hoja ya Muswada wa barabara ambao upo mbele ya Bunge lako Tukufu.Lakini kabla sijafanya hivyo na mini napenda nichukue nafasi hiyo kuungana na Wabunge wenzangu kwa kutoa salam za rambirambi kwa Mheshimiwa Harith Mwapachu, kwa kufiwa na mama yake mpendwa, ambaye mimi ni ndugu yake. Pia kwa Prof. Msolla kwa kufiwa na mdogo wake, tunaomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu hawa mahali pema peponi.

Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri Dr. Makongoro Mahanga kwa kunisaidia kujibu baadhi ya hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge katika mkutano wako. Kama kawaida, maana imesemwa na waliopata nafasi ya kuchangia Muswada huu wa barabara ni roho ya maendeleo. Barabara ni siasa, barabara ni uchumi, barabara zinafuata bidhaa na yote haya katika mwisho wake, ndiyo yamezaa mchango mzuri ambao tumeupata kutoka kwa Wabunge, lakini pia kwa idadi kubwa ya Waheshimiwa Wabunge ambao wameomba wachangie hoja hii. Kwangu na Wizara yangu na wasaidizi wangu imekuwa ni kama tupo kwenye mkutano wa bajeti, lakini imetusaidia sasa kuyafahamu maeneo mengi ambayo Waheshimiwa Wabunge wangelipenda kupata maelezo ya Serikali sio kupitia kwenye Muswada huu maana Muswada unaweka misingi tu lakini katika bajeti ijayo na zijazo za Serikali, tunawashukuruni sana Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, sasa nianze kwanza kwa kuwatambua Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia kwa kuongea humu Bungeni. Nianze na msemaji wa Kamati ya Miundombinu ambaye alisema kwa niaba ya Mwenyekiti, Mheshimiwa Hafidh Ali, Mheshimiwa Bakar Shamsi Faki, Mheshimiwa Pascal Degera, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Katagira, Mheshimiwa Mpesya, Mheshimiwa Janeth Kahama, Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa Chacha Wangwe, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mheshimiwa *Eng*. Benito Malangalila, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Suleiman Sadiq, na mwisho kwa kutajwa sio kwa umuhimu ni Mheshimiwa Yono Kevela.

Mheshimiwa Spika, idadi ya Wabunge waliochangia Muswada huu kwa maandishi ni 63, naomba sasa niwatambue tu kwa haraka haraka kwa sababu ya muda. Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Ussi Pandu, Mheshimiwa Omar Kwangw', Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Gosber Blandes, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Said Arfi, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Meryce Mussa Emmanuel, Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Dr. Harison Mwakyembe, Mheshimiwa Paul

Kimiti, Mheshimiwa *Eng.* Luisa Mhina, Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mheshimiwa Grace Sindato Kiwelu, Mheshimiwa John Momose Cheyo, Mheshimiwa *Eng*. Benito William Malangalila, Mheshimiwa Antony Diallo, Mheshimiwa Janeth Masuburi, Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, Mheshimiwa Anastazia Wambura, Mheshimiwa Janet Kahama, Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, Mheshimiwa *Eng*. Stella Manyanya, Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mheshimiwa Stephen Wasira, Mheshimiwa Zuleikha Haji, Mheshimiwa Saidi Nkumba, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Juma Kilimbah, Mheshimiwa Mpesya, Mheshimiwa Jackson Makweta, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Stephen Galinoma, Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Fatuma Abdallah Mikidadi, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Athumani Said Janguo, Mheshimiwa Castor Ligalama, Mheshimiwa Zuberi Ali Maulid, Mheshimiwa Clemence Beatus Lyamba, Mheshimiwa Nazir Karamagi, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Elieta Switi, Mheshimiwa Prof. Idris Ali Mtulia, Mheshimiwa Abdu Marombwa, Mheshimiwa Idd Azzan, Mheshimiwa Ephraim Madeje, Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge na mwisho kwa kutajwa lakini sio kwa muhimu ni Mheshimiwa Kajenge.

Tunawashukuru sana wote mliochangia na wengi mmetupongeza kuwa Muswada huu umeandikwa vizuri, mtu muungwana anapokupongeza ni kawaida kusema asante. Kwa niaba ya Wizara, napenda niwashukuru sana kwa pongezi ambazo mmeipatia Wizara hii lakini na Serikali kwa ujumla kwa kuleta Muswada huu. Kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ya msingi wakati nawasilisha Muswada huu, tunatekeleza sera ya uchukuzi ya mwaka 2002 ya sera ya ujenzi ya mwaka 2003.

Ukiyasoma haya ndiyo Serikali iliahidi kuyatekeleza hayo kwa kupitia sheria. Sasa tuna zoezi lingine ambalo linaendelea sasa hivi Wizarani ambalo tunashirikiana na Wizara ya Usalama wa Raia. Ni suala zima la usalama barabarani. Tunataka kuja na sera mpya ya usalama barabarani na baadaye na sheria mpya, ili ziaendane na sheria hii.

Mheshimiwa Spika, ajali nyingi ambazo zinatokea katika barabara zetu nchini zinatisha sana, zingine zinatokana na uzembe na madereva, ubovu wa magari lakini katika sehemu nyingi unaweza ukasema pia na hali ya barabara zetu. Lakini yote haya tunataka tuyashughulikie kwa pamoja.

Nishukuru sana Kamati ya Miundombinu, katika kuiunga mkono hoja hii imeelezea tatizo kubwa ni fedha, na Wabunge wengine waliofuata, Mheshimiwa Peter Serukamba na wengine wamelisemea vizuri sana suala hili, tatizo ni fedha. Serikali ingelipenda barabara zitengenezwe, tena zipitike kwa usalama, tuweze kufika tunakokwenda kwa haraka. Lakini kama tunavyoeleza hapa sasa hivi kupitia mfuko wa barabara, tunaweza tu kukusanya shilingi bilioni 78 na ukizigawa hizo asilimia 30 ziende kwenye Halmashauri TAMISEMI, na asilimia 70 unakuta mgawanyo wa shilingi 59.9 au 60 bilioni ndiyo zinazoenda kwenye matengenezo ya mtandao wa barabara kuu na barabara za mikoa. Sasa kwa mtandao huo wa kilomita 30,000 ni hatari, huwezi ukatengeneza na linakuwa baya zaidi sasa unapoangalia zinabaki shilingi 18.1 bilioni za barabara za vijijini. Kwa hiyo, ukiangalia mahitaji halisi ili tuweze kutengeneza barabara huu mtandao wetu ambao tunasema wenye sura ya kitaifa, na ukaingiza na zingine hizi tunazosema asilimia 30 za wilaya, tunahitaji takribani shilingi bilioni 221, huo ndiyo ukweli.

Tunaweza tukaangaliana hapa, tunafukuza mbuyu, tunatafuta mchawi lakini huo ndiyo ukweli. Kwa hiyo, lazima tuendelee kukubali tutafute mapato tuyapate wapi, nashukuru

jana tulisikia ushauri kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge, mwendelee kuishauri Serikali yetu, kwa sababu huko ndiko lazima tuelekee. Kama alivyosema Mheshimiwa Serukumba, hawa tunaoshirikiana nao katika kuzitengeneza hizi, na wao wanasema jamani, hivi ninyi Tanzania mkoje? Tunashirikiana na ninyi kutengeneza barabara hizi ambazo wote mnajua mnazijenga kwa gharama kubwa, lakini mbona hamzitengenezi? Hamuweki fedha ya kutosha kwa matengenezo ya barabara! (*Makofi*)

Sasa kupanga ni kuchangua. Mwalimu alikuwa anatukumbusha kila wakati, sasa huwezi ukaendelea kwa hali hii kuendelea kudai barabara nyingi za lami huo ndiyo ukweli, huwezi ukaendelea kudai barabara za lami katika hali hii. Tukubali tuzitengeneze kwanza zile ambazo tunazo, ni akili ya kawaida tu, kwa hiyo, mimi nasema tukienda vizuri kwa maeneo yaliyotajwa tuongeze tozo kwa mafuta, sasa lita moja shilingi 100. Nilimsikia Mheshimiwa Kimiti, tena kaongea kitaalamu sana, tunaogopa mfumuko gani wa bei hiyo hata ukiongeza kwa asilimia mia, haya ndiyo mawazo lakini tuyapime pia, kwa sababu hutaki tu ukaangalia upande mmoja wa sarafu. Lakini sisi upande wa Serikali na wenzetu wa Wizara ya Fedha na Mipango tunaangalia uwezekano maana sasa hivi kuna hiyo *flat* hiyo *rate* ya kodi ya magari kwa mwaka, *Tshs*. 20,000, uwe na pikipiki ya *cc* ya 50, shilingi 20,000.

Mheshimiwa Spika, uwe na shangingi, shilingi 20,000 uwe na *pick-up* kubwa ile shilingi 20,000, ndiyo nasema ni vizuri utaratibu huu tuuangalie hii *annual access fee,* tuiangalie maana Uganda wenzetu wamefanikiwa sana katika eneo hili, tunaamini hili tukilisimamia vizuri litatupatia fedha za ziada, na *road fund* zitaongeza kidogo kwa lita ukizichanganya hizi tutapata *mileage*. Wenzetu hawa wanatuambia hivyo hivyo watu wa MCC wanasema, “hivi Tanzania jamani barabara hizi ni muhimu sana kama mnataka kuibua uchumi wenu”. Sasa hali ndiyo hiyo, wanasema pia kwamba tuna hili zoezi tunalifanya pamoja na hazina na benki ya dunia na Wizarani pale, wanasema hata shilingi milioni 100 kwa lita makusanyo yake hatuna uhakika kama kweli zote zinarudi, sasa tunalifanya zoezi hili na lenyewe tuone kama makusanyo hayo yanaweza yakawa zaidi kulivyo ilivyo sasa.

Tumesikia labda tuangalie madini yachangie, ni ushauri tutauangalia tuweze kuona nini cha kufanya. Nilisahau na yeye kumwingiza Mheshimiwa Naibu Waziri katika Wabunge waliochangia kwa kuongea humu Bungeni, Mheshimiwa Dr. Makongoro Mahanga, Mbunge wa Ukonga. Hiyo ninahitimisha kwa orodha ya waliochangi kwa kuongea humu Bungeni. Nilikuwa nasema katika barabara hizi ambazo miradi maalumu ambayo ilikuwa imekwama, tunaijua ilikuwa mitatu, Dodoma Manyoni, ingawa tulianzia kwa ujenzi Singida, Manyoni, na upande wa Kusini ni barabara ya Mbwe Mkulu-Lindi-Mingoyo.

Katika historia tumefanya mazungumzo na wakandarasi hawa tumefikia mahali pazuri ili waanze kazi na dalili mkipitia sasa unaona *visibility,* wameanza kurejea katika maeneo ya kazi. Ni azima yetu tuhakikishe kuwa muungwana anapokubali kitu, hutekeleza. Kitendo hiki tunategemea katika bajeti ijayo ya Serikali ambayo tumekubaliana nayo tutaweza kuyatengea fedha ili barabara hizi tuzikwamue.

Niunganishe tu hapa kwa kusema kabisa kabisa kwa moyo wa dhati, sehemu ya Singida, Iguguno, Senkenke mpaka Sherui Mkandarasi anaendelea vizuri. Kwa hiyo Mheshimiwa Msindai na wengine wa maeneo hayo msiwe na wasiwasi. Lakini kwa ndugu zangu Watanzania wanaotumia barabara ya kutoka Dar es Salaam, Mkuranga, Kibiti, mpaka Mtwara, nataka tuwahakikishie kupitia Bunge lako Tukufu kwamba sehemu korofi hiyo ya sasa iliyobaki ya Ndundu-Somanga, Serikali imeshatoa tangazo la kuitisha zabuni, na

tunatarajia wazabuni ambao watapenda kuifanya kazi hii watarejesha zabuni zao ifikapo tarehe 19 Juni., 2007. Hiyo ndiyo hali ya ukanda huo.

Mheshimiwa Bakar Faki, akiongea kwa niaba ya Kambi ya Upinzani alitoa ushauri kwa Waziri aonyeshe jinsi sheria hii inavyokidhi matakwa ya usimamizi wa barabara. Sheria yoyote hata hii tunayopendekeza ifutwe, iliyotungwa mwaka 1932, ambayo imetufanyia kazi nzuri, tunaileta haya ambayo Mheshimiwa Mbunge anauliza kwa usimamizi wa barabara, unaiona ile sura nzima katika Muswada huo. Uliuliza pia kwanini Kamanda wa Trafiki wa Mkoa au ofisa asiwe mjumbe wa Bodi ya barabara ya mkoa. Nadhani alikuwa amesahau kwamba katika sheria ya Usalama barabarani ya mwaka 1973, *RTO* ndiyo Katibu wa baraza la usalama barabarani la mkoa.

Kwa hiyo, ana ile kazi ya kiutendaji ya *enforcement* katika sheria hii. Pia aliuliza kuwe na kifungu mahususi kwa *TANROADS* kuingia ubia na sekta binafsi, hii ni hoja nzuri na ndiyo maana Muswada huu mnaona tunakuja na ile tuipatie *private sector* nafasi yake katika kujenga na kutengeneza barabara zetu na madaraja. Sasa kifungu cha 6(2)(c) kinaelezea bayana hiyo na kinafafanuliwa pia na kifungu cha 60 cha Muswada huu, kwa hiyo tunaelekea huko. Je, madaraja?

Mheshimiwa Naibu Waziri ameelezea ni nini hasa *number three* ukiona tatu ni *district road*, barabara ya wilaya, *number four* ni *feeder road*, namba tano ni *urban road,* utambalisho tu, lakini nikazie hilo hilo alilosema Mheshimiwa Naibu Waziri Dr. Mahanga, jedwali namba moja limewavutia sana Waheshimiwa Wabunge kwa sababu tulitaka iwe hivyo. Ndiyo linaonyesha hali halisi ya mtandao wa barabara zetu, yawezekana maeneo mengine tumeyakosea, ninyi ndiyo mnazijua zaidi barabara hizi kwa sababu mnazitumia kila siku katika kampeni kwenda kutembelea wananchi kuhamasisha maendeleo.

Kwa hiyo, tunaomba mtupe ule ushauri na sisi tutauunganisha pamoja na mapendekezo mengine ambayo ofisi ya Waziri Mkuu watakuwa wametuletea ili tukamilishe jedwali hili, litoke kwa uhakika. Fidia ilipwe kwa kuzingatia bei ya soko, sawa! Sheria ya Ardhi kama tulivyoeleza, maana tumegusia *Land Act,* tumeingiza pia *Village Land Act*, lakini pia kuna ile *Land Acquisition Act*, lakini pia kuna ile *Land Acquisition Act* ya mwaka 1967.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa fidia tunasema Mwananchi ambaye ardhi yake inaguswa kwa shughuli hizi afidiwe fidia iliyo kamilifu na ndio maana Sheria ya Ardhi ipo wazi kwa suala hili, apate fidia iliyo kamilifu. Mheshimiwa Degera amenisaidia sana, amesema suala zima la *road reserve* lifanywe haraka watu wajue kwa sababu maendeleo ndio yanatokana na hayo.Ninachoweza kusema hapa ni kwamba kwa mujibu wa kifungu cha 60 (2), kanuni zinazosimamia upana wa hifadhi ya barabara zinazotumika hivi sasa ndio kifungu hicho kinasema kanuni hizo zitaendelea kutumika hadi hapo kanuni mpya zitakapotungwa. Kwa hiyo, kupitia Bunge lako Tukufu tunapeda kusema wazi kwamba kwa barabara kuu, isipokuwa pale nimesema vinginevyo, ndio zile mita 22.5 kutoka katikati mwa barabara na unapokuwa na hiyo *carriage way* ile sehemu ya katikati inayobaki ni sehemu ya barabara kwa hiyo tunaanzia pale katikati kuzihesabu hizi.

Pia tuelimishe wananchi kuhusu matumizi ya barabara, *road reserve*, wengine wanatumia kutupa takataka, wengine wanatumia kuchukua mchanga, ni hoja nzuri na ndio maana sheria ipo wazi kwa suala hilo tunasema tuhakikishe kwamba inatumika kwa madhumuni ya kupanua barabara na *utility* zetu kama *TANESCO*, maji na wengine waambiwa wataruhusiwa tu kutumia eneo hilo kwa muda. Muda ukiiva wa kupanua barabara hiyo

itabidi nguzo za umeme, mabomba ya maji yahamishwe kwa gharama zao na siyo gharama za mamlaka ya barabara husika.

Mheshimiwa Mgana Msindai jedwali namba moja limeelezwa tutaendelea kuliboresha hakuna matatizo kama kuna barabara zimekosekana kama ilivyo kwa Mkoa wa Manyara hakuna tatizo na Wabunge wengi walivyoomba hapa walisema barabara zetu za Wilaya hizi zina umuhimu wa kipekee kwa masuala ya uchumi zipandishwe na ziwe daraja za mkoa.

Mheshimiwa Spika, baada ya sheria hiyo kupita, naomba Bunge lako likubali sheria ipite na ndio itawezesha sasa kufika katika hatua hii ya kujua maombi yaliyotoka mikoani kupitia *Regional Board*s zetu na mengine yametoka kwenye *RCC* yanashughulikiwa vipi. Sasa tunakuwa na vigezo angalau vya kuanzia siyo tu mtu anaamka, Andrew Chenge labda amekasirishwa na mke kule anakuja Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga anasema leo nataka barabara hii tuishushe daraja iwe ya wilaya, hii barabara leo ipande, hapana! Hatuwezi kwenda namna hiyo. Sasa tunaweka vigezo ambavyo vipo wazi, yawezekana siyo *perfect* lakini angalau tuna mahali pa kuanzia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, barabara ya Movigo mpaka Uganda ipandishwe, ni haya haya Mheshimiwa Eustace Katagira aliyaseme hayo. Mheshimiwa Benson Mpesya alizungumzia kuhusu fidia, masuala ya fidia yanashughulikiwa na Sheria ya Ardhi na siyo sheria hii. Ninachoweza kumjibu Mheshimiwa Mbunge ni kwamba masula ya ardhi fidia yake huwezi ukaiweka kwenye sheria nyingine, kwa hiyo, unkwenda kuitafuta fidia hiyo huko ndio maana tumezitaja sheria zote mbili kwa sababu tunajua vinginevyo kutaleta mgongano na lazima sheria zetu zisomwe kwa pamoja. Wizara ifanye *design* ya barabara zake ambazo usanifu wake umepitwa na wakati. Ushauri huu unazingatiwa sana na suala hili litatekelezwa kulingana na mahitaji ya wakati. Mheshimiwa Janeth Kahama amesema majina ya barabara utambulisho wake haupo? Unatembea Dar es Salaam nzima tabu tu, sasa ni kweli kabisa kwa sababu Wizara yetu kupitia sera ya mawasiliano ya posta na kwa kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI, Wizara ya Ardhi, Usalama wa Raia, Shirika la Posta lenyewe na Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano nchini, sasa tumebuni mradi wa kutumia anwani na namba za makazi zitakazowezesha makazi, barabara kutambulika kirahisi pamoja na kutumia anwani za barabara, makazi na mitaa kutumia namba maalumu zijulikanazo kama *post code.* Marekani wanaita *zip code* lakini ni hiyo hiyo zitatumika kupitia teknolojia iliyopo ya kompyuta ya kuwezesha kutambua kwa urahisi na tungependa mradi huu uanze mwezi Septemba. Sasa hapa ningependa Serikali twenda pamoja kwa sababu unakuta kila Wizara ina mradi unaofanana fanana lakini *information* ni ile ile na ndio maana tumezitaja Wizara hizi kwa sababu tunajua kuna ile ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa upande wa vitambulisho kwa sababu ungependa taarifa fulani ingawa ile ina mambo tofauti ya *allocation,* ungependa mkafika mahali mkaziunganisha hizo, mtandao wa Barabara za Afrika Mashariki tumeulizwa hasa ni zipi kwa sababu mnatukanganya kanganya tu hapa.

Mheshimiwa Spika, barabara ambazo zimekubalika kuwa zina sura ya mtandao wa nchi za Afrika Mashariki zina kilomita 12 LF 805 na kati ya hizo kilomita 8,214 yaani asilimia 64 zipo katika nchi yetu. Barabara hizo ni zipi? Barabara hizo ni Tunduma, Laela, Sumbawanga, Mpanda, Kasulu, Nyakanazi na ukiendeleza Nyakanazi unapanda nayo unaweza ukaenda upande wako mwingine unaenda mpaka Nyakasanza, unaenda Lusumo, Rwanda, unaenda Kobero, unaenda Burundi ndio dhana ya *connectivity* ambayo tunayo katika *Region* yetu hii na ukipanda juu unaenda mpaka Kyaka, Mtukura, Masaka. Barabara ya pili ni Dar es Salaam, Dodoma, Singida, Nzega, Tinde, Isaka, Lusahunga, unakwenda Kyaka,

Mtukura unaishia Masaka, Uganda na barabara ya tatu ni Tunduma, Mbeya, Iringa, Dodoma, Arusha, Namanga, Athi *River* unapita Nairobi unaenda Isiolo mpaka Moyale unaingia Ethiopia.

Mheshimiwa Spika, barabara ya nne ni Biharamlo, Geita, Mwanza, Musoma, Sirari unavuka unkwenda Badwa mpaka Chogio mpakani na Sudani na barabara ya tano inatoka Mombasa, Malaba, Kampala, Mbarara mpaka unafika Katuna, Rwanda. Hiyo ndiyo sura na kama unavyoona sasa hivi tumefanikiwa kwa barabara ya Arusha, Namanga kwa upande wa Tanzania na Namanga Athi *River* kwa upande wa Kenya. Hizi zinafanywa, tumeziombea fedha kwa pamoja na *executive executing emergency* ya utendaji huu utakuwa unasimamiwa na *EAC secretariat* lakini kwa kushirikiana na Serikali zote mbili kwa maana ya upande wetu wa *TANROADS* na wengine.

Mheshimiwa Shellukindo ametoa ushauri mzuri tunauchukua. Kasma ya vikao vya bodi, kuwepo kwa utaratibu wa kukagua barabara zetu hizi kabla ya vikao ni kweli kabisa kifungu cha 18 *notes* ya 14 muda hautoshi, sisi tunaamini unatosha kwa sababu hapa hatukusudii kuhamisha watu unaenda tu kumjulisha bwana tunakusudia hapa tumeona kuna mawe au miamba ambayo itatusaidia katika kutengeneza barabara hii, unampa taarifa hiyo siyo kwamba unamuhamisha pale hapana, kwa hiyo, ndio maana tunakuja katika hiyo. Je, hifadhi ya barabara izingatie maumbile *geographical* ya pale? *Correct* kama huku kuna miamba haiwezekani isipokuwa kama wewe una pesa ya kuweza kubomoa ule mwamba ili ufikie upana wa barabara yako unayotaka utafanya, lakini ukweli ni kwamba sisi kwa sasa hatuna uwezo huo, kwa hiyo, tutazingatia hali hiyo. Je, kuna alama za X ambazo zinatolewa kwa ubaguzi kwa Mbunge na mtu wa kawaida? Hapana hatuna vitu vya namna hiyo.

Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, amependekeza kifungu cha 19 (2), neno lisiwe *may*, lisiwe hiari kwa mamlaka kuchimba kokoto au mchanga kwenye maeneo ya watu. Sasa amesema ikiwe *may* italeta matatizo, hapana! Sisi tunasema hivi, limetumika neno hili kwa kuzingatia kuwa mamlaka ya barabara inapaswa itoe fidia kwa mwenye eneo hilo ukifanya ni *shall,* inaleta ubabe na Serikali inaongozwa na Wananchi au viongozi kwa niaba ya Wananchi lakini unataka Serikali hiyo iwe na staha, iwe ya waungwana na mambo yake yafanywe kwa mashauriano na maridhiano.

Mheshimiwa Spika, Odiani *junction* Mheshimiwa Naibu Waziri ameielezea vizuri sana na sisi tutaendelea kuliangalia hili, haimo kwenye jedwali kwa sababu haipo sasa katika sura hii ndio unataka uingize je, iwe ya mkoa au iwe nini? Kuhusu ahadi zilizotolewa tumeupokea ushauru huo tutaendelea kuufanyia kazi. Mheshimiwa Chacha Wangwe kasema maneno mazito jana lakini ninamshukuru sana Mheshimiwa Paul Kimiti aliliweka sawa suala hili. Nchi yetu ni kubwa lakini tujivunie mtandao ambao tumefikia sasa hivi na tutaendelea kuupanua.

Mheshimiwa Spika, wewe umefika Tarime siku za karibuni, ningependa tu nimuulize Mheshimiwa Chacha Wangwe kwamba hiyo lami iliyofika Tarime si imeletwa na Serikali yako? Tutambue yale mazuri ambayo yanafanyika, mimi nimesomea maeneo ya kwenu huko haikuwa hivyo, wananchi leo wamefurahi sana kwa lami kufika mjini Tarime. Ushauri wako tunaukubali sana kutumia Wananchi vijijini katika matengenezo na imetolewa hoja hii na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge ipo katika hotuba yangu na ipo katika Muswada ukiangalia kifungu cha 60 (2) (r).

Mheshimiwa Spika, eneo hili tunaweza tukawa na ajira kubwa sana lakini pia kubwa zaidi tukajenga ujuzi kwa wananchi wetu vijijini kuweza kusimamia barabara zao hizi ambazo ndizo wanazitumia wao na tunataka tuondokane na huu mtazamo ambao umo miongoni mwetu Serikalini kwamba ni *only an equipment best technology* ndio inayofaa. Sasa hili tayari sisi Wizarani tumeliandalia kanuni na miongozo, litakalofuata sasa ni kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu ili tuweze kuhakikisha kwamba zabuni zinazotolewa na Halmashauri zetu zizingatie suala hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa wale ambao hawapendi kutumia hii tutaona na tunaweza tukasema tu asilimia fulani ya fedha inayopelekwa katika Halmashauri zetu kwa matengenezo itumike kwa utaratibu huu, tutajenga ajira, tutapambana na umaskini katika maeneo ya vijijini. Mheshimiwa Paul Kimiti alitoa ushauri mzuri sana kwa kupanua wigo wa kodi, ndio hoja ya Kamati ya Miundombinu na Waheshimiwa Wabunge wengi walioongea humu Bungeni tunashukuru sana. Tushirikiane katika kuishauri Serikali ni maeneo yapi ambayo tunaweza kuongeza tukatunisha mfuko wa barabara. Lakini alikuja na hoja akasema tumesikia miaka mingi barabara ya Tunduma, Sumbawanga sasa hatuoni na tuliambiwa bilioni za fedha zitaletwa.

Mheshimiwa Spika, napenda niseme kuwa ni kweli ahadi ya Serikali katika barabara hiyo imekuwa ya siku nyingi na hii ni moja ya mtandao wa barabara ambao nimewaambia tunauona unatoka Zambia unakupeleka mpaka Rwanda, Burundi, unakupeleka mpaka Uganda , ni barabara muhimu sana. Sasa tumekuwa tukiongea na Serikali ya Marekani kupitia *Millennium Challenge Corporation (MCC)*.

Mheshimiwa Spika, mazungumzo yetu yanaenda vizuri na wameridhika sana na utendaji wa Serikali yetu katika maeneo haya na wao wanasema iwapo taarifa nyingine ambazo walikuwa wameomba zitakamilika yawezekana mwezi ujao au mwezi wa sita tutakuwa tumekamilisha zoezi hili, tujue sasa kwa barabara tunapewa kiasi gani. Kwa hiyo, tunategemea bado kwa Serikali ya Marekani kwa sehemu ya Tunduma, Laela mpaka Simbawanga. Sehemu ya Sumbawanga mpaka Mpanda, Kigoma, Kasulu na Nyakanazi, sehemu kubwa ya barabara hii sasa hivi inafanyiwa upembuzi yakinifu ipo katika hatua mbalimbali na baada ya pale ndio tutaanza kuzitafutia fedha.

Mheshimiwa Spika, lakini *MCC* hawaishii tu na barabara hii ya Tunduma, Sumbawanga, tumekubaliana nao watachukua sehemu ya barabara ya Tunduru, Natemanga, Songea, Peramiho *junction,* Mbinga mpaka Mbaba *Bay* ni barabara ndefu lakini tunaamini mazungumzo yalikwenda vizuri. Sehemu ya Masasi, Mangaka tumepata fedha za Serikali ya Japan tunaishukuru Serikali ya Japan. Sehemu ya kutoka Mangaka Lumesule kuja Tunduru ndio ilikuwa bado haijapata fedha, sasa tumekubaliana na Benki ya Maendeleo ya Afrika pamoja na *Japanese International Bank Corporation,* watashirikiana katika kutoa fedha za ujenzi wa barabara hii. Kuna Tanga -Holoholo lakini pia tunajaribu tuwa-c tuwashawishi na wao wafikirie kuchukua barabara ya makutano na hata Mgumu, Longido mpaka Mto wa Mbu, tunaomba anayeomba anaweza akakubaliwa au anaweza akakataliwa lakini pia tumeomba kiwanja cha Ndege cha Mafia na Kigoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tukifanikiwa haya tutakuwa tumeanza mwanzo mzuri. Mheshimiwa Peter Serukamba amesema kwamba pamoja na ubora wa Muswada na sheria itakayozaliwa na Muswada huu kama fedha haipo kazi itakuwa haijaenda, tunakubaliana na

wewe, ninashukuru sana na tunachukua na kuzingatia ushauri ulioutoa. Mheshimiwa Cynthia Ngoye barabara ya Katumba, Mbambo, Tukuyu iwekewe lami kwa hali kama alivyosema Rais, sawa kabisa ndivyo tunavyotaka na tutatekeleza ahadi hiyo kwa kuzingatia uwezo wa bajeti ya Serikali katika kipindi hiki tulichonacho mpaka 2010 na *Inshallah* CCM itarejea tena 2010 mpaka 2015 tukamilishe ahadi zote hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu uharibifu wa barabara unaotokana kulishwa wanyama barabarani udhibitiwe, Muswada huu umeweka suala hili vizuri sana katika Ibara ya 28 na Ibara ya 49 ya Muswada. Mheshimiwa Lekule Laizer, majina ya barabara si sahihi na hata Mheshimiwa Waziri Mkuu amenithibitishia hilo lakini ndio uzuri wa kuwa na viongozi ambao wanafuatilia kwa makini.

Mheshimiwa Spika, katika historia ya Bunge lako Tukufu, nadhani huu ndio Muswada wa pekee ambao umekuwa na majedwali manene yanayotisha lakini cha kufurahisha ni kwamba hilo halikuwatisha Waheshimiwa Wabunge wameweza kuzisoma barabara hizi na kugundua baadhi ya hitilafu hizi, tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, haya tutayasahisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Getrude Mongella alitoa ushauri mzuri sana wigo wa fedha za barabara uongezwe hoja hiyo hiyo, *technical audit* iimarishwe. Mapendekezo haya sasa kama utakavyoona katika *Additional Schedule of Amendment* tumeingiza hoja hii, iongezwe orodha hawa wanaolala barabarani walevi hawa wanakaa wanafanya vikao barabarani na wewe unapita na gari sasa tumekiweka sawa ili kionekane waziwazi. Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Suleiman Saddiq walitoa ushauri mzuri Serikali iimarishe matumizi ya miradi hasa ukaguzi, usimamizi wake lakini pia taa za barabarani hasa maeneo ya mijini.

Mheshimiwa Spika, tumeng'ang'ania umeme wa *TANESCO* tu wakati Mwenyezi Mungu ametujalia jua hili, mionzi hii! Kwa teknolojia ya leo wote tunajua inawasha taa na kufanya mambo mengine makubwa sana. Wizarani tunaliangalia suala hili na tungependa tutekeleze maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu *central business* ya Dar es Salaam lazima taa ziwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hicho ndicho kioo cha nchi yetu, kwa kadri fedha zinavyoruhusu tuhakikishe kwamba kweli barabara hasa katikati ya Jiji la Dar es Salaam, taa zinawaka usiku. Mheshimiwa Murad *TANROADS* usimamizi ni huo huo tutayachukua ni ushauri mzuri tu, barabara nyingi hazijitokezi katika jedwali, ni kweli kabisa lakini tumeeleza kwa nini na mmetusaidia kuyafafanua hayo.

Alama za barabarani, mapendekezo ni kwamba angalau ziwekwe mahali ambapo hazihatarishi, maana alama za barabarani ni kumsaidia mtumiaji tumpe angalizo kwamba mbele yako kule barabara inakata kona kali au kuna daraja. Sasa kama kuna matuta unaweka tu mita 20 unakuja kule unalipuliza ukijaribu breki pale ni hatari sana. Sasa ushauri huu ni mzuri sana na ndio maana Muswada ulivyoandikwa ni kwamba tahadhari hiyo iwekwe ambapo pia hapahatarishi usalama wa watumiaji wa barabara hiyo na eneo hili tutalieleza vizuri sana tutakapokuja na ile Sheria ya Usalama Barabarani.

Mheshimiwa Spika, hili *book* lote ni michango ya Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi, mengi wameyasema na baadhi yake ameyasema Mheshimiwa

Naibu Waziri. Mimi nisingependa sana nitumie muda mwingi kurudia yale ambayo ni yale yale hasa ya kuomba barabara zetu ziwe katika daraja hili lakini yote hayo tutayazingatia na nimwambie tu Mheshimiwa Mgana Msindai kwa Daraja la Mto Sibiti, tutajitahidi katika mwaka ujao wa fedha hatua ya kwanza iwe ni kwa ajili ya upembuzi yakinifu, tukimaliza hiyo tukajua gharama zake tuanze kutafuta fedha ya kulijenga daraja hili muhimu ambalo linaunganisha siyo tu Mkoa wa Singida na Shinyanga lakini na mikoa mingine jirani.

Mheshimiwa Spika, nimalize kama nilivyoanza kwa kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, lakini labda kidogo tu kwa sababu yawezekana ikawa siyo, Mheshimiwa Steven Galinoma amekuja kuniona mara mbili ameniandikia na katika mchango wake karudia tena anauliza ni lini barabara ya Iringa – Dodoma itajengwa kwa kiwango cha lami?

Mheshimiwa Spika, ni kweli tumekuwa tukilisemea sana suala hili na kweli tangu wakati huo tumechelewa sana, lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Wananchi wa Jimbo lake la Kalenga lakini pia na Wananchi wa Mikoa ya Iringa na Dodoma kwamba kwa sasa kupitia ufadhili wa *NORDC Development Fund* pamoja na Benki ya Dunia, Mkataba wa kuifanyia usanifu wa kina barabara hii tunatarajia uwekwe saini mwezi ujao mwaka huu. Kazi hii itatumia miezi kumi na nane.

Baada ya hapo sasa tutaanza kuhangaika kutafuta fedha na tunachofanya sasa Wizarani kwa sababu tunajua *ADB* wametuhakikishia kabisa kwamba katika *funding* ya *ADF* 11 ambayo ndiyo inaanza sasa hivi sehemu kubwa ya fedha itaenda kwenye kutengeneza miundombinu ya barabara. Sasa sisi Wizarani tunafanya kila liwezekanalo tuandae kwa barabara zote muhimu tufike katika ngazi ya kufanya upembuzi tumalize lakini tufanye upembuzi wa kina. Lakini tunakuwa tunazi-*pipe line* hizi barabara *ready* kuzi- *package* na kuzitoa kwa Wafadhili wakewemo hawa wa *ADB*. Kwa nafasi ya sekta binasfi nataka niseme tu kwamba itapendeza pia kwa upande wa Serikali na ndiyo tunafanya sisi Wizarani. Tuainishe barabara ambazo unaweza ukazi-*package* kwa utaratibu huo wa kuzipatia sekta binafsi. Kuna barabara zingine hata ufanye nini haziwezi kulipa kwa tozo.

Kwa hiyo, tunataka tuangalie ni zipi ukipiga mahesabu, hii inaweza kulipa haraka. Nimemsikia na namshukuru sana Mheshimiwa Kaboyonga asubuhi aliuliza kuhusiana daraja la Kigamboni. Naibu Waziri amejibu vizuri lakini haya ndiyo ungeweza kuyafanya kwa sababu *there is a lot of money* ambayo ipo *idle* kwenye *private sector*. Kwa hiyo, na sisi Serikali tusiwe tunashabikia tu kwa sababu nimeshika mimi kwanza, hapana. Hizo fedha tungeliweza kuzitumia kwa shughuli nyingine kama kujenga mashule, hospitali na barabara zetu, tukaiachia *private sector* ikayafanya haya. Kwa hiyo, tutaendelea kujipanga vizuri ili tuhakikishe tunatekeleza uhai.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema yote hayo, napenda nikushukuru tena wewe, niwashukuru sana viongozi, Wabunge, Mawaziri walionisaidia katika shughuli hii tangu maandalizi ya Muswada huu ulipoanza.

Niishukuru sana Kamati ya Miundombinu pamoja na wadau wote waliofika Dar es Salaam tarehe 4 na 5 kushiriki katika mchakato wa Muswada huu. Hayo mliyoyafanya ndiyo yamewezesha kile mnachosema Muswada umeandikwa vizuri sana umetokana na mchango mzuri wa wadau mbalimbali tunawashukuruni sana. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, nimalizie kama Kanuni zinavyotaka, kwa kusema naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu. Waheshimiwa Wabunge hoja hiyo imekwishatolewa na imeungwa mkono lakini kama Kanuni zinavyohitaji tutaiamua baada ya hatua ya Kamati ya Bunge Zima.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*
*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Barabara wa Mwaka 2007**
***(The Roads Bill, 2007)***

**SPIKA:** Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, bado hajataja vifungu, ametaja ukurasa tu.

Kifungu cha 1

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nilikuwa na hoja kwenye *title* ya *bill* yenyewe ndiyo maana nilisimama wakati inatajwa *bill.* Nahitaji tu ufafanuzi, kama sikosei Wizara hii siyo inayoshughulikia viwanja vya ndege? Isingekuwa wakati muafaka *bill* hii ingejumlisha na *air drops*?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Juma S. Kaboyonga kwa swali hili, lakini ni kweli kabisa Wizara hii inashughulika na viwanja vya ndege lakini kwa maana ya sera zetu, sera ya uchukuzi ukiisoma na Sera ya Ujenzi ipo *very clear* kwa hili ndiyo maana tumekuja hapa kushughulikia barabara peke yake.

Niishukuru sana Kamati ya Miundombinu pamoja na wadau wote waliofika Dar es Salaam tarehe 4 na 5 kushiriki katika mchakato wa Muswada huu. Hayo mliyoyafanya ndiyo yamewezesha kile mnachosema Muswada umeandikwa vizuri sana umetokana na mchango mzuri wa wadau mbalimbali tunawashukuruni sana. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, nimalizie kama Kanuni zinavyotaka, kwa kusema naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu. Waheshimiwa Wabunge hoja hiyo imekwishatolewa na imeungwa mkono lakini kama Kanuni zinavyohitaji tutaiamua baada ya hatua ya Kamati ya Bunge Zima.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*
*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Barabara wa Mwaka 2007**

*(The Roads Bill, 2007)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, bado hajataja vifungu, ametaja ukurasa tu.

Kifungu cha 1

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nilikuwa na hoja kwenye *title* ya *bill* yenyewe ndiyo maana nilisimama wakati inatajwa *bill.* Nahitaji tu ufafanuzi, kama sikosei Wizara hii siyo inayoshughulikia viwanja vya ndege? Isingekuwa wakati muafaka *bill* hii ingejumlisha na *air drops*?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Juma S. Kaboyonga kwa swali hili, lakini ni kweli kabisa Wizara hii inashughulika na viwanja vya ndege lakini kwa maana ya sera zetu, sera ya uchukuzi ukiisoma na Sera ya Ujenzi ipo *very clear* kwa hili ndiyo maana tumekuja hapa kushughulikia barabara peke yake.

Lakini katika mpango tulionao Wizarani wa *Transport Sector Investment Program* ambao ni Mpango wa Miaka 10, sasa hapo ndipo unaiangalia Sekta ya Uchukuzi katika upana wake. Mfano, barabara *component* ndogo, reli, viwanja vya ndege na hata *Ports* yote hiyo utaikuta huko lakini katika Muswada huu, hapana.

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila ya Mabadiliko Yoyote)*

Kifungu cha 2

*(Kifungu Kilichotajwa hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila ya marekebisho Yoyote)*

Kifungu cha 3

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Pamoja na Marekebisho Yake)*

Kifungu cha 4

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Pamoja na Marekebisho Yake)*

Kifungu cha 5

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kaboyonga!

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu cha 5, Muswada unatoa nafasi kwa Waziri kuteua mamlaka lakini tofauti na maeneo mengine ya uteuzi wa Waziri ,hapa haijatamkwa muundo wa hiyo mamlaka.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kwa ufafanuzi!

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 5 ndicho kinachotoa tu yale Mamlaka ya jumla ya Waziri kukasimu kwa Mamlaka nyingine za barabara. Kama ni *TANROADS* itakuwa ni *TANROADS* na kupitia Muswada huu tunaona muundo wake y kama utakwenda kwenye Serikali za Mitaa tunajua muundo na Uongozi unavyokaa, kama ni *TANAPA* tunajua, kwa hiyo, hiyo ndiyo sura hiyo.

Ndiyo maana tulifanya marekebisho kupitia Jedwali la Marekebisho ambapo panasomeka kwamba badala ya ofisa pale panasomeka Taasisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Benito William Malangalila!

**MHE. BENITO WILLIAM MALANGALILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwa kuwa jana nilizungumzia sana juu ya barabara ya Nyigo-Mgololo, barabara hii kimsingi haina mwenyewe barabara hii….!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Benito Malangalila sehemu hiyo tunayopitisha, kifungu hicho hakihusiani na hayo unayoyasema labda tukija kwenye *schedules,* yaani uangalie tutakapofikia hizo *schedules,* zinataja hizo barabara patakuwa ni mahali muafaka kutoa hoja yako.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Pamoja na Marekebisho yake)*

Kifungu cha 6
Kifungu cha 7

*(Vifungu Vilivyotajwa Hapo Juu Vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Pamoja na Marekebisho Yake)*

Kifungu cha 8
Kifungu cha 9
Kufungu cha 10

(*Vifungu Vilivyotajwa Hapo Juu Vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Pamoja na Marekebisho Yake)*

Kifungu cha 11

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dr. Chrisant Majiyatanga Mzindakaya, karibu!

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, najua maelezo ya Waziri ni ya jumla kwa watu wazima wote, naona tumeelewa kwamba mikoa yetu itakaa vikao na kuleta mapendekezo.

Lakini nilikuwa nataka niseme kwa jambo ambalo Wizara wanajua na walishaanza kulishughulikia na Waziri alikuja mwenyewe akatembea na akaona mwenyewe barabara ya kutoka Miangalua kwenda mpaka Kipeta, na kutoka Ilemba Mpaka Kahambazita na akaahidi na kwenye vikao vya jumla tulikubaliana kwamba ……..!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dr. Chrisant Majiyatanga Mzindakaya, unaitoa kama mfano tu kwa sababu hapa siyo mahali pake.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa kama mfano kwa sababu nazungumzia kifungu namba ……..!

Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani ! Naomba radhi, nilikuwa nataka kwenda kifungu namba 12, nikuombe radhi nitasemea kifungu namba 12.

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Pamoja na Marekebisho yake)*

Kifungu cha 12

**MWENYEKITI:** Kifungu Na. 12, namwona Mheshimiwa Dr. Chrisant Majiyatanga Mzindakaya, Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, Mheshimiwa Susan Anselm Jerome Lyimo.

Mheshimiwa Dr. Chrisant Majiyatanga Mzindakaya.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba radhi kwamba nilikwenda haraka kidogo. *(Makofi)*

Lakini kama nilivyosema ni kwamba ni kweli Halmashauri zitakutana lakini ipo pia hadhi na msimamo na heshima ya kawaida ya Serikali yetu kwamba kwa mfano kama Waziri au Naibu waziri amekuja ameona jambo na amezungumza na viongozi wa mkoa unaohusika na kuahidi kwamba Serikali itatoa majibu kwa sababu kwa ahadi aliyotoa Waziri wakati ule alipotembelea barabara hii sisi tulitarajia kwamba linapotokea jambo hili hizi barabara mbili zingekuwa kwenye Jedwali.

Nilikuwa naomba ufafanuzi juu ya jambo hili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ufafanuzi tafadhali!

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kama anavyosema Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri alipotembelea Mkoa wa Rukwa na kutoa ripoti yake ya safari moja ya maombi ambayo aliyakuta katika Mkoa huo zilikuwa ni barabara ambazo Mheshimiwa Chrisant Mzindakaya amezitaja.

Sasa kwa jedwali hili kwamba hazionekani kwa nini? Ndiyo hiyo tulikuwa tunasema kwamba yawezekana vipande fulani fulani vya barabara hiyo vimeachwa kwa makosa, sasa ametusaidia na sisi tutawasiliana na Ofisi ya Waziri Mkuu ihakikishe na haya ambayo Mheshimiwa Chrisant Mzindaya anasema.

Sasa kuhusiana na maombi yao kama barabara hiyo iwe ya Mkoa au nyingine ndiyo tunasema kwamba baada ya sheria hii kuanza kutumika maombi hayo sasa ndiyo yatapimwa kwa kutumia vigezo ambavyo tunapendekeza kupitia Muswada huu.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri, ngoja nianzie hapa Mheshimiwa Bakari Shamis Faki!

**MHE. BAKAR SHAMIS FAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nikiwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani nilimtaka Mheshimiwa Waziri atupatie maelezo mahususi juu ya vigezo vilivyotumika katika kuweka madaraja ya barabara.

Nikachukua mfano wa barabara ya Bunge – CBE, ni daraja la sita na ile ya Msalato – Lugala ni daraja la tatu, wakati barabara zote hizi zipo katika Wilaya moja na yeye katika majumuisho yake hakutaja hivyo, kwa hiyo, hivi sasa naomba maelezo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri maelezo ya ufafanuzi tafadhali!

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli nakumbuka swali hili kutoka kwa Kambi ya Upinzani katika mchango kutaka kupata ufafanuzi kwa hilo.

Lakini kwa vile hizi ni barabara ambazo zipo katika manispaa ya Dodoma, ningelipenda tu na mimi nikajiridhisha kabla sijatoa kitu kimoja cha uhakika kwamba je, *grading* au *classification* ambayo imefanyika ndani ya eneo hilo hilo ni nini ambacho kimepelekea hivyo? Na mimi ningelipenda nikajiridhisha kabla ya kumpatia jibu la moja kwa moja na mpaka ninasimama mbele ya Bunge lako Tukufu tulikuwa bado hatujapata taarifa kutoka kwenye Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan Anselm Jerome Lyimo.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

Wakati nimechangia kwenye hoja hii nilikuwa nimemwomba Mheshimiwa Waziri atuambie kwa nini *classification* ya *Urban Road* haipo kwa sababu najua katika nchi nyingi *Urban Roads* zinakuwa *classified separately,* kwa hiyo, nilikuwa naomba atusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ile sehemu ya tano wote tunaona ni jinsi gani wananchi wanavyobomolewa nyumba na hapa inaeleza kwamba Waziri ndiye atakuwa na Mamlaka ya kuamua juu ya upana wa barabara. Kwa hiyo, naomba ni kwa nini kwenye huu Muswada tusiweke kabisa eneo la barabara *minimum with* hili baadaye kusiwe na kubomoabomoa? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ufafanuzi Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu kwa hayo mawili.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tu nimjibu Mheshimiwa Susan Anselm Jerome Lyimo kama ifuatavyo:

Muswada huu unatumbua kuwepo kwa barabara za mijini na ndiyo maana ukisoma kifungu hicho cha 12 ukiangalia kifungu kidogo cha 3 ambacho zamani kilikuwa cha 4 (iv), unapata jibu hilo. Niseme tu hapa tumeona ni vizuri tukaendelea kutumia *terminology* ambayo imezoeleka na Watanzania ndiyo maana tunasema Barabara Kuu, Barabara ya Mkoa, Barabara ya Wilaya na Barabara za Mijini lakini zote zile tunajua kabisa kwamba mtu ukimwambia hivyo anaelewa ni nini na ndiyo maana barabara za Mijini unakuta sasa tume-*collect a road* kwa sababu tunajua ina maana gani. Dhana ni hiyohiyo kuwezesha barabara zetu tukazifahamu *from the functional law* lakini pia *Administrative Function*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na upana wa *road reserve*, haipendezi wala siyo utaratibu mzuri ukataja upana wa barabara katika sheria yenyewe kwa sababu ukitaka kubadilisha upana huo baadaye ni lazima urudi Bungeni ndiyo maana nasema tulete unyumbulifu kama ilivyo sasa kwamba Waziri mwenye Mamlaka au mwenye Dhamana ya Barabara apewe Mamlaka ya kuweza kutangaza upana wa barabara hizi na *from time to time*. Kwa sasa kama nilivyokuwa nahitimisha hoja yangu ni kwamba kupitia Ibara ya 60 (2), Kanuni zinazofafanua upana wa barabara zetu zitaendelea kutumika hadi hapo kanuni mpya zitakapotengenezwa, zikitengenezwa hizi zilizopo zitafutwa na mpya ambazo zinataja upande ndiyo zitatangazwa. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri kwa ufafanuzi mzuri, Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto!

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi lakini pia naomba kwa dhati kabisa nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwanza kwa Muswada lakini pia kwa majibu mazuri sana ambayo amekuwa akiyatoa Wabunge wanapohoji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa basi, katika kifungu hiki cha 12 mimi nina mambo mawili tu ambayo napenda nipante ufafanuzi au mapendekezo. Katika hizi *definitions* za *District Road* ambazo ni pamoja na *Community Road* sasa hivi tunafanya shughuli zetu kutokana na malengo ya MKUKUTA na moja ya kitu ambacho MKUKUTA unasisitiza sana ni *Rural Growth* na katika eneo *very critical* ambalo ripoti zote za Mkutano zinaonyesha kwamba ni lazima litiliwe nguvu sana ni katika *Rural Infrastructure* sasa.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri ajaribu kuangalia kama kuna uwezekano wa kuwa na *Rural Roads Agency* katika ngazi za Mikoa kwa sababu moja ya tatizo kubwa sana ambalo tunalo mikoani ni kwamba Halmashauri hazina vifaa vya kutosha na unakuta kila Halmashauri inajifanyia kazi kivyake. Lakini tukiwa na *Rural Roads Agency at the Regional level* ina maana kwamba tutakuwa na uwezo wa kununua vifaa vya kutosha na kuweza kuvitengeneza kwa ku-*share* kwenye Halmashauri zote. Waziri anaweza kuliangalia hili ili labda baadaye na kwa sababu itakukuwa kwenye *regulations* tu akaweza kuhakikisha kwamba barabara zote za Wilaya yaani *Collector Roads*, *Community Roads* na *Districts Roads* zikawa *managed* na *Rural Agency* badala ya kuwa na Halmashauri peke yake.

La pili, ambalo namwomba Mheshimiwa Waziri anipatie maelezo kidogo, ni hii barabara ya T 19 ambayo kipande chake cha kama kilomita 58 ni ya Mwandiga-Manyovu. Sasa ulikuwa unazielezea barabara ambazo zipo chini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na zinazounganisha nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hii T 19 ambayo inaanzia Mwandiga kwenda Manyovu inaunganisha Mji wa Kigoma na Mji Mkuu wa Burundi Bujumbura na kuanzia Julai Burundi itakuwa ni sehemu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Sasa Mheshimiwa Waziri na kwa bahati nzuri kabla ya kuwa Waziri wa Miundombinu ulikuwa Waziri wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Unaweza kuangalia uwezekano wa kuchukua barabara hii kuifanya ni sehemu ya barabara za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa sababu inaunganisha nchi yetu na Makao makuu ya nchi ya Burundi? ahsante!

**WAZIRI WA MIUNDOMBUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi niweze kutoa ufafanuzi kwa maswali mawili aliyouliza Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto. La kwanza, nakubaliana na yeye kwamba MKUKUTA unaweka mkazo mkubwa katika *Rural Growth* kwa sababu huko ndiko kwenye watu na huko ndiko tunakoweza tukaibua uchumi na hivyo kupambana na umaskini, na barabara ni kichocheo muhimu sana cha maendeleo kwa watu wetu, hilo wote tunalitambua.Amependekeza kwamba Serikali isione uwezekano kama tulivyofanya kwa barabara za kitaifa kuwa na *Rural Roads Agency*, ni wazo zuri sisi mawazo haya yapo. Wakati wa *Public Hearing* Dar es Salaam na kwenye Kamati ya Miundombinu nilielezea kwa kirefu kwamba yamekuwepo mawazo haya ndani ya Serikali lakini pia na miongoni mwa wadau mbalimbali. Kwa upande wa Serikali tunasema ni mawazo mazuri lazima tuyatafakari lakini hoja ya msingi inabaki palepale. Niliwauliza wahisani, walipoanza kuyasema haya nikawauliza hivi sasa hata fedha tunazoongelea kwa mtandao uliopo huu ambao unaibua haraka sana, uchumi bado tunashindwa na ndiyo hoja hii ya matengenezo shilingi bilioni 78 *versus* shilingi bilioni 221 ya mahitaji halisi. Wakasema tutaangalia. Sasa kwa hiyo, kuna mahitaji ya raslimali kwa upande wa Bajeti ya Serikali kwa sababu lazima hiyo tuilipie kutokana na fedha ya makusanyo ya kodi iliyopo ndani ya Bajeti ya Serikali. Lakini tunauchukua kama ni ushauri mzuri tu ambao na baadhi yetu tunao mtazamo huo.

La pili, kuhusiana na *T19* Mwandiga - Manyovu, tunaitambua wote kwamba hii inaunganisha nchi yetu na nchi jirani na rafiki ya Burundi na ni makusudio yetu kama tumekuwa tukisema humu kwamba barabara hii ni muhimu sana na lazima hatimaye tuje tuijenge kwa kiwango cha lami ili kuunganisha nchi hiyo na Tanzania na ujio wa nchi ya Burundi katika Jumuiya ya Afrika mashariki una sura hiyohiyo.

Hapa nirudie ambacho nimekisema wakati wa Kamati ya Bunge Zima, kwamba Benki ya Afrika ya Maendeleo ndiyo imekuwa na dhana hii ya kutaka kusaidia katika kuziunganisha nchi zetu kwa maana ya usafiri wa uhakika na salama na tunaamini tutakapokamilisha usanifu wa kina katika eneo hili tutawafuata tena na wenyewe waseme hiyo ndiyo imekuwa ahadi yenu ya *connectivity within the region* tuone kama tunaweza tukapata fedha kwa ajili ya kugharamia kilomita 60 kati ya Mwandinga -Manyovu. Nakushukuru sana.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Pamoja na Marekebisho yake)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa kuzingatia muda ulivyo na nachelea isije ikatokea tusije tukafika muda wa kanuni wa kusitisha Shughuli za Bunge kwa mchana huu bila kuwa tumemaliza Muswada huu na kwa kuzingatia kwamba kwa Kanuni inabidi tupate Azimio tukubaliwe na Bunge kutoka kwa Waziri wa Nchi ili tuzidishe muda kidogo basi namwomba Katibu kwamba sasa Bunge lirudie ili tuweze kufanya Azimio hilo.

*(Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Tukae! Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Bunge na Uratibu)!

**KUONGEZA MUDA WA KUKAA BUNGE**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. DR. BATILDA S. BURIAN):** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liongeze muda ili Kamati ya Bunge Zima ikamilishe kazi iliyokuwa ikifanya. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja iliyopo mbele yetu iliyoletwa na Waziri wa Nchi ni kwamba tuongeze muda wa Bunge kupita ule muda wa saa 7 kamili ili tuweze kumaliza shughuli za Muswada huu wa Barabara 2007.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Kamati ya Bunge Zima ilirudia)*

**MWENYEKITI:** Tuendelee na Vifungu vilivyobaki.

Kifungu 13

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila ya Mabadiliko Yoyote)*

Kifungu cha 14
Kifungu cha 15
Kifungu cha 16

*(Vifungu Vilivyotajwa Hapo Juu Vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Pamoja na Marekebisho Yake)*

Kifungu cha 17

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, kifungu cha 17.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa najaribu kuangalia nafasi ya *Build, Operate and Transfer* katika Muswada huu sikuiona.Sasa hapa nahisi ndiyo kama mahali pake lakini haijitokezi tokezi vizuri, naomba maelezo ya ziada

kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kuhusu hiyo *Build, Operate and Transfer as a private involvement* kwenye ujenzi wa Miundombinu.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheeshimiwa Siraju Juma Kaboyonga kwa hilo. *Private Roads* ni *Private Roads* kabisa, hatuzichanganyi, na hiyo dhana nzima ambayo Mheshimiwa Mbunge ameizungumzia na wengi wetu ndiyo tunakubaliana naye kabisa. Lakini kwa upande wa dhana hiyo tumeanza kujenga msingi wake kwenye Kifungu cha 6, kwanza, unakuta kwenye kifungu cha 6(2) (c ) ni *Negotiate Concession Agreements with Private Sector Entities to Facilitate Financing Development of Selected Roads in accordance with guidelines prescribed by the Minister,* halafu ukitoka hapo ndiyo unakwenda sasa kwenye kitungu cha 60 (2) uende kwenye *Schedule of Amendments* ambayo imefanyika lakini hata kama huna hiyo *Schedule of Amendments* ukikisoma sasa hicho cha T ambacho kinaongelea *guidelines* yaani Kutengeneza Kanuni kuweka Miongozo yaani *Management of Public Private Partnership* lakini imeimarishwa zaidi sasa kuwa *Regulationa on the Participation and Management of Privately Financed Infrastructure Projects through PPP's.* Hiyo ndiyo dhana ambayo tunasema Waziri sasa atatengeneza miongozo ambayo itasimamia masuala haya lakini kwa msingi wa Sheria hii.

*(Kifungu Kilichotajwa hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila ya Mabadiliko Yoyote)*

Kifungu cha 18

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila ya Mabadiliko Yoyote)*

Kifungu cha 19

**MHE. ENG. STELLA MARTIN MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na marekebisho naomba maelezo kuhusu kifungu hiki kinachozungumzia Sheria kutoa Mamlaka ya kuweza kutengeneza barabara pamoja na kuweza kuchukua kokoto na mawe na vitu vinginevyo katika maeneo hayo yatakayohusika.Sasa naomba nifahamu baada ya kutoa kokoto au mawe kufuatia uharibifu wa mazingira naona sheria imenyamaza, je, ni jinsi gani tunaweza tukairejesha katika hali yake. Ahsante sana.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Mheshimiwa *Eng.* Manyanya ni ya msingi sana na maana Muswada ni lazima uusome kwa ukamilifu yaani kwa vifungu vyote vilivyopo.Sasa napenda tu nimwelekeze kwenye kifungu cha 29 na 30 ambapo hatujafika cha Muswada ambapo suala hili linazingatiwa sana sana kwa masuala ya utunzaji wa mazingira katika maeneo ambayo yanatumika kwa ujenzi wa barabara.

*(Kifungu Kilichotajwa hapo Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Pamoja na Mabadiliko Yoyote)*

Kifungu cha 20

(*Kifungu Kilichotajwa hapo Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Pamoja na Mabadiliko Yoyote)*

Kifungu cha 21
Kifungu cha 22
Kifungu cha 23

*(Vifungu Vilichotajwa Hapo Juu Vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila ya Mabadiliko Yoyote*)

Kifungu cha 24

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan Anselm Jerome Lyimo!

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na ninaendelea kuipongeza Wizara kwa huu Muswada iliouleta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ombi tu kwa sababau tunajua kwamba wakulima wengi katika nchi ya Tanzania wanalima kwenye sehemu za miinuko au miteremko mikali na kwamba tunajua kwamba mkulima anapaswa kupanda miti ili kuzuia mimonyonyoko hii, lakini kuna mambo mengine ya mabadiliko ya kijiografia, kwa mfano, inapotokea labda mvua kubwa. Je, huyo mkulima anapaswa kweli kutengeneza shamba lake kuweka mipaka ili ule udongo usiendelee barabarani? Kwa nini isiwe ni kazi ya hii *Authority* kwa sababu tunajua ni gharama kubwa sana kwa mkulima wetu kuweza kuzuia mmomonyoko wa udongo hasa inapotokea hizo *natural disasters*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri atueleze itakuwa vipi hapo?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wasiwasi alionao Mheshimiwa Susan Lyimo ni sahihi. Matukio ambayo yatafanywa mwananchi asibanwe na kifungu hiki ni yale ambayo yako nje ya uwezo wa binadamu. Sasa kama kuna maporomoko kule yametoka juu ya milima yakaja mpaka huko, hatusemi sasa mwananchi wa eneo hilo ndilo awajibike.

Lakini tunawataka hao ambao wako karibu na eneo la barabara ambapo ndipo inapita, wahakikishe kabisa kwamba kutokana na vitendo vyao *(human activities)* hawaathiri barabara hizo kwa kuruhusu udongo unaotoka katika sehemu wanazoishi wao au kutengeneza njia ya maji yaje yamwagwe kwenye barabara, ndiyo tunasema hao ndiyo tunataka tuhangaike nao kwa namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini matukio mengine ya dharura, hayambani mwananchi katika Muswada huu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana. Nadhani matumizi ya neno *"may"* inasaidia wanaosimamia sheria watumie hekima zao.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 25

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 26
Kifungu cha 27
Kifungu cha 28

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 29

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza kabisa na mimi niungane na wenzangu kuishukuru Wizara na Serikali kwa kujitahidi kuweka mapendekezo mengi ya wananchi. Wizara imekuwa sikivu. Naomba niwashukuru sana na hasa kwangu mimi mengi niliyoyatoa wamenisaidia. Ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba tu ufafanuzi mmoja nisaidiwe. *Use of Road Reserve* 29(1): "*The road reserve is exclusively for the use of road development and expansion or any other road related activities.*"

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu, nilikuwa nimeuliza, kuna maeneo ya barabara hasa hizo *trank roads* na barabara zinazopita Mkoa wa Pwani, yaani barabara kuu. Ni kwamba kuna maeneo ya barabara *road reserve* ni ndogo, kwa mfano, 22.5 *meters,* lakini kuna maeneo ya barabara *road reserve* ni kubwa sana kwa mfano 121.5 *meters*. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri anieleze, hapo kuna matumizi gani *specific* na hasa eneo la Mailimoja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tu nimjibu Mheshimiwa Dr. Zainab Gama kama ifuatavyo:-

Ni kweli katika maeneo aliyoyataja, hali ndivyo ilivyo kwa mujibu wa sheria na siyo hapo tu, ukitoka Ubungo, pale eneo la Kimara siyo mita 22.5 lakini tunakwenda mpaka mita 100. Kuna maeneo ambayo tunajua kwamba maendeleo ya nchi yetu lazima tuyaangalie katika miaka ijayo na ndiyo maana nilivyomsikia Mheshimiwa Paul Kimiti akichangia na wengine waliochangia kwa maandishi walisema, ni vizuri basi hiyo *road reserve* ambayo mnasema sasa hivi ni mita 45 yanawezekana huko mbele ya safari ikawa ni ndogo sana. Sasa lengo ni maendeleo na unapotaka kupanua barabara, gharama moja kubwa ambayo tunakumbana nayo hasa katika maeneo ambayo *road reserve* ilikuwa finyu ni kulipa fidia kwa mali za wananchi wetu. Sasa eneo hilo la Mailimoja kama ilivyo katika maeneo mengine katika hii T 3 ni mtazamo huo huo wa uono wa mbali, maendeleo hayatabakia hivyo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana humu ndani ya Bunge katika mchango uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge walisema, barabara ya kutoka Chalinze kwenda Dar es Salaam sehemu fulani ni nzuri, lakini sasa *traffic* imeanza kuwa ni kubwa, barabara hiyo ipanuliwe. Yote hayo tunataka ili kuepuka gharama za baadaye za malipo ya fidia. Wananchi

wajulishwe kwamba ni kwa faida ya maendeleo yao, lakini pia kwa faida ya maendeleo ya nchi yetu na uchumi wake kwamba *road reserve* pale inapoonekana tuipanue zaidi. Kwa hiyo, hayo ndiyo maelezo yetu kwa eneo la Mailimoja.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 30

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 31

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nilikuwa naomba tu Mheshimiwa Waziri anisaidie kwamba kile kifungu cha 31(4), ni watu gani hao watakaokuwa *exempted?* Labda na sisi Waheshimiwa Wabunge tutakuwa *exempted?* Na ni kwa nini?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna huduma fulani fulani kama Zimamoto, kuna ajali imetokea huwezi ukasema lazima apitie njia hiyo hiyo. *Traffic direction* anaweza akaja *the opposite direction* kwa sababu anaona ndiyo njia nzuri ya kuweza kuwahi. *Ambulance* ina mgonjwa, huwezi ukasema nisuburi tu hapa kwa sababu kuna *traffic* hapa inakwenda huko, hapana. Ndiyo maana wamepewa haki ya kupita. Polisi wanafukuza majambazi, gari la Polisi linaweza likaja *for any direction* ilimradi wao wanajua kwamba jambazi huyo anapita hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hizo ndizo *situations* ambazo tunaziangalia katika hali hiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ahsante kwa ufafanuzi huo. Nadhani imesaidia sana.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 32

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kifungu cha 32(2), nafikiri hiyo *penalty* ni ndogo sana. Nilitegemea wange-*distinguish* kati ya magari madogo na magari makubwa ya abiria. Kwa sababu ukiangalia *speed* ambazo zinatokea kwenye barabara siku hizi na *penalty* ya Sh. 100,000/= au kifungo kisichozidi mwaka moja ni kidogo sana. Naomba maelezo.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Mheshimiwa Mbunge ni ya msingi sana, hata kwenye Kamati ilijitokeza hivyo hivyo, ndiyo maana katika orodha ya marekebisho tumefanya marekebisho yanayosema: *"Not less than two hundred thousand.*"

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya*

*Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 33
Kifungu cha 34
Kifungu cha 35
Kifungu cha 36
Kifungu cha 37
Kifungu cha 38
Kifungu cha 39

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 40

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zimapamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 41

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 42
Kifungu cha 43

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 44

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa namwomba Waziri mhusika ajaribu kukubali ombi ninalotoa sasa hivi kwamba katika njia za kupatia fedha tuweke *long term government bonds* na *Municipal bonds* kama eneo tofauti ili tujenge utamaduni wa kuelewa hayo maeneo nayo vilevile ni *source of funds.*

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana sana na Mheshimiwa Siraju Kaboyonga kwa sababu yeye kwanza ni mtaalamu wa masuala ya fedha. Lakini kubwa zaidi ni kwamba na sisi dhana hiyo tunaikubali na ndiyo maana tunatumia *loans* kwa sababu *Municipal bonds*, au *city bonds* ni *loan* kwamba mtu ametoa na wewe ume-*float* hizo *bonds* kwa matarajio kwamba utapata watu wenye fedha za ziada waje wawekeze kwa kivutio cha riba utakayotoa na hatimaye wewe *bonds* hizo zikiiva uweze kuwalipa, lakini umekuwa umefanyia shughuli zako muhimu. Lakini dhana ni hiyo hiyo tunaikubali iko *covered very well* katika neno *loans*.

**MWENYEKITI:** Nadhani hakuna madhara kuipa Manispaa *bonds. Bonds* zina *specific meaning* tu. Mtavutana bure, atasimama, utajibu, ataingiza utaalamu wa fedha.

Nadhani haitupi taabu sana *point* ya Mheshimiwa Mbunge. Ni kwamba sasa *Local Government entities* zielewe hiyo. Kwa hiyo, ikiwapo pengine si vibaya.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi Halmashauri zetu haziruhusiwi kwenda kukopa bila ruhusa ya Waziri wa Fedha na ndiyo maana hili suala tumekuwa tunaliangalia kwa umakini sana. Lakini pale ambapo kuna hoja, sisi tuliliona katika upana wake kwamba Serikali tungeanza kujielekeza sisi wenyewe katika ku-*float bonds for specific public investments* na hili tunalo. Nadhani katika hoja hiyo hatutofautiani sana na Mheshimiwa Siraju Kaboyonga kwamba hiyo ndiyo dhana. Kama tunataka barabara hizi zijengwe, lazima tupanue pia wigo wa kupata mapato.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, nadhani uridhike kwamba ndani ya *loans, your point is made* na ni vizuri *Hansard* imekwishaingiza yote hayo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 45
Kifungu cha 46
Kifungu cha 47

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 48

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi niko sana na upande *penalty.* Kwa mfano, kuna mtu ambaye anaweza akaharibu daraja kwa sababu ya *manufacturer* ya gari, lakini kuna mwingine anaweza akaharibu kwa sababu alikuwa amelewa, sasa hawa wote kuwapa adhabu moja, nafikiri siyo sahihi. Nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri labda atoe ufafanuzi.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli anachosema Mheshimiwa Charles Kajege. Nadhani *discretion* iliyopo hapa ni kwamba unaachia Mahakama, kwa mfano alioueleza yeye mwenyewe. Maana ushahidi utathibitisha kwamba huyu hakukusudia kufanya hivyo, kulikuwa na utelezi siku ile, gari likaserereka mpaka kwenye daraja, yakatokea yaliyotokea. Ni tofauti na huyo anayekuja anajua mimi *limit* ya mzigo kwenye daraja hilo imeandika hapo, lakini amekuja badala ya tani 15, amekuja na tani 40, ni kwa makusudi kabisa! Sasa huyo ndiyo tutambana kwa kuanzia hapo. Hiyo *limit* tunaweka adhabu hiyo ilinganelingane na kosa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna kifungu kingine tumekipita, dereva mara nyingi ndiye anayeendesha gari na ndiye aliyefanya hivyo ili tuonyeshe ukali. Kwa suala hili tunapenda pia katika *situation* ambazo zinafaa mwenye gari na yeye aunganishwe katika kufidia gharama ambazo zimetokana na uharibifu uliofanywa na lori lake.

Kwa hiyo, Mahakama itapima na likithibitika hilo zinalipwa. Na tuendelea kusema kwenye Jedwali ambalo tutaliona huko katika hali ambayo inadhihirika kwamba mamlaka ya barabara imeridhika kwamba huyo alifanya uharibifu huo, unatoa hati ile unakwenda

unakamata mali ile ili kufidia gharama ambayo mamlaka ya barabara imefidia katika kulijenga daraja hilo au kutengeneza barabara hiyo. Kwa sasa hivi vifungu vilikuwa havipo. Ndiyo tunaanza kuimarisha. Lakini kwa hoja ya Mheshimiwa Charles Kajege, hilo ndilo jibu la kwanza ambalo tumelitoa kwamba tunatofautishwa kwa utaratibu huo kwa kuiachia Mahakama.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 49

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 50

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 50 kimeeleza juu ya *assumption on roads.* Katika kueleza kwake, kimeeleza mambo mengi sana, lakini ile sehemu (d) yote yaliyoelezwa pale, sipendi niyasome, lakini kuna kosa ambalo hutokea sana barabarani na liko wazi sana na sioni kama vilivyotajwa pale vinaweza vika -*cover* hii *situation* kama mtu gari lake limeharibika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, umekatiza baina ya Spika na msemaji. Naomba basi ukae hapo hapo sasa. Endelee Mheshimiwa George Simbachawene.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama gari limeharibika, mtu anatakiwa kwa taratibu au kwa sheria aweke *triangle* inayo-*reflect.* Lakini watu wanaweka miti au matawi kwa umbali mrefu sana na kwa kweli inasababisha ajali nyingi sana. Mimi nimeshanusurika karibu mara mbili na wakiondoka wanaacha. Sasa mimi hapo nilikuwa nadhani pamoja na kwamba vimetajwa hapo tafsiri kisheria unaipata. Lakini kwa sababu hii iko wazi sana, ingetajwa yenyewe kabisa kwamba kuweka matawi hayo na miti na vitu kama hivyo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Mheshimiwa George Simbachawene ni ya msingi sana, tunayaona wote tunaotumia barabara zetu na ndiyo maana hata katika hotuba ya kuwasilisha Muswada huu, hilo nililisema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kifungu hiki, ile (d*) straw, dung , rubbish* yote hayo yanambana huyo mwenye vitendo vya namna hiyo. Wanapaswa wawe na *reflector* litakapowafika jambo la kuharibikiwa kwenye barabara, usalama barabarani ndiyo unahimizwa, lazima sasa uwe na *reflector* ambayo utaweka katika umbali fulani kutoka kwenye gari ambalo limeharibika.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 51

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 52
Kifungu cha 53

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 54

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 55
Kifungu cha 56
Kifungu cha 57

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 58

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 59

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 60

**MHE. MOHAMMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kifungu hicho cha 60(t) Mheshimiwa Waziri hapa alizungumzia suala nzima la *guidelines and regulations on management of Public - Private Partnership.* Sasa hivi tuna *crisis* katika Jiji la Dar es Salaam na zile barabara ni za *trank roads*. Sasa ili kutatua matatizo hayo, ukichukua kwa mfano barabara ya *Tanganyika Motors* kwenda Ali Hassan Mwinyi mpaka Mbezi *Beach*, Akiba kwenda mpaka Kimara - Akiba kupitia UWT kwenda *TAZARA junction* - Chang'ombe hayo maeneo kwa kweli ni *problem* kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuuliza, kwa kifungu hiki zinaweza zikakidhi haja ya *private investment* au kuna haja ya kutunga sheria nyingine pana zaidi pamoja na kuwa na sera ili kutoa *security* kwa yule mwekezaji, hatimaye aweze kuwa na uwekezaji salama na kuona kwamba sheria inamlinda vizuri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu ni kwamba je, kwa kifungu hiki cha sheria na nyingine zinazofanana katika Muswada huu zinakidhi haja kwa kuwekeza katika masuala kama hayo? Ahsante sana.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza, kwa dhana nzima ya kushirikisha sekta binafsi katika ujenzi wa barabara zetu na madaraja kwamba humo tunaanza kujenga ule msingi tunauona wote, halafu sasa tunakwenda kufafanua miongozo kwenye *guidelines* na hivi sasa Wizara ya Miundombinu ikishirikiana na Benki ya Dunia pamoja na wataalam wa *Central Corridor Secretariat* yenye Makao yake Kigali. Suala la *guidelines* yaani kwa maana kwamba Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah alisema kile ambacho kitamvutia mwekezaji, yaani kwa sekta binafsi aje kwenye eneo husika. Ndiyo tunasema tufafanue vizuri *guidelines* miongozo hii. Waziri atatoa humo ndiyo katika kanuni sasa atafafanua vizuri nini kinachotolewa kama kivutio, na nini kitazingatiwa katika kutekeleza shughuli hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwa sababu itatuchukua muda kidogo kwa hili. Lakini Wizara kwa kuona umuhimu wa masuala haya, hatuwezi kuwaambia wawekezaji nendeni mrudi mwaka kesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona suala hili ni muhimu sana kwetu, tumeunda timu ya wataalam wa ndani na wa nje waliobobea kwenye masuala hayo. Tunaanza na kiwanja cha ndege cha Dar es Salaam na kukipanua, tunaanza na kiwanja cha ndege cha Mwanza, tunafanya hivyo hivyo kwa *ASM* kwa upande wa Bandari ya Dar es Salaam. Kwa hiyo, hiyo ndiyo dhana ambayo tunataka tuanze nayo kwa sababu tunajua ni kwa faida sana kwa uchumi wetu.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho)*

Kifungu cha 61

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Jedwali la Kwanza

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa na mimi nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa namna alivyowasilisha vizuri sana Muswada huu. Lakini jana nilichangia juu ya barabara Nyigo-Mgogolo ambayo kimsingi barabara hiyo ilikuwa ni ya Serikali Kuu. Mwaka 1970 na 1980 mimi nilikuwa mwajiri wa Wizara ya Ujenzi, nilifanya katika barabara hiyo. Lakini katika Jedwali hili wala haikuandikwa popote.

Kwa hiyo, ninachomwomba Waziri leo hii akubali kuipokea barabara hiyo, siyo barabara ya Wilaya ya Mufindi ni barabara ya Wizara ya Miundombinu, zamani ilikuwa inaitwa Wizara ya Ujenzi. Hilo ndilo ombi langu.

**WAZIRI WA MIUNBOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara zote ni barabara za umma, ndiyo maana tunazitambua kwa namna hiyo. Sasa kwa barabara hii *specifically* tulisikia kilio cha Mheshimiwa Mbunge. Kwanza kwa nini haionekani humu?

Ni katika hayo hayo ya michango mizuri ambayo imetoka kwa Waheshimiwa Wabunge, tunashukuru kwa hilo. Acha tukakae na wenzangu pia na uongozi wa Mkoa Iringa ili suala hili tujue tunaiweka wapi barabara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siwezi kumjibu moja kwa moja kwamba inarejeshwa kuwa ni barabara ya Kitaifa sasa hivi humu katika Kamati ya Bunge Zima, hapana. Atupe nafasi tu tuweze kulifanyia kazi suala hili. Lakini tuko pamoja naye katika kilio chake.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kupata ufafanuzi wa hoja mbili. Hoja ya kwanza, naishukuru sana Serikali, ina nia njema ya kutaka kutengeneza barabara ya kutoka Iringa - Dodoma - Babati kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeingia Bungeni tangu mwaka 1990 na ninakumbuka *feasibility stud*y ilifanyika tangu mwaka 1995 na mpaka sasa *ni feasibility study*. Sasa naomba maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kitakachofanyika. Maana amesema kwamba inawezekana mikataba ikatiwa saini mwezi ujao. Sasa kitakachofanyika ni *feasibility study* au *design*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu katika mchango wangu wa maandishi niliomba barabara ya Mbande-Kongwa-Mpwapwa kutengenezwa kwa kiwango cha lami kwa sababu ilikuwa ni ahadi ya Serikali wakati wa kampeni. Ni lini hilo litatekelezwa? Ahsante.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa George Lubeleje. Nianze na hilo la pili, ahadi za viongozi wetu kwa barabara iliyotajwa kwa kujengwa kwa kiwango cha lami. Ndiyo maana nimesema Muswada huu sio wa kugawa fedha au kutengeneza barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Bunge lako Tukufu likubali maombi ya Serikali ya kupitisha Muswada huu wa Sheria ili tuweze kufanya mambo mengi tuliyoyataja humo ukiwemo mtandao wa barabara na kujua madaraja yake. Hiyo ahadi ambayo ameitaja Mheshimiwa George Lubeleje, itatekelezwa na Serikali kwa kutegemea uwezo wa Serikali na kama nilivyosema wakati nafanya majumuisho, Serikali iliyopo madarakani ni ya Chama cha Mapinduzi, iko makini sana katika kuzifuatili ahadi hizo. Tuna miaka mitatu mbele yetu tutayafanya yale ambayo tuna uwezo nayo. Lakini *inshallah* mwaka 2010 mpaka 2015 ridhaa ya wananchi itaelekezwa kwa Chama cha Mapinduzi na kuendelea kuyafanya hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kwanza la *feasibility study*,, ninavyokumbuka mimi mwaka 1995 ndiyo ulifanyika upembuzi yakinifu ikachukua muda. Wamekuwa wana *update* huo upembuzi yakinifu uliofanyika wakati ule. Sasa hivi tunaongelea usanifu wa kina. Tutajua barabara hiyo itapita wapi, gharama zake zitakuwa nini, *environmental* na *social impact assessment* zitafanyika na yote hayo ambayo yanatakiwa kufanywa yatakuwa yamefahamika. Baada ya hapo ndipo tunaanza kutafutia fedha ili barabara hiyo iweze kujengwa kwa kiwango cha lami.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Nami nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa jinsi alivyoweza kufanya

*presentation* ambayo inaeleweka na kutupa matumaini ya kwamba sasa Serikali inajiandaa kushughulikia suala la barabara ipasavyo. Naimpongeza sana kwa hilo na pia napenda kugusia kilio cha watu wa Tarime kuhusu hasa barabara ambayo ni *regional road* ambayo ni *R83* inayotoka Tarime - Nyamwaga - Runabere - Mugumu - Nata. Napenda kuipongeza Serikali kwa kukubali kutengeneza barabara kutoka Arusha kuja Mara Musoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba, Mkoa wa Mara hauna mawasiliano na Arusha ndiyo maana hata biashara inakuwa labda ni Uganda na Kenya peke yake na kwa hilo Tarime imeathirika sana kwa sababu hiyo barabara ambayo ninaizungumzia inaunganisha Mugumu yaani Serengeti, Tarime na mpakani Sirari. Ndiyo wananchi wanaitegemea kwa ajili ya biashara na kilimo na sisi tunalima ndizi kwa ajili ya Mwanza na Musoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi hatuli ndizi lakini ni kwa ajili yao na sasa ndizi zile haziendi, inabidi zitoke Kenya na wananchi baada barabara kuharibiwa na migodi inabidi wazunguke Kenya ili waweze kwenda Musoma na Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri a-*take note* kwamba, hiyo barabara ni muhimu sana kwa huo Mkoa na Mikoa ya jirani na nchi jirani iweze kutengenezwa hata kiwango cha changarawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu amekuja hapa Naibu Waziri ambaye ni mzaliwa wa pale amekulia, amesoma pale, tukatembea naye akakwama pale na pia nashukuru kwamba hata Waziri mwenyewe amesomea pale anafahamu hiyo shida ya watu wa Tarime. Ili watu wa Tarime wasiwe na hisia kwamba wanabaguliwa na kuadhibiwa kwa sababu walichagua Mbunge wa Chama kingine, naomba hilo uliangalie katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambayo mnaiangalia.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, tunapokea ushauri wa Mheshimiwa Wangwe. Ni kama ilivyo kwa barabara nyingine za Mkoa. Niseme hapa kwamba kweli wote tunapenda hizi barabara zetu ziimarike, lakini kuomba barabara hata kama itatimiza vigezo ambavyo leo tunaomba Bunge lako lipitishe, hata kama itatimiza vigezo hivi, haimaanishi kwamba sasa uwezo wa Serikali wa kuzitengeneza barabara hizi ambazo zimepandishwa daraja kwamba umepatikana. Tunachoendelea kuomba na kushauri ni kwamba tuhakikishe uchumi wetu unaendelea kukua kwa sababu ndiyo nji pekee itakayowezesha barabara hizi zitengenezwe na kupitika kwa kiwango chote cha mwaka. Lakini tunaupokea ushauri wake.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi katika mchango wangu, nilimpa Mheshimiwa Waziri *minutes* ya Kikao kilichokaa wananchi wa Kibaha, Maili Moja eneo la *trunk road* na wakapendekeza mambo. Matokeo yake, kuna watu ambao walipewa hati kwa kukosa *coordination* kati ya Wizara, Mkoa na Halmashauri. Kuna watu walipewa hati ndani ya hiyo *road reserve.* Je, hawa watu watalipwa fidia? Lakini la pili, baada ya maelezo wananchi bado hawajaelewa Mkoa, Wilaya, nikamwomba Waziri kama inawezekana, basi aje Kibaha tuzungumze na hawa hawa 54, walikaa katika kikao hiki. Hilo moja.

La pili, barabara ya Mlandizi – Chalinze eneo la daraja la Ruvu, sisi katika Kikao cha *Road Board* ya Mkoa nilipata bahati kwa kikundi kilichopelekwa eneo lile la darajani tukakuta hao wahandisi wamesimama kujenga. Tuliwapowauliza wakasema tumesimama kwa

sababu tunasubiri Serikali iamue kwa ajili ya bomba la mafuta. Kwa hiyo, mpaka leo nazungumza wamesimama. Sasa naomba Waziri atuambie tatizo ni nini na kwa nini wahaliazimia hili daraja lijengwe?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Dr. Zainab Gama. Ni kweli kabisa kwamba jana aliniletea *minutes* ile, lakini kwa vile nilikuwa katika shughuli ya zege na zege kama unavyojua hailali, nimepeleka zile taarifa na kuzichukua tukazifanyie kazi na sisi tuna *interest* kujua.

Lakini moja ambalo nataka niseme, hawa wananchi waliopewa hati na sisi tunashangaa sana kwamba *unless* kulikuwa na mchezo mchafu tu. Ile anayoiita yeye kutokuwa na mawasiliano mazuri kati ya Halmashauri au na Wizara na Ardhi na Wizara ya Ujenzi wakati ule kidogo mimi halikai vizuri akilini, kwa sababu unajua kabisa pale ni *road reserve* na sheria iko *very clear* na nini. Lakini tukasema acha tuyachukue basi tuone ni jinsi gani tunaweza kuwasaidia.

La pili, ni kweli kabisa pale Ruvu wote tunapita, Mkandarasi Chico alikuwa ameanza kwa ukakamavu, sasa hivi kazi imesimama kabisa. Moja ya sababu ni hiyo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameielezea. Tumekuwa na mawasiliano na uongozi wa kampuni ya TAZAMA, walitujibu wakasema ndiyo watalisogeza bomba hilo na kulihamisha lipite sehemu nyingine ili kuruhusu ujenzi wa daraja hili muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme kwamba kwenye Kamati yako kwamba tutaendelea kushauriana na wenzetu kwa sababu TAZAMA ni kampuni Serikali ya Tanzania na Zambia, kwa hiyo, linatuhusu wote. Kwa hiyo, atupe muda ili tuweze kukamilisha.

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko)*

Jedwali la Pili

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko)*

Jedwali la Tatu

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko)*

Jedwali la Nne

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru sana. Pamoja na kumwandikia maelezo Mheshimiwa Waziri, labda nitaelezea kidogo. Ni kwamba, hizi barabara ambazo nimwemwandikia ni muhimu sana kiuchumi katika Jimbo la Mwibara.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jedwali la Nne linahusu *proceedings* za regional *road, Roads Boards.*

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti kwa sababu unakwenda haraka, tunakuwa *confused,* labda nitasubiri.

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Jedwali la Tano

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Barabara ya Mwaka 2007**
***(The Road Bill 2007)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Barabara wa Mwaka 2007 *(The Road Bill 2007)* Kifungu kwa Kifungu na kukubali pamoja na marekebisho yaliyowasilishwa. Hivyo naomba kutoa hoja kwamba Mswada wa Sheria ya Barabara wa Mwaka 2007 *(The Road Bill 2007)* sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Spika naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, naafiki!

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, matangazo kutokana na msiba uliowapata familia ya Waziri, kwa maana hiyo Balozi Juma Mwapachu ile Semina ya mambo ya Afrika Mashariki tuliyoipanga Jumamosi haitakuwepo, badala yake siku hiyo saa 4.00 asubuhi Ukumbi wa Pius Msekwa ile Tume ya kukusanya maoni kuhusu Afrika Mashariki itaomba kupokea maoni ya Waheshimiwa Wabunge katika Ukumbi huo.

Kwa hiyo, badala ya Semina, itakuwa ni Waheshimiwa Wabunge kutoa maoni kuhusu mchakato wa kuharakisha kuundwa kwa Shirikisho la Afrika Mashariki saa 4.00 asubuhi katika Ukumbi wa Msekwa Jumamosi.

Nikumbushe pia kwamba Jumapili saa 5.00 tutapokea taarifa za Viongozi za Misafara ya Wabunge waliokwenda nchi mbalimbali. Kwenye hilo nithibitishe tu kwamba mazingira yake yote yamezingatiwa na Ofisi ya Bunge.

Mwisho ni kwamba, Kamati ya Kanuni sasa Mkutano wake utakuwa ni kesho saa 7.30 mchana kwa kuzingatia kwamba sasa hivi tunakwenda kwenye *briefing* itakayoongozwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo, naomba kutangaza kusitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa 11.00 leo jioni.

*(Saa 07.47 Mchana Bunge lilifungwa Mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mheshimiwa Jenista J. Mhagama) Alikalia Kiti*

**MISWADA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Zimamoto na Uokoaji wa Mwaka 2007**
***(The Fire and Rescue Force Bill, 2007)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kuwa Muswada wa Sheria ya Zimamoto na Uokoaji ya Mwaka 2007 *(The Fire and Rescue Act, 2007)* inayoambatana na orodha ya marekebisho iliyosambazwa, sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kutolea maelezo ya hoja hii, napenda kutumia fursa hii kutambua kuwemo ndani ya Bunge hili Wabunge wapya. Nawapongeza sana Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura aliyechaguliwa kwa ushindi wa kishindo kuwa Mbunge mpya wa Jimbo la Tunduru na Mheshimiwa Florence Essa Kyendesya, aliyechaguliwa kuwa Mbunge wa Viti Maalum. Nawaomba tuendeleze ushirikiano mzuri tuliokuwa nao na wale mliowapokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, naomba nianze kwa maelezo ya utangulizi kuhusu Muswada huu. Hivi sasa hakuna Sheria inayotumika kuendesha shughuli za Zimamoto na Uokoaji hapa nchini. Hali hii inatokana na kufutwa kwa Sheria ya Kikosi cha Huduma za Zimamoto na Uokoaji ya mwaka 1985 kulikofanyika kupitia Sheria ya Utumishi wa Umma ya mwaka, 2002. Kinachofanyika kupitia Muswada huu ni kuihuisha Sheria hiyo ikiwa na mabadiliko machache yanayoendana na changamoto za sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli za Zimamoto na Uokoaji ni muhimu kwa mustakabali wa Taifa lolote. Serikali yoyote inawajibika katika kulinda na kutetea maisha ya raia wake hususan pale maisha ya raia hao yanapokuwa hatarini kutokana na majanga mbalimbali. Utaratibu wa sasa wa shughuli za Zimamoto na Uokoaji husimamiwa na kuongozwa na taasisi tofauti. Hali hiyo inasababisha shughuli hizo kutokuwa na ufanisi unaotakiwa. Kwa sasa mambo ya Zimamoto na Uokoaji husimamiwa na vyombo mbalimbali kama Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, Mamlaka ya Bandari na Serikali Kuu kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema hapo awali, kugawanyika kwa usimamizi wa shughuli hizi katika mamlaka mbalimbali sanjari na kukosekana kwa Sheria inayoratibu shughuli za Zimamoto na Uokoaji, kwa kiasi kikubwa kumechangia kutokuwepo kwa ufanisi unaotakiwa katika utekelezaji wa mambo ya kila siku ya Vikosi vya Zimamoto na Uokoaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua matatizo yanayovikabili Vikosi vyetu vya Zimamoto na Uokoaji, kunakosababishwa na utaratibu wa Vikosi hivyo kuwa chini ya usimamizi wa vyombo tofauti na kukosekana kwa sheria inayoratibu shughuli hizo, na baada ya utafiti wa kina uliotanabaisha ukweli huo, Serikali imeamua kuwasilisha Muswada huu mbele ya Bunge lako Tukufu ili kupata ridhaa ya Bunge, kwa nia nzuri ya Serikali katika kupambana na majanga ya moto na majanga mengine yanayoweza kuathiri maisha na mali za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini sisi wote humu ndani ni mashahidi wa majanga mbalimbali ambayo yamewahi kutokea nchini na kupoteza maisha ya Watanzania wenzetu katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Hivyo basi, Muswada huu kwa kuzingatia uzoefu tulioupata katika kukabiliana na majanga hayo, unakusudia kuweka mfumo mzuri utakaosaidia katika kukabili majanga ya aina yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru kwa dhati Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa William Kusilla na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa George Mkuchika na Wajumbe wote wa Kamati kwa ushauri, maoni na mapendekezo ambayo kwa kiasi kikubwa yameboresha maudhui ya Muswada huu na hivyo kutuwezesha kukamilisha mchakato wa kuwasilisha Muswada huu mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii sio mara ya kwanza kwa Kamati hii kutoa ushauri na mapendekezo ambayo yamesaidia sana kufanikisha utekezaji wa majukumu ya Wizara yangu, na kwa sababu hiyo, Wizara yangu inaahidi mbele ya Bunge hili kuendelea kuthamini na kuenzi busara za Wajumbe wa Kamati hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuishukuru Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali hususan Wataalam wake kutoka Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria kwa kuufanya Muswada huu uwe na sura uliyonayo hivi sasa, unasomeka na kueleweka vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maudhui ya Muswada, Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji kinachopendekezwa kitakuwa ni chombo cha Umma kama lilivyo Jeshi la Polisi au Jeshi la Magereza na kitasimamiwa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi za kila siku za chombo hiki zitasimamiwa au zitakuwa chini ya uongozi wa Kamishna Mkuu kama ilivyoainishwa ndani ya kipengele husika cha Muswada huu. Muswada unapendekeza kuweka shughuli zote za Zimamoto na Uokoaji chini ya chombo kimoja kwa malengo ya kuleta ufanisi katika shughuli hizo. Jeshi la Zimamoto na Uokoaji litakuwa chini ya Uongozi mmoja unaoongozwa na Kamishna Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuupitia Muswada, Kamati ilitoa mapendekezo ya kufanya marekebisho katika Ibara kadhaa za Muswada. Baada ya kutafakari mapendekezo ya Kamati, Serikali imekubali kufanya marekebisho katika baadhi ya Ibara za Muswada kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Marekebisho *(Schedule of Amendments)* ambalo limegawiwa kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza, Lengo kuu la Muswada huu ni kuitunga upya Sheria ya Zimamoto na Uokoaji lakini pia kuliimarisha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ili liweze kukabiliana na majukumu ya kileo ya mambo yote ya Zimamoto na Uokoaji. Nina hakika sisi wote, Wajumbe wa Bunge hili, tunakubaliana kuwa tunahitaji kuwa na Jeshi la

Zimamoto na Uokoaji lenye Askari wa Zimamoto na Uokoaji wenye mafunzo mazuri, nidhamu ya hali ya juu na vifaa vya kisasa vya kutosha kukabiliana na matatizo ya kileo ya Zimamoto na Uokoaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mswada huu umegawanyika katika sehemu kuu nne. Sehemu ya Kwanza ya Muswada yenye kifungu cha kwanza hadi cha tatu inatoa maelezo ya awali kama jina la sheria, tafsiri ya misamiati mbalimbali, tarehe ya kuanza kutumika kwa sheria na pia inataarifu kuwa Sheria hii itatumika Tanzania Bara peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili ya muswada yenye kifungu cha 4 - 13 inaliunda Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na kuyaainisha majukumu yake, pamoja na kuwaingiza ndani ya Jeshi hilo askari wa Zimamoto na Uokoaji na Watumishi wengine wote waliopo. Aidha, sehemu hii inatoa taratibu za tahadhari ya moto, uzimaji wa moto na inalipa Jeshi hilo jukumu la uokoaji kwenye matukio ya maafa mbalimbali yakiwemo ya moto, mafuriko, matetemeko ya ardhi, ajali za barabarani na maafa mengineyo yoyote. Sehemu hii pia inatoa mamlaka kwa Waziri wakati wa dharura kuweza kuamrisha vikosi vyote hata vya binafsi kushiriki kupambana na janga lolote linapotokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tatu ya muswada yenye kifungu cha 14 - 20 inaweka utaratibu wa uteuzi wa Kamishna Mkuu, Kamishna na Naibu Kamishna ambao watateuliwa na Rais. Aidha, sehemu hii pia inatoa utaratibu wa uteuzi na majukumu ya Maafisa wengine wa Ngazi ya Juu na Wasimamizi wa Mikoa na Wilaya ambao watateuliwa na Tume ya Ajira ya Polisi na Magereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya nne ya muswada yenye kifungu cha 21 - 32 inahusu vipengele mchanganyiko na vifaa vya tahadhari ya moto vitakavyowekwa kwenye maghorofa kuanzia nne na vile vitakavyowekwa kwenye jengo linalozidi ghorofa nane. Vifungu hivyo pia vinaweka masharti ya kuajiriwa kwa Msimamizi wa Usalama wa Moto kwenye majengo makubwa. Kifungu cha 32 kinampa uwezo Waziri, kwa kuzingatia ushauri wa Kamishna Mkuu, kutunga Kanuni *(Regulations)* zinazoweka utaratibu na adhabu kuhusu mambo mbalimbali ya kuimarisha utekelezaji wa Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, nakushukuru sana kwa fursa uliyonipa kutoa maelezo ya Muswada huu na kupitia kwako nawaomba Waheshimiwa Wabunge waupitishe na nawashukuru sana kwa kunisikiliza kwa makini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki!

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. CAPT. GEORGE H. MKUCHIKA (MAKAMU MWENYEKITI – KAMATI YA ULINZI NA USALAMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa maoni ya Kamati ya Ulinzi na Usalama baada ya kuchambua na kujadili Muswada wa Sheria ya Zima Moto na Uokoaji *(The Fire and Rescue Act, 2007)* wa Mwaka 2007. Muswada huu ukipitishwa, utafanya Idara ya Zimamoto

na Uokoaji ifanye kazi zake kwa ufanisi na tija inayotosheleza huduma za Kitaifa na Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuwasilisha maoni ya Kamati, naomba nitumie fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kuishauri Serikali kuhusiana na masuala ya ulinzi na usalama. Kwa heshima yao, ningependa kuwataja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa William J. Kusila - Mwenyekiti, Mheshimiwa Capt. George H. Mkuchika - Makamu Mwenyekiti, Mohamed Abdulaziz, Mheshimiwa Col. Saleh A. Farrah, Mheshimiwa Maria I. Hewa, Mheshimiwa Vita R. Kawawa, Mheshimiwa Wilson M. Masilingi, Mheshimiwa Jackson M. Makwetta, Mheshimiwa Janeth M. Massaburi, Mheshimiwa Dr. John S. Malecela, Mheshimiwa Col. Feteh Saad Mgeni, Mheshimiwa Benson M. Mpesya, Mheshimiwa Brig. Jen.(mst) Hassan A. Ngwilizi, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa Muhammad I. Sanya na Mheshimiwa Dr. Guido G. Sigonda. *(Makofi)*

Aidha, nawapongeza Mheshimiwa Mtutura A. Mtutura - Mbunge wa Jimbo la Tunduru na Mheshimiwa Florence Kyendesya - Mbunge wa Viti Maalum ambao ni Waheshimiwa Wabunge wapya na kwa niaba ya Kamati, napenda kuwakaribisha katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuungana na Wabunge wenzangu, wananchi wa Jimbo la Gairo na Watanzania kwa ujumla, kutoa rambirambi kwa kifo cha Dr. Aaron Chiduo, ambaye aliwahi kuwa Mbunge wa Jimbo la Gairo na Waziri wa Afya na mwenzetu katika Bunge hili kwa muda mrefu. Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema Peponi. Amina.

Napenda pia kuchukua nafasi hii kutoa rambirambi zetu kwa Waziri wa Usalama wa Raia na Mjumbe mwenzetu wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Harith B. Mwapachu, kwa kufiwa na Mama yake mzazi. Aidha, tunatoa rambirambi kwa Watanzania wenzetu waliopoteza maisha yao katika ajali ya Basi la Buffalo huko Kilimanjaro. Tunawapa pole familia zilizopoteza ndugu zao kutokana na ajali hiyo. Mwenyezi Mungu aziweke roho za Marehemu mahali pema Peponi. Amin.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo furaha pia kumpongeza Mheshimiwa Spika kwa jinsi anavyoliendesha Bunge hili pamoja na Naibu Spika na ninyi Wenyeviti ambao kwa pamoja mmelifanya Bunge liwe na mchango mkubwa kwa wananchi na Serikali katika kufanikisha utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005. Aidha, napenda kumpongeza Waziri Mkuu - Mheshimiwa Edward N. Lowassa, kwa kusimamia vizuri shughuli za Serikali ndani ya Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu cha 70(2) Toleo la Mwaka 2004, naomba sasa niwasilishe maoni ya Kamati yangu kuhusu Muswada uliotajwa hapo juu ambao madhumuni na sababu zake ni kupendekeza kutungwa kwa Sheria ya Zimamoto na Uokoaji ya Mwaka 2007 kwa dhamira ya kuunda mfumo mpya wa Kisheria, Kiutawala na nidhamu katika Jeshi hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada uliopo mbele yetu umezingatia mambo muhimu yafuatayo:-

(1) Kuanzisha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji;

(2) Kuainisha Mamlaka ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji;

(3) Kuainisha taratibu za kuendesha Jeshi la Zimamoto na Uokaji kuwa ni wa Kijeshi na unaotumia Amri *(Coordinated Central Command and Command of Force Discipline)* kwa vikosi vyote vya Zimamoto na Uokoaji vya Serikali na binafsi nchini;

(4) Kuweka bayana na kuainisha majukumu ya Kamishna Mkuu wa Zimamoto na Vikosi vilivyoko chini yake, Miji, Bandari, Viwanja vya Ndege na Vikosi binafsi *(Private Units)* kiutawala na kiutendaji wakati wa majanga;

(5) Majukumu ya Jeshi katika kuzima moto, kuokoa maisha na mali, ukaguzi wa tahadhari za moto kwenye majengo na vyombo vya usafiri;

(6) Majukumu ya kuelimisha Umma kuhusu tahadhari za moto;

(7) Kuweka taratibu za kuhifadhi na kusafirisha madawa ya hatari;

(7) Kuainisha taratibu za tahadhari ya moto kwenye maeneo yanayohifadhi mafuta, yanayochimba gesi na mabomba yanayosafirisha mafuta ya gesi;

(9) Kuratibu shughuli za uokoaji kwenye majanga kama vile moto, mafuriko, matetemeko ya ardhi, ajali za vyombo vya usafiri na kuporomoka kwa majengo;

(10) Kuwa kiungo kati ya Idara ya Maafa ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Vikosi vya Zimamoto kwenye Utekelezaji wa majukumu ya uokoaji; na

(11) Kuainisha Sheria ya adhabu zitakazotolewa kwa wanaovunja sheria, taratibu na kanuni za tahadhari za moto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kikao cha pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Wataalam kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kilichofanyika tarehe 17/04/2007, Kamati ilipitia vifungu vyote vya Muswada ambapo baada ya majadiliano, Kamati uliupokea muswada huu na kutoa mapendekezo mbalimbali yaliyolenga kuuboresha muswada ambayo kimsingi yalikubaliwa na Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo yaliyoangaliwa ni pamoja na Uanzishwaji wa Sheria, Kazi pamoja na Mamlaka ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Utawala, nidhamu na shughuli mbalimbali zitakazolihusu Jeshi hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo pamoja na kuuafiki Muswada huu wa Serikali, Kamati ina maoni yafuatayo:-

(1) Kwa kuwa Sheria hii inalenga kuimarisha huduma za Zimamoto na uokoaji, ni vyema Serikali ikatenga fedha za kutosha ili kuhakikisha kwamba miundombinu na vitendea kazi vya kisasa vinapatikana.
(2) Kuwepo na mpango endelevu wa mafunzo kwa Watumishi na Askari ili waweze kutoa huduma bora, elimu na mafunzo kwa umma kuhusu tahadhari ya Kinga za Moto na majanga mengine hapa nchini.

(3) Watumishi wa iliyokuwa Idara ya Zimamoto pamoja na vifaa *(equipments)* vilivyokuwa vinamilikiwa na Idara hiyo, vyote kwa sasa vimilikiwe na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. Aidha, maslahi yao yaboreshwe na haki zao za nyuma zizingatiwe chini taratibu za Tume ya Polisi na Magereza.

(4) Kifungu cha 10 (6) kimeweka adhabu ya shilingi laki tano kwa wanaovunja sheria hii. Kamati inashauri kwamba ingekuwa vizuri kuweka adhabu zaidi ya moja *(alternative punishment)*, kwa kwa kueleza kwa maana ya faini, kifungo au vyote viwili.

(5) Serikali iweke wazi Muundo wa Utumishi *(Scheme of Service)* katika Jeshi hili la Zimamoto ili kubainisha utaratibu wa kutoka cheo kimoja kwenda kingine.

(6) Kamati inashauri Sheria iweke wazi taratibu za wananchi kupata huduma hii muhimu.

(7) Kamati inashauri kuwe na usimamizi wa karibu kwa Kampuni binafsi zinazotoa huduma ya Zimamoto.

(8) Serikali iwe na mpango madhubuti wa utekelezaji wa Sheria ya Mipango Miji ili kuhakikisha kwamba Miji inajengwa katika mfumo ambao utaruhusu vifaa na magari ya uokoaji, kupita kwa urahisi kukabili janga linapotokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, napenda kumshukuru na kumpongeza Waziri wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Joseph Mungai, Naibu wake Mheshimiwa Lawrence K. Masha, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Johnson Mwanyika na Katibu Mkuu wa Wizara Ndugu Solomon Odunga, pamoja na Maafisa wao kwa kuisaidia Kamati kufanikisha kujadili na kutoa mapendekezo kuhusu muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge - Ndugu Damian S. L. Foka na Katibu wa Kamati hii Ndugu Peter Magati, kwa kuhakikisha kuwa maoni ya Kamati hii yanakamilika kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHESHIMIWA MHONGA SAID RUHWANYA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI – WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kutoa maoni ya Kamabi ya Upinzani. Kabla sijatoa maoni hayo, naomba nitoe pole kwa familia ya Mheshimiwa Mwapachu kwa kufiwa na mama yao mzazi, vile vile familia ya Mheshimiwa Msolwa kwa

kufiwa na mdogo wake na kwa familia za wote waliopoteza ndugu zao katika ajali ya basi la Buffalo, Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kutoa maoni kuhusu Muswada wa Sheria ya Zimamoto na Uokoaji ya mwaka 2007, kwa mujibu wa kanuni zetu za Bunge kifungu cha 43(5)(b)(c) na 70(2) toleo la 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali, imepokea ushauri wetu kama tulivyopendekeza katika Hotuba yetu ya Kambi ya Upinzani kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na mimi ndiye niliyetoa maoni hayo. Kwa hiyo, tunaishukuru sana Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Zimamoto ni moja ya idara nyeti nchini mwetu lakini hadi hivi karibuni imekuwa ikiangaliwa kwa umuhimu usio kidhi matakwa yake. Watanzania wengi wamepoteza maisha na mali zao kutokana na mfumo duni wenye kukatisha tamaa wa Idara ya Zimamoto katika miji yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haki ya kulindwa na majanga ya Zimamoto imeyumbishwa sana na wanyonge wa nchi hii wanaendelea kufukarishwa kutokana na majanga ya moto. Ilikuwa ni vigumu kujua nani hasa anawajibika na Zimamoto, lakini kwa muswada huu unatoa matumaini kuwa mambo ya kutupiana mpira wa majukumu umepatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunafahamu kuwa kazi ya kulinda usalama wa raia na mali zake ni kazi ya Polisi (chini ya Wizara ya Usalama wa Raia). Hivyo basi, tunadhani hata Kikosi hiki cha Zimamoto kinatakiwa kiwe chini ya Wizara hii na ni makosa kikosi hiki cha Zimamoto kuwa chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Kambi ya Upinzani inasema hivyo kwa sababu Polisi kwa sasa ina mtandao wa vituo takriban kila kata katika nchi nzima. Hivyo basi, kwa kikosi hiki kuwa chini ya Wizara hii, kitakachotakiwa kufanyika ni kutumia mtandao wa Polisi uliopo katika kutekeleza shughuli zake kwani majanga hayachagui ni wapi yatatokea mjini ama vijijini, jambo la msingi ni kuwa tayari na karibu muda wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sehemu ya tafsiri ya maneno sehemu ya kwanza, neno *'premises'*, tunashauri maneno kama *'public transport and vessels'* yahusishwe katika tafsiri hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili kifungu cha 5(1) naomba kununukuu: *"General duties of the force shall be to prevent and minimize death rates, injury to the people, and damage to properties arising from fire floods, earthquakes, roads accidents and other disasters."* Kwa kuangalia kazi hizo, ina maana kwamba Kikosi kitakuwa na uwezo wa kukagua vyombo vyote vya usafiri kuangalia viko katika ubora unaoridhisha, kukagua majengo yote kuangalia kama yamejengwa kulingana na vigezo vyao vya kuzuia na kurahisisha uokoaji pamoja na kuangalia ubora wa vifaa vya ujenzi ambavyo vinahusika moja kwa moja na moto kama vile vifaa vya umeme kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inadhani Kikosi hiki kimepewa mamlaka ya kupitiliza, kwani kinachukua kazi za mamlaka ya Bodi ya Kandarasi na ile ya Usanifu Majengo, pia wanachukua kazi ya *SUMATRA*. Ni bora ikawekwa wazi kuwa utendaji wao uendane na mamlaka husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 5(2)(c) kikosi kinapewa mamlaka ya kufanya uchunguzi kuhusiana na vyanzo vya moto pamoja na hasara isababishwayo na moto. Kambi inadhani, ni bora Polisi ichukue nafasi yake kwani kwa hali ilivyo, wataalam wa kuchunguza wapo Polisi. Tusianze kuchanganya majukumu, kwani mwishoni itakuja kuleta mkanganyiko na kuanza kutupiana lawama pale uzembe utakapotokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 7(1) (b), naomba kunukuu: *"Protecting life and property in the event of fires in its area."* Kambi ya Upinzani inadhani hili litaleta maana zaidi kama kutakuwa na kifungu kinachoeleza pia madhara yanayosababishwa na majanga ya moto na yanayofikiriwa *(fire has got other side effect disasters and these should be included).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 9(2) (b), naomba kunukuu: *"Harm to the environment, including the life and health of plants and animals"* Hapa tunaomba ufafanuzi, ni kikosi hicho hicho au ni kikosi kingine kilicho chini ya Idara ya Misitu au kuna utaratibu gani kisheria katika utendaji kazi baina ya vikosi hivi, kwani tumeshuhudia milima, misitu mingi ya hifadhi ikiteketea na Taifa kupoteza fedha nyingi kutokana na uharibifu unaotokana na mioto hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 12 (5) tunadhani itakuwa ni kuchukua madaraka ya kamishina generala kwa Waziri husika moja kwa moja katika matukio ambayo *Commissioner General* anaweza kuyatolea kauli. Na hili litakuwa ni jambo la busara kwani kauli za kisiasa hazitakuwepo badala yake kauli zitakuwa za kitalaam zinazotumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani, inaomba kutoa mapendekezo ya Jumla kuhusiana na Muswada huu. Moja, kunatakiwa kuwekwa kifungu maalumu katika muswada huu, upigaji marufuku kuhifadhi au kutunza bidhaa ambazo ni rahisi kulipuka na kusababisha moto kama vile *petrol* katika makazi ya raia; na pili, ni muhimu kuweka kifungu ambacho kitasimamia shughuli zote za vyombo binafsi vinavyohusiana na Zimamoto pamoja uokoaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunakushuru sana Mheshimiwa Mhonga kwa kuwakilisha maoni ya Kambi ya Upinzani.

Waheshimiwa Wabunge, sasa tutaanza mjadala wa pamoja na mpaka sasa katika Meza yangu ninao wasemaje wawili, Mheshimiwa Mgana Msindai na Mheshimiwa Fatma Mikidadi. Kwa hiyo, naomba nimwite Mheshimiwa Mgana halafu Mheshimiwa Fatma Mikidadi ajiandae. Karibu Mheshimiwa Mgana Msindai.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Muswada huu kwa kifupi kabisa. Kwanza, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa waliyoifanya. Pia niishukuru Kamati ya Ulinzi na Usalama kwa kazi nzuri waliyofanya ya kuchambua Muswada huu na kutoa mapendekezo yao. Nina imani kabisa kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama, Wajumbe wa Kambi zote wapo kwa sababu Kamati zetu hazibagui, zinawachukua Wajumbe kutoka pande zote, yaani vyama vyote. Sasa mandhali Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ametoa mapendekezo na kwamba wamekubaliana na Wajumbe wote wa Kamati, haya aliyoyasema ni sahihi. Mimi nisingeona umuhimu wa upande mwingine kuanza kukosoa. Walikuwa na muda wa kukosoa kwenye Kamati na sio hapa ndani ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashukuru sana kuanzishwa kwa kikosi hiki cha kuzima moto na uokoaji. Kwa kweli ni kikosi muhimu sana. Tulisikitika sana pale kilipohamishwa na kupelekwa chini ya Utumishi wa Umma. Naishukuru Serikali kwa kuona umuhimu wa kukifanya kijitegemee. *(Makofi)*

Lakini ninaloomba ni kikosi hiki kiwezeshwe. Sasa hivi tunapata taabu sana, wananchi wetu wengi wanaunguliwa na nyumba, mpaka inateketea bila msaada wa Zimamoto. Ukienda Dar es Salam, jiji letu lina magari lakini hayafanyi kazi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya magari yametengenezwa kisasa na gari la Jiji lililopo pale linatumia dakika mbili na nusu mpaka dakika tano kumwaga maji yote yaliyoko humo kwenye ma-*tank* yake. Lakini tatizo tulilonalo ni kwamba hatuna mtandao wa maji wa mabomba au vituo vya maji kwa ajili ya kuzimia moto, ndio maana gari ya *fire* ikienda eneo moja ikishamwaga maji dakika tano moto hauzimiki wananchi tunaanza kusema gari yenyewe imekuja bila maji. Sasa ili kukisaidia kikosi hiki kuwe na mtandao wa maeneo ya kupata maji kwa ajili ya kazi hii.

Pia naipongeza Serikali kwa kusema kwamba sasa vikosi vyote vya zimamoto vya binafsi, vya Serikali, vya mashirika, vitakuwa chini ya sheria hii. Sasa hivi ukienda katikati ya Jiji la Dar es Salaam, hatuna vituo vya Zimamoto, ukienda Mbezi, Tabata, maeneo mengi tu hakuna hivi vituo. Sasa umefika wakati Waswahili kupata kitu kizuri. Ni gharama, lakini Serikali ni lazima sasa ijenge vituo vipya, inunue magari mapya, itandaze mtandao wa maji na iwape elimu hawa watu watakaofanya hii kazi. Watu wanaofanya hii kazi ni kikosi cha kijeshi. Wale ambao walikuwa humu wahamishwe waingie kwenye hiyo, mpaka hapa muda wao wa kustaafu utakapokwisha na maslahi yao yalindwe. Lakini kikubwa zaidi, kwa sababu tumeanzisha kitu kipya, tupeleke vijana wengi wakasome ili tuwe na kikosi cha kisasa. Vijana wakishasoma na wapate vifaa vya kutosha, kwa kweli hii kazi itakwenda vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi miji bado imepangwa vibaya mno. Mara nyingi moto umetokea maeneo kama ya Buguruni, Tandale, wanashindwa kwenda kuzima kwa sababu magari hayawezi kupita. Kwa hiyo, ningeomba mpango wa kupanga miji yetu uanze mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali kwa kazi inayofanyika pale Temeke wakishirikiana na Wafadhili wetu. Kwa kweli, Manzese siyo ile ya zamani ambayo ulikuwa huwezi kupita hata kwa mguu unapata taabu. Sasa hivi barabara nzuri zimetengenezwa na hata pakitokea ajali, haya magari yanaweza kupita kirahisi sana. Sasa mpango unaofanyika pale Manzese uende Buguruni na maeneo mengine yote ya Jiji la Dar es Salaam na hata kwenye miji yetu mingine, miji yote ya Mkoa iwe na mpango mzuri na wapate hivi vifaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nipongeze sana baadhi ya Manispaa zetu na miji kwa kununua magari ya Zimamoto. Lakini ukweli ni kwamba, watalaamu hawana. Mimi nina uhakika kabisa hii sheria itapita na sheria hii ikishapita mfumo utengenezwe mara moja na iwe ni lazima kwa kila miji yetu kuwe na vifaa vya Zimamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la ufungaji wa vifaa vya umeme kwenye nyumba zetu. Kwa kweli nyumba nyingi zinafungwa kienyeji na hiyo inakuwa ni hatari kwa

sababu hakuna watalaam wanaoshauri jinsi ya kufunga hizi nyaya na mara kwa mara zinapata *shot* na nyumba zinaungua. Hili jukumu lichukuliwe na wenzetu wa Shirika la umeme Tanzania, wana makandarasi wao wanaofanya hii kazi. Wengine wameshaanza kufanya kazi hii kwa mazoea. Tunaomba mfumo mzima kuanzia Zimamoto uende mpaka kwenye Shirika la Umeme, kuwe na *cordination* nzuri kwa kazi hii. Hapa tumesema ni Zimamoto na Uokoaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uokoaji uko wa aina nyingi. Kuna uokoaji wa majini, sijui nayo imeunganishwa hapa! Mimi nitashukuru sana nikiambiwa na yenyewe imeunganishwa hapa. Hata huko hatuna vifaa. Nashauri kwamba, kwa sababu hivi tunatengeneza bajeti ya mwaka 2007/2008, basi hiki kikosi kipewe umuhimu wa kwanza wa kutengewa fedha za kutosha ili kianze kazi hii vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yangu yalikuwa hayo. Nashukuru sana kwa kunipa nafasi tena na naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu. Kanuni ya 50 (8): "Ni marufuku kwa Mbunge yeyote kujiingiza katika mambo ya kuwasema wenzake au kuleta malumbano ya kisiasa ndani ya Bunge."

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi binafsi namheshimu sana Mheshimiwa Msindai, ni Mzee wangu, ni Mbunge wa muda mrefu na nasononeka tu kusimama kuzungumzia kuhusu utaratibu juu ya kauli yake. Lakini kwa sababu ni taratibu za Kibunge na rekodi zinatakiwa kuwekwa, inabidi niliseme hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Msindai anazungumza, amesema kwamba Kamati za Bunge, zina Wabunge wa pande zote, Kambi ya Upinzania na Wabunge wa Chama kinachoongoza Serikali na kwamba kwa kuwa maoni ya Kamati yanakuwa yanaletwa na Kiongozi wa Kamati kwa niaba ya Kamati nzima, kwa hiyo, Wabunge wa Upinzani, hawana haki au hawapaswi kukosoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hii siyo sahihi, kwa sababu ni haki kama Wabunge na ni kanuni zetu na ni taratibu zetu kwamba baada ya Mheshimiwa Waziri kuzungumza, Msemaji wa Upinzani naye huzungumza. Kwa hiyo, nahisi kama ni la kutusema na kutunyima kuzungumza. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Mheshimiwa Msindai afute kauli yake. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naona Mheshimiwa Kabwe Zitto ameomba mwongozo wa Kiti changu kuhusiana na hicho ambacho amekileta mbele yetu.

Waheshimiwa Wabunge Mheshimiwa Msindai alipokuwa anachangia, amekuwa wazi kulingana na mtazamo anaouona yeye mwenyewe. Kwa hiyo, kama ni mtazamo ambao anauona yeye mwenyewe, mimi nafikiri kama tu mtu atakuwa ameudhika kwa mtazamo huo anaweza akaleta kwa utaratibu mwingine, lakini sio kwamba Mheshimiwa Msindai kwa kusema hayo amevunja kanuni ya kifungu hicho ambacho Mheshimiwa Zitto unakisema. Vinginevyo ungetumia kile kifungu, labda angekuwa amevunja kile kifungu ambacho kimetoa utaratibu wa Kamati kuwasilisha maoni yao mbele ya Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, naomba tuendelee na nimwite Mheshimiwa Fatma Mikidadi aendelee na mchango wake. *(Makofi)*

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia Muswada huu wa kuanzisha Jeshi la Zimamoto na uokoaji la Serikali.

Kwanza, nami kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Lindi, nitoe salamu zangu za rambirambi kwa Mheshimiwa Mbunge, Marehemu Dr. Aaron Chiduo ambaye amefariki. Namkumbuka sana Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo, alikuja kwetu Mkoani Lindi Mpaka Liwale akiwa Mbunge wa Zamu akifuatana na Mheshimiwa Kawawa, kuja kututembelea Mkoa wa Lindi. Kwa kweli tunamkumbuka sana wananchi wa Mkoa wa Lindi.

Vile vile natoa salaam za rambirambi kwa familia ya mama wa Mheshimiwa Mwapachu na vile vile ndugu wa Mheshimiwa Msolla, kwa kufiwa na ndugu yake. Pia natoa pole kwa wafiwa kutokana na ajali ya iliyotokea Wilaya ya Mwanga ya basi la Buffalo.

Halafu nimesikia kifo kimetokea cha aliyekuwa Mheshimiwa Mbunge Abdillah Namkulala, ingawa taarifa haijafika bado, lakini naye amefariki. Kwa hiyo, ninatoa pole kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa niendelee kutoa mchango wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hii kwa kweli imefika wakati muafaka. Nasema hivyo kwa sababu wakati huu ni wakati wa ajali mbalimbali za moto kubwa kubwa. Ni wakati ambao teknolojia imekua, ni wakati ambao tunahitaji hasa vyombo hivi kuwa makini na vyenye uthabiti, yaani vyenye umakini ndani yake kwa sababu teknolojia imekua, kwa sababu sasa hivi majumba yamekuwa marefu, yanahitaji Zimamoto zenye teknolojia kubwa. Sasa hivi tunahitaji Zimamoto ambazo ni za kisayansi kuliko zile za zamani. Kwa hiyo, nasema kwamba agenda hii imekuja kwa wakati wake. Kabla sijaendelea kuzungumza, nasema kwamba kweli naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea kuchangia, nasema kwamba nashukuru kwamba suala la kuanzisha Jeshi la Zimamoto na Ukoaji kuwa chini ya Serikali ni suala muhimu sana kwa sababu lilipokuwa tu limeachwa hivi hivi lilikuwa na matatizo mengi sana. Magari mengi ya Zimamoto yalikuwa ni mabovu karibu nchi nzima. Halafu magari yenyewe hayapo na sana sana ni mabovu. Halafu wale waliopata kununua magari yalikuwa ni ghali sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio hilo tu, wale waliobahatika kuyanunua, mathalani nyumba imeungua moto, ukiwaambia haya sasa lete Zimamoto, kuitoa pale ilipokuwa labda Halmashauri kuipeleka kwenye eneo la tukio haitoki. Hawawezi kuitoa pale kituoni kwao kuipeleka kwenye eneo la ajali kuzima moto mpaka nyumba inaungua inakwisha, maana yake hawakusomea kuitoa kutoa pale kwenda kuzima moto. Ina vyombo vya kisasa na wale walisomea zamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema kuwekwa vyombo hivi chini ya Serikali kutakuwa na uimarishaji kidogo. Kwa hiyo, tunaomba sasa hivi kitakapokuwa chini ya

Serikali, basi tuimarishe huduma hii. Elimu itolewe kwa vyombo hivyo, vyombo viwe vya kisayansi na maji ya Zimamoto yawepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna uhaba wa magari ya Zimamoto. Nasikia siku moja nyumba iliungua moto, gari ya Zimamoto ilipokwenda kuchukuliwa mpaka nyumba inakwisha Zimamoto haijafika, iko bado inatafuta maji haijui itapata wapi. Kwa hiyo, tunasema hili likiwa chini ya Serikali ni muhimu sana na ni wakati muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu. Sasa hivi visa ni vingi. Utakumbuka kule Dar es Salaam wakati Ubalozi wa Marekani ulipopigwa na maeneo mengine karibu na sisi, visa hivyo! Sisi tunasema ni visa. Maeneo mengine duniani yanalipuliwa bila sababu, ni visa. Sasa visa kama vile, siku hizi ni vingi, huwezi kujua. Bahati nzuri Tanzania ni nchi ya amani, hatuwezi kutegemea mambo kama hayo. Lakini ni bora kujihami kuwa na vyombo imara kama hivi vya uokoaji na Zimamoto imara chini ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli suala hili mimi naliunga mkono kwa asilimia mia kwa mia. Baada ya kusema hayo kwa kweli nashukuru sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Fatma Mikidadi kwa mchango wako. Tunaomba uzime *microphone* yako ili tuweze kupata mawasiliano vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, naomba nimwite Naibu Waziri kwa sababu wachangiaji wamekwisha ili aanze kuchangia mada hii na baadaye atafuatiwa na mtoa hoja mwenyewe. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Wizara kwa kufanya kazi nzuri ya kuona umuhimu wa kuleta Muswada huu wa sheria ya Zimamoto.

Nilidhani muswada huu unahusu mijini tu lakini kipengele cha 5(b) na 3(d) *respectively* kinaonyesha kuwa huduma hii inatakiwa itolewe hata vijijini. Sijaona kama imejitokeza waziwazi huduma hii kwenye Halmashauri na vijijini. Aidha, hata 2(j) *Public awareness* haipo, ndiyo maana moto unapotokea zinaungana hata 10 na hasa ukizingatia maji yenyewe ni ya shida. Lakini panapotokea mafuriko ndiyo mbaya zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba suala la huduma ya Zimamoto kwenye hizi ngazi nyingine yaani Wilaya, Kata, Vijiji ambapo majanga haya ni mengi, lijitokeze kwenye muswada hu, na namna ambavyo Serikali inakusudia kutoa msaada ili huduma hiyo iwe na manufaa kwa wananchi wa huko. Ahsante.

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kutoa rambirambi kwa Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia, Mheshimiwa Harith Mwapachu na wengine waliopoteza ndugu zao katika basi la *Buffalo* Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura na Mheshimiwa Florence Kyendesya, kwa kuweza kujiunga na sisi hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwneyekiti, baada ya hapo nianze kwa kusema kuwa kuna gari za Zimamoto nyingine ambazo hazina wataalamu wa Zimamoto kwa sababu panapotokea moto katika uwanja wa ndege, unakuta ndege yote inaungua. Hii inachangiwa pia na kwamba kunapotokea semina za kujua jinsi ya kuzima moto kwenye gari la kuzima moto ambalo ni jipya, wanaokwenda kwenye semina hizo ni wale wakubwa tu ambao hawahusiki na kuzima moto wakati wa ajali na mtumiaji wa gari anakuwa ni mtu mwingine ambaye hakwenda semina hiyo ya jinsi ya kutumia gari hilo.

Nitoe mfano katika Manispaa ya Kigoma Ujiji walileta gari la Zimamoto jipya na aliyekwenda kwenye semina hiyo alikuwa mtu mwingine kabisa na mara ajali ya ndege ilitokea katika uwanja wa ndege wa Kigoma na ndege ilianza kuungua moto, mara lile gari jipya likafika ili kuzima ile ndege iliyokuwa inaanza kuwaka. Cha ajabu ni kwamba, gari lile halikutoa hata tone la maji kwa sababu aliyekuwa analitumia gari hilo siku hiyo siyo mtu aliyesomea jinsi ya kutumia gari hilo na mwisho ndege yote ikawaka moto na yule aliyepata mafunzo ambayo siyo yake, hakuhusika na uzimaji wa moto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iweze kuwachukulia hatua hao ambao wanachukua nafasi za wenzao na kazi inapotokea hawahusiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naomba kuunga hoja mkono kwa asilimia mia moja.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na wachangiaji wengine kutoa pole kwa familia ya Mheshimiwa Harith Mwapachu, kwa kufiwa na mama yao mzazi, pia pole kwa Mheshimiwa Profesa Msolla, kwa kufiwa na mdogo wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Joseph Mungai - Waziri wa Mambo ya Ndani na Mheshimiwa Lawrence Masha, Naibu Waziri, pamoja na Katibu Mkuu Bwana Odunga na timu nzima ya Wizara ya Mambo ya Ndani kwa kuandaa Muswada huu ambao ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mweyekiti, napongeza Kamati ya Ulinzi na Usalama kwa kazi nzuri na mapendekezo waliyopata katika kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zimamoto ni chombo muhimu sana hasa kwa kuzingatia sheria mbalimbali zinazohusu Mipango Miji na Makazi. Muswada huu umekuja wakati muafaka wakati maeneo mengi ya nchi yetu yanaendelea na ujenzi wa nyumba, maeneo haya yanayojengwa kufuatana na taratibu za Mipango miji hivyo ni wazi sasa huduma ya Zimamoto itahitajika sana. Pamoja na Muswada huu kuwa mzuri, pia Wizara ihakikishe yafuatayo:-

(i) Kuimarisha mtandao wa kikosi hiki na kuwa na vijana wa kutosha wenye mafunzo bora na nyenzo bora; na

(ii) Pia kikosi kiandae majarida mbalimbali yenye kutoa ujumbe wa kuelimisha wananchi juu ya kujikinga na moto na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naishukuru Serikali na kuipongeza kwa kuleta Muswada huu muhimu. Kimsingi tumechelewa hata kuupitisha. Masuala ya moto nchini kwetu ni mengi mijini na vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu la kwanza, Muswada huu utafsiriwe na kupelekwa vijijini haraka na mapema maana nako kuna mioto mingi hasa maeneo ya Iringa kwenye mashamba ya miti Mufindi na kwingineko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la Msingi kushirikisha sekta binafsi kama ilivyo katika ibara ya tano *(Voluntary Fire Fighter)* na kuwatambua kuwa ndio wadau wakubwa na hata hiyo mioto hutokea huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali iweke utaratibu pia wa kuruhusu sekta binafsi waweze ku-*register Voluntary Fire Fighter Stations* zao kwa gharama ndogo ili moto ukitokea mtu aweze kupiga simu hospitali binafsi, *Security* binafsi na kadhalika.

Aidha, kifungu cha 13(3) na 13(4) kimeelezea *offence* na *penalty.* Kifungu kinaeleza: *"Imprisonment for a term not exceeding three months."* Nashauri *imprisonment* iwe *for a term, not exceeding six months,* kama hiyo Ibara ya 12(3), lakini *six months* ndio inafanana na faini zilizotajwa 13(3) na 13(4).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 14, *part III, Administration and discipline,* mfumo umeishia katika *District level.* Baadhi ya Wilaya ni kubwa sana na majanga hutokea vijijini. Mfano Wilaya ya Kilolo ambako kuna milima ya *Eastern Arc Mountains* na misitu mikubwa na kama huduma hii itakuwa *centralized* Wilayani, bado ni tatizo. Tuangalie huduma hizi zifike Tarafa, Kata na Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara ya tano inaongelea suala la *summary dismissal,* 5(c) na 5(d). Nashauri suala hili lisiongelewe kwenye Muswada huu, sio mahali pake kwani tunazo *labour laws* zinazo-*govern* masuala ya kazi na zinaeleza vizuri kabisa juu ya *summary dismissal* kwani Muswada huu unaweza ukapingana na *labour laws.* Hivyo, kifungu 5(c) na (d) nashauri kifutwe au kitoe maelezo kwa mujibu wa *labour laws* zinazo- *govern summary dismissal,* vinginevyo sheria zitapingana.

Kifungu 5(b) kinasema: *"If fireman is connected of a criminal offence he may be dismissed from force."* Hiki kimekaa vizuri, kwani itategemeana na sheria za kazi zinatuongozaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 22, *provision and maintenance of fire escape,* ningependa kuhakikishiwa juu ya kifungu hiki na sheria za Ukandarasi (ujenzi): Je, kifungu hiki kipo kwenye sheria zozote za ujenzi? Maana Idara za Ujenzi ndio washauri wa ujenzi. Isije ikawa kipo hapo, lakini washauri wa ujenzi hawajashirikishwa *at all*. Naomba majibu.

Mheshimiwa Mwneyekiti, kwa mujibu wa sheria hii, ni muhimu sasa tuanze ukaguzi wa Kifungu cha 22 katika kila jengo nchini maana majengo mengi hayana *fire escape. Fire alarm* kama zipo zimeharibika na ni majengo ya ghorofa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 23(2) kinaeleza *penalty.* Nashauri iwe *fine, not exceeding one million,* badala ya *fifty thousand shillings,* iwe kama kifungu cha 22(3).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 25 kinaeleza *awards,* lakini anayetoa ni *President, why president? It could be any one, any company, why President?* Hakuna *definition* ya *President.* Nashauri kifutwe maana hata bila ya kifungu hiki *President* anaweza aka-*award what so ever in his country,* maana hatuelewi kama ni *President* wa Muungano au Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kifungu cha 27, ni muhimu juu ya *compensation,* lakini hakijitoshelezi. Kinahitaji maelezo zaidi juu ya *formula* na utaratibu na muhimu kukawa na *insurance policy* ya *compensation* maana *government* peke yake haitoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara ya 29(c) inaeleza mikopo kwa *firemen.* Nadhani hapa sio mahali pake, lengo la muswada ni kuzuia moto, masuala ya mikopo kwa mabenki, taasisi mbalimbali, vinginevyo lengo la Muswada halitakuwa *achieved* na hata fedha za mkopo zitatoka wapi? Maana hii ni huduma! Naomba kipengele hicho kifutwe.

Ibara ya 31(b), nashauri: " *fine of one hundred thousands shillings",* iwe *"fire not exceeding five hundred thousands."* 31(3) nashauri iwe:*"shall be liable to a fine not exceeding fire hundred thousand or imprisonment not exceeding three months",* ili hakimu awe na uhuru wa kuamua.

Kwa kuzingatia umuhimu, madhumuni na sababu za Muswada huu muhumu, kwa niaba ya watu wa Iringa, naunga mkono hoja baada ya marekebisho na majibu ya mchango wangu tajwa hapo juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia Muswada huu muhimu wa Zimamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza Waziri na Naibu Waziri pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa kuandaa miswada hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti,magari mengi ya Zimamoto yapo, lakini mara nyingi yanakuwa hayana maji ya kuzimia moto. Mfano, hivi majuzi moto ulitokea *TPC,* magari ya Zimamoto kutoka Moshi ni mapya tu. Cha kujiuliza, gari ya Zimamoto haikuwa na nguvu ya kurusha maji mpaka gari ikatoka *Kilimanjaro Airport* kuja kuzima moto ule. Pengine wafadhili walituma gari ambalo halifanyi kazi vizuri? Msaada ichunguzwe kama ipo katika hali nzuri, nchi yetu isiwe jalala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia sheria hii isisitize *public places* kama maofisini, misikitini, makanisani, kuwepo na vifaa vya kuzuia moto kwa *fire extinguisher,* hii itasaidia kuokoa moto kusambaa zaidi.

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia machache yanayohusu Muswada huu wa Zimamoto. Awali ya yote, napenda kusema naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwa na kikosi cha Zimamoto ni jambo muhimu sana katika nchi yetu, lakini naona ni jambo ambalo halipewi kipaumbele kwani kila miji ina vifaa

vya Zimamoto na kama vipo, basi hali yake ni duni sana. Serikali imepuuza sana uwepo wa vifaa vya Zimamoto na uokoaji. Tumeona nyumba zikiteketea na watu wakifa kutokana na majanga ya moto bila kuwa na msaada wowote kutoka Idara ya Zimamoto. Inaelekea Zimamoto kama jeshi, kwa mtazamo wa sasa ni kwa ajili ya miji mikubwa tu na sehemu ya miji midogo au ya kati inakuwa haina vikosi vya Zimamoto. Hivyo, nashauri miji midogo na ya kati nayo iwe na vifaa vya Zimamoto na uokoaji

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zimamoto kuwa ni Idara inayojitegemea chini ya Serikali, ni jambo ambalo litaongeza ufanisi mkubwa. Lakini inakuwa vigumu kwa kikosi cha Zimamoto bila kuwa na vitendea kazi madhubuti itakuwa ni kazi bure na pia naomba kikosi kinachotaka kuundwa kiendane na wakati kwa kuwapatia watumishi wake mafunzo ya kisasa na vifaa vya kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kusema kwamba, naunga mkono hoja hii.

**NAIBU WAZIRI WA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi pia nichangie hoja ambayo iko mbele yetu kwa kujibu baadhi ya hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kujibu hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge, naomba nami niungane na Wabunge wenzangu katika kutoa rambirambi zangu kwa familia ya Marehemu Dr. Aaron Chiduo, pia kwa familia ya Mheshimiwa Harith Mwapachu na familia za Watanzania wenzetu ambao wamepoteza maisha kwenye ajali ya basi la Buffalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ningependa kuanza kwa kusema kwamba naiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. Nitachukua muda wangu kuangalia hoja ambazo zimetolewa na Kambi ya Upinzani na Mheshimiwa Mbunge mwenzangu, Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maoni ya Kambi ya Upinzani, tumeshauri kwamba *definition* ya *premises* ambayo imetolewa ndani ya sheria hii ipanuliwe ili tafsiri yake ihusishe *public transport* pamoja na *versus*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kumfahamisha kwamba tayari katika *amendment* ambazo zimesambazwa kwa Waheshimiwa Wabunge, chini ya *amendment* (a) ushauri huu umeshafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ushauri ambao tumesomewa na Kambi ya Upinzani, wakiongelea sehemu ya pili kifungu (5) (1) ambapo tulikuwa tunaongelea suala la *general duties* za Kikosi cha Zimamoto, Kambi ya Upinzani imetueleza kwamba mamlaka ambayo imepewa kikosi cha Zimamoto imevuka mipaka na kwamba imeingilia baadhi ya madaraka na taasisi na asasi nyingine kama *SUMATRA*, bodi ya kandarasi na usanifu wa majengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge na Kambi ya Upinzani kwamba sheria ambayo iko mbele yetu siyo Sheria ya Zimamoto peke yake, lakini ni sheria ya Zimamoto na Uokoaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuokoa maisha ya watu inabidi kikosi cha Zimamoto kiwe kina uwezo wa kuingilia sehemu nyingi. kiwe kina uwezo wa kushauri kuhusu ujenzi wa majengo ili pale ambapo kuna masuala ya *fire hazards* watu wasijenge majengo ambayo watashindwa kutoka moto ukitokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inabidi kikosi hiki kiwe na uwezo wa kuwashauri wananchi kuhusu jinsi umeme unavyounganishwa kwenye majengo ambayo yanayojengwa ili kuhakikisha kwamba hizo nyumba haziungui kutokana na kuunganisha nyaya za umeme vibaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumhakikishia Mheshimiwa Ruhwanya kwamba siyo kwamba mamlaka haya yamepitiliza lakini mamlaka ambayo imepewa kikosi cha Zimamoto, imelenga katika kuhakikisha maisha ya Watanzania yanabaki salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani ikichangia kuhusu *section* 5 (2) (c) wameshauri kwamba uwezo wa kufanya uchunguzi, yaani *investigations* wasipewe kikosi cha Zimamoto na mamlaka haya yabaki na Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoanza kuelezea nilipokuwa naelezea *section* 5 (1), ni dhahiri kabisa kwamba mamlaka ya Zimamoto lazima iwawezeshe kuchunguza na kujua moto unaanzaje au ulianzaje, matatizo yalikuwa wapi au kuweza kuchunguza pale ambapo moto unaweza ukatokea. Hii siyo kazi ya Polisi peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kufanya *investigation,* ziko taasisi na asasi nyingi ndani ya nchi yetu ambazo zina uwezo wa kufanya *investigation* na siyo Polisi peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilishauriwa pia kwamba Jeshi la Zimamoto liwe chini ya Wizara ya Usalama wa Raia na siyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Nafikiri itakumbukwa pale ambapo Wizara ya Mambo ya Ndani ilivyotenganishwa ili kuwe na Wizara ya Usalama wa Raia na Wizara ya Mambo ya Ndani, ilifanya makusudi kabisa ili kuliwezesha Jeshi la Polisi kufanya kazi yake kwa ufasaha zaidi. Isingekuwa vyema kuiongezea Wizara ya Usalama wa Raia, kazi ya kuwa na kikosi cha Zimamoto chini yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaamini kabisa Wizara ya Mambo ya Ndani inao uwezo wa kuendelea kuwa na kikosi cha Zimamoto na kuiongoza na kuhakikisha maisha ya Watanzania yaendelea kuwa salama.

Katika kuchangia *section* 12 *sub section* (5) tumeambiwa kwamba *section* hiyo inamfanya Waziri achukue madaraka ambayo yangekuwa *commission general*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia *section* hiyo ya sheria inamwezesha Mheshimiwa Waziri kuamuru vikosi binafsi vya Zimamoto kushiriki katika majanga ya moto ambayo yametokea ndani ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaamini kwamba suala la kuweza kuamuru watu binafsi kushiriki katika suala kama hilo ni suala ambalo linatakiwa kupewa uzito wote na uzito huo imani yetu inatakiwa kuwa chini ya Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Tumeelezwa na Kamati ya Upinzani, kwamba ingekuwa vema kwamba tuwe tuna kipengele ndani ya sheria yetu ambayo inaongelea utunzaji wa bidhaa ambazo zina uwezo wa kulipuka yaani *explosives.* Ningependa kuwafahamisha kwamba tunayo sheria tayari ambayo inahusika na suala la *management to explosive* ndani ya taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho tumeshauriwa kwamba kuwe kuna kifungu maalum ndani ya Sheria yetu ambacho kinamwezesha Mheshimiwa Waziri kusimamia vikosi binafsi na kuwapatia *regulations*. Nilivyoeleza awali chini ya *section* 12 (5) Waziri anao uwezo wa kuamuru vikosi binafsi kusaidia katika majanga ambayo yatatokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaamini kwamba suala la kuweza kuamuru watu binafsi kushiriki katika suala kama hilo ni suala ambalo linatakiwa kupewa uzito wote na uzito huo imani yetu inatakiwa kuwa chini ya Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeelezwa na Kamati ya Upinzani, kwamba ingekuwa vema kwamba tuwe tuna kipengele ndani ya sheria yetu ambayo inaongelea utunzaji wa bidhaa ambazo zina uwezo wa kulipuka yaani *explosives.* Ningependa kuwafahamisha kwamba tunayo sheria tayari ambayo inahusika na suala la *management to explosive* ndani ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho tumeshauriwa kwamba kuwe kuna kifungu maalum ndani ya Sheria yetu ambacho kinamwezesha Mheshimiwa Waziri kusimamia vikosi binafsi na kuwapatia *regulations*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilivyoeleza awali chini ya *section* 12 (5) Waziri anao uwezo wa kuamuru vikosi binafsi kusaidia katika majanga ambayo yatatokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia chini ya kifungu namba 33, Waziri anao uwezo wa kuandaa *regulations* za kuwadhibiti na kuwaongoza vikosi binafsi vya Zimamoto ambavyo tunavyo hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa maelezo hayo kuhusu hoja ambazo zimeletwa mbele yetu na Kambi ya Upinzani naomba kwa mara nyingine tena kusema naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Napenda nianze kwa kuwashukuru sana wachangiaji wote katika mjadala mfupi tumepata wachangiaji 10, wanne kwa kuzungumza ndani ya Bunge na sita wamechangia kwa maandishi kama ifuatavyo:-

Napenda niwashukuru waliochangia humu ndani ya Bunge kwanza Mheshimiwa George Mkuchika, Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, wa pili Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya na wa tatu Mheshimiwa Mgana Msindai na wa nne Mheshimiwa Fatma Mikidadi. *(Makofi)*

Nawashukuru kwa michango yao ambayo sisi wote humu ndani ya Bunge tumesikia na waliochangia kwa maandishi ambao nao napenda niwashukuru ambaye sasa anayefuata anakuwa ni wa tano, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, wa sita Mheshimiwa Lucy Owenya, wa saba ni Mheshimiwa Dunstan Mkapa, wa nane Mheshimiwa Sipata Mkayamba, wa tisa Mheshimiwa Juma Killimbah na wa kumi ni Mheshimiwa Pindi Chana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote hao nawashukuru kwa michango yao. Napenda nikiri kwamba wale waliotuletea michango kwa maandishi hatukupata muda wa kusoma yote, lakini nawahakikishia kwamba tumehifadhi maoni yao na nina hakika tutayatumia katika utekelezaji. Itakuwa ni *reference* yetu kuona wenzetu walikuwa na maoni gani, kwa sababu kutokana na mwelekeo wa mjadala haionekani kwamba jambo hili lina upinzani. Inaonekana kila Mheshimiwa Mbunge hapa anakubali kwamba tuwe na sheria ya kusimamia jambo hili na tuwe na chombo maalumu cha kusimamia masuala ya zimamoto na uokoaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwneyekiti, tutajitahidi katika utekelezaji, wapo waliochangia kwamba tupange bajeti ya kutosha na hivyo ndivyo Serikali tutakavyojitahidi kufanya kwa sababu tunatambua umuhimu wa huduma hii. Ningependa nichukue nafasi hii nimshukuru pia Mheshimiwa Naibu Waziri kwa sababu amenisaidia sana kujibu zile hoja nzito ambazo zilihitaji majibu hapa Bungeni.

Lakini napenda pia nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba hata katika ngazi ya Kamati aliniwakilisha kwa sababu mimi nilikwenda nyumbani kidogo kuhudhuria mazishi ya mdogo wake Waziri mwenzangu kule Kijiji cha Mazombe, Wilaya ya Kilolo, Mheshimiwa Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, mdogo wake alifariki dunia na kulikuwa na mazishi na wakati huo huo kulikuwa na Kamati.

Lakini kama alivyosema Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Naibu Waziri aliniwakilisha vizuri sana. Aliweza kufafanua mambo yote, kwa hiyo, namshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipenda tu nifafanue eneo moja, kuliweka wazi ingawa Mheshimiwa Naibu Waziri amelisema, ni kile kipengele ambacho Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani amesema ingefaa labda *Commissioner General* ndiyo atunge *regulations.*

Napenda nifafanue mbele ya Bunge kwa kukisoma kwamba kinavyosema hakitawi kilete wasi wasi wote kinavyosomeka kwa sababu kinasema kama ifuatavyo na kwa ruhusa yako naomba kunukuu kifungu cha 32 kimesema; *"the Minister may, after consultation with or upon the recomendation of the Commissioner General make regulations, prescribing for.* Waziri anaweza kutoa *regulations* lakini Waziri hapa anafungwa kwamba hata kama anaamua Waziri mwenyewe kutunga hizi Kanuni inatakiwa afanye hivyo baada ya kushauriana na *Commissioner General* kwa hiyo lile suala la kusema labda mambo yatakwenda kisiasa kwa sababu Waziri mwanasiasa, uandishi wa sheria unamfunga Waziri kwamba hata linapoanzia kwake, lazima afanye *consultation* na *Commissioner General* na kama halianzii kwake anaweza akafanya hivyo kwa mapendekezo ya *Commissioner General.*

Kwa hiyo, utakuta hapa uzito umewekwa kwenye usimamiaji wa kitaalamu, siyo wa kisiasa katika kutunga hizi *regulations*. Kwa hiyo, kwa kweli hakuna sababu ya kuwa na wasi wasi wowote. Napenda niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba mkipitisha sheria hii ambayo tunawaomba mpitishe, sisi tunaosimamia tutajihadi kusimamia kwa ufanisi na pale inapohitajika tutatoa taarifa kwenye Kamati husika na hapa Bungeni kama taratibu zetu zinavyotuhitaji. Kwa hiyo, kwa ufafanuzi huo na maelezo hayo naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*
*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Zimamoto na Uokoaji wa Mwaka 2007 *(The Fire and Resque Force Bill, 2007)***

Kifungu cha 1
Kifungu cha 2

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 3
Kifungu cha 4
Kifungu cha 5

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 6
Kifungu cha 7

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 8

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 9

*(Kifungu kilichotajwa hapo kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*
Kifungu cha 10

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 11

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, pale kwenye (iii) inasema ile sentensi inaanza, lakini pale ambapo inasema; *"upon the occupier of the owner of the premises in which such fire hazzard exists," exists* ni *permanent* nilifikiri hapa tungeweka neno *occour* au *existed.* Lakini zaidi nadhani *occour is the best world.* Hali kadhalika katika kifungu hicho hicho ukishuka chini inasema; *"not with standing"* katika (b); *"not with standing at the fire hazzard to which is relates." It relates* badala ya *is.* Naona ingesomeka vizuri zaidi *to which it relates.*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nimemwelewa vizuri naona ni utumiaji wa maneno. Kwa hiyo, katika *final editing* ya sheria hizi *perfection* hiyo inaweza ikachukuliwa na waandishi wa sheria.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 12

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napenda kuweka rikodi sawa tu, sikusema katika kifungu hiki, katika ufafanuzi sikusema kwamba yaani tunampa madaraka makubwa Waziri ya kutunga Kanuni. Nilikuwa nasema kwamba yale masuala ya kitaalamu yaachiwe zaidi *Commissioner General.* Kwa hiyo, nilikuwa tu hapo nitoe ufafanuzi na anaweza akaangalia katika karatasi yangu jinsi ilivyoandikwa, siyo kwamba asitunge Kanuni. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Tunakushukuru, Mheshimiwa Waziri halina jibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli nimwelewa vizuri zaidi. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Nafikiri halina tatizo, tunaendelea tu.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 13

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Muswada huu katika wakati huu. Nilikuwa nataka kupendekeza kwamba kufuatana na hali halisi ya hizi *Water High Drants* za zimamoto kwamba mara nyingi huwa zinakuwa kavu. Zimamoto wanapofika pale wanatafuta *the nearest high drant* wanakwenda wanafungua, haina maji. Sasa nilikuwa nataka kupendekeza kwamba *Section* hii itengenezwe *in such a manner* i-*hold responsible authority* wa ku-*provide water* katika *city* ku-*ensure* kwamba kila inapopita *high drant* mara zote kuna maji. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, kwamba hali hiyo anayoizungumzia

tunaifahamu na mwenzangu Naibu Waziri alipotembelea Jiji la Dar es Salaam alikuta hali mbaya sana kwa sababu jambo hili limekwenda bila ukaguzi. Kwa hiyo, ni *high drant* chache sana zinazofanya kazi. Kwa hiyo, tunatarajia kwamba mapema iwezekanavyo katika utungaji wetu wa madaraka ambayo Bunge hili linatupatia kupitia sheria hii tutaweka *regulation* maalum ya kusimamia masuala kama alivyoyaeleza Mheshimiwa Siraju Kaboyonga. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 14

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 15
Kifungu cha 16
*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*
Kifungu cha 17
Kifungu cha 18
Kifungu cha 19

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 20

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 21
Kifungu cha 22
Kifungu cha 23
Kifungu cha 24
Kifungu cha 25
Kifungu cha 26
Kifungu cha 27
Kifungu cha 28
Kifungu cha 29
Kifungu cha 30
Kifungu cha 31
Kifungu cha 32

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Zimamoto na Uokoaji wa Mwaka 2007**
***(The Fire and Resque Force Bill, 2007)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, Kamati ya Bunge Zima limeufikiria Muswada wa Sheria ya Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji yaani *The Fire and Resque Force Bill, 2007* pamoja na marekebisho yake na kuukubali. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba kutoa hoja kwamba Muswada huu pamoja na marekebisho yake sasa ukubaliwe na Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa kwa mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**HOJA ZA SERIKALI**

**Taarifa ya Kamati ya Huduma za Jamii pamoja na Mapendekezo na Maoni yaliyomo katika Taarifa hiyo**

**MHE. OMAR S. KWAANGW' – MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Bunge sasa lipokee na kuikubali taarifa ya Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii kwa mwaka 2006 pamoja na mapendekezo na maoni yaliyomo katika taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijafanya hivyo, naomba niitumie nafasi hii kutoa rambirambi kwanza kwa familia ya Marehemu Dr. Aaron Chiduo ambaye aliwahi kuwa Waziri wa Afya, pili nitoe pole pia kwa familia ya Mheshimiwa Profesa Msolla, Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia pamoja na Mheshimiwa Harith Mwapachu, Waziri wa Usalama wa Raia, wote kwa misiba waliyopata. Pia natoa pole kwa familia na wote walioguswa na ajali mbaya ya basi la Buffalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa taarifa ya Mheshimiwa Fatma Mikidadi, muda uliopita naomba nitoe pole kwa familia ya marehemu Abdillah Namkulala, ambaye aliwahi kuwa Mbunge katika Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ni ya Wizara tatu ni ndefu lakini nitajitahidi kusoma muhtasari wake kwa muda ambao unaotakiwa kwa Kanuni.

Katika Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Kamati ilitekeleza kazi zake kwa kuweka maanani taarifa ya mapitio ya sekta ya afya nchini mwaka 2006 ambayo ilieleza mafanikio yafuatayo katika sekta hii:-

Kwanza, ukarabati wa majengo ya hospitali, vituo vya afya na zahanati umepewa kipaumbele na mipango ya kuimarisha huduma za hospitali za Mikoa na Wilaya inaendelea.

Pili, vituo vya kutolea dawa za kupunguza makali ya UKIMWI zikiwemo hospitali zimefikia 200 na idadi ya wanaopewa dawa imeongezeka kutoka 2,500 mwaka 2003 na kufikia 56,000 kwa mwaka 2006.

Tatu, kiwango cha chanjo zote kwa watoto ni zaidi ya asilimia 90. Pamoja na Wizara kutoa taarifa ya mafanikio hayo, sekta ya afya bado inakabiliwa na matatizo na changamoto zifuatazo:-

Moja, mfumo wa kutolea taarifa na takwimu mbalimbali bado haujatengamaa. Pili, mahusiano baina ya watoa huduma katika Serikali na sekta binafsi *(Public and Private Partnership)* yanahitaji kuimarishwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, bado kuna tatizo la uwajibikaji, usimamizi usioridhisha na kutozingatiwa kwa maadili ya kazi kwa baadhi ya watumishi katika kutoa huduma za afya.

Nne, ugonjwa wa malaria bado unaendelea kuwa chanzo kikuu cha kuugua na vifo kwa watoto na watu wazima na gharama za tiba zinaongezeka sana. Pia umuhimu wa kudhibiti mazalio ya mbu hayapewi uzito unaostahili.

Tano, vifo vya watoto na akinamama wajawazito unaonyesha kupungua, lakini bado vipo juu kwa mfano kutoka vifo 147 kati ya akinamama 1000 hadi 112 kati ya akinamama1000 na watoto wachanga kutoka 99 kwa watoto 1000 hadi 68 kwa watoto 1000 na kiwango cha mama wajawazito pia bado vifo vipo juu ambapo takwimu inaonyesha akinamama 6 hufa katika 1000 au akinamama 578 kati ya 100,000.

Sita, kuna upungufu mkubwa wa wataalamu katika ngazi zote na kwa waliopo ufanisi wao unaonyesha kupungua sana kutokana na ongezeko kubwa la wagonjwa, upungufu wa vitendea kazi na kukosa motisha. Vile vile matumizi na usimamizi wa vyombo vya usafiri na usambazaji bado ni dhaifu.

Saba, bajeti ya sekta ya afya bado haikidhi mahitaji na haijafikia makubaliano ya Azimio la Abuja *(The Abuja Declaration)* inayotaka nchi kutenga asilimia 15 ya Bajeti yake kwa sekta ya afya.

Nane, bado kuna huduma hafifu kwa makundi maalumu yakiwemo watoto yatima, watu wenye ulemavu na wazee wasiojiweza. Tisa, bado azma ya Serikali ya kutoa huduma muhimu za afya zenye uwiano kwa kuzingatia maeneo ya nchi haijapewa kipaumbele. Mfano ni jinsi huduma zinavyotolewa kwa baadhi ya sehemu huduma zipo hadi vijijini na sehemu nyingine zipo ngazi ya Tarafa tu. Hivyo Kamati inashauri Serikali ichukue hatua za makusudi kurebisha matatizo hayo na kuleta ufanisi katika utekelezaji hasa kwa kuhakikisha kuwa kila kijiji au mitaa kuna zahanati na kila Kata kuna Kituo cha Afya.

Kuhusu Idara ya Bohari ya Madawa *(MSD),* Kamati imepata malalamiko mengi kutoka kwa watendaji wa Serikali kuhusu uhafifu katika ubora wa dawa na vifaa vya hospitali vilivyoagizwa na kusambazwa na Idara ya Bohari ya Madawa *(MSD),* Kamati imeshuhudia

matatizo ya mashine za kufulia kutokutumika kwa zaidi ya miezi nane baada ya kufungwa katika hospitali ya Mkoa wa Ruvuma na Seko Toure, Mkoani Mwanza.

Aidha, Kamati ilipata taarifa ya vifaa vya hospitali vya ubora hafifu kukataliwa na hospitali ya Bugando. Kamati vile vile iliona uwezo mdogo wa utendaji wa *MSD* pale ilipogundua kwamba shilingi bilioni 1.2 zililipwa *MSD* na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa ajili ya kununulia dawa na vifaa vya hospitali ya Rufaa ya Bugando zilikuwa hazijatumika wakati hospitali ilikwisha kukabidhi orodha ya mahitaji yake *MSD* na wakati huo huo wagonjwa wanateseka. Serikali inashauriwa kutoa maelezo kuhusu fedha hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na changamoto nyingi za kiutendaji kwa *MSD,* Idara ya Bohari ya Madawa imefanikiwa kujiendesha vyema bila kutegemea ruzuku ya Serikali na imeweza kuuza mtaji wake sambamba na kupanua shughuli zake. Pia shughuli za ujenzi wa maghala ya kisasa zinaendelea. Pia Idara inaendelea na mpango mzuri wa kusambaza dawa kwa njia ya *indent* na *ILS* ambao unazingatia mahitaji halisi ya dawa badala ya utaratibu wa *kits*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali kutoa msukumo maalumu kwa *MSD* ili iweze kukabiliana na changamoto hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu shughuli za Mamlaka ya Chakula na Dawa, *(TFDA)*. Mamlaka ya Chakula na Dawa inafanya kazi nzuri katika kulinda afya za walaji ikiwa ni pamoja na kubaini dawa zisizokidhi, hivi viwango na kuzuia matumizi na kuingizwa vyakula visivyofaa nchini na vipodozi vyenye kemikali hatari. Tunaipongeza Mamlaka ya Chakula na Dawa kwa kazi yao nzuri na kwa kufanya kazi kwa uzalendo. *(Makofi)*

Kuhusu mpango wa *ADO,* Kamati ilitembelea na kushuhudia mafanikio ya mradi wa majaribio wa maduka muhimu Mkoani Ruvuma unaoitwa *Acredited Drugs Dispensing Outlets (ADO)*. Kamati inashauri mradi huu usambazwe nchini kote kutokana na manufaa yake ambayo ni pamojana na wagonjwa kupata dawa kamili yaani dozi vile vile umeongeza ajira kwa watoa dawa. Kuondoa ulanguzi wa kuuza dawa za moto yaani *antibiotics* kwa kificho. Mpango huu mzuri pia unaondoa tatizo la wagonjwa kutopona kutokana na usugu unaotokana na utoaji wa dawa pungufu ya dozi na kwa baadhi ya dawa kuuzwa kwa njia ya kificho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hospitali ya Rufaa ya Bugando, hospitali hii inatoa huduma za rufaa kwa mikoa ya Kagera, Mwanza, Mara, Shinyanga, Tabora na Kigoma. Kamati imeridhika na huduma zinazotolewa na hospitali hii ya rufaa na tunashauri Serikali iendelee kutoa ushirikiano kwa kuongeza bajeti na misaada mingine. Tunaipongeza menejimenti ya hospitali ya Bugando na Baraza la Maaskofu wa Kanisa Katoliki Tanzania kwa kutoa huduma ya afya kwa Watanzania wote kwa uwajibikaji wa hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali ya Bugando pia inakabiliwa na upungufu wa madaktari wa ngazi zote na watumishi wengine. Kamati pia inashauri Idara zote zinazohusika na kuzifanyia uchunguzi maiti yaani *postmoterm* ikiwa ni pamoja na Polisi Mkoani Mwanza wasicheleweshe utekelezaji kwa sababu maiti zinazotokana na ajali ya maji na moto hupelekwa zikiwa zimevimba na hivyo kuhifadhiwa ndani ya majokofu inakuwa tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hospitali ya Mkoa wa Mwanza Sekou Toure, majengo ya hospitali ni mazuri na usafi unaridhisha. Hospitali ina upungufu wa madaktari bingwa na watumishi wa kada nyingine wa hospitali. Kamati yangu inashauri kuangalia kwa undani madai ya watumishi wa hospitali hii ambao wanalalamika kuhusu ufinyu wa bajeti katika kulipa maslahi yao ya posho, *on call allowances* na *extra duty allowances* na nauli za likizo.

Mheshimiwa mwenyekiti, hospitali ya Wilaya ya Geita na Kituo cha Afya Katoro kwa ujumla hospitali hii ni safi. Hata hivyo, Kamati haikuridhika na ujenzi wa baraza yaani *corridor* ambayo umegharimu shilingi milioni 12 na ujenzi wa uzio kuonyesha fedha kulipwa karibu yote kabla ya ujenzi kukamilika. Tumeshauri kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Geita ifanye ukaguzi maalumu hasa kwa ujenzi wa baraza na tunashauri Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kufuatilia suala hili. *(Makofi)*

Kamati inashauri Halmashauri ya Wilaya ya Geita iwasiliane na *TASAF* kuharakisha utoaji wa fedha za kituo cha afya, baada ya wananchi na viongozi kuibua mradi huo na kuchangia nguvu zao. Tunawapongeza wananchi wa Katoro na viongozi wao akiwemo Mheshimiwa Faustine Kabuzi, Mbunge wa Busanda, kwa kuhamasisha wananchi kuchangia nguvu zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu janga la UKIMWI, janga hili ni tatizo kubwa katika jamii kwani ugonjwa huu hauna mipaka kwa namna unavyosambaa. Ni vigumu sana kujua gharama za huduma kwa wagonjwa na mara nyingi imeangukia akinamama. Ni vigumu sana kukisia gharama za vifo na mazishi yanayotokana na UKIMWI kwa familia na Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo yanayotokana na athari za kisaikolojia na unyanyapaa *(stigma)* hayapimiki na gharama za chakula na dawa ni zaidi ya uwezo wa kawaida wa familia na umaskini unazidi kujikita katika familia. UKIMWI sasa umejikita sasa katika kila familia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa UKIMWI hauna mipaka, Kamati inashauri yafuatayo:-

Bunge litumie madaraka iliyopewa na Ibara 96(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuunda Kamati ya Kudumu itakayoshughulikia na kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa mipango ya mapambano ya kudhibiti UKIMWI kama ilivyo kwenye nchi nyingi za *SADC.*

Ushauri huo unatokana na kuzingatia kuwa Tume ya Kudhibiti UKIMWI *(TACAIDS)* ipo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na shughuli za UKIMWI zipo kwenye Wizara zote na ipo Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii haina uwezo wa Kanuni kwa Kanuni za Bunge kufuatilia utekelezaji wa mikakati ya kupambana na UKIMWI katika Wizara zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa zilizowasilishwa kwenye kikao cha *SADC Parliamentary Forum,* Gabon, Botswana, tarehe 21 mpaka 24 Januari kuhusu UKIMWI zimeonyesha mambo makubwa matatu kwa Tanzania.

Kwanza, Tanzania inashauri itumie rasilimali zake kwa nguvu zaidi kutilia mkazo kwenye kuwalinda watu, asilimia 93 wanasadikiwa kuwa hawajaambukizwa virusi vya UKIMWI na wakati huo huo juhudi ziendelee katika kuwajali watu asilimia 7 wanaoishi na virusi vya UKIMWI na wagonjwa kwa kuwapatia huduma muhimu na dawa za kuwapunguzia makali ya UKIMWI.

Pili, taarifa ya utafiti iliyotolewa kwenye mkutano huo huko Gabon, Botswana ilionesha kuwa Tanzania imengia kwenye hatua ya kuwa kwenye maambukizi ya virusi aina ya *highbreds sype HIV one A C D,* wakati nchi nyingine za *SADC* zina *HIV one C* pekee. Tatizo hili limeelezwa kuwa linatokana na mwingiliano wa watu kutoka sehemu mbalimbali katika miji mikubwa ya Tanzania hasa Dar es Salaam na miji ya Kaskazini mwa nchi yetu. Hatari ya aina hii ya virusi ni kutokea kwa usugu kwa dawa hapo baadaye. Wizara inashauri kufuatilia matokeo ya utafiti huu kwa karibu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, mgawo wa Bajeti ya sekta ya afya ni muhimu uwe na mwelekeo wa kutekeleza maazimio ya Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika walipokutana Abuja, yaani *Abuja Declaration,* yanayotaka kila nchi kutenga asilimia 15 ya Bajeti yake kwa sekta ya afya. Kamati inashauri kuwa Serikali ionyeshe mwelekeo huu katika Bajeti ya mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi *(MMEM),* ulilenga kuwapeleka watoto wote wenye umri wa kwenda shule ili wapate elimu bora ya msingi. Kupitia mpango huu taarifa ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi inaonyesha kuwa idadi ya wanafunzi katika shule za msingi iliongezeka kutoka milioni 4.8 na kufikia milioni 7.9 mwaka 2006. Tunaipongeza Serikali na wadau wote waliofanikisha mafanikio haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2007 idadi ya wanafunzi waliosajiliwa daraja la kwanza ni milioni 1.6 na wanatarajiwa kumaliza darasa la saba mwaka ujao. Ni muhimu pia kufahamu kuwa asilimia ya wanaofaulu mtihani wa darasa la saba, inaongezeka kila mwaka, mwaka 2002 ilikuwa asilimia 27.1, mwaka 2006 ilifikia asilimia 70.48 pia wanaochaguliwa kwenda sekondari, ilifikia asilimia 49.3 kwa mwaka 2005 na inaendelea kuongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio haya yanaitaka Serikali na jamii nzima kujitayarisha sasa ili kupokea mafanikio haya.

(1) Tunahitaji kujenga majengo yote muhimu ya madarasa, nyumba za walimu, vyoo, ofisi za utawala na kadhalika kwa kushirikisha wananchi;

(2) Serikali inahitaji kujitayarisha kwa fedha za kuendesha shule, vifaa vya kujifunzia na kufundishia na fedha za matengenezo; na

(3) Tunahitaji kuwa na walimu wenye sifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri kuwa kila nguvu ya Mtanzania itumike katika kupokea mafaniko hayo na wadau wote wajipange sasa kuanzia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Wizara ya Fedha, TAMISEMI, Mipango, Utumishi, Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia, Halmashauri za Wilaya, Taasisi na Mashirika mbalimbali viongozi na wananchi, tunashauri mkakati maalumu uandaliwe kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba sherehe za miaka 45 ya Uhuru zilifana kwa sababu ya uzalendo ulionyeshwa na wadau wote. Vivyo hivyo michezo hasa mpira wa miguu mfano timu ya Taifa sasa inachangiwa kwa uzalendo na zaidi ya wananchi huchangia sana vile vile shughuli zingine kama harusi kwa kiwango kikubwa. Hivyo inawezekana kwenye sekta ya elimu ambayo inahitaji uwekezaji kuliko wakati wowote ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipotembelea Wilaya ya Geita iliona udhaifu mkubwa katika matumizi ya fedha za *MMES* hasa katika shule ya sekondari ya Butundwe ambayo nyumba ya mwalimu iliyokwishajengwa kwa nguvu za wananchi hadi lenta iligharimu shilingi milioni 9 za Serikali kuipaua na sehemu nyingine chache tu. Ni wazi kuwa matumizi mabaya ya fedha za Serikali yalionekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ubadhilifu wa wazi pia ulionekana shule ya sekondari ya Bukori, Nyarugusu, ambapo Kamati ilielezwa kuwa Mkandarasi alilipwa fedha karibu yote ya ujenzi na kutoroka bila kufanya kazi iliyokusudiwa. Huu ni udhaifu wa wazi kwa upande wa watendaji wa Serikali, kwani pamoja na kuelewa tatizo hilo, haukuchukua hatua zinazostahili kwa wizi wa wazi wa fedha za umma, hata hivyo Kamati ilipewa taarifa tu kuwa Taasisi ya Kuzuia Rushwa *(PCB)* ilikuwa imejulishwa kuhusu sakata hilo ambayo Kamati inaona kuwa ni kosa la jinai na lilitakiwa kupelekwa polisi bila kuchelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaitaka Serikali ichukue hatua za kisheria mapema iwezekanavyo. Elimu bora inatokana kwa kiasi kikubwa na mafunzo ya ualimu, walimu ni chimbuko la uzalendo wa Kitaifa na Utaifa. Walimu ni wazalishaji pekee wa nguvu kazi ya Taifa katika nyanja zote za kiuchumi na kijamii. Vile vile ni muhimu kuenzi ujumbe wa mwaka jana wa siku ya mwalimu duniani ambayo hufanyika kila tarehe 5 Oktoba kila mwaka. Ujumbe wa mwaka 2006 ulikuwa kila mwanafunzi anahitaji mwalimu bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia ujumbe huo, Kamati yangu ilitembelea Chuo cha Walimu Butimba, Mwanza ambacho ni kati ya vyuo vikongwe vya Serikali kinachotoa mafunzo ya ualimu hadi ngazi ya *Diploma* katika fani za sayansi na sayansi za jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapongeza sana juhudi za Mkuu wa Chuo hicho na wakufunzi wote kwa kazi yao nzuri ya kutayarisha walimu bora. Hata hivyo, chuo hiki kinatoa elimu bora kwenye mazingira ya uchakavu mkubwa wa miundombinu hasa majengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashauri kuwa Serikali itoe kipaumbele katika kukarabati chuo hiki, sambamba na vinavyofanana na hiki. Kamati baada ya kuongea na wanafunzi na wanachuo inapenda kutumia nafasi kuikumbusha Serikali kuendelea kutoa kipaumbele kwa matatizo yanayowakabili walimu kama vile kutokulimbikiza madai yao, kujenga nyumba za walimu, malipo ya mirathi na pesheni yawekewe mikakati mipya, kupandishwa madaraja kwa walimu kufanyike kwa wakati unaotakiwa, bima za maisha zilizoiva kwa walimu sasa ni kero na walimu ni wadau wakubwa wa elimu, hivyo wao wakishirikishwa katika hatua za awali za kuboresha sera ya elimu mipango na utekelezaji ili kuleta ufanisi na maelewano katika jamii, mfano wakati wa kubadilisha mitaala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa mafunzo kazini upewe umuhimu wa kipekee kwenye bajeti, kazi ya ualimu ni taaluma yaani *profession* na hivyo mafunzo yake yana programu maalumu kwa kila ngazi. Pamoja na mpango wa sasa wa kozi ya muda mfupi ya

kuandaa walimu ili kukidhi mahitaji maalumu ya sasa, Kamati inapongeza mpango wa Wizara wa mkakati kupata walimu wa shule za sekondari unaolenga kuwa na mikakati ya muda wa kati na muda mrefu. Kamati yangu inaunga mkono kuanzishwa kwa mafunzo ya walimu kwa ngazi ya shahada, kupitia Chuo Kikuu Huria cha Tanzania ambapo kwa kuanzia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi inawagharamia walimu wa leseni 1,500 kwa miaka mitatu, kwa shilingi 950,000 kila mwaka kwa kila mwalimu. Tunaupongeza mpango huu ambao utaendelea kulinda dhamira ya Serikali ya kutoa elimu bora kwa walimu waliopata mafunzo ya kutosha na kulinda taaluma ya ualimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashauri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, ipate nafasi maalumu ya kuelezea Bunge lako na wananchi kwa ujumla kuhusu mkakati wa kupata walimu wa shule za sekondari kwa ujumla, ili kujenga uelewa na maelewano ya pamoja katika kuboresha elimu nchini. Hatua hii itasaidia wadau wote kuwa na kauli moja ya kuboresha elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Baraza la Mitihani Tanzania, Kamati ilifanya ziara ya kikazi kwenye chombo hiki nyeti kilichopewa jukumu la kupima na kudhibiti ubora wa elimu utolewao nchini na kukuta kuwa viongozi na watumishi wake wanafanya kazi katika mazingira magumu kwa kukosa nyezo zinazotakiwa ikiwa ni pamoja na vifaa na wataalam wa kutosha. Aidha, Kamati ilibaini kuwa Serikali huchukulia Baraza la Mitihani, sawa na taasisi nyingine za kawaida na hivyo kutolipa uzito unaostahili hasa katika masuala ya Bajeti na hivyo kuwa na upungufu mkubwa wa vitendea kazi na kuathirika kwa ufanisi wa shughuli zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri kuwa chombo hiki ambacho ni nyeti na jicho la Taifa kinachoipatia nchi uhalali wa viwango vya elimu, hivyo kipewe umuhimu unaostahili hasa katika kuboresha vitendea kazi na kukamilisha ujenzi wa kituo cha kusahihisha mitihani ambacho kipo katika hatua za mwisho na kwamba Baraza linadaiwa fedha nyingi na wakandarasi ambao sasa wanataka kulifikisha Baraza la Mitihani kwenye vyombo vya sheria. Kamati inashauri Serikali iingilie tatizo hili haraka iwezekanavyo.

Kuhusu Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia, Kamati yetu ilipata nafasi ya kujielimisha shughuli za Bodi ya Mikopo Elimu ya Juu na Vyuo Vikuu na Taasisi zake. Hata hivyo, kuhusu Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu sheria Na. 9 ya mwaka 2004 ilikuwa na madhumuni ya kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu wanaostahili kutokana na uwezo mdogo wa wazazi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza sheria hiyo Kamati imebaini matatizo yafuatayo baada ya mjadala na bodi ya mikopo:-

(1) Baadhi ya wakopaji wanafunzi wanaona mikopo kuwa sehemu ya misaada yaani gramu au chanzo cha mapato kutoka Serikalini kwa ajili ya masomo yao.

(2) Waombaji wamekuwa wengi zaidi kuzidi uwezo wa bodi ya Bajeti ya Serikali iliyotengwa kwa ajili hiyo.

(3) Uwezo mdogo wa kiutendaji wa bodi na taarifa zisizo sahihi zilizotolewa na wanafunzi umechangia bodi kushindwa kufanya tathimini yaani *means test* wa nani hasa wanahitaji au wanaostahili mkopo na nani wenye uwezo wasiohitaji mikopo.

(4) Taarifa ya bodi inadhihirisha kuwa wanafunzi wanaotoka kwenye familia zenye uwezo vile vile walipewa mikopo na baadhi ya wanafunzi walipewa mikopo mara mbili.

(5) Baadhi ya wafadhili waajiri na wazazi walijitoa kugharamia wanafunzi baada ya bodi hiyo kuanzishwa.

(6) Bodi ililazimika kutoa sehemu tu ya mkopo kutokana na wingi wa waombaji na ufinyu wa bajeti.

(7) Kumekuwa na ucheleweshaji wa utoaji wa mikopo kutokana na uwezo na idadi ndogo ya watumishi.

(8) Wanafunzi kufanya maandamano katika harakati za kuishinikiza Serikali kutoa mkopo kwa asilimia mia moja kukidhi mahitaji yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msimamo wa Serikali kuhusu utoaji wa mikopo kwamba upo katika maeneo matatu:-

(i) Ni kwamba wanaostahili kupewa mikopo ni wale tu waliopata *division one* kwa wavulana na *division one, two* kwa wasichana.

(ii) Wanafunzi wanaosoma kozi zenye programu za kipaumbele kwa Taifa kama vile elimu, afya, kilimo na uhandisi.

(iii) Wanafunzi watachangia asilimia 40 ya gharama za mafunzo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatiwa msimamo huu kumekuwepo na maandamano ya wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu wakipinga kuchangia asilimia 40 ya mafunzo. Pia kumekuwepo na maoni mbalimbali ya wadau wa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu inaushauri ufuatao:-

(1) Serikali ilete marekebisho ya sheria Na. 9 ya mwaka 2004 ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ambayo yatazingatia hoja zilizoainishwa na Kamati na kuzingatia maoni ya wadau ya elimu.

(2) Serikali iweke mkakati mpya na wa kipekee wa kupata fedha zaidi kuweza kwenye sekta ya elimu, tunaishauri Serikali kuwa kipaumbele chake kwanza iwe elimu, kipaumbele cha pili iwe elimu na kipaumbele chake cha tatu iwe elimu na kwa sababu zingine zote zitawezeshwa na elimu, vipaumbele vingine vifuate. Kwa rasilimali tulizonazo inawezekana, tuamue sasa.

(3) Kwa kuwa kumekuwepo maoni tofauti kuhusu msimamo wa Serikali, Kamati inashauri Serikali ifanye utafiti wa kina kwa takwimu na kupata maoni ya wananchi kwenye maeneo manne yafuatayo:-

(i) Kwamba watoto wengi ambao wazazi wao hawana uwezo wanaosoma kwenye shule za kawaida ambapo kuna miundombinu duni ikiwa ni pamoja na walimu kuwa wachache, kutokuwepo maabara, vitabu, samani na kadhalika. Wanafunzi wanaoandaliwa

katika mazingira hayo si rahisi kufaulu mtihani katika daraja la kwanza na la pili na kwamba wale wanaofaulu ni wachache sana na hao watakuwa wale wenye vipaji maalumu. Wadau wanadai kuwa utaratibu huu unawaondoa moja kwa moja katika kupata mikopo.

(ii) Kwamba mwelekeo wa Serikali kutoa mikopo kwa waliopata *division one* na *two* utawafanya wanafunzi kuacha masomo ambayo kwa kawaida ni vigumu kupata *division one* na *two* na hivyo hali hii itawafanya wakimbilie masomo mengine kama ya sanaa. Hali hii itapelekea tatizo la uwiano wa wataalamu katika maendeleo ya nchi na sekta ya sayansi na teknolojia itaathirika zaidi.

(iii) Yapo madai vile vile ya wadau kwamba athari ya kuchanganya vigezo vya umaskini na vya kufaulu ni kuleta tabaka na madaraja katika jamii kwa maelezo kuwa wananchi wengi maskini wapo vijijini na wenye uwezo wa kupeleka kwenye shule nzuri zenye vifaa na walimu wazuri wako mijini ambapo pia mazingira ni mazuri zaidi kumsaidia mtoto. Hali hii itawagawanya wazazi waanze kutafuta shule nzuri zaidi popote ili hatimaye watoto wao wapate division one na two ili kuwawezesha kupata mikopo.

(iv) Ushauri wa wadau ni kwamba ni vema Serikali itafute motisha nyingine kwa wanafunzi watakaofanya vizuri sana katika masomo yao. Kamati inaona ni vema maoni ya wadau yafanyiwe utafiti wa kina kwa takwimu za tosha ili kuepuka hali ya kutoelewana katika jamii tuzingatia tofauti iliyowahi kutokea, kati ya maamuzi ya Serikali na maoni ya wadau, pale Serikali ipofuta baadhi ya masomo na Serikali baadaye kukubaliana na maoni ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu taarifa za Mamlaka ya Elimu Tanzania, Kamati ya Huduma za Jamii imekuwa ikishauri Serikali na sasa kwa mara ya tatu kuchangia kiasi kisichopungua asilimia mbili ya Pato la Taifa baada ya kutoa gharama za Madeni ya Taifa. Asilimia ya Bajeti inayotengwa kila mwaka imekuwa inashuka kila mwaka kutoka asilimia 0.45 mwaka 2001/2002 hadi asilimia 0.17 mwaka 2006/2007. Kamati inapenda Bunge ielezwe kama kweli dhamira ya Serikali ya kuimarisha mfuko wa kuweza kwenye elimu na hatua gani inachukua kuondoa tatizo hili. Vile vile Kamati inapenda kufahamu sasa kama Serikali itazingatia ushauri huu au hapana, taarifa za utendaji wa hesabu taasisi na mashirika ya umma, tumeweka kwenye taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Spika, kwa kututeua sisi wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Huduma za Jamii, mwezi Januari, 2006 kwa mujibu wa Kanuni ya 87(4) ya Kanuni za Bunge na naomba niwatambue wajumbea hao ambao ni Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mheshimiwa Dr. Ali Taarab, Mheshimiwa Nuru Bafadhili, Mheshimiwa Prof. Feethman Banyikwa, Mheshimiwa Husnain Dewji, Mheshimiwa Mercy Emmanuel, Mheshimiwa Ali Juma Haji, Mheshimiwa Phares Kabuye,Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed, Mheshimiwa Janet Kahama, Mheshimiwa Mariam Kasembe, Mheshimiwa Sameer Lotto, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Benito Malangalila, Mheshimiwa Margreth Mkanga, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Prof. Idris Mtulia, Mheshimiwa Omar Mzee, Mheshimiwa Hadija Saleh Ngozi, Mheshimiwa Sijapata Nkayamba, Mheshimiwa Ussi Ame Pandu, Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, Mheshimiwa Mwanahamisi Said na Mheshimiwa Fatuma Abdallah Tamim. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru kwa niaba ya Kamati, Mawaziri na Naibu Mawaziri wa Wizara tatu zinazohusika na huduma za jamii na pamoja na watendaji wote wakiongozwa na Makatibu Wakuu jinsi walivyoshirikiana na Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho namshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Damian S. L. Foka na ofisi yake kwa kutuhudumia vyema kipindi chote Kamati ilipokuwa kazini. Nawapongeza Makatibu wa Kamati Ndugu Theonest Ruhilabake na Ndugu Lina Kitosi, kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi taarifa hii kutoka.Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba utoe hoja ili kuweka rikodi zetu sawasawa kwa sababu ulichowasilisha mbele ni hoja na si kuwasilisha.

**MHE. OMAR S. KWAANGW' - MWENYEKITI YA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilianza kwa kutoa hoja.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Hapana unamalizia pia.

**MHE. OMAR S. KWAANGW' - MWENYEKITI YA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi angalau nimekuwa mchangiaji wa kwanza katika hoja hii ambayo imewasilishwa na Kamati mbele yetu. Awali ya yote napenda nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii kwa taarifa nzuri ambayo imeweka picha halisi ya hali ilivyo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati, nilikuwa na mambo mawili tu ambayo nilikuwa nataka nichangie katika hoja hii. Awali ya yote, wakati tukichangia hotuba nzuri ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mara baada ya kulihutubia Bunge, Tarehe 30 Desemba, 2005 mimi nilikuwa na hofu na nikasema maneno yafuatayo:-

"Hotuba nzuri ilikuwa ikionyesha dira na mweleko na matumaini ya Watanzania, je, ilikuwa ni dhamira ya Mheshimiwa Rais peke yake au ilikuwa ni dhamira ya chama na Serikali."

Mheshimiwa Rais alisema maneno mazuri sana na bahati nzuri imewekwa ndani ya kitabu. Sasa sina uhakika kama kitabu hiki tunakitumia kama rejea, tunaomba ruhusa yako ni rejee kifungu kidogo katika hotuba ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Rais katika maneno mengi mazuri ya hekima na ya busara ambayo yalikuwa yanaliekeza Taifa na wapi tunakwenda alisema maneno yafuatayo nanukuu; "nitataka watakaokuwa kwenye Serikali ya awamu ya nne, wajijengee tabia ya mara kwa mara wao wenyewe kujiuliza iwapo kwa maamuzi yao, kwa vitendo vyao na kwa tabia zao, wanajenga au wanabomoa heshima ya Serikali machoni pa Serikali pa wananchi." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha sana kwamba viongozi wengi wa Serikali ya awamu ya nne wamekuwa kwa wakati fulani wanashindwa kuyasimamia ipasavyo maelekezo ya Mheshimiwa Rais. Kwa mara nyingi Rais amesema kwamba watoto hawa watafukuzwa chuoni, haya ni maneno ya Mheshimiwa Rais na mara ya mwisho kama kumbukumbu zangu zipo sahihi aliyazungumza pale *Diamond Jubilee* wakati wa sherehe za kutimiza miaka 30 ya Chama cha Mapinduzi. Aliwahakikishia watoto wetu kwamba kila mtoto wa Kitanzania atasoma na wakati Mheshimiwa Rais anasema haya ilikuwa tayari kumekuwa na vurugu za wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu kuhusu kuchangia asilimia 40 ni ukweli usiopingika, jamii kubwa ya Tanzania ni maskini, uwezo wao mdogo na ndiyo maana Mheshimiwa Rais katika hotuba hiyo hiyo alisema ukurasa wa 10 wa kitabu chake anasema mwalimu alirithishwa nchi ya watu maskini, wanaoteseka kwa maradhi na wasio na elimu ya kutosha, kuongoza nchi na kuendesha uchumi wa kisasa, yeye na baadaye wakishirikiana na mzee Karume wakatoa kipaumbele kwenye vita dhidi ujinga, umaskini na maradhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtandao mkubwa wa huduma za jamii hasa elimu na afya tunaojivunia leo una mizizi yake katika falsafa ya maendeleo ya Baba wa Taifa, wengi wetu nao tulionao humu ndani wa makamu yangu, tusingesoma na kufikia hapa tulipo kama si kuona mbali kwa sera nzuri za Baba wa Taifa, tunashukuru yeye na mzee Karume daima." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ndiyo ilikuwa sera nzuri ya muasisi wa Taifa hili hayati Baba wa Taifa iliyowawezesha viongozi wengi kama alivyosema Mheshimiwa Rais waliomo humu ndani leo, kupata elimu kutokana na sera nzuri ya hayati Baba wa Taifa. Sasa inashangaza, ni kwa nini tunashindwa kuiendeleza sera nzuri ya Hayati Baba wa Taifa, kuhakikisha kwamba kizazi chetu nacho kinapata elimu, kwa sababu Mheshimiwa Rais tena alisema maneno yafuatayo, naomba kunukuu kwa ruhusa yako, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri Muungano alisema maneno yafuatayo; "hakuna Taifa lililopata maendeleo bila kuendeleza elimu, hivyo huendeleza elimu nchini itakuwa *agenda* muhimu ya Serikali ya awamu ya nne." Mwisho wa kunukuu.

Elimu ndiyo *agenda* kuu, Serikali hii ya awamu ya nne, lakini kwa namna gani wanalisimamia tatizo hili la migomo ya wanafunzi katika vyuo vikuu, inachafua heshima nzuri jitihada zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya nne machoni mwa wananchi. Mimi nilikuwa nafikiri kwamba ni vyema kwamba Serikali ikachukua maamuzi ya dhati kuangalia kwamba tatizo hili wanalimaliza, katika taratibu ambazo zitawafanya watoto hawa waendelee kusoma na baadaye kulitumikia Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika kwa mfano sasa hivi tuna upungufu mkubwa sana wa walimu pamoja na jitihada nzuri zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Nne katika kulikabili tatizo hili ikaamua baadhi ya vyuo kuvipandisha daraja na kuwa sehemu ya Chuo Kikuu Mkwawa na Chang'ombe kwa ajili ya kufundisha walimu leo vimefungwa. Taifa lina tatizo la walimu, sijui sasa tunakwenda wapi, wananchi wamehamasishwa wamejenga shule, shule zimetapakaa nchi nzima, uhaba wa walimu unafahamika, tumeamua kwa makusudi kabisa kuongeza idadi, leo tunawafukuza walimu vyuoni, tunakwenda wapi? *(Makofi)*

Katika eneo hili nafikiri ni lazima tulitazame, yanawezekana ni upungufu wa watendaji tu wanafanya maamuzi ya pupa na haraka, bila kutafakari, sasa umefika wakati Serikali ambayo inaongozwa na Mheshimiwa Edward Lowassa, Waziri Mkuu, tunakuomba Mheshimiwa liingilie kati tatizo hili la wanafunzi na hususan walimu. Miongoni mwa hao

Watanzania ambao wako katika vyuo vya ualimu wengi wao ni maskini, wanatakiwa wachangie ada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kibaya zaidi sasa hivi walikuwa wanakwenda katika kipindi cha majaribio kazini, walikuwa wanapewa *allowance* ya shilingi 6,000 pamoja na kwamba shilingi 6,000 haitoshelezi lakini angalau kwa kiwango hicho wangeweza. Sasa wanapewa shilingi 3,600, mtoto ametoka Kapala, Msenga kule Mpanda, anasoma Iringa, anaondolewa Iringa anapelekwa Handeni, Tanga kwenda kufanya majaribio, unampa shilingi 3,600, Mheshimiwa Waziri Mkuu hawa ni watoto wetu, Serikali ijukusanye kuhakikisha kwamba walimu wasibugudhiwe, wamalize mafunzo yao ili waje watusaidie katika hili tatizo la ukosefu wa walimu katika shule zetu za sekondari, hilo lilikuwa ombi langu kwa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu muda wenyewe umekuwa ni mdogo sana nilikuwa na mengi ya kuzungumza lakini niruke haraka haraka nizungumzie kidogo kipengele cha afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika afya tuna tatizo kubwa la idadi ya vifo kutokana na malaria, watoto chini ya umri wa miaka mitano, akinamama wajawazito na watu wazima wanaume kwa wanawake mamia kwa maelefu wanakufa kutokana na malaria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba sasa Serikali ilitazeme ili waweze kufanya mkakati madhubuti kwa kuweza kupambana na malaria ipasavyo. Kama Zanzibar wamefanikiwa kwa kiasi walichofanikiwa kutokomeza malaria nafikiri hata Tanzania Bara tunaweza. Ni kiasi cha kufanya maamuzi tu ni namna gani tunaanza sasa katika kupambana na tatizo la malaria kwa ajili ya kupunguza idadi ya vifo ambavyo vinaweza kuepukika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho nilikuwa naiomba Serikali ianze kuchukua tahadhari hasa baada ya sera nzuri ya kutaka kupanua wigo wa huduma ya afya, ni jambo jema mimi binafsi naliunga mkono na tutalisimamia kuhakikisha kwamba linatekelezeka kila Kijiji kuwa na zahanati na kila Kata kuwa na Kituo cha Afya ni wazo zuri na naliunga mkono kwa asilimia mia moja. Hofu yangu na tahadhari ambayo nataka kuitoa Serikalini ni kwamba bado tuna upungufu mkubwa katika eneo hili na Idara ya Afya kwa wataalamu waandaliwe tusipate matatizo kama katika elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ni kengele ya pili ninakushukuru, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi jioni hii na mimi nichangie katika taarifa yetu ya Kamati ya Huduma za Jamii. Kwanza niseme kwamba taarifa hii ni nzuri, imeandaliwa kitaalamu, ninakupongeza Mwenyekiti pamoja na Wajumbe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitazungumzia mambo mawili ili nisichukue muda mrefu, nitazungumzia hasa upande wa sekta ya elimu na nitazungumzia kuhusu ujenzi wa *hostel* pamoja na usafiri kwa wanafunzi hasa wa kike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa naomba sana Serikali kwamba sasa hivi tunajenga sekondari nyingi lakini sekondari hizi zinajumuisha pamoja na watoto wa kike. Tatizo tulilonalo sasa ambalo kama hatutalichukua mapema ni kwamba ukiangalia idadi kubwa ya wanafunzi wa kike wanaoingia *form one, form two, form three* na *form four* ukichukua miaka minne ijayo idadi ya wanafunzi wa kike kama waliingia 50 *form one* nina mashaka kama wanaweza kumaliza kidato cha nne wakiwa na idadi hiyo ya 50 kwa sababu ya mazingira ambayo tunajua wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni tofauti na enzi zenu, dada yangu Mheshimiwa Jenista Mhagama na Mheshimiwa Margaret Sitta na Waheshimiwa wengine ambao wamo humu ndani akinamama, enzi zile kulikuwa hakuna usumbufu kwa vijana wa kiume, lakini leo kufuatana na mazingira yaliyopo wanafunzi wengi wa kike kama hatutachukua sababu za makusudi za kuwajengea *hostel* hawa watoto wa kike nina uhakika kazi itakuwa ni bure, watakaokuwa wanamaliza kidato cha nne wengi watakuwa ni wanaume au wavulana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kupitia kwa Waziri Mkuu, moto uliouwasha wa ujenzi wa sekondari na najua ukiamua huwa unaamua kweli kweli. Naomba uwashe moto ikiwezekana kwa kuanzia najua kazi ya ujenzi haiishi siku moja angalau kila tarafa iwe na *hostel* moja moja kama siyo mbili kwa ajili ya watoto wa kike, tukifanya hivyo tutakuwa tunasaidia wasichana hawa wanaosoma kidato cha kwanza hadi cha nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili napata taabu kweli kweli inawezekana tatizo hili labda tunaliona kama ni dogo kwa sisi viongozi ambao tuna magari yetu tuna watoto wetu wanasoma Dar es Salaam, wanasoma Arusha, wanasoma Mwanza tunawachukua kwenye magari yetu tunawapeleka shuleni. Lakini wapo watoto ambao wazazi wao hawana magari, tunataka watoto hao waondoke saa moja na ikiwezekana saa moja na nusu wawe wameshafika darasani. Ukienda Dar es Salaam, ukienda Arusha, ukienda Mwanza watoto wanapata taabu kweli kweli kuhusu usafiri wa kwenda shuleni hasa watoto wa kike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri nyie ni wazoefu na huwa tunawaona hawa watoto hivi kweli hakuna ufumbuzi? Hivi kweli hawa watoto wetu tunaotaka wasome vizuri hakuna ufumbuzi kweli wa kuweza kuwasaidia hawa watoto usafiri wenye uhakika? Wenzetu huwa mnasafiri na kwenda nchi za mbali na mnaona hivi wenzetu wanafanyaje? Tunafurahia hawa watoto tunapowaona saa moja, saa mbili, saa tatu wapo kwenye kituo saa nne asubuhi anaenda shuleni. Hivi Serikali haioni?

Je, tunawasaidiaje hawa watoto ili waende shuleni wafike mapema wakasoma? Siyo waishie kwenye vituo vya mabasi, wakiendelea kukaa kwenye vituo vya mabasi ni mawili kama ni mtoto wa kike atafanya anavyoweza kufanya na mtoto wa kiume atatoka hapo, ataenda kuvuta bangi, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali hebu tujipange vizuri tulione hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unaweza kusema jamani naagiza Mkoa wa Dar es Salaam sasa tatizo la kipindupindu likome, uliwasha moto huo ukasafiri na uliporudi sikusikia kipindupindu mpaka leo Dar es Salaam. Mheshimiwa Waziri Mkuu, ni aibu vijana wetu, wajengee shule nyingi Mikoani na wakati watoto wetu hawawezi kufika shuleni kwa wakati muafaka hasa kwa sehemu za mijini Dar es Salaam, Arusha na Mwanza naomba sana Serikali ilifuatilia hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu sekta ya afya, sekta ya afya hivi sasa ukienda kwenye Majimbo ukahutubia wananchi watakuuliza Mheshimiwa Mbunge katika zahanati fulani, katika Kituo cha Afya fulani hakuna dawa ya kutosha, ukienda Wilayani ukakutana na Mganga Mkuu atakuambia Mheshimiwa tatizo liko Dar es Salaam, Bohari ya Dawa. Pale Bohari ya Dawa kuna matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hili kila mtu anajua, mtu anapoenda hospitali anaumwa, anatakiwa afike kwa Mganga, atibiwe na apewe dawa siyo apewe karatasi. Mwananchi wa kijijini kule Kadachi, Baligisu, Ng'aya, Magu, Fimba na Mvomero atazipata wapi dawa? Kama ni bohari ya dawa imeshindwa kufanya kazi yake vizuri, kama waliopo wameshindwa kufanya kazi, tunashindwa kuwaondoa, hivi utaratibu wa Serikali ni kukaa na mtu mmoja tu, kwa sababu unapougua unatakiwa kupata tiba. Sasa kama tiba haitolewi ikiwa pamoja na dawa na wenzetu bahati nzuri Kamati ya Mheshimiwa Omar Kwaangw', imetembea na imeona, imeenda bohari ya dawa na tatizo la kusambaza lipo. Lakini Wizara imekaa kimya na watu wanaosababisha hayo tunawajua. Naomba Serikali tufanye kazi ya kuzima moto na wala tusiwe na kipingamizi kuhusu suala la dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni kuhusu maduka ya dawa. Dawa ni sumu, lakini kwetu Tanzania tunaachia tu kama vile unaweza kwenda kununua njugu, ukanunua mayai, ukanunua maembe bila kujali unaenda dukani unasema naomba dawa fulani na unapewa bila hata *prescription* mimi sijaona, lakini Tanzania hiyo ipo, nimesema dawa ni sumu na hatuwezi kujua haya dawa tunayoenda kuchukua bila kushauriwa na daktari inawezekana ndio inayotufikisha hapa.

Naomba Serikali isiwe na kigugumizi kwenye suala hili la dawa, kama duka fulani limeagizwa liuze dawa fulani basi iuze hizo dawa na ili mtu huyu apewe dawa fulani lazima kuwe na *prescription* inayotoka kwa daktari anayejulikana na mhuri wake uwe pale kwamba huyu daktari ndio aliyethibitisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yangu yalikuwa ni hayo lakini naomba sana suala la wanafunzi kuhusu usafiri lipewe kipaumbele, suala la wanafunzi wa sekondari, wanafunzi wa *hostel* lipewe kipaumbele.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. HASNAIN G. DEWJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi katika kuchangia hoja iliopo mbele yetu ya Huduma za Jamii nikiwa mmojawapo wa wajumbe katika Kamati ya Huduma za Jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka niongee kuhusu elimu, nimeona nianze na elimu halafu nitamalizia na afya. Elimu tunaendelea vizuri, elimu ya msingi tunayo na tunaendelea nayo vizuri, elimu ya sekondari inaboreshwa, tuna shule nyingi sana na sasa hivi takwimu zinasema tuna madarasa zaidi ya 1,000 nchi nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tatizo litakuja baada ya kipindi cha miaka minne au mitano ijayo tutakukwa na *drop out* wanafunzi wa sekondari pa kwenda, wazazi watapata matatizo kuwapeleka wanafunzi hao sehemu nyingine, asilimia 70 watazagaa mitaani, asilimia 30 tu watakuwa na uwezo wa kwenda *high school* na Chuo Kikuu tulione hili, Wizara ilione hili, Serikali ilione hili, mimi mapendekezo yangu baada ya sekondari ni nini? Nasema shule ya ufundi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufundi stadi ndio utakaookoa wanafunzi wetu, vijana wetu ili wasiende kwenye tabia mbaya, tutampunguzia mzigo mzazi katika hili. Mimi Wilayani kwangu Kilwa kuna majengo mazuri ya miundombinu, kambi nzuri za Wachina zimekaa tu leo miaka miwili Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu anasikia hapo, nataka niombe ile kambi ifanywe shule ya ufundi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu tutafuata ili tuweze kupata shule ya ufundi na ninaishauri Serikali baada ya sekondari tuwe na mkazo ili tupate shule nyingi za ufundi, wapigakura wangu wengi wanakuja wanaiambia Mheshimiwa tuombee kazi kwa Mkurugenzi akiulizwa taaluma gani, ana elimu ya sekondari hajasoma udereva, hajawa na fani mbalimbali wanazagaa tu pale Jimboni hawana kazi na tatizo kubwa wanakuja wageni ambao wanapata kazi na wenyeji hatuna ajira, kwa hiyo, nimeona niseme hili la sekondari kwamba baadhi ya sekondari tuwe na ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuongea habari za elimu nataka nichangie kuhusu *MSD,* nchi hii hatuwezi tukawa na *exclusive right* ya kumpa mamlaka *MSD* peke yake, ningeshauri tungehusisha *private sector* ili maboharia wawe *supplier* wa kwenye *districts, regions* tuna matatizo makubwa sana ya dawa kama alivyoongea Mbunge mwenzangu. Mimi nimeenda kuomba kura jimboni kwangu kuna sehemu inaitwa Limariao, mpigakura wangu ananionyesha *panadol* nne ametoka nazo zahanati, *pain killer* nne anazo ananiambia mtarajiwa kweli mimi nitapona kwa *pain killer* hizi nne? Nikiulizwa *kit* iliyoleta ni kwamba imeleta *panadol* 1,000 tu. Tunayo matatizo *MSD* makubwa kwa kuwa niko kwenye Kamati ninayajua tulienda Songea tumeuziwa mashine za ajabu mpaka leo hazifanyi kazi, tumeenda hospitali ya Bugando, Mwanza wameandika *cheque* ya mabilioni, *supply* ya dawa haijafanyika mpaka leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hatutakuwa na changamoto au ushindani, nchi hii ni kubwa sana, inahitaji dawa sehemu zote haswa mikoa yetu iliyokuwa pembezoni dawa ndio hayafiki, barabara zetu ni mbovu kwa hiyo, tunapata matatizo ya dawa. Nimeona bora Serikali iangalie hili la kuwa na changamoto, kuwa na *supplier* wengine ambao wenye uwezo wa ku-*supply* dawa ili tutokane na matatizo ya dawa, wataalamu wapo, *prescription* zinaandikwa lakini dawa hakuna. Tatizo hili kama tutakuwa na changamoto au tutakuwa na mshindani mwingine tunaweza kupata dawa za *band name* kwa bei ile ile, tuko kwenye soko huria tunaweza kupata dawa rahisi kuliko yale ya *MSD* ili wagonjwa waweze kupona na kupata nafuu haraka, *panadol* nne hazimponyeshi mtu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali yetu tujaribu kuwa na *supply* kama watatu na *MSD* iwepo, sisemi kama *MSD* haifanyi kazi vizuri, inajitahidi kufanya kazi vizuri lakini iko peke yake tuna watu 32,000,000 wanaotegemea dawa, 36 ni *total population* lakini wenye uwezo wa kwenda *private* labda ni 2,000,000 kwa hiyo, hili tulione tusiilaumu *MSD* kila wakati tukisema *MSD* haiwezi kutosheleza kwa watu 32,000,000. Mimi ushauri wangu kwa Serikali ni kwamba tusiwe na *exclusive supplier,* litatuumiza sana na tuliangalie hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, nashukuru kwa kunipa nafasi hii, ninaona Serikali imenisikiliza na italifanyia kazi jambo hili. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema tunajaribu kuona namna gani tunaweza kuendana na muda tuliobakia nao wa siku ya leo na kesho, baada ya kuisikiliza taarifa yenyewe ya Kamati kama ilivyo na hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maneno na kwa maandishi na ninaamini wengi pia wangependa kuchangia zaidi, nafikiri tukubaliane kwamba kwa kuwa tunaelekea katika kipindi cha bajeti basi tutapata muda wa ziada wa kuweza kuishauri zaidi Wizara hiyo na tunaamini kabisa kwamba Kamati itaendelea kufanya kazi zake wakati wa mijadala mbalimbali ndani ya Kamati. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kimsingi hoja hii ni ya Mwenyekiti wa Kamati kwa niaba ya Kamati yake lakini kadri ya utaratibu wetu wa Kanuni na utendaji wetu wa kazi masuala mengi tunayoyajadili na kushauri Serikali yanatakiwa yafike kwenye mikono ya Serikali na Serikali itusaidie kutoa ufafanuzi.

Waheshimiwa Wabunge, kabla mtoa hoja hajaja kuhitimisha hoja yake ningeomba nitoe nafasi kwa Serikali hata kama ni kwa muda mfupi angalau Mawaziri wanaohusika na hoja hiyo waweze kutuambia maneno machache ambayo yamejitokeza katika mjadala wetu wa leo na katika taarifa yetu. Nitaanza kumpa nafasi Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Mheshimiwa Margaret Sitta, halafu baada ya hapa tutafuatiwa na Naibu Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. WILSON M. MASILINGI:** Mheshimiwa mwenyekiti, kabla ya kutoa mchango wangu napenda kutoa salaam za rambirambi kwa Mheshimiwa Profesa Peter Msolla, Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia kwa kufiwa na mdogo wake, Mheshimiaw Harith Mwapachu, Waziri wa Usalama wa Raia kwa kufiwa na mama yake, familia ya Mbunge wa zamani, Marehemu Abdillah Namkulala, ambaye tumearifiwa kwamba amefariki leo na familia za Marehemu waliofariki katika basi la Buffalo huko Kilimanjaro. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Muleba Kusini, nami binafsi naomba Mwenyezi Mungu, azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, *Amin!*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mwenyekiti mwasilishaji wa hoja na Kamati nzima ya Huduma za Jamii kwa ushauri mzuri kwa Serikali baada ya uchambuzi wa kina katika sekta ya huduma za jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Kamati ya Huduma za Jamii kwamba kwa kupendelea vijana wenye *division I* na *II* katika kutoa mikopo ni kuwabagua watoto wetu wenye sifa kwa mujibu wa masharti ya kujiunga na Chuo Kikuu. Serikali iongeze juhudi za kujenga uwezo kiuchumi ili tusomeshe watoto wetu wote bila kubagua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Huduma za Jamii kwa kazi nzuri wanayoifanya yeye pamoja na Wajumbe wote wa Kamati nzima kwa maelekezo, ushauri na mambo mengi ambayo yamekuwa msaada kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, katika utendaji wake wa kazi wa kila siku, nashukuru sana Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge waliochangia mchana huu kwa kuzungumzia masuala muhimu ya *hostel,* usafiri kwa wanafunzi na

umuhimu wa Vyuo vya Ufundi. Samahani sitasema yote kwa sababu muda tuliopewa na mfupi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepokea ushauri wote uliotolewa ndani ya taarifa ya Kamati, kwa mfano, la kwanza amezungumzia juu ya mafanikio makubwa ya *MMEM* kweli mafanikio ni makubwa na mimi nataka kusema kwamba tutunze haya mafanikio tuliyoyapata kwa kutoa wito ufuatao, kwanza tuzitunze shule za msingi, mkazo tumeweka katika shule za sekondari lakini badi shule za msingi tuupe umuhimu wa pekee na ninatoa wito kwenu kutokuzibadilisha shule za msingi kwa shule za sekondari na pia kuomba kwamba shule za msingi zisihamishwe kupelekwa mahali pengine ili kupisha shule za sekondari. Bado tunahitaji shule za msingi na wakati huo huo tunaomba sana kuwasaidia wanafunzi wetu wapate madawati ili wasikae chini kama tulivyoona juzi kwenye picha mojawapo kwenye magazeti. Shule za msingi bado tunazihitaji na tunatakiwa tufikie asilimia mia ya wanafunzi wanaoingia darasa la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mafanikio ya *MMES,* mimi kwa niaba ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, natoa pongezi kubwa sana kwa wananchi wote na Serikali kwa jinsi ambavyo tumeshughulikia ujenzi wa shule za sekondari ikionyesha wazi kwamba palipo na nia pana njia, wananchi wakiamua lolote linawezekana. Kuanzia Januari mpaka sasa hivi shule 994 tayari zimeshaandikishwa hadi kufikia mwisho wa mwaka zaidi shule1,000 zitakuwa zimeandikishwa. *(Makofi)*

Naomba nitoe ushauri ufuatao wa shule za msingi na shule za sekondari kama tulivyoshauriwa na Kamati ya Huduma za Jamii, kwamba tujiandae kupokea mafanikio haya na kupokea mafanikio haya na kupokea mafanikio haya ni kuendelea na kujenga shule kila siku bila kupunguza kasi na nilitaka kusema tu kwamba jinsi wananchi walivyoitikia wito wa Serikali kwa kuchangia kwa hali na mali ni *document* ya *SADP* yaani ya Mpango wa Maendeleo ya Sekondari, umeshapitwa na wakati sasa hivi Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, inaandaa andiko jipya kabisa ambalo linaangalia kwa undani upanuzi wa shule *A-level*, Vyuo vya Walimu ili tupate walimu zaidi lakini pia inaangalia upanuzi wa Vyuo vya Ufundi ili iweze kukabiliana na ongezeko la wanafunzi wanaomaliza shule za msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia mpango wa kuzitumia fedha za *MMES* kuzituma Mikoani na Wilayani, hata namna ya kuzitunza mpango mzima au utaratibu mzima unaangaliwa upya ili kupunguza wizi na matumizi mabaya. Kwa upande wa kuongeza madarasa mimi ningependa nitoe picha kwa haraka kwamba mwaka 2008 tunategemea walimu zaidi ya 1,200,000 na mwaka 2009 vile vile tunategemea zaidi ya wanafunzi 1,200,000 na mwaka 2010 ndio tutakuwa na wanafunzi 1,319,478.

Wito wangu kwenu nyie Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla ni kwamba tuangalie wanafunzi wetu kwenye mikoa yetu walioko darasa la tano, darasa la sita na darasa la saba ili tuanze kupanga madarasa watakayohitaji watakapomaliza darasa la saba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuhusu uzingatiaji wa viwango, shule ni zetu kwa ajili ya watoto wetu au wanafunzi wetu, kwa hiyo, tuangalie sana viwango na pia tuwe na ramani, ramani zitatusaidia kuchagua mahali palipokaa vizuri na tuhusishe pia ufundi na ningewasihi sana wakati wa kuamua shule tusiamua kisiasa, tufuate ufundi ni wapi shule inaweza kukaa

vizuri kuna wengine wameshajenga shule wamejikuta wakati wa masika wanafunzi hawawezi kufika au mahali ambapo hakuna barabara wala hakuna maji wala huduma za afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wakati wa uamuzi wa mahali pa kujenga shule, naomba hilo suala lizingatiwe sana ili tuweke mahali ambapo itanufaisha watu wengi lakini bila kusahau pia tukijenga mbali na kule wanafunzi wanakotoka maana yake ni kwamba kama alivyozungumzia Mheshimiwa Richard Ndassa tutahitaji *hostel* kwa hiyo, tuangalie sana maamuzi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika katika ujenzi wa vyoo, tunapoanza vyumba vya madarasa pale pale tuanze kujenga vyoo, tusingoje mpaka shule iishe ndio tuanze kujenga vyoo, vyoo ni suala la msingi sana. Lingine ambalo nilitaka kuzungumzia ni kuhusu suala la walimu, tunajua Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi inajua kwamba lazima tuwe na mipango ya walimu, kwa mfano, mwaka huu tulikuwa tunahitaji walimu 9,671 mpaka kufikia mwezi huu tayari tumeshapata walimu 6,588 bado tunahitaji kupata walimu 3,500 ambao tutawapata mwezi Mei. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kikubwa hapa ni jinsi gani ambavyo tunaendelea kuimarisha hawa walimu, katika bajeti yetu jambo mojawapo ambalo limetiliwa umuhimu ni mafunzo kazini ambayo tutawaimarisha hawa vijana wetu, kwa hiyo, ushauri wa kuwaimarisha pia tumeuchukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ila ombi langu kwenu Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla walimu wanahitaji nyumba, tunaomba tunapojenga vyumba vya madarasa au shule kwa ujumla nyumba za walimu tusiache nyuma, nyumba za walimu ndio zinazosababisha walimu kukaa mahali pa kazi lakini wakati huo huo pia tuweke maandalizi ya mapokezi. Vijana wetu wanatoka mbali na shule tunazojenga kwenye Kata ziko mbali, tuangalie nyumba lakini na hata jinsi ambavyo tutakavyowapokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nilitaka kulizungumzia ni ajira ya walimu, Kamati ya Kudumu ya Huduma za Jamii imezungumzia pia suala la ajira ya walimu kwamba wana kero nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi sasa hivi inalifanyia kazi suala la kuangalia ajira nzima ya walimu, tumeshafanya vikao vingi vinavyoshirikisha wadau na juzi tu kikundi cha maafisa nane wametoka Kenya kuangalia wenzetu wanavyohudumia walimu, kwa hiyo, tunaamini kabisa kwamba tukishamalizia kuweka utaratibu mzuri wa ajira ya walimu kero nyingi zitakwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nilitaka kusema ni kwamba suala la ushirikishaji wa wadau, tutawashirikisha wadau wakiwemo walimu, chama chao na wengine wote wenye shule zisizo za Serikali ili kwa pamoja tuangalie jinsi ambavyo tunaweza kushirikiana katika kuendeleza elimu nchini.

Mimi ningependa kusema kwamba ili mradi Serikali imeamua kuendeleza elimu ya sekondari na wananchi wakaitikia kwa hali na mali wamechangia, naomba uzi uwe huo huo, tunawashukuru sana kwa jinsi ambavyo mmejitolea lakini tuendelee kwa sababu mpaka sasa hivi elimu ya sekondari ni ya muhimu sana na tunaangalie pia baada ya kutoka sekondari kitu

gani kifuate, ndio hayo kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba tunaangalia Vyuo vya Ufundi pia kuvipanua ili angalau vifikie kila Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na ninampongeza Mwenyekiti wa Kamati na wajumbe kwa ujumla, naunga mkono hoja ya Mwenyekiti wangu. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri na hasa kwa kuunga hoja ya Mwenyekiti wa Kamati na ninaamini yale mengine yameshindwa kujibika hapa kwa ujumla unaweza ukatusaidia kutupa majibu kwa maandishi kwa faida ya Waheshimiwa Wabunge wote.

Ninaomba nimwite Naibu Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa Gaudentia Kabaka na yeye kwa muda mfupi aweze kusema *commitment* za Serikali katika hayo yaliyojitokeza kwenye mjadala wa Kamati. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kusema machache tu kuhusiana na hoja hii iliyopo hapa mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabla sijazungumza naomba nichukue nafasi hii fupi kutoa pole nyingi kwa Mheshimiwa Profesa Peter Msolla, pamoja na familia yake kwa kuondokewa na mpendwa wao Marehemu Galusi, ambaye nimemfahamu baada tu ya kuingia Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia, lakini pia mke wake ambaye alinikuta shule ya sekondari. Kwa hiyo, familia nilikuwa naifahamu.

Pia nimpe pole Mheshimiwa Harith Mwapachu, kwa kufiwa na mama yake mpendwa pamoja na wafiwa wote na wale waliokuwa wahanga wa lile basi la Buffalo kule Mwanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba nimshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii kwa taarifa hii yenye mapana na iliyokuwa na ufasaha katika maeneo yote hususan eneo la Elimu ya Juu. *(Makofi)*

Kwa kuanzia naomba tu niwataarifu Waheshimiwa Wabunge kwamba Wizara yangu inaandaa marekebisho ya sheria ambayo ilianzisha Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Mchakato umeshafikia hatua nzuri na uko tayari kuletwa hapa Bungeni na ikiwezekana mwezi wa sita tutaupitisha kusudi uweze kutumika mwezi wa saba wakati tunaanza kipindi cha masomo.

Pamoja na hiyo naomba niseme tu machache kuhusiana na yale aliyoyazungumza Mheshimiwa Said Arfi, lakini nikiri tu kwamba katika haya yaliyozungumzwa na Mwenyekiti wa Kamati mengi tutayajibu kwa maandishi kwa sababu muda hautoshi.

Sasa naomba niseme hivi ukweli ni kwamba wanafunzi kulipa 40% haitaweza kukwepeka kwa mwaka huu wa fedha, asilimia hii 40% ilifikiwa baada ya wanafunzi kujaza fomu na kutoa taarifa kuhusiana na uwezo wao wa kuweza kulipa. Niwaarifu tu kwamba wengi waliangukia katika kundi la kulipa 60% yaani Serikali ichangie 40% na wao wachangie 60%. Wachache waliangukia katika 60% na 40%, Serikali kwa kuona hali halisi na kulingana na kiasi cha fedha kilichokuwepo tukaona wote tuwalipie angalau *maximum 60%* na wao wachangie 40%. Hii ina maana gani? Ukichukua kwa mfano upande wa ada Chuo

Kikuu cha Dar es Salaam 60% Serikali ilichangia 360,000/= na wao wanapaswa kuchangia 240,000/=. Hii pesa ambayo sasa hivi imeleta mgogoro ambayo ni pesa ya *practical,* Serikali imechangia 201,600/= na wao wanapaswa kuchangia 134,000/=. Ukiangalia vitu vingine ambavyo Serikali imechangia, imechangia chakula na malazi, imechangia kwa masuala ya *research,* imechangia kwa masuala ya viandikwa na vitabu. Kwa hiyo, vipengele vilivyobaki vilikuwa vya kuchangia asilimia kidogo kusudi mwanafunzi aweze kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ilikuwa kwa vyuo vyote yaani Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Vyuo vyake vishiriki pamoja na Vyuo vya Mzumbe, vyuo vya binafsi vilikuwa na ada tofauti. Sasa kwa nini Chuo cha Dar es Salaam chenyewe kione kwamba watoto wale ni maskini kuliko Chuo cha Mzumbe? Ni kwa sababu wakati wanaingia Mzumbe walilipa na ndiyo maana hamjasikia wamegoma.

Sasa huu mgomo hauna maana kwamba watoto hawa hawawezi kulipa ada kwa sababu imechukuliwa tahadhari kuwaeleza nini maana ya kulipa 40% angalau kwa mwaka huu wa fedha tuweze kufika kipindi cha mwaka wa fedha ujao ambapo taratibu na wakati sheria inarekebishwa tutaweza kurekebisha masuala yote hayo. Lakini wanafunzi wale wamekataa katakata, wameongea na Katibu Mkuu kwa saa nne wamekataa, uongozi wa Chuo Kikuu umewaeleza wamekaa. Nilipenda tu niweke wazi kwamba baada ya hapo wanafunzi walionekana wanataka kufanya fujo na siyo zaidi ya hapo. Katika hali hiyo, tusingeendelea kuwaweka chuoni kwa sababu kuna wenzao waliopigwa hata kule Chang'ombe kwa ajili ya kwamba walitaka kwenda madarasani na wenzao wakawakataza.

Nilifikiri niliweke hili wazi kwamba wanafunzi hao hawakufukuzwa na kwamba ahadi ya Mheshimiwa Rais iko pale pale, walipaswa kusubiri mpaka mwezi wa sita wakati wanakwenda kwenye *practical* kwa sababu *practical* ni mwezi wa sita, kwa nini waanze kufanya fujo sasa hivi?

Kwa hiyo, ni makusudi. Kwa hiyo, katika taratibu za Chuo huwezi kuendelea ku-*contain* wanafunzi wanatembea na magongo, fimbo na wanawatoa wenzao madarasani, ni lazima kwanza warudi nyumbani, tutafanya mchakato, tutaendelea kusudi ni nani hakuhusika na nani amehusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naahidi kwamba Wizara yangu itaendelea kupata pesa ya kutosha kwa mwaka wa fedha ujao tume-*commit* shilingi bilioni 117 kwa ajili ya Bodi ya Mikopo na tuna hakika kwamba kwa kurekebisha sheria ya elimu, tutaendelea kufanya kazi nzuri na kwa uzoefu tulioupata hasa kwa kutumia kupima uwezo yaani *means testing* tutaweza kujua mhitaji wa mkopo ni nani, nani anahitaji 100%, nani anahitaji 20% na nani anahitaji 80%.

Kwa hiyo, ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla, naomba tuwe pamoja kwa sababu hili suala lisiwe zaidi la kisiasa lakini muangalie hali halisi. *(Makofi)*

Kuhusu *division I* na *II,* mimi nafikiri ninyi nyote ni wazazi, ukiwa na pesa kidogo na una watoto watano, utawapeleka zaidi shuleni wale ambao wana uwezo zaidi. Kwa hiyo, kama una pesa kidogo kama nilivyojibu swali hapa juzi kulingana na uwezo huo utaangalia wale watoto waliofaulu vizuri zaidi kusudi hao ndio watumie kutumia zile pesa kidogo ulizonazo.

Kwa hiyo, suala la *division I* na ushindi mzuri hatutaweza kulikwepa katika utoaji mikopo kwa sababu tunataka tuwakopeshe na tuwasomeshe wale watoto wanaofaulu vizuri ambao ndiyo mtaji wa Taifa, lazima twende kimkukuta hata katika suala la utoaji mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina muda wa kuendelea kuzungumza mengi lakini naomba kwa kweli tuwe pamoja, tuvumilie na tuangalie hali halisi kwani Wizara iko tayari kurekebisha sheria yake na Waheshimiwa Wabunge tutawaomba mtusaidie kutoa mawazo yenu kusudi tuweze kuweka sheria hii katika matumizi mazuri kwa vijana wetu. Baada ya kusema hayo sijagongewa kengele sijui niendelee? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kuunga hoja mkono. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Tunakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia, kwa majibu ya hoja ambazo zimejitokeza mbele yetu. Sasa naomba nimuite Mtoa Hoja mwenyewe aweze kuhitimisha hoja yake, Mheshimiwa Omar Shabani Kwaangw', Mbunge wa Jimbo la Babati Mjini, karibu.

**MHE. OMAR S. KWAANGW' - MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii kwa kunipa nafasi tena ya kuhitimisha hoja yangu na nitumie nafasi hii kuwashukuru wale wote waliopata nafasi ya kusema hapa Bungeni kwa hoja hii na ninaomba niwatambue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Said Arfi Mbunge, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Hasnain Dewji, Mheshimiwa Margaret Sitta, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Mheshimiwa Gaudentia Kabaka, Naibu Waziri Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia. Waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mheshimiwa Yono Kevela , Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed na Mheshimiwa George Lubeleje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote ninawashukuru sana kwa michango yote na kwa jinsi ambavyo Waheshimiwa Naibu Mawaziri walivyoweza kujibu, nina hakika hawajapata nafasi ya kutosha kujibu hoja zote vizuri lakini ni imani yangu kwamba katika kipindi muafaka wataweza kujibu hoja zote ambazo zimejitokeza na hasa pamoja na hizi ambazo zimeletwa kwa maandishi tutahakikisha kwamba zinaingizwa kwenye *Hansard* na Mawaziri wote wanaohusika waweze kujibu kwa sababu zote zinagusa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba kwa bahati mbaya inaonekana muda haukutosha sana kwa ajili ya hoja hii kujadiliwa kwa kina na kwa sababu taarifa ni ndefu nadhani ni imani yangu kwamba wakati ujao hoja za Kamati tunaomba zipate muda wa kutosha, zijadiliwe kwa kina na kama nilivyosema kwenye hoja yangu kwamba ni vizuri mambo yanayotoka kwenye Kamati yaangaliwe kwa undani na Serikali ifanye utafiti wa kina hasa katika maeneo kama nilivyosema hili ambalo linahusu elimu ya juu na hasa linalogusa mikopo kama kama tulivyosema.

Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia kwa kusema kwamba Serikali iko tayari kuleta Muswada wa Sheria kama tulivyoomba ili tatizo hili la mikopo liweze kutatuliwa kwa kuzingatia vilevile maoni ya wadau. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge sasa likubali taarifa ya Kamati ya Huduma za Jamii kwa mwaka 2006 pamoja na mapendekezo na maoni yaliyomo katika taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja ya Kamati iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Taarifa ya Kamati ya Huduma za Jamii ilipitishwa na Bunge)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mbunge wa Babati Mjini na Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mwenyekiti ametoa hoja yake na Waheshimiwa Wabunge na hasa Wajumbe wa Kamati husika nimewaona wamesimama kuunga mkono hoja hiyo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nina furaha kuwatangazia kwamba hoja hiyo imeungwa mkono na Wabunge takribani wote na sasa imepokelewa rasmi. Naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati husika, kwa kweli kazi yenu imekuwa ni kazi nzuri na kadri mlivyoiwasilisha hapa Bungeni kwa kweli wote tumeona kwamba mmefanya kazi ya kutosha kwa niaba ya wananchi wa Tanzania.

Niwashukuru Serikali kwa kupokea na kuiunga mkono hoja hiyo, ninaamini kwamba tutashirikiana katika kuyafanyia kazi maoni na ushauri na Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Bunge linaendelea kufanya utaratibu wa kuona ni namna gani linaweza kuboresha muundo na mtindo huu wa kuwaruhusu Wabunge kuchangia vya kutosha na kwa undani shughuli ambazo zimefanywa na Kamati katika kipindi cha mwaka husika.

Kwa hiyo, nadhani tuvute subira na hasa katika shughuli nzima ya mabadiliko ya Kanuni zetu nadhani tunaweza tukajipanga vizuri zaidi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, shughuli ambazo zilikuwa kwenye meza yangu kwa siku ya leo na hasa katika kipindi hiki cha jioni ninaona zote zimekamilika, lakini ninalo tangazo moja kutoka kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, ameniomba niwatangazie

Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii kukutana kesho tarehe 20 Aprili, 2007 saa 02.15 asubuhi chumba namba 231, Jengo la Utawala.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, mtatakiwa muwahi kabla ya shughuli za Bunge hazijaanza. *(Makofi)*

Anasema kwamba kutakuwa na mkutano wa Wajumbe wa Kamati hiyo na wageni wetu Wabunge kutoka Bunge la Denmark, kwa hiyo, anaomba sana Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hiyo ifikapo saa mbili asubuhi wote muwe tayari mmeshaketi katika chumba husika tayari kwa kuwapokea wageni na kuanza huo mkutano wenu wa mashauriano, Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hiyo nafikiri mmelielewa vizuri tangazo.

Baada ya shughuli hizo za leo nawashukuru kwa ushirikiano na kazi nzito ambazo zimefanyika leo toka asubuhi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa naahirisha shughuli hizi za Bunge mpaka kesho saa 03.00 asubuhi.

*(Saa 01.45 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Ijumaa, Tarehe 20 Aprili, 2007 saa tatu asubuhi)*